15 MEI, 2013

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

### MKUTANO WA KUMI NA MOJA

**Kikao cha Ishirini na Sita - Tarehe 15 Mei, 2013**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa Z. Azzan) Alisoma Dua*

### HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Randama za Makadirio ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. JOSEPHINE J. NGENZABUKE (K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA):**

Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI – MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI WA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa Wizara ya Viwanda na Biashara Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014.

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Swali letu la kwanza leo ni Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, litaulizwa na Mheshimiwa Philipa Mturano.

Na. 209

### Taasisi za NIDA na RITA Kuunganishwa

**MHE. PHILIPA G. MTURANO** aliuliza:-

Kuna ushabihiano mkubwa kati ya kazi zinazofanywa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini *(RITA).*

Je, kwa nini Serikali isiziunganishe Taasisi hizi ili moja iwe Idara chini ya nyingine ili kupunguza gharama kubwa za uendeshaji?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kwa ridhaa yako naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philipa G. Mturano, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa *NIDA* ni Taasisi ya Muungano iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 36(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kupitia amri ya Rais iliyotolewa katika tangazo

la Serikali Namba 112 la tarehe 30 Julai, 2008. *NIDA* imeanzishwa kwa lengo la kuweka mfumo na kuwezesha utoaji wa vitambulisho vya Taifa katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa usajili, Ufilisi na Udhamini yaani RITA ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Sura ya 245 kwa lengo la kushughulikia masuala ya Usajili, Ufilisi na Udhamini kwa upande wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Upande wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar masuala ya Usajili, Ufilisi na Udhamini yanashughulikiwa na vyombo viwili kwa mujibu wa Sheria za Zanzibar. Kuna Ofisi ya Mrajisi wa Vizazi na Vifo ambayo inashughulikia usajili wa vizazi na vifo na Ofisi ya Mrajisi Mkuu ambayo inashughulikia masuala ya Ufilisi na Udhamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa vyombo hivi vimeundwa kwa malengo tofauti haiwezekani kuviunganisha kutokana na Sheria ilizovianzisha. Hata hivyo Serikali imeupokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na itaufanyia kazi ili kuona namna bora ya kuviwezesha vyombo hivi kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

**MHE. PHILIPA G. MTURANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa moja ya sifa ya kupata vitambulisho vya Taifa ni kuwa na cheti cha kuzaliwa na kwa kuwa wananchi wengi hasa vijijini hawana vyeti vya kuzaliwa. Je, Serikali inampango gani wa kuhakikisha kwamba wananchi hawa wanapata vyeti vya kuzaliwa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Philipa Mturano kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa kama ambavyo tulieleza katika hotuba yetu ya Bajeti ya tarehe 3, May mwaka huu RITA imeshaanza kampeni ya usajili kupitia mpango wa Usajili wa Watoto chini ya miaka 5 lakini pia tunayo kampeni ya usajili wa watoto wenye miaka 6 mpaka 18 katika shule mbalimbali.

Lakini pia tunajitahidi kufanya kampeni zingine kwa watu wazima ambao hawana vyeti vya kuzaliwa lakini si hii tu tunataka tubadilishe sheria yetu ya usajili wa vizazi na vifo ili ikiwezekana tuweke masharti maalum mtu asipate ajira kabla hajaonyesha cheti za kuzaliwa, mtu asipate leseni ya biashara kabla hajaonyesha cheti cha kuzaliwa pamoja na leseni nyingine mbalimbali na tunaamini kwa kufanya hivi itatusaidia kuongeza viwango vya usajili, ahsante sana.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, asante. Kwa kuwa Mamlaka ya vitambulisho vya Taifa imekuwa ikienda pole pole sana na hadi sasa tunavyoongea Watanzania wengi hasa walioko Mikoani hawajaanza kupata kabisa vitambulisho. Nini mpango wa Serikali kuhakikisha na wale walioko Mikoani wanaanza kupata haraka iwezekanavyo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Utumishi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Njwayo kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NIDA* ni chombo kipya na wote tunafahamu masuala haya ya utambuzi siyo masuala ya kuyafanyia haraka mimi nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira. Tumeanza sasa hivi kutoa vitambulisho kwa Watumishi wa Taasisi za Serikali pamoja na vyombo vingine na tayari usajili ulikwisha anza katika watu wengine mbalimbali katika Mikoa mbalimbali.

Suala hili si dogo inabidi pia *NIDA* wajitahidi kuwasiliana na mifumo mingine ya usajili wa vizazi lakini pia ya vifo. Kuna wengine wanaweza wakawa wamefariki lakini

ukajikuta umetoa kitambulisho cha Taifa kwa hiyo ni masuala ambayo lazima kuwa waangalifu lakini tunajitahidi na tutaongeza kasi. *(Makofi)*

Na. 210

**Suala la Watoto Wanaozagaa Mitaani/Mijini Wakiombaomba**

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE** aliuliza:-

Idadi ya watoto wanaozagaa mitaani na mijini wakiombaomba imezidi kuongezeka.

(a) Je, Serikali imefanya utafiti wowote kujua idadi ya watoto wanaoishi katika mazingira hayo?

(b) Je, kuna mpango gani mahsusi uliokusudiwa na Serikali wa kuwasaidia watoto hao ili waondokane na shughuli hiyo ya kuombaomba?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Luckson N. Mwanjale, Mbeya vijijini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la kuhudumia watoto Duniani yaani *UNICEF* na wadau wa masuala ya watoto ilifanya utafiti katika jiji la Dar es Salaam mwezi Juni 2012 ili kubaini kuwa ukubwa wa tatizo la watoto wanaoishi mitaani. Utafiti huu ulilenga Dar es Salaam zaidi kutokana na ukweli kwamba wengi wa watoto hawa wanaishi katika jiji hili ukilinganisha na Mikoa mingine. Matokeo ya utafiti huu yalibaini kuwa jumla ya watoto 5580 wanaishi na kufanya kazi mitaani. Wavulana walikuwa 4520 ambao ni sawa na 81% na wasichana walikuwa 1060 sawa na 19% ya watoto wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha utafiti huu ulibaini kwamba watoto hao wanatoka katika Mikoa karibu yote nchini na hata nje ya nchi. Vile vile ilibainika kwamba ziko sababu mbalimbali zinazochangia watoto hawa kukimbia familia zao na kuingia mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika zoezi la utafiti huo jumla ya watoto 185 waliweza kurudishwa na kuunganishwa na familia zao toka Dar es salaam kwenda Mikoa mbalimbali. Kati ya idadi hiyo watoto 128 ni wavulana na 57 ni wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha ulinzi na usalama wa watoto wote wanaoishi katika mazingira hatarishi nchini Waziri Mkuu wa jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, alizindua Mpango Kazi wa Taifa awamu ya pili yaani 2013/2017 wa huduma na matunzo kwa watoto mwezi Frebuari, 2013. Mpango kazi huu wa taifa umeainisha hatua mbalimbali zitakazochukuliwa na jamii, wadau na Serikali kwa upande mmoja ili kukabiliana na changamoto zinazohusu watoto walio katika mazingira hatarishi.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Waziri au ya Serikali. Lakini kwa kuwa karibu nchi zote duniani zinakuwa na ombaomba, ukienda Marekani, ukienda Ulaya hapo, ukienda Asia, ombaomba wako wengi kila mahali.

Lakini aina ya ombaomba walioko mitaani ni watu wazima lakini kitu kinachonishangaza ni hawa watoto vijana hawa wanakuwa omba omba mitaani na je, haki yao ya kupata elimu hawa watoto iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili. Je, Wizara itakuwa tayari kutenga pesa za kutosha au Bajeti kubwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba Ustawi wa Jamii unashughulikia watoto hawa ambao wanazagaa mitaani?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haki ya kupata elimu kwa watoto wote ni haki ya msingi na ni jukumu la kwetu sisi wote yaani wazazi, jamii, halmashauri na serikali kuu kwa pamoja.

Ni matumaini yangu kwamba Wizara kwa upande mmoja inaainisha miongozo, inatoa taratibu inawezesha wataalam wetu kufahamu na kuweza kutekeleza kazi zao za kuweza kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na kuweza kuwapatia huduma kwa misingi na taratibu zilizoainishwa. Lakini vile vile Halmashauri zina jukumu kubwa baada ya kufanya zoezi la kuwatambua watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi zoezi ambalo limefanyika toka mwaka 2005 hadi 2012 ambalo watoto zaidi ya 850,000 wameweza kutambuliwa katika mazingira hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuzichambua asasi zinazoshiriki katika kuwasaidia watoto bado jukumu la kuelimisha watoto na kupata haki zao za msingi limo katika kila Halmashauri ambazo sisi ni wajumbe katika mabaraza hayo ya Halmashauri. Ni wajibu wetu katika kila Halmashauri kuhakikisha kwamba inawatambua watoto hao na inaandaa taratibu za kimsingi kuweza kupata haki zao za msingi hasa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Wizara kutenga Bajeti, Bajeti zimetengwa na nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kupitisha Bajeti yetu ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na naamini katika ustawi huo wa jamii kuna maeneo kadhaa ambayo Wizara imetenga fedha katika matumizi yakeikiwemo kutoa uwezeshaji wa kufundisha wataalam ambao wakifika kwenye Halmashauri zetu wataweza kutoa jukumu la kuweza kuhakikisha watoto hawa wanapata huduma za msingi lakini vile vile kuzitambua asasi zinazotoa huduma hizo kwa watoto na kushirikiana nazo katika kutoa hizo huduma lakini vile vile kuwezesha

Halmashauri zetu kuhakikisha kwamba wanatoa huduma stahili kwa watoto. *(Makofi)*

**MHE. MARIAM R. KASEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa katika majibu ya msingi ya Mheshimiwa Waziri amesema watoto waliopo mitaani wengine wanatoka nje ya nchi. Je hawa waliotoka nje ya nchi wameingiaje nchini na kuweza kuwa ombaomba katika nchi yetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri jibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo.

Watoto wanaweza kutoka nje ya nchi haina maana kwamba ametoka nje ya nchi akaingia hiyo ni upande mmoja lakini upande wa pili tukubali kwamba tuna kambi za Wakimbizi na tuna watu kutoka nje ambao wako nchini na watoto wanaweza kutoroka katika maeneo hayo wakaingia katika miji yetu. Kwa hiyo, utaratibu wa mtoto kuingia ambaye ametoka nje ya nchi anaweza kuingia kwa njia mbalimbali ambazo zinamruhusu mtoto kuingia.

**MHE. SUSAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuwa suala la watoto hawa ombaomba asilimia kubwa hasa Dar es Salaam utakuta wazazi wao wako pembeni. Kwa hiyo, wao ndiyo wanaosababisha watoto wao wanasakizia kuja kuomba kule barabarani. Je, Serikali ina mpango gani kuchukulia hatua hawa wazazi kabla ya hawa watoto ili kuepusha watoto hawa kuomba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoainisha katika jibu la msingi kwamba katika maeneo ya kushughulikia watoto wa mitaani na watoto ambao wanashiriki katika zoezi la kufanya ombaomba na hasa wale wazazi ambao wanakuwepo na watoto wao pembeni ni suala ambalo Halmashauri zetu zinatakiwa kulishughulikia na tuna toa agizo kwa Halmashauri kuweza kuwashughulikia wale wazazi ambao wanajimudu lakini wanatumia watoto kama sehemu ya mtaji wa kuweza kujinufaisha.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea tunaingia sasa Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Anne Kilango.

Na. 211

**Afya Bora kwa Mtoto wa Tanzania**

**MHE. ANNE K. MALLECELA** aliuliza:-

Jukumu la kuhakikisha afya bora ya mtoto ni la wazazi, lakini Serikali nayo inao wajibu wa kuweka mazingira mazuri ya kuweza kupata watoto wenye afya bora na hivyo kupata Taifa bora lenye nguvu.

Je, Serikali inajihusisha vipi kikamilifu kufanya maandalizi ya mazingira bora ya kuhakikisha kwamba Taifa linapata watoto wenye afya bora na hivyo kupata Taifa la kizazi kizuri zaidi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anne K. Malecela, kutoka Same Mashariki, kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo kuu la Sera ya afya ni kuboresha afya na Ustawi wa Jamii kwa Watanzania wote kwa kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuwa na jamii ya watu

wenye afya bora wanaoweza kujipatia maendeleo yao wenyewe na Taifa kwa ujumla. Sera hii pia imeweka msisitizo na kipaumbele kwa makundi maalum ya jamii wakiwemo wanawake na watoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kwamba Taifa linakuwa na watoto wenye Afya bora Serikali inatekeleza mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na mkakati wa tatu wa Sekta ya Afya yaani *Health Sector Strategic Plan III* na mkakati wa Taifa wa lishe. Mikakati hii inalenga katika kuhakikisha kuwa watoto wanapata huduma za kinga, tiba, lishe zenye ubora, gharama nafuu, endelevu na zenye kuzingatia usawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inahakikisha kuwa, watoto wanapatiwa chanjo ya kudhibiti magonjwa yanayozuilika kwa chanjo kama kifua kikuu, polio, *tetanus, nimonia*, homa ya ini, homa ya uti wa mgongo na kuharisha. Aidha watoto wamekuwa wakipatiwa vyandarua ili kuwakinga na mbu wanaoeneza malaria na pia kuwapatia dawa za minyoo na *vitamin A* kila baada ya miezi sita.

Vile vile, mtoto anapozaliwa anapatiwa joto, dawa ya macho, anaanzishiwa kunyonya ya mama ambayo ni muhimu sana katika ukuaji na afya ya mtoto kimwili, kiakili na kisaikolijia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Wizara imeweka mazingira mazuri ya kutoa huduma ya ufuatiliaji na ukuaji wa maendeleo ya mtoto katika kliniki zote za afya ya uzazi na mtoto nchini. Aidha Taasisi ya chakula na lishe yaani *TFNC* inatoa ushauri wa lishe kwa kuzingatia utumiaji wa maziwa ya mama pekee hadi umri wa miezi sita na baadae kuanza vyakula vya nyongeza, matumizi ya madini joto na nyongeza ya matone ya *vitamin A.* Watoa huduma za afya nchini wameendelea kujengewa uwezo ili kuboresha huduma za afya kwa watoto. Dawa muhimu hotolewa bure kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano aidha elimu ya afya kwa jamii na mazingira zimeendelea kutolewa kwa kutumia njia mbalimbali, ili kuwa na watoto wenye afya bora.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata majibu ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Tanzania tuna watoto wengi sana ambao hawapati malezi ya uhakika na mtoto ni mali ya Jamhuri.

Kwa kuwa wakati mtoto yule anakuwa, ubongo wake unakuwa na maswali mengi sana, ambayo maswali haya yasipopata majibu ya uhakika wakati anapokuwa. Mtoto huyo anaweza akaishia kuwa binadamu asiye na maadili au akaishia hata kuwa jambazi kwa sababu ya kutokupata malezi mazuri aliyopata majibu wakati ubongo wake unataka majibu.

Je, Serikali inasaidiaje hawa watoto wadogo ambao hawapati malezi ya uhakika na mwisho tunaishia kupata Taifa ambalo lina watoto wengi ambao hawana maadili na wengi wanaishia kuwa majambazi.

Pili, kwa kuwa takwimu za uhakika zinaonyesha kwamba, takribani asilimia arobaini na mbili (42%) ya Watoto wa Tanzania wanapata utapiamlo na utapiamlo unawaathiri katika kukua kimwili na kiakili pia.

Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kinadharia wa kurejesha wa akina mama Afya ambao mimi niliwaona miaka ya 60 nilipokuwa ninakuwa na nikaona michango yao ambayo ilinisaidia hata mimi kufika hapa nilipofika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA Na USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba malezi ya mtoto katika umri mdogo yanachangia kwa kiwango kikubwa sana namna mtoto huyo atakavyokuwa na atakavyoweza kumudu maisha yake hapo baadaye. Suala la malezi kama Serikali tumeainisha katika sehemu mbili kubwa.

Kwanza, baada ya mama kujifungua na kupata huduma zote stahili zinazotolewa, lakini pia mama huyo anapata ruhusa ya uzazi, likizo siku 84 na baada ya likizo ya siku 84, anapata muda saa mbili karibu kila siku ili aweze kutoa fursa ya kuweza kunyonyesha na kuhudumia mtoto wake. Baada ya pale, tumeanza na sera ya kuanzisha elimu ya awali kwa watoto kwenye shule zetu.

Katika tafsiri hiyo maana yake, mtoto anakuwa anaingia katika mazingira ya shule na kupata mafundisho na baadhi majibu ya maswali ambayo anakuwa anajiuliza mtoto huyu, anapokuwa maeneo ya shule na majibu hayo anapatiwa na walimu ambao wanawasaidia watoto katika makuzi.

Vilevile, ni kweli utapiamlo ni moja katika changamoto zinazowakabili watoto wetu. Hata hivyo, umuhimu wa kuwepo akina mama lishe kama Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii tumeanza kuweza kuona namna ambavyo vituo vyetu vya Afya vinatoa huduma na wataalam waliopo katika kliniki wanatoa huduma kwa mama juu ya lishe yake na mtoto. Pia, anapata *Vitamins* na Chanjo.

Hata hivyo, tuna mpango tunaoungalia hivi sasa kama tafiti juu ya uwepo wa watoa huduma vijijini ambao watakuwa na uwezo huo. Hivi sasa mpango huo umeanza maeneo ya Ifakara na vijana wenye kiwango cha elimu ya kidato cha nne, wanapata mafundisho ya miezi tisa na baada ya mafunzo wanarudi katika maeneo ya Kaya zao na kuanza kuwahudumia wananchi. Moja katika mambo ambayo wanaweza kuhudumia ni pamoja na kutoa elimu ya lishe.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa, takwimu za Mheshimiwa Anne K. Malecela, za asilimia arobaini na mbili (42%) za watoto walioko kwenye tatizo la utapiamulo ni za mwishoni mwa miaka ya sabini, (1970) na Ubongo wa mtoto unakuwa kwa asilimia themanini (80%)akiwa na mwaka 0-8. *Mental stagnation* ya miaka 1970 imesababisha sana wataalam

wetu wa sasa kukalili zaidi, ndiyo maana tunapata madaktari ambao baada ya kufanya *operation* ya mguu, wanafanya ya kichwa, wahandisi wanafanya maamuzi magumu ambayo yanasababisha magorofa yanaanguka na mambo ya namna hiyo.

Je, takwimu za sasa za *mental stagnation* ya kizazi ya cha sasa ukilinganisha cha miaka ya sabini ikoje?

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu waziri unajibu vizuri na kuwa makini lakini jaribu kujibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali kama ifuatavyo:-

Sina hakika juu ya tafsiri ya *mental stagnations* ambayo anaielezea na hasa akihusisha juu ya mambo kadhaa ambayo yanatokea na moja wapo likiwa ni janga la ghorofa kuanguka. Nachoweza kusema ni kwamba, ukuwaji wa mtoto na Afya njema unachangia sana katika kumwezesha kuwa na akili na uwezo mkubwa wa kutambua mazingira yake na kuweza kumudu maisha yake.

Vilevile kuwa na uwezo wa kusoma na kuwa na uwezo wa kuweza kutumia yale aliyosoma vizuri kwa maendeleo ya maisha yake. Hicho ndicho ambacho naweza kusema kwa sasa, lakini juu ya takwimu ya kwamba sasa *mental stagnation* imepungua kwa kiasi gani au imeongezeka kwa kiasi gani nafikiri hii inahitaji utafiti zaidi.

**MHE. EUGIN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, wajibu wa kwanza wa kulinda na kuhakikisha kwamba mtoto anakuwa na afya njema ni wajibu wa mzazi au wazazi wote wawili. Kwa kuwa wako wanawake wenye afya nzuri lakini kutwa hutembea na watoto wachanga barabarani wakuwa wanaomba omba

na kwa kuwa jambo hili linaathiri sana afya za watoto hao. Je, Serikali inawaambia nini wakina mama hawa ambao wana afya nzuri, waaache kutembea na watoto kama omba omba?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Mwenyekiti**,** naomba kujibu kama ifuatavyo:-

Nilishaeleza kwamba, katika kuhudumia watoto maeneo yamegawanyika na kila mmoja anapata eneo lake la kuweza kushughulikia. Nimeelezea kwamba, Halmashauri ndiyo Serikali iliyopo kwenye maeneo ambayo watu tunaishi na sisi wenyewe kama viongozi kwenye kila Halmashauri, tunatakiwa kutambua watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi, wakiwemo wakina mama ambao wanatembea na watoto mtaani wakiwa wanaomba.

Hata hivyo, kila Halmashauri inabidi itafute namna abavyo inaweza kuwasaidia akina mama ambao hawana namna ya kujiwezesha kiuchumi waweze kujihudumia wao na watoto na hivyo kuachana na tabia ya kuombaomba.

Na. 212

**Kuboresha Huduma za TBC Nchini**

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR** aliuliza**:-**

*TBC* Taifa ni chombo chenye ubora katika kutoa habari hapa nchini.

(a) Je, ni Mikoa mingapi inakosa matangazo ya *TBC* hadi sasa?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani kuhakikisha kuwa *TBC* inasikika nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Abdullah Amour, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ambayo haipati huduma ya *radio* ni mikoa tisa (9) ambayo ni kaskazini Unguja, Kusini Unguja, Mjini Magharibi, Kaskazini Pemba, Kusini Pemba, Mtwara, Geita, Njombe na Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mikoa ambayo haipati huduma ya Televesheni ni kumi na mbili (12) ambayo ni Kaskazini Pemba, Kusini Pemba, Geita, Iringa, Katavi, Manyara, Mtwara, Njombe, Ruvuma, Shinyanga na Simiyu. Upatikanaji wa huduma ya Televisheni katika mikoa hiyo uko kwenye mpango wa utekelezaji wa huduma ya Televisheni kupitia mradi wa Dijitali.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua tatizo la usikuvu wa Radio na uonekanaji wa Televisheni kwa baadhi ya maeneo ya nchi. Mpango wa Serikali ni kuhakikisha matangazo ya *TBC* yanamfikia kila Mtanzania popote alipo nchini. Katika kutekeleza mpango huo, Serikali inaendelea na mpango wake wa kufunga mitambo ya *FM Radio* katika miji mikuu na Mikoa yote nchini kwa kadri fedha zinavyopatikana na baada ya hapo katika miji yote ya Wilaya. Hadi sasa *TBC* imefunga mitambo ya *Radio* ambayo matangazo yake yanasikika katika mikoa ishirini na moja (21) na matangazo ya Televisheni ya *TBC* yanapatikana katika mikoa kumi na nane (18). *(Makofi)*

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri yenye kuleta matumaini. Nitakuwa na maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa, Bajeti yako ni ndogo. Je, mipango hii itatekeleza?

Pili, Kwa kuwa *TBC* inaendeshwa kibiashara, kwa nini hizo pesa zinazopatikana zisitekeleze mipango hii?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli kwamba, Bajeti yetu ya Wizara ya Habari bado ni ndogo na tunaendelea kufanya mazungumzo na kamati ya Bajeti kuona kwamba tunaweza kuongeza fedha. Hata hivyo, bado kazi hiyo mnayo ninyi wenyewe tarehe 20, siku ambayo tutawasilisha Bajeti hii na kuipitisha hapa ili mipango yetu hiyo iweze kutekelezeka.

Pili, *TBC* tayari inayo mpango mkakati, *management* na Bodi inaendelea kujipanga na kuona kwamba fedha zinazopatikana zinaelekezwa katika kutekeleza miradi mbalimbali katika shirika hili la *TBC*.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa kuwa, usikivu wa Shirika la Utangazaji *TBC* ni hafifu sana katika Wilaya ya Ngorongoro, hivyo wananchi wa Ngorongoro kulazimika kusikiliza shirika la utangazaji la *KBC* Kenya. Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba eneo hilo la Tanzania usikivu wa Shirika lake la Utangazaji unakuwa murua?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Ni kweli tunatambua kwamba, maeneo mengi hata Wabunge wengi hapa watasimama kuona kwamba lipo tatizo la usikivu wa *radio* katika maeneo mbalimbali. Lengo la Serikali ni kuhakikisha matangazo haya yanafika mahali popote. Naomba sana tarehe 20 mtupitishie Bajeti yetu, ili tuje na mikakati ambayo tunaweza tukatekeleza na kuondoa tatizo hili katika mikoa mbalimbali hapa nchini.

**MHE. MCH. PETER MSINGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa kuwa, Shirika la *TBC* wakati Mkurugenzi wake alikuwa ni Tido Muhando lilikuwa ni kama ndege inayopaa na lilikuwa linatangaza matangazo yake kwa ufasaha bila lawama. Na kwa kuwa sasa hivi ni kama Ndege ambayo iko *grounded* na limekuwa likifanya shughuli zake kwa upendeleo hasa kukibeba Chama cha Mapinduzi. Ni lini sasa Shirika hili litafanya kazi vizuri ili Watanzania warudishe imani kama enzi za Tido Muhando?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo:-

Nataka niseme tu kwamba sisi kama Serikali tungependa kuona Shirika la *TBC* linafanya kazi vizuri katika viwango vizuri na tayari tumewataka *management* na bodi ya *TBC* kuja na mpango mkakati ili shirika hili liweze kufanya kazi kwa ufanisi. Nikuhakikishie tu kwamba, Serikali itaendelea kusimamia shirika hili na kuona kwamba linafanya kazi vizuri. Hata hivyo, shirika hili linafanya kazi bila upendeleo wowote wa chama chochote cha siasa.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Bali na changamoto za *TBC* kushindwa kutanua wigo na changamoto zinazowakabili za vifaa, lakini pia kumekuwa na tatizo kubwa la wafanyakazi wa *TBC* kupata maslahi duni. Hata hawa ambao unawaona Dodoma wanashindwa kuongea tu, lakini maslahi yao ni duni sana, na hiyo inatokana na Serikali kutotenga fedha za kutosha na wanafanya kazi kwa sababu ni wazalendo wa Taifa lao. Je, ni lini Serikali mtaboresha mishahara ya wafanyakazi wa *TBC*?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu kama ifuatavyo:- TBC inawafanyakazi ambao ni sawasawa na wafanyakazi wengine katika Serikali. Kwa hiyo, suala la maslahi madogo ni la watanzania wote ambao wanafanya kazi Serikalini. Tutaliangalia kadri ambavyo maslahi yanaboreshwa kwa wafanyakazi wengine, hili tunalipokea

na mimi naamini kabisa itakapofika wakati wa kusoma bajeti ya mishahara, tutakuwa tunaelewa kwamba *TBC* mishahara yao imeongezeka kwa kiasi gani. *(Makofi)*

Na. 213

**Kujenga Barabara za Mkoa kwa Lami**

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA** aliuliza:-

Je, Serikali itaanza lini kujenga barabara za mikoa zitokazo Tunduru – Wenje, Nalasi – Njenga na Azimio – Makande kupitia Lukumbule kwa lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura Mbunge wa Tunduru Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge yaani; Tunduru – Wenje (Chamba) yenye urefu wa kilometa 85.57; Azimio – Lukumbule hadi Makande yenye urefu wa kilometa 65.69 na Nalasi – Njenga yenye urefu wa kilometa 20; zote ni barabara za mkoa na zinahudumiwa na Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa kipaumbele cha Serikali ni kukamilisha ujenzi wa barabara kuu kwa kiwango cha lami na kuendelea kutenga fedha kila mwaka kwa ajili ya matengenezo ya barabara tajwa ili ziendelee kupitika majira yote ya mwaka katika kiwango cha changarawe.

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Barabara ambazo zimetajwa za Tunduru – Wenje na Azimio –Makande, licha ya kwamba ni barabara za Mkoa vilevile ni barabara za kuisalama kwani zinaunganishwa na nchi jirani ya Msumbiji. Hivi punde tumeona barabara kadhaa

ambazo zinaunganisha nchi yetu na nchi nyingine zimekuwa zikiwekewa lami. Je, Serikali haioni umuhimu kwamba, barabara hizi zina sifa sawasawa na zile nyingine ambazo zinawekewa lami nazo ziwekwe lami?

Pili, katika Jibu la msingi, Mheshimiwa Naibu Waziri amesema kwamba sasa hivi kipaumbele ni barabara kuu kwa maana ya *trunk road*, ndizo zinazowekewa lami. Je, Naibu Waziri utasema nini juu ya barabara za vijiji na za Halmashauri ambazo zinawekewa lami katika baadhi ya Mikoa? (*Makofi*)

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Naibu Waziri swali fupi na wewe jibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Mtutura A. Mtutura, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa, ni kweli barabara anazozisema zinaweza zikawa za kiusalama, hata hivyo kutokana na mpango ambao tumeuweka, barabara ziko nyingi zaidi ya kilometa 86,000 kwa nchi nzima na barabara za Halmashauri ziko kilomita 52,000. Sasa tunasema kwamba ngoja tumalize kwanza hizi barabara kuu, pamoja na umuhimu wake kwamba zingine ni za usalama, zingine zinaunganisha Mikoa, tutakapomaliza hiyo *network* ya barabara kuu, tutaanza kuangalia barabara za Mikoa na vilevile tutazi-*rank* kulingana na umuhimu wa barabara husika, ndiyo tutaanza kuzijenga kwa kiwango cha lami.

Kuhusu barabara za vijiji, au za vijijini ambazo unasema kwamba zingine zimewekewa lami, ni kweli inawezekana kuna baadhi ya barabara ambazo zinahudumiwa na Halmashauri. Kwa mfano tumesema kwenye Miji, Makao Makuu ya Wilaya, ziko barabara angalau waanze kujenga kilomita mbili mbili kwa kutumia fedha za mfuko wa barabara. Kwa hiyo, kuna baadhi ya barabara kwa mazingira fulani, tumeanza kuzishughulikia kwa utaratibu wa namna hiyo.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Kwa kuwa tatizo la Tunduru Kusini linalingana kabisa na la Korogwe Vijijini, haswa kwenye barabara ya kutoka *Old* Korogwe, Kwashemshi, Bumbuli na kutokea Soni, ambayo ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais ya mwaka 2010. Je, barabara hii itawekwa lini lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, lami, wewe mwambie tu Bajeti ikipita imeshapita, utamwekea?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ngonyani kama ifuatavyo:-

Kama tulivyoelezea jana kwamba, ahadi zile za Rais za Uchaguzi za mwaka 2010, tutazishughulikia, namna jinsi tutakavyokuwa tunapata fedha. Kwa hiyo, miradi yote ile, malengo yetu tujitahidi tuweze kufika, kwenye 2015 tuwe tumetekeleza ahadi hizo. (*Makofi*)

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi hii. Kwa kuwa barabara ya Sumbawanga-Kanazi kilomita 75 na Kanazi-Kizi-Kistalike kilomita 76, Kizi-Kistalike-Mpanda, kilomita 95 na Mpanda-Mishamu, kilomita 100, zimetengewa shilingi bilioni 28, ni miujiza ipi itakayotumika kuzijenga barabara hizi zenye kilomita 346 kwa bilioni 28? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kachomekea lakini wewe jibu tu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kakoso kama ifuatavyo:-

Naomba nilieleze Bunge hili kwamba, barabara hizi anazozungumza, kasoro hii inayotoka Mpanda kwenda Mishamu, hiyo ni barabara ambayo tutatangaza *tender* mwaka huu wa fedha 2013/2014, kwa hiyo, hiyo haijaanza.

Kwa hiyo, suala la idadi ya fedha zilizotengwa, tunakwenda kwa ujenzi, tunajenga kwa awamu, kwa hiyo, Makandarasi hawa ambao wako kule kwenye hizo *sites*, wanapoleta zile *certificates* ndiyo tutawalipa, kwa hiyo, fedha hiz kwa mipango yetu ni kwamba zinatosha angalau wao waendelee na kazi, wakizalisha zaidi, Serikali itatafuta fedha za ziada kuweza kuwalipa.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Wizara ya Katiba na Sheria.

Na. 214

**Kujenga Mahakama za Mwanzo Chunya**

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA** aliuliza **:-**

Wilaya ya Chunya inakabiliwa na upungufu wa Mahakama za Mwanzo.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama za Mwanzo katika Kata zote za Wilaya hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria na kwa ridhaa yako naomba kujibu swali la Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa (Mbunge wa Rukwa) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Wilaya ya Chunya inakabiliwa na upungufu mkubwa wa Mahakama za Mwanzo.

Baadhi ya Mahakama zimesitisha kufanya kazi kutokana na ubovu wa majengo, lakini ili haki iwafikie wananchi ipasavyo ingefaa kila Kata iwe na Mahakama ya Mwanzo na hiyo siyo kwa Chunya tu ila ni kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo ni uwezo wa Serikali wa kujenga Mahakama zote hizo. Kwa sasa upo upungufu wa Mahakama za Mwanzo 751, za Wilaya 62 na za Hakimu Mkazi 13 nchi nzima. Mahakama ikishirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI imeandaa mpango kabambe wa kujenga Mahakama hizi. *(Makofi)*

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa kumcheleweshea haki mwananchi ni sawasawa na kumnyima haki na kwa kuwa wananchi wengi wenye makosa hayo ambayo hayajahakikiwa hukaa sana Rumande kwa sababu tu ya kutokuwa na Mahakama ya Mwanzo, pia kutokuwa na Watumishi, huu mpango ambao Mheshimiwa Waziri anasema wameandaa mpango, ni mpango gani, maana yake Wizara ya Elimu na Wizara ya Afya zina mipango ambayo inaonekana ya kujenga vyumba na kuandaa Watumishi, sasa Wizara ya Katiba na Sheria ina mpango gani?

La pili, kwa kuwa kwa Wilaya ya Chunya, acha Mahakama ya mwanzo, hata Mahakama ya Wilaya, wamepata chumba kwenye jengo la Mkuu wa Wilaya ndiyo wanajibanza huko.

Je, Serikali inasemaje kuhusu kuijengea Chunya Mahakama ya Wilaya? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, *specific*.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Victor K. Mwambalaswa, kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza kuhusiana na Mahakama inampango gani wa kujenga Mahakama hizi za Mwanzo ili wananchi waweze kupata haki. Sisi pia tunalitambua hili na sisi pia tunatambua na tunaumia, lakini ndiyo kama ambavyo nimeeleza Takwimu.

Mahakama za Mwanzo ni 751, za Wilaya napenda kurudia tena ni 62 tunazihitaji na za Hakimu Mkazi 13, lakini kwa kushirikiana na TAMISEMI, lakini pia kwa kushirikiana na ninyi Wabunge, kupitia wananchi wenu na sehemu nyingi wamejitahidi kufanya, ukiangalia katika Mahakama ya Wilaya ya Mkuranga, tayari hivi sasa tumekwenda pale tumehamasisha wameshajenga jengo la Mahakama ya Wilaya wamefikia sehemu ya *linter*, lakini pia katika Mahakama ya Mwanzo Karatu tayari na wenyewe wamefika sehemu nzuri tu hivi sasa wanakwamishwa na mvua.

Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge washirikiane na TAMISEMI lakini pia washirikiane na wananchi kuhamasisha na pale ambapo ninyi mtaishia, sisi kama Mahakama tutajitahidi kuwaunga mkono ili Mahakama hizi tuweze kuzijenga kwa wingi zaidi.

Sisi kama Mahakama pia hatujakaa bure, katika mpango wetu wa Mahakama kwa mwaka huu kwa Bajeti ambayo mmetupitishia, tumeahidi kujenga Mahakama za Mwanzo10, lakini kwa kuwa Bajeti yenyewe ni ndogo hatuwezi kusema tutajenga zote kwa pamoja.

Katika swali la pili, ametaka kujua ni lini tutajenga Mahakama ya Wilaya ya Chunya, kwa kweli nimpongeze sana Mheshimiwa Mwambalaswa, toka mwaka 2008, wakati Mheshimiwa Chikawe akiwa Waziri wa Katiba na Sheria, tarehe 14, Februari, aliulizia Mahakama hizi za Mwanzo na Mahakama ya Wilaya ya Chunya. Napenda kumwahidi kwamba kwa mwaka 2014/2015 tutajenga Mahakama ya Wilaya ya Chunya.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Mkoa wetu wa Iringa una uhaba mkubwa sana wa Mahakama za Mwanzo na hivyo kusababisha Mahakama za Mwanzo kama Iramba, Mahenge, Mlolo, kutembelewa na Mahakimu wengine wa Mahakama za Mwanzo, hii inasababisha wananchi wanapokwenda kwenye Mahakama, wanakosa Mahakimu na kusababisha kesi nyingi sana kuchelewa.

Naomba Mheshimiwa Waziri, ni lini sasa tatizo hili litakwisha ili Mahakimu waweze kuenea kwenye Mahakama zote za Mwanzo? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri jibu kwa kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa napenda tu kutoa utangulizi kwamba, tuna upungufu wa Mahakimu 1600, lakini kama Serikali hatujakaa kimya, tunajitahidi kila mwaka basi kuajiri walau Mahakimu 300 na tumeanza mpango huu kuanzia mwaka 2011/2012 tumeshaajiri Mahakimu 300 na katika mwaka 2012/2013 kipindi kinachoishia Juni, 2013 tutaajiri tena Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo 300, mpaka hapo tatizo hili litakapokwisha.

Napenda tu kumhakikishia Mheshimiwa Ritta Kabati, kuhusiana na Mahakama ya Mwanzo ya Mahenge na Mlolo kutembelewa, tutajitahidi pindi watakapoajiriwa tupeleke Mahakimu katika Mahakama hizo ili wananchi waweze kupata haki.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru, na mimi niulize swali moja dogo la nyongeza.

Tatizo ambalo liko Chunya, kama jinsi ambavyo swali la msingi lilikuwa, ni sawasawa kabisa na tatizo ambalo liko Arumeru, kwenye Halmashauri yangu ya Meru na mwaka jana nilimwuliza Waziri na nikajibiwa na Naibu Waziri ambaye ametoka kujibu swali hapa, kwamba wangekuja Arumeru, na kwa sababu hapa watu wanaulizia ujenzi wa Mahakama mpya, lakini kule kwangu Arumeru yako majengo ya Mahakama ambayo yalikuwa yanatumika ambayo yalishajengwa siku nyingi. Lakini leo hii hayatumiki kabisa. Mfano mzuri, ni Mahakama iliyokuwa King'ori, ambayo jengo lipo tu leo hii ni mazalia ya Popo, jengo la pale Nkwangua, jengo la Mahakama pale Pori Barazani ambalo lina kila kitu, kuna umeme, maji, chumba cha Mahakama, cha Mahabusu, lakini majengo yote haya hayatumiki.

Sasa kwa sababu sisi hatuombi kwenda kutujengea majengo mapya ya Mahakama...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nassari, swali, swali.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba Mheshimiwa Naibu Waziri atuambie tu kwamba ni lini au Wizara ina mpango gani basi kuhakikisha kwamba Mahakama zinaanza kufanya kazi ili wananchi waweze kupata haki zao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi, muda wetu ni mdogo sana.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nassari kama ifuatavyo:-

Kwanza kabisa kama Mahakama haipendi kuacha jengo lifikie hatua hiyo na mpaka limefikia hatua hiyo itakuwa ni masuala ya uchakavu na kwa kuwa ina ufinyu wa Bajeti ndiyo maana imeshindwa kutekeleza adhima hiyo ili Mahakama iweze kufanya kazi. Lakini napenda tu kukuhakikishia kwamba kwa Bajeti ya mwaka huu ya mfuko wa Mahakama tutajitahidi kuzipa kipaumbele Mahakama

hizo ili wananchi wa Arumeru, hususan King'ori na Pori Barazani, waweze kupata haki yao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Wizara ya Fedha.

Na. 215

**Hatima ya Wanahisa wa *National Investiment Company Limited (NICOL)***

**MHE. PHILEMON K. NDESAMBURO** aliuliza:-

Kampuni ya *National Investiment Company Limited (NICOL)* iliyoasisiwa na Watanzania na kuhamasishwa na Viongozi Wakuu wa Serikali na Siasa kwa kuwataka wananchi wajiunge na kununua Hisa, haisikiki tena kwa zaidi ya miaka mitano sasa na inasemekana kuwa Kampuni hiyo imefilisika:-

(a) Je, ni nini hatima ya wanahisa wa Kampuni hiyo?

(b) Je, Serikali inachukua hatua gani kwa uongozi wa *NICOL* kwa kuwatapeli wananchi?

(c) Je, Serikali inasema nini juu ya utapeli wa aina hiyo ni pamoja na ule wa *DECI*, UPATU, DOLA JETI?

**WAZIRI WA FEDHA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Philemon Ndensamburo, Mbunge wa Moshi Mjini, lenye vipengele (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, hatima ya wanahisa wa Kampuni ya *NICOL* itaamuliwa na wanahisa wenyewe kwa kuzingatia sheria iliyoanzisha Kampuni hii. *NICOL* ilianzishwa na kusajiliwa chini ya Sheria ya Kampuni, Sura ya 212 ya Sheria za Tanzania. Sheria hii inazo Kanuni na taratibu zinazoelekeza namna ya kuendesha Kampuni na kulinda maslahi ya wanahisa wenyewe.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari wanahisa wenyewe wamechukua hatua dhidi ya uongozi wa Kampuni yao wakati wa mkutano wa mwaka wa wanahisa uliofanyika Januari, 2013. Ikumbukwe kwamba, uongozi huo wa Kampuni haukuwekwa na Serikali bali na wanahisa wenyewe kupitia Bodi ya Wakurugenzi na pindi wanahisa wanapoona kuna umuhimu wa kuchukua hatua dhidi ya uongozi, wanafuata Katiba na Sheria zilizopo.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna utapeli wowote kuhusiana na uanzishwaji na uendeshaji wa shughuli za *NICOL*. Serikali kupitia Bunge lako Tukufu ilipitisha marekebisho ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania) ili kuruhusu uanzishwaji wa Mipango ya Uwekezaji wa Pamoja *(Collective Investmebt Schemes),* ambapo, kupitia utaratibu huu Kampuni ya *NICOL*, *Unit Trust of Tanzania (UTT)* na *TTCIA* zinaendesha shughuli zake. Hivyo Kampuni ya *NICOL* ipo kisheria na haifananishwi na *DECI*, UPATU na *DOLA JET.*

Kilichotokea katika Kampuni ya *NICOL* siyo utapeli hasa, bali kutokuwa na weledi wa kutosha katika menejimenti ya fedha, kwani *NICOL* ilichukua mikopo mikubwa na wakaiwekeza katika vitega uchumi ambavyo baadhi yake vimefilisika na hivyo kuiletea *NICOL* hasara, hiyo hasara imepunguza thamani ya Kampuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inapinga na haitambui uendeshaji wa shughuli za kifedha kwa mifumo ya udanganyifu. Serikali kupitia Bunge lako Tukufu ilifanya marekebisho ya Sheria Na. 8 ya mwaka 2006 kwa kuongeza mafungu ya 171(b) na (c) kwenye Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura ya 16 kuharamisha mifumo isiyo rasmi ambayo ndiyo hiyo aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge Ndesamburo.

Kwa mujibu wa vifungu hivyo vya sheria, ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kuendesha au kushiriki katika mifumo ya fedha ambayo siyo rasmi. Mfumo usiyo rasmi ulioendeshwa na *DECI* uliweza kudhibitiwa kwa kutumia sheria hiyo na wahusika waliweza kufikishwa Mahakamani.

**MHE. PHILEMON K. NDESAMBURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, sasa ninayo maswali mawili madogo ambayo ningependa kupata majibu kwa niaba ya wanahisa wa *NICOL*.

Viongozi wa *NICOL* ni wanahisa tena wakubwa wa *NICOL* na ndiyo wanaoiendesha *NICOL*, inaeleweka wazi kwamba, katika dunia ya sasa, si rahisi kuwekeza kwenye Kampuni au kwenye kitega uchumi ambacho kitaleta hasara, wanahisa wanaamini, ni ujanja ujanja ulitumika kununua Viwanda vilivyokuwa vimeharibika, havina faida yoyote, ila wale waliohusika walifaidika kwa fedha zile.

Je, Serikali haioni kuna haja ya kuchunguza na kuchukua hatua kwa wale walihusika? (*Makofi*)

La pili, *DECI* ilipostopishwa, Serikali ilichukua zile fedha na kuziweka wanakojua, lakini wale watu waliokuwa wamewekeza, mpaka sasa hawajapata faida yoyote na fedha zao hawajapata, ni lini Serikali itawapa zile fedha ambazo zilikuwa zimechukuliwa kutoka Benki? (*Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ndesamburo kama ifutavyo:-

La kwanza, ni kweli, ilibainika kwamba, viongozi yaani Bodi ya Wakurugenzi wa Kampuni ya *NICOL*, walikuwa ndiyo sehemu ya ushauri, wanahisa walipogudua kwamba utaratibu ule ulikuwa haufai, ndiyo maana walichukua hatua.

La pili, kwa nini Kampuni kuwekeza katika vyombo vinavyoleta hasara. Ni kweli inatakiwa kuwekeza katika vyombo ambavyo vinaleta faida, na ndiyo maana Mamlaka (*CMSA)* yenye mamlaka ya kuratibu iliwashauri wawekeze katika Makampuni mengine yanayoleta faida, na hatua hiyo ilikuwa haijakamilika baada ya kuwa Bodi ya Wakurugenzi ilikuwa imesimamishwa, lakini suala hili liko Mahakamani, kwa mgogoro wa wanahisa kutaka haki yao.

La pili, kwa nini na kwa sababu gani mpaka sasa hivi *NICOL,* wanahisa wake hawajapata faida zao. Suala hili linashughulikiwa na baadaye Waheshimiwa Wabunge na wananchi watapata matokeo yake.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea, Wizara ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Riziki S. Lulida. Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali kwa kweli ni mdogo sana.

Na. 216

**Kupeleka Umeme Vijijini**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU (K.n.y. MHE. RIZIKI S. LULIDA)** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme vijiji vya Ngongo-Mikole, Mchinga-Kitomanga na Mchinga - Kijiweni?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE GEORGE B. SIMBACHAWENE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati na Madini, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki S. Lulida, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa kuwafikishia umeme wananchi wa vijiji vya Ngongo-Mikole, Mchinga-kitomanga na Mchinga- Kijiweni, umejumuishwa katika Mpango Kabambe wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili chini ya uwezeshaji wa Wakala wa Nishati Vijijini (*REA*). Zabuni ya kuwapata wakandarasi wa kazi hizi ilitangazwa mwezi Desemba, mwaka 2012 na kufunguliwa mwezi Machi, mwaka 2013 na kazi za ujenzi zinatarajiwa kuanza wakati wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za mradi huu zitajumuisha ujenzi wa njia za umeme za misongo mbalimbali, ufungaji wa *transfoma* na kuwaunganishia wateja wa awali 1,237. Gharama za Mradi zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 4.64. *(Makofi)*

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa majibu ya Mheshimwa Waziri, ningependa nimwulize maswali yafuatayo:-

Kwanza, ahadi za utekelezaji wa miradi katika maeneo yaliyotamkwa na Mheshimwa Waziri, pamoja na maeneo mengine kama vile Matandu, Somanga, pamoja na Miteja, imekuwa inachukua muda mrefu sana na majibu ya Wizara kwamba, muda wowote itakekeleza.

Sasa ningependa kujua *time frame*, kwamba ni muda gani ambapo hii miradi itakuwa imekamilika na wananchi hawa wakanufaika na miradi hiyo ya umeme?

Swali la pili, kipindi ambacho Mheshimiwa Waziri ulifanya ziara katika Mikoa ya Kusini, ulitoa punguzo kwa wananchi kuweza kulipia *rate* maalum kwa ajili ya Mikoa hiyo ya Lindi na Mtwara kwa maana ya maeneo ambayo inapatikana gesi, punguzo lile lilikwisha muda na ukaongezea tena muda, lakini bado muda ule unakaribia kwisha, wananchi bado hawajahamasika kwenda kulipia umeme.

Je, pale ambapo umeme utakuwa umeshashushwa katika maeneo yale punguzo hili litaendelea kuwepo?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu, kama hivi ifuatavyo.

Ni kweli katika awamu ya pili *REA* tunavyo vijiji vingi sana zaidi ya 1,200 katika nchi nzima, ambavyo tunatarajia kuvitekeleza katika mwaka 2013/2014. Lakini kubwa hapa ni wakati wa Bajeti yetu, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge pamoja na fedha kwamba bado tunaendelea kujiweka sawa, lakini katika hizo zilizopo basi mtusaidie tuweze kupitisha Bajeti yetu ili tutekeleze miradi hii.

Mheshimwia Mwenyekiti, ni kwamba nilipofanya ziara, ni kweli katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, tuliamua kuwahamasisha wananchi kwa kupunguza bei ya kuweka umeme kwenye majumba yao. Tulipunguza na kuweka kiasi cha shilingi 99,000/=. *Offer* hii inakaribia kwisha. Kwa hivyo tutajaribu kuangalia hali ya mazingira yatakavyokuwa na pengine tutakuja na makubaliano mengine mapya kwa wakati huo.

**MHE. ZAYNABU M. VULLU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Ninalo swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Serikali kupitia mradi wa *REA,* imeishanza kusambazo nguzo za umeme, kwenye Wilaya ya Kisarawe, kutokea Mlandizi, Mzenga, Kuruwi. Kutokea Kisarawe mjini kuelekea Mwanarumango – Msanga.

Kwa kuwa waya hizo zimewekwa hazijawekwa *transformer* wala kufikishwa umeme kuna hatari ya watu kuiba hizo nyaya za umeme na serikali kupata hasara. Kwa kuwa kuna viwanda vimeanza kujengwa kule vinategemea kupata umeme ili viweze kufanya kazi ya kuzalisha na hali kadhalika kupata ajira kwa vijana na wananchi wanaoishi maeneo ya Wilaya hiyo ya Kisarawe.

Je, Serikali inasema nini, kuhusu kupeleka umeme huo na kuanza kufanyakazi ili kuwapa matumaini wananchi wa Wilaya hiyo ya Kisarawe?

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vullu, kama hivi ifuatavyo.

Ni kweli tuna mpango na Mradi unatekelezwa wa kusamba umeme katika maeneo ya Kisarawe, Mwanarumango hadi Msanga. Utekelezaji wake uko katika hatua hiyo aliyoisema Mheshimiwa Mbunge, ambayo inaashiria ukamilifu wake, kilichobakia pale ni kuwasha na kufanya majaribio. Nimwondoe wasi wasi Mheshimiwa Mbunge, kwamba wakati wowote mradi huu utakapowashwa wananchi watafurahia tu.

Kwa kweli shughuli iliyokwishafanywa na Mkandarasi ni kubwa na inafikia ukingoni. Tuvute subira muda wowote mwezi na ujao unaweza umeme ule ukawashwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea swali linalofuata la Mheshimiwa Vicky Paschal Kamata. Litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Maria I. Hewa.

Na. 217

**Hitaji la Umeme Kama Nishati Mbadala ya Kupikia**

**MHE. MARIA I. HEWA (K.n.y. MHE. VICKY P. KAMATA)** aliuliza:-

Umeme ni nishati mbadala ya kupikia inayoweza kuwasaidia wanawake wa vijijini ambao hutumia muda mwingi na kutembea muda mrefu kutafuta kuni hasa katika mikoa inayozunguka Ziwa Victoria:-

(a) Je, ni vijiji vingapi vimepatiwa umeme katika wilaya za Geita, Nyang'wale na Chato ambazo ndizo zinaunda Mkoa wa Geita?

(b) Je, asilimia ngapi ya wanawake waishio vijijini waliounganishiwa umeme katika wilaya nili zozitaja?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inafikia lengo la kufikia 30% ya wananchi waishio vijijini katika Mkoa wa Geita kama Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya 2010 inavyoelekeza?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE)** Mheshimiwa Mwenyekiti napenda kujibu swali la Mheshimiwa Vicky P. Kamata, lenye sehemu (a) (b) na (c) kama itufavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti maeneo ya Wilaya ya Geita ambayo tayari yanapata umeme wa gridi ya taifa ni pamoja na vijiji vya Kaswama, Kanyara, Mwatulole, Kalangalala, Mseto na Mji wa Geita. Kwa Wilaya ya Chato vijiji vya Mganza, Nyisanzi, Nyamilembe na kazunguti vinapata umeme kutoka Wilaya ya Biharamulo, unaozalishwa kwa mitambo inayotumia mafuta ya dizeli.

Aidha Wilaya za Mkoa wa Geita ni miongoni mwa Wilaya zinakazonufaika na mradi wa umeme unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani yaani *Millenium Challenge Corporation (MCC).* Baada ya mradi kukamilika, jumla ya vijiji 14 vitanufaika. Vijiji hivyo kwa Wilaya ya Geia ni:- (i) Bukondo, Saragulwa, Nyamigota, Katoro, Nyarugusu, Rwamugasa, Ikina, Bukoli, Chigunga na Chikobe. Lakini kwa wilaya ya Chato ni Buselesele na kwa Wilaya ya Nyang'wale ni Nyarubele, Nyangwale na Msalala. Jumla ya wateja waliounganishiwa umeme kwa wilaya ya Geita kwa sasa ni 6,121.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti,ili kuhakikisha kuwa lengo la Serikali la kufikia 30% ya wananchi wanafikiwa na huduma ya umeme, Serikali imejipanga kusambaza umeme kwa awamu kadiri ya upatikanaji wa fedha chini ya Wakala wa Nishati Vijijini *(REA).* Vijiji na maeneo yatakayopatiwa umeme kaika awamu ya pili ya *REA* mkoa wa Geita inayotarajiwa kutekelezwa kuanzia mwaka huu ni vijiji 68. Aidha mradi utawaunganisha na wateja wa awali 6,902 na Gharama zinakadiriwa kuwa shilingi bilioni 16.6. Orodha ya ijiji husika vipo kwenye jibu la msingi ambalo nimekwisha mpatia Mheshimwia Mbunge.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, niulize maswali mafupi mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilishawahi kukaa muda mfupi Biharamulo na nikawa nimelala pale. Umeme wa pale ni hafifu kabisa. Ambapo ndiyo unategemewa kutumiwa katika maeneo mbali mbali.

Umeme huo, kama ndiyo huo ninouzungumza. Je, utatosheleza kuusambaza tena, kama ndiyo Biharamulo yenyewe, umeme ni hafifu? *(Makofi)*

La pili, umetoa orodha ya vijiji na sekondari nyingi tu za mkoa wa Geita, ambazo zitapatiwa umeme kwa kutuma *REA II,* unaniruhusu nimpe orodha hii Mheshimiwa Vicky Kamata, kwa maana ya kuzungumza sasa ni lini, hivi vijiji na sekondari karibu zote za Geita zitapatiwa umeme, wakati atakapoanza ziara zake katika mkoa wa Geita, ni lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, unaombwa ujibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (MHE. GEORGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimwia Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maria I. Hewa, kama hivi ifuatavyo:-

Kwamba umeme ule unaotoka Biharamulo kama ndiyo unaotarajiwa kusambazwa ni hafifu. Tatizo hili tumelishughulikia na linaenda sambaba na ufungaji wa mashine mpya katika wilaya za Biharamulo, Ngara na Mpanda.

Ni hiyo jana tarehe 14 Mei, 2013 nilikuwa ninazungumza na Mpanda pale wanajaribu hawana *crane* kubwa ya kushushia *generator* ile lakini imeishafika. Napenda kusema ya kwamba kama Ngara wanahangaika kushuka *generator,* inawezekana zija-*check,* lakini inawezekana hata Biharamulo napo wanajaribu kushusha *generator* na hata Mpanda wanajaribu kushusha *generator* yao.

Napenda nimhakikishie ya kwamba mradi huu na mashime zile *generator* zitaboreshwa na Biharamulo kutakuwa kuna umeme ambao utakuwa wa uhakika sana. Lakini *REA II* ni linini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ni kuhakikisha kwamba tunasambazo umeme kwa vijiji vya *REA II,* kama tulivyo ahidi na kama tulivyoviorodhesha. Kwa hiyo, nimhakikishe kwamba hiyo orodha niliyompatia ampatie Mheshimiwa Mbunge, aende akatambe nayo na kwamba CCM, itahakikisha inatekeleza miradi ya umeme.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi katika nchi hii leo kumekuwa kuna utaratibu wa wananchi kulilipia umeme. Gharama za kuunganishia umeme *TANESCO,* ikiwemo kulipia na nguzo na badala yake wanachukua muda mrefu sana kabla hawajapelekewa umeme.

Kwa mfano, Maeneo ya Kata ya Buongwa Jiji la Mwanza na Kata ya Mkolani, wananchi wamelipia gharama za kuunganisha umeme toka mwaka 2012, mwezi Desemba, mpaka sasa hawajapewa umeme. Sasa ninaiuliza Serikali huu mfumo wa *TANESCO,* kukopa fedha kwa wananchi na kufanya nazo biashara na wanakaa nazo muda mrefu, halafu wanapeleka umeme pale ambapo wataamua wao. Huu mfumo umeanza lini na Serikali itaukomesha lini? Ili wananchi wanapolipia umeme waunganishiwe haraka kwa kadiri inavyowezekana?

**NAIBU WAZIRI NISHATI NA MADINI (MHE. GERGE B. SIMBACHAWENE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Wenje, kama hivi ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninasikitika kwamba kama kweli Mwanza hali ndiyo hiyo na taarifa hizi mimi ninazipata kila mara. Ucheleweshaji siyo wa kiasi hicho. Niseme tu kama wako mahali popote iwe wilayani au mkoani, wanakochelewa kuwafungia wateja wao wakishakuwa wamelipia, hili ni kosa kubwa na wanapaswa kwa hakika kuchukuliwa hatua kwa sababu kwenye takwimu zetu haionekani hiyo.

Ucheleweshaji unakuwepo kidogo kwa muda wa wiki moja, wiki mbili au wiki tatu, lakini siyo wa kiasi hicho. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge tuonane baada ya hapa tuelezane ukweli huo na tushughulikie.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Swali la Wizara ya Maji linatakaloulizwa na Mheshimwa Jerome D. Bwanausi.

Na. 218

**Mradi wa Maji – Chiwambo**

**MHE. JEROME D. BWANAUSI** aliuliza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ninaomba Kabla ya swali langu halijabiwa, lisomeke kama hivi ifuatayo.

Serikali iliahidi kutoa Sh.580,000,000/= kwenye mabano imeandikwa (Milioni mia tano themanini elfu tu). Iwe Serikali iliahidi kutoa Sh.580,000,000/= (Milioni mia tano themanini) kwa ajili ya kukamilisha ukarabati wa miundombinu ya maji ya mradi wa Chiwambo katika Jimbo la Lulindi kupitia ahadi ya Mheshimiwa Rais:-

Je, ni lini fedha zitakamilishwa ili mradi huo uwanufaishe wananchi wanaokabiliwa na tatizo kubwa la maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jerome D. Bwanausi, Mbunge wa Jimbo la Lulindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa Serikali iliahidi kutoa Shilingi millioni 580 kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa maji wa Chiwambo katika wilaya ya Masasi. Maradi huo unahudumia wakazi wapatao 45,994 katika vijiji 23 vya Kata sita (6) za Namalenga, Chiungutwa, Lulindi, Sindano, Mchauru na Mbuyuni. Serikali imeanza kutekeleza ahadi yake ya Mheshimiwa Rais kwa mradi huo wa Chiwambo ambapo

hadi sasa shilingi milioni 130 zimetolewa kwa ajili ya ukarabati wa mradi huo. Fedha hizo zimetumika kununua na kulaza mabomba mapya ya nchi 6 yenye urefu wa kilomita 5.4 kati ya kilometa 11 za bomba kuu la kutoa maji kwenye chanzo cha chemche ya Lulindi hadi kwenye tanki la kuhifadhia maji lililopo katika kijiji cha Nagaga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha wa 2013/2014, kiasi cha shilingi milioni 530 kimetengwa katika Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa ajili ya ukarabati wa mradi huo.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Lakini ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, amekiri kwamba mradi huu ni ahadi ya Mheshimiwa Rais, aliyoitoa alipotembelea kwenye jimbo la Lulindi.

Je, anawadhibitishiaje wananchi wa Kata hizi (6), kwamba mradi huo ambao unatekelezwa na Serikali na siyo Halmashauri, utakuwa umepata fedha katika kipindi hiki cha Bajeti ya 2013/2014?

Kwa kuwa katika jibu la msingi la Mheshimiwa Waziri.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaomba utulivu kidogo. Samahani.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Kwa kuwa kwenye swali lake la msingi Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba upelekaji wa fedha hizi umekuwa wa kusuasua. Je, yuko tayari sasa Wizara ya Maji kutangaza tenda ili kumpata Mkandarasi makini atakayemaliza mradi huu kwa pamoja?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ametaka tuwahakikishie wananchi kwamba ule mradi sasa utatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni muhimu sana. Ni mradi ambao ulijengwa mwaka 1955 na umekarabatiwa tu kidogo mwaka 1990. Kama ilivyo kwenye jibu la msingi, mradi huu unahudumia vijiji 23. Kwa hiyo, umuhimu wa kuukarabati haraka ni mkubwa sana, kwa sababu *impact* yake itakua kubwa kwa wananachi.

Kwa hiyo jibu langu la msingi ni kwamba tumejipanga, na ndiyo maana Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya imetenga milioni 530 hizi siyo hela ndogo ni hela nyingi. Niwapongeze Halmashauri ya Wilaya ya Masasi kwa kuliona hili na kutoa kipaumbele kwa Miradi ya Maji, na wilaya nyingine ziige mfano huo. *(Makofi)*

Sasa kwamba tunaahidi vipi Wizara ya Maji kupeleka fedha. Ninataka nimhakikishie tutafuatilia na mimi nitapanga ziara kwenye kuukagua Mradi huu vizuri ili tuone kwamba unatekelezwa kwa wakati na wananchi wa wilaya ya Masasi katika sehemu ya Jimbola Lulindi wanapata maji.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha, na ni vigumu kumpa kila mtu nafasi kwenye swali la nyongeza, kutokana na muda uliokuwepo.

Matangazo. Wageni waliopo jukwaa la Spika. Ni mgeni wa Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mbunge na Waziri wa Uchukuzi, ambaye ni *Enginer* Deogratius Rumiruzu (Mbunge na Waziri wa Uchukuzi wa Burundi). Karibu sana Mheshimiwa Waziri kutoka Burundi. *Welcome to The Parliament of Tanzania. (Makofi)*

Wageni waliofika Bungeni kwa ajili ya mafunzo. Wageni wa Wabunge wa Mkoa wa Dar es Salaaam, ambao ni wenyeviti wa Serikali za Mitaa 60 kutoka Dar es Salaam, karibuni. Pamoja na hao wameambatana na Danyl Kapwani na Dominic Malindi kwenye mafunzo hapa Bungeni. Karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa John Joel, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote wanaotoka Mkoa wa Mtwara, Lindi na Pwani, kuwa wanaombwa kuhudhuria mkutano wa mashauriano wa kujadili changamoto, zilizojitokeza katika tasnia ya Korosho msimu wa 2012/2013. Mkutano huo utafanyika siku ya Alhamisi tarehe 16 Mei, 2013 kuanzia saa 8.00 mchana katika ukumbi wa *Royal Village,* hapa Dodoma. Wabunge wote wa mikoa hiyo wanaombwa kuhudhuria.

Mheshimiwa Margareth S. Sitta, - Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Huduma za Jamii, anawatangazia Waheshimiwa Wabuge wote kuwa leo Jumatano tarehe 15 Mei, 2013 saa 8.00 mchana kutakuwa na shughuli ya utoaji vyeti vya kuwatambua wadau waliochangia maendeleo ya Chuo Kikuu HUria. Shughuli hiyo itafanyika katika ukumbi wa Pius Msekwa.

Mgeni rasmi katika shughuli hiyo atakuwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi, Dkt. Shukuru Kawamba, Mbunge, akiambatana na Mkuu wa Chuo Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro. Aidha Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge ambao mtapokea vyeti hivyo mnaombwa kuzingatia muda.

Mheshimiwa Victor Mwambalaswa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Nishati na Madini, anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Nishati na Madini, kuwa leo tarehe 15 Mei, saa 7.00 mchana kutakuwa na kikao cha Kamati. Kikao hicho kitafanyika katika ukumbi Namba 231 ghorofa ya pili jengo la utawala.

Nachukua nafasi hii Waheshimiwa Wabunge kwanza kuipongeza Klabu ya *Dar es Salaam Young Africans* kuchukua ubingwa wa nchi hii katika soka na ninatoa pongezi hizi kwa klabu hiyo na Mwenyekiti wake Yssuf Manji na mimi nikiwa kama Mbunge wa Klabu hiyo inatoka katika Jimbo langu. *(Kicheko/Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2013/2014 Wizara ya Viwanda na Biashara

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba. Kutokana na taarifa ilyowasiizhwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara, pamoja na Taasisi zake ambayo ilichambua Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Tasisi zake zilizochini yake tarehe 4 Aprili, 2013. Sasa Bunge lako Tukufu, likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha ya Wiwara ya Viwanda na Biashara, na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, WahEshimwia Wabugne, wakirejea hotuba niliyoisoma Bungeni mwaka 2012/2013. Wataona kuwa tuliazimia kwanza kuendeleza Viwanda vikubwa na vya kati. Pili kuendeleza viwanda vidogo na biashara ndogo, tatu kuendeleza biashara ya ndani ya a nje. Nne kuendeleza masoko ya ndani na ya nje na tano kutoa huduma bora kwa wadau wa Sekta za viwanda na Biashara.

Aidha nilisisitiza kuwa katika kukuza uchumi wa viwanda mtazamo wetu usjielekeze kwenye ujenzi wa kiwanda kimoja kimoja, bali ujielekeze kwenye mchakato mpana wa ujenzi wa viwanda na kutengeneza ajira za kutosha kwa Watanzania. Kwa maana ya *Industrializatization.* Fikra zetu na mtazaomo wetu tuvielekeze huko na ndiko tunakokwenda hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeamua sasa masuala ya Viwanda Biashara na Maksoko yatafanywa na Wantanzaia wote na ninatoa wito kuwa wakati umefika na wakati ni huu. Kama msimamizi wa Wizara hii tutahakisha kuwa Wantanzia wote bila mlolongo au urasimu kwa waliokwishanza na wanaotaka kuanza kuendeleza viwanda biashara na masoko, tutendelea kuwawezesha.

Mhehimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kuwa buheri wa afya na hivyo kutekeleza majukumu yetu ya kustawisha maisha ya jamii ya Watanzania. Kipekee sana, namshukuru Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwa na imani nami pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Gregory George Teu, Mbunge wa Mpwapwa, kwa kuendelea kutupa dhamana ya kuongoza na kusimami majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Rais kuwa tunaendelea kwa ari na nguvu zaidi kuyatekeleza majukumu hayo kwa kutoa ushirikiano unaotakiwa kwa Baraza la Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uchumi , Viwanda na Bishara chini ya uongozi wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa, Mbunge wa Jimbo la Mufumdi Kaskazini (CCM) na Makamu wake Mheshimiwa Dunstun Luka Kitandula, Mbunge wa Mkinga (CCM) kwa kuiongoza kamati hiyo. Ni matumaini yetu kuwa Kamati hiyo itaoa msukumo mpya katika kushughulikla masuala ya sheria, sera na mikakati ya kisekta.

Vile vile, napenda kuwapongeza wanakamati wote kwa umakini wao katika kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yangu. Napenda KuwathibitIshia kuwa, maoni yao yamezingatiwa na ndiyo yalikuwa msingi mkuu katika kuboresha Hotuba ninayoiwasilisha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Niruhusu pia niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara ambayo imemaliza muda wake chini ya aliyekwua Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa Mbunge wa Jimbo la Mufindi Kaskazini (CCM) na Makamu wake Mheshimiwa Gaudence Cassian Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki (CCM). Nikiri kuwa tulinufaika sana na umahiri wao na ushirikiano makini katika kuchambua kushauri na kusimamia maendeleo ya sekta yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe, Naibu Spika, Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge, Katibu wa Bunge na Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge pamoja na Bunge lako Tukufu, kwa ushirikiano tunaoupata kutoka kwenu katika kuwasilisha masuala mbalimbali ya Wizara yangu, ikiwemo Miswada ya Sheria na mapendekezo ya Bajeti ya Wizara hii. Napenda kuwahakikishia kwamba, Wizara yangu itaendelea kutoa ushirikiano unaohitajika ili kuleta matokeo yanayokusudiwa katika sekta yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Jimbo la Katavi (CCM) kwa Hotuba yake inayobainisha mafanikio na mwelekeo wa utendaji wa Serikali ya Awamu ya Nne. Vilevile, nawapongeza Mawaziri walionitangulia kuwasilisha hoja zao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Handeni kwa ushirikiano wao unaoniwezesha kuendelea kutekeleza ipasavyo majukumu yangu kama Waziri na yale ya kuwawakilisha katika Bunge lako Tukufu. Pia, kwa namna ya kipekee naishukuru familia yangu hususan mke wangu, watoto, ndugu na marafiki zangu wote kwa ushirikiano, upendo na dua zao ambazo zimekuwa nguzo muhimu katika ufanisi wa kutekeleza majukumu hayo ya kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazishukuru pia Wizara, Taasisi za Serikali na wadau wote, hususan Asasi za Sekta Binafsi zikiwemo Chama cha Wadau wa Ngozi Tanzania - *LAT*; Baraza la Kilimo Tanzania - *ACT*; Baraza la Taifa la Biashara - *TNBC*; Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania - *CTI*; Chama cha Wafanyabiashara, wenye Viwanda na Kilimo Tanzania - *TCCIA*; Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania - *TPSF*; Chama cha Wafanyabiashara Wanawake - *TWCC* na Vikundi vya Biashara Ndogo *(VIBINDO)* kwa michango yao katika kuendeleza Sekta ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ambazo Wizara yangu inaisimamia. Aidha,

nawashukuru wananchi wote na vyombo vya habari kwa ushirikiano wao hususan kwa maoni yenye kujenga na kuelimisha umma kuhusiana na utendaji wa Wizara na sekta kwa ujumla. Ari hiyo ambayo ni chachu muhimu katika maendeleo ya sekta na uchumi wetu kwa ujumla naomba iendelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nawashukuru Naibu Waziri, Mheshimiwa Gregory George Teu; Katibu Mkuu - Bi. Joyce K. G. Mapunjo, Naibu Katibu Mkuu - Dkt. Shaaban R. Mwinjaka; na Wakuu wa Idara, Vitengo na Taasisi zilizo chini ya Wizara, kwa mshikamano na ueledi wao katika kuongoza na kusimamia utekelezaji wa majukumu ya kisekta. Nawapongeza na kuwashukuru pia wataalam na watumishi wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kujituma na kutuandalia ushauri wa kitaalamu unaotuwezesha kufanya maamuzi mbalimbali yenye lengo la kuendeleza Sekta ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Vilevile, napenda kuwashukuru wale wote ambao kwa njia moja ama nyingine, tulishirikiana nao katika maandalizi ya hotuba hii ninayoiwasilisha leo. Namshukuru pia Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali na wachapishaji wengine kwa kuchapisha machapisho ya Wizara yangu kwa ubora na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuungana na Waheshimiwa Mawaziri na Wabunge wenzangu kuwapa pole ndugu na jamaa kwa kuondokewa na mpendwa wetu, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis - Mbunge wa Chambani(CCM), Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema amrehemu na ampumzishe kwa amani mahali pema Peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2012/2013. Katika Hotuba ya Bajeti ya mwaka 2012/2013, Wizara iliazimia kutekeleza yafuatayo:-

· Kuendeleza viwanda vikubwa;

· Kuendeleza viwanda vidogo na biashara ndogo;

· Kuendeleza biashara ya ndani na nje;

· Kuendeleza masoko; na

· Kutoa huduma bora kwa wadau wa Sekta ya Viwanda na Biashara.

Katika eneo la kukuza uchumi wetu kupitia viwanda, mwelekeo wetu ulikuwa kwenye mchakato mzima wa ujenzi wa viwanda *(industrialization)* badala ya mtazamo wa ujenzi wa kiwanda kimoja kimoja *(Industries).* Fikra zetu *(mindset)* na mtazamo wetu *(attitude)* ni vyema tukauelekeza huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imedhamiria kuendeleza Sekta za Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo licha ya changamoto tunazokutana nazo hasa uhaba wa rasilimali fedha. Nia yetu ni kushirikiana na sekta zinazozalisha mali moja kwa moja ili tuelekee kwenye uchumi wa viwanda tunapoelekea mwaka 2025. Lengo hilo linawezekana, kwani hata taarifa za uchumi zinaonesha dhahiri kuwa hivi sasa uzalishaji viwandani pamoja na Sekta za Huduma, Ujenzi, Utalii na Miundombinu hasa ya barabara, reli na bandari inachangia kwa kiasi kikubwa katika Pato la Taifa. Huo ni mwelekeo mzuri hasa tukizingatia kuwa duniani kote, ushahidi, uzoefu na historia ya uchumi vinaonesha hakuna uchumi ulioendelea, hata kwa nchi zinazoendelea hivi sasa *(emerging economies)* kwa kutegemea kilimo pekee. Hivyo, napenda kutumia fursa hii kulieleza Bunge lako Tukufu utekelezaji uliofanyika katika kipindi cha 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya sekta ya viwanda, biashara, masoko, viwanda vidogo na biashara ndogo; Wizara imekuwa ikisimamia na kutekeleza sera na mikakati ya sekta kupitia Mpango mkakati wa Wizara wenye kubainisha dira, dhima na malengo ya Wizara kwa kipindi cha miaka mitano. Katika kutekeleza mipango ya kisekta, Wizara imekuwa ikizingatia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010; Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini

(MKUKUTA II), Kilimo Kwanza, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016) na Mpango Elekezi wa Mwaka 2011 – 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda. Katika kipindi cha mwaka 2012, Sekta ya Viwanda ilikua kwa asilimia 8.2 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.8 mwaka 2011. Kiwango hicho kimetokana na kuongezeka kwa shughuli za uzalishaji viwandani hususan usindikaji wa vyakula, utayarishaji wa vyakula vya wanyama, mafuta ya alizeti, uzalishaji wa vinywaji, saruji na bidhaa za chuma. Pamoja na ukuaji wa sekta kuongezeka, bado ongezeko hilo liko chini ya lengo la asilimia 15 lililoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo *(Vision 2025).* Mchango wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 9.7 mwaka 2011 na kufikia asilimia 9.85 mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012, uzalishaji katika baadhi ya viwanda kama vile vya chuma, vinywaji na sigara uliongezeka. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa hizo katika soko la ndani. Uzalishaji wa chuma uliongezeka kwa asilimia 16.9 kutoka tani 39,955 mwaka 2011 hadi kufikia tani 46,690 mwaka 2012. Uzalishaji wa bati uliongezeka kwa asilimia 5.9 kutoka tani 76,912 mwaka 2011 hadi tani 81,427 mwaka 2012. Uzalishaji wa saruji uliongezeka kwa asilimia 7.2 kutoka tani milioni 2.4 mwaka 2011 hadi tani milioni 2.6 mwaka 2012. Uzalishaji wa nyavu za uvuvi uliongezeka kwa asilimia 79.9 kutoka tani 164 mwaka 2011 hadi tani 295 mwaka 2012. Vilevile, uzalishaji wa bia uliongezeka kwa asilimia 4.7 kutoka lita milioni 323.4 mwaka 2011 hadi kufikia lita milioni 338.7 kwa mwaka 2012 na uzalishaji wa sigara uliongezeka kutoka sigara milioni 6,630 mwaka 2011 hadi kufikia sigara milioni 7,558 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 14.0, na uzalishaji wa konyagi uliongezeka kwa asilimia 8.7 kutoka lita milioni 15.4 mwaka 2011 hadi lita milioni 16.8 mwaka 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imechangia asilimia 27.9 katika Pato la Taifa. Sekta hiyo imeajiri Watanzania

milioni 5.2 wanaofanya kazi katika jasiriamali *(enterprises)* zipatazo milioni tatu. Kati ya hizo, jasiriamali 1,675,385 ziko vijijini, jasiriamali 466,049 zipo Dar es Salaam na zilizobaki 935,256 zipo katika maeneo mengine ya mijini. Asilimia 54.3 ya jasiriamali hizo zinamilikiwa na wanawake na asilimia 45.7 zinamilikiwa na wanaume. Shughuli za uzalishaji na kuongeza thamani zinachukua asilimia 13.6 ya jasiriamali hizo. Hii inaashiria kwamba msukumo mkubwa zaidi unahitajika katika kukuza sekta ya uzalishaji na uongezaji thamani ili iweze kutoa mchango zaidi katika ajira na pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Biashara kwa ujumla ilikua kwa asilimia 7.7 kwa mwaka 2012 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.1 mwaka 2011, ikiwa ni pungufu kwa asilimia 0.4. Hii ni kutokana na kushuka kwa bei ya baadhi ya mazao katika soko la kimataifa kama vile pamba (asilimia 18.3), korosho (asilimia 1.9), karafuu (asilimia 14.9), kahawa (asilimia 6.9) na madini (asilimia 4.2). Aidha, mchango wa sekta katika pato la Taifa ulikuwa asilimia 12.3 mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 12.2 mwaka 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya mauzo nje iliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 5,097.3 mwaka 2011 hadi Dola za Marekani milioni 5,912.3 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 16. Ongezeko hilo lilitokana na kuongezeka kwa wingi wa bidhaa zilizouzwa nje. Kwa mfano, mauzo ya pamba yaliongezeka kutoka tani 40,300 mwaka 2011 hadi tani 132,000 mwaka 2012, ikiwa ni ongezeko la asilimia 227.4.

Vilevile, mauzo ya pamba yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 61.1 mwaka 2011 hadi Dola za Marekani 164.9 mwaka 2012, sawa na ongezeko la asilimia 167.6. Thamani ya mauzo ya bidhaa za viwandani iliongezeka kufikia Dola za Marekani milioni 1,047.3 mwaka 2012 ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 861.5 mwaka 2011, sawa na ongezeko la asilimia 21.6. Takwimu hizo na za miaka ya nyuma zinadhihirisha kuwa bei ya bidhaa za viwandani zimekuwa haziyumbi ikilinganishwa na mazao ghafi. Serikali inaendelea kuhamasisha uanzishwaji wa viwanda vya

kuongeza thamani mazao ili kupunguza uuzaji wa bidhaa na mazao ghafi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nije kwenye Sekta ya Masoko. Bei ya mazao makuu ya chakula ya mahindi, mchele, maharage, ngano, ulezi, na mtama zimeongezeka katika kipindi cha mwaka 2012/2013. Kwa mfano, wastani wa bei ya jumla kwa gunia la mahindi la kilo 100 ilipanda kutoka Sh. 43,309/= mwaka 2011/2012 na kufikia Sh. 65,028.3 mwaka 2012/2013 sawa na ongezeko la asilimia 50.2; na bei ya gunia la maharage la kilo 100 ilipanda kutoka Sh. 123,606/= hadi Sh. 131,336.90 sawa na ongezeko la asilimia 6.89. Kupanda kwa bei ya mazao makuu ya chakula pamoja na sababu nyingine ni kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta ya petroli kulikosababisha ongezeko la gharama za uzalishaji na usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya baadhi ya mazao ya biashara kama vile chai, kahawa aina ya robusta na mkonge ziliongezeka katika kipindi cha mwaka 2012/2013, kutokana na ongezeko la bei za mazao katika soko la nje. Kwa mfano, bei ya zao la chai ilikuwa wastani wa Sh. 206/= kwa kilo ikilinganishwa na wastani wa Sh. 196/= mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la asilimia 5.1. Vilevile, bei ya mkonge ilipanda hadi Sh. 1,249.80 kwa kilo ikilinganishwa na Sh. 1,114/= mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la asilimia 12.2. Bei ya mbegu ya pamba ilipanda kutoka wastani wa Sh. 1,000/= mwaka 2011/2012 mpaka Sh. 1,200/= kwa kilo mwaka 2012/2013, sawa na ongezeko la asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, kumekuwa na ongezeko la bei ya mifugo kwa ng'ombe, mbuzi na kondoo. Kupanda kwa bei hizo kumechangiwa na ongezeko la ubora wa mifugo na ongezeko la mahitaji. Wastani wa bei ya jumla ya ng'ombe daraja la pili iliongezeka hadi Sh. 480,467/= ikilinganishwa na Sh. 427,438/= mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la asilimia 12.41. Bei ya ng'ombe daraja la tatu ilipanda hadi Sh. 367,393/= kutoka Sh. 328,151/= mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la asilimia 11.96. Bei ya mbuzi ilipanda hadi Sh. 46,576/= kutoka

Sh. 42,323/= mwaka 2011/2012, sawa na ongezeko la asilimia 10.05, wakati bei ya kondoo ilipanda hadi Sh. 38,482/= kutoka Sh. 37,078/= katika kipindi hicho hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010. Wizara kwa kushirikiana na Taasisi 18 zilizo chini Wizara yangu, imeendelea kutekeleza malengo ya Sekta za Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kama yalivyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa Wizara *(Strategic Plan 2011/2012 – 2016/2017)* ambao umezingatia utekelezaji wa maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM. Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi wa CCM ya mwaka 2010, umewezesha kupatikana kwa mafanikio mbalimbali ya kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika uwekezaji na biashara katika soko la ushindani, Wizara imechukua hatua kuimarisha ushiriki wa Sekta Binafsi katika uwekezaji na biashara ili kushiriki vyema katika soko la ushindani. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuipa nguvu ya kisheria Mamlaka ya Maeneo Huru ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje *(EPZA)* kusimamia uwekezaji katika Maeneo Maalum ya Uwekezaji *(Special Economic Zones – SEZ).*

Katika maeneo hayo, wawekezaji wa sekta mbalimbali wataweza kuzalisha na kuuza bidhaa katika masoko ya ndani na nje ya nchi. Wizara kupitia *EPZA* kwa kushirikiana na Serikali za Mitaa, imeendelea na jitihada za kutenga maeneo maalum ya uwekezaji katika Mikoa iliyobaki ya Simiyu, Katavi, Geita na Njombe. Vilevile, *EPZA* imelipa fidia katika maeneo ya *SEZ* ya Mbegani - Bagamoyo na Ujiji - Kigoma. Jitihada za kutafuta fedha kwa ajili ya maeneo ya Bandari - Mtwara, Bunda - Mara, Mererani – Manyara na mengineyo zinaendelea. Pia, *NDC* imetenga maeneo kwa ajili ya kuvutia uwekezaji: *TAMCO* - Kibaha, Kange - Tanga na *KMTC* - Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kujenga na Kuimarisha Ujuzi Katika Biashara na Kuweka Msukumo Zaidi

Katika Kutumia Fursa za Masokol; katika mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Chuo cha Elimu ya Biashara *(College of Business Education – CBE)* imeendesha mafunzo ya ujasiriamali ya muda mfupi ambapo jumla ya washiriki 53 walipata mafunzo hayo. Mafunzo yalihusu mbinu za kubuni biashara, namna ya kupata mtaji, ujuzi wa kusimamia na kuendeleza biashara, utafutaji masoko na stadi za kuimarisha ubora wa bidhaa. Vilevile, *SIDO* iliendesha mafunzo kwa wajasiriamali 4,766 katika Mikoa yote ya Tanzania Bara na kutoa elimu ya ujasiriamali, uongozi wa biashara, stadi za kazi, usindikaji wa vyakula, ujuzi wa kiufundi katika uzalishaji wa mafuta ya kula, ngozi, ubanguaji korosho na uhifadhi wa vyakula vya aina mbalimbali.

Chini ya Mradi wa *EDF10,* jumla ya Wajasiriamali 125 na Maafisa Biashara 16 kutoka Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Kanda ya Kusini na Kanda ya Ziwa walipata mafunzo chini ya uwezeshaji wa wataalam kutoka *SIDO*, *BRELA*, *GS1* na *TBS*. Mafunzo yalihusu utumiaji wa nembo za ubora, kuweka mipango ya biashara vizuri na kuitekeleza, kudhibiti ubora wa bidhaa, utengenezaji na utunzaji wa mitambo na ujasiriamali. Aidha, mafunzo hayo yamewezesha wajasiriamali kuanza na kuweza kuuza bidhaa zao kwenye *'Supermarkets".* Vilevile, Wizara kupitia *SIDO* iliweza kutoa huduma za ugani kwa wajasiriamali 9,660 nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuimarisha na kuwezesha Kituo cha Mafunzo na Uzalishaji wa Bidhaa za Ngozi Dodoma, *DIT* kampasi ya Mwanza hapo awali ikiitwa *Tanzania Institute of Leather Technology (TILT)* na Vituo vya Chama cha Wadau wa Ngozi *Tanzania (Leather Association of Tanzania - LAT)* vya Dar es Salaam na Morogoro. Vituo hivyo vilitoa mafunzo ya usindikaji wa ngozi na utengenezaji wa bidhaa za ngozi kwa washiriki 351 katika Mikoa tisa ya Tanzania Bara ambayo ni Arusha, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Mwanza, Ruvuma, Shinyanga, Dodoma na Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ina sera, mikakati, sheria na kanuni mbalimbali zinazoongoza Sekta za Viwanda,

Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo, ambazo ndiyo msingi wa kuimarisha uendelezaji na ukuzaji wa mauzo nje.

Katika kuendeleza na kukuza mauzo nje, Wizara imetayarisha na kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje unaojumuisha Mfumo wa Kuendeleza Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje *(EPZ),* Maeneo Maalum ya Kiuchumi *(SEZ),* Masoko ya Mipakani *(Border Markets),* Kamati ya Kitaifa na za Kikanda *(EAC na SADC)* za Kuondoa Vikwazo Visivyo vya Kiushuru *(Non Tariff Barriers-NTBs),* Vituo vya Pamoja vya Mipakani *(One Stop Border Posts - OSBPs)*, Alama ya Utambuzi wa Bidhaa *(GS1),* Kamati za Pamoja Mipakani *(Joint Border Committees - JBCs)* na Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani.

Vilevile, kwa kutambua umuhimu wa biashara katika mazingira ya utandawazi, Wizara inaandaa Mfumo wa Soko la Bidhaa *(Commodity Exchange)* na kutumia mfumo wa uhamasishaji biashara na masoko kupitia maonesho ya kitaifa na kimataifa *(Trade Fairs, Exhibitions, Expos and Trade Missions).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarisha kifedha Benki ya Maendeleo *TIB* ili Kiwe chombo madhubuti cha kuchochea mapinduzi ya viwanda nchini kwa kutoa mikopo ya muda mrefu na riba nafuu kwa wawekezaji wakubwa, wa kati na wadogo nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imelenga kuiongezea Benki ya Maendeleo *TIB* mtaji wa Shilingi bilioni 500 katika kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2010, ili kuimarisha uwezo wa utoaji mikopo ya muda mrefu kwa wawekezaji hususan kwenye kilimo na viwanda. Mwaka 2010/2011, Serikali ilitoa jumla ya Shilingi bilioni 50 na mwaka 2012/2013, Shilingi bilioni 50. Hadi sasa, Serikali imekwishatoa Shilingi bilioni 100 kwa Benki hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee kuhusu kuwekeza katika mradi wa makaa ya mawe ya mchuchuma,

chuma cha liganga na viwanda vya kemikali na mbolea katika kanda za maendeleo kikiwemo kiwanda cha mbolea aina ya *urea* Mkoani Mtwara na kuwezesha Kiwanda cha Minjingu kuzalisha mbolea bora ya *NPK* na *MPR* ili kufikia lengo lililowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia kusainiwa kwa mkataba wa ubia kati ya *NDC* na Kampuni ya *Sichuan Hongda Group*, tarehe 21 Septemba, 2011, Kampuni ya ubia iitwayo *Tanzania China International Mineral Resources Limited (TCIMRL)* ilianzishwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Chuma cha Liganga kwa mfumo unganishi.

Mradi wa Makaa ya Mawe unatarajiwa kuzalisha umeme wa megawati 600 ambao utatumika katika uchenjuaji na uyeyushaji wa madini ya chuma na ziada kuingizwa kwenye gridi ya Taifa. Tayari uchorongaji wa makaa ya mawe ili kubainisha wingi na ubora umekamilika ambapo makaa yaliyohakikiwa yanatosheleza kuzalisha umeme wa megawati 600 kwa kipindi cha miaka 80. Kampuni ya *TCIMRL* inatarajia kufua umeme kwa kuanzia na Megawati 300 mwaka 2015/2016.

Kazi ya uchorongaji kwa upande wa chuma cha Linganga inaendelea na inatarajiwa kukamilika Desemba, 2013. Ujenzi wa mgodi unatarajiwa kuanza Januari, 2014, ili uzalishaji wa chuma uanze mwaka 2015/2016. Awali ilipangwa kuzalisha tani 500,000 za chuma kwa mwaka, lakini baada ya tafiti za mahitaji ya soko, kiwanda kitakachojengwa kinatarajiwa kuzalisha tani milioni moja za chuma kwa mwaka.

Hata hivyo, utekelezaji wa mradi unakabiliwa na changamoto ya ubovu wa barabara hususan eneo la Itoni – Mchuchuma – Liganga ambapo Serikali ilikubali kutoa Shilingi bilioni 1.7 mwaka 2012/2013 kukarabati eneo hilo. Wizara inashirikiana na Hazina kuharakisha upatikanaji wa fedha hizo ili kuimarisha barabara katika eneo hilo na kurahisisha usafirishaji wa mitambo mikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kuanzisha viwanda vya kemikali na mbolea kwa kutumia gesi asili ya Mtwara, makampuni matatu kati ya 10 yaliyojitokeza yalichaguliwa katika awamu ya kwanza ili baadaye yachujwe kupata mwekezaji mahiri. Makampuni hayo ni *Deepak Fertilizer and Petrochemical Ltd* ya India; *TATA Chemicals Ltd* ya India na *Polyserve Group Ltd* ya Misri.

Hata hivyo, hatua ya kushindanisha makampuni matatu haikufikiwa kufuatia makubaliano kati ya Kampuni ya *Wentworth Resources Limited (WRL)* na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania *(TPDC)* ya kuanzisha kiwanda cha mbolea kwa kutumia gesi asili. Tayari upembuzi yakinifu na uchimbaji wa visima zaidi vya gesi ili kupata malighafi ya kutosha ya kuzalisha mbolea aina ya Urea na kemikali ya *Methanol* kwa matumizi ya viwanda umefanyika. Kutokana na tatizo kubwa la umeme nchini, kipaumbele cha kutumia gesi asili ya *Mnazi Bay* kimeelekezwa kwenye uzalishaji wa umeme na hivyo kuleta changamoto ya uanzishaji wa viwanda vya *Urea* na kemikali ya *Methanol*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Minjingu Mines and Fertilizer Ltd (MMFL)* inayozalisha mbolea aina ya *Minjingu Rock Phosphate (MRP*), ilifanya upanuzi wa kiwanda na sasa kina uwezo wa kuzalisha tani 100,000 za *MRP* kwa mwaka ikilinganishwa na tani 75,000 za awali. Kufuatia kuboreshwa kwa mbolea ya *MRP* kwa kuongezwa virutubisho vya *sulphur* na *micro nutrients* za zinc *(Zn), boron (B), magnesium (Mg)* na kuongeza wingi wa *nitrogen (N)* hadi kufikia asilimia 10 na Serikali kutoa ruzuku kwa mbolea ya Minjingu - Mazao, mahitaji yameongezeka. Mbolea ya *MRP* iliyoboreshwa (Minjingu - Mazao) ina ubora sawa na *NPK*.

Hivyo, *MMFL* wana mpango wa kupanua uwezo wa uzalishaji hadi tani 600,000 kwa mwaka. Kwa upande mwingine, Kampuni ya *Paradeep Phosphate Ltd* kutoka India imekwishaleta maombi ya kuwekeza katika utengenezaji wa mbolea katika Kanda ya Kusini. Kiwanda hicho kinatarajia kuzalisha tani 750,000 za mbolea kwa mwaka na kitagharimu Dola za Marekani Shilingi bilioni 1.5 na kuajiri watu 3,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vilivyobinafsishwa chini ya Sekta ya Viwanda na Biashara ni 74 na kati yake ni viwanda 17 tu ndivyo havifanyi kazi. Juhudi za kufufua viwanda hivyo zinafanyika chini ya *Consolidated Holding Corporation (CHC)* iliyoko chini ya Wizara ya Fedha, kwa kuzingatia utaratibu wa urekebishaji wa mashirika ya umma. Hivi sasa, majadiliano yanaendelea kwa kushirikiana na wadau mbalimbali na wamiliki wa viwanda hivyo ili kukubaliana jinsi ya kuvifufua. Ni matarajio ya Wizara kuwa zoezi linaloendelea litakamilika haraka iwezekanavyo ili ufufuaji wa viwanda hivyo uanze. Kama inavyoonekana, ni viwanda vichache (17) havifanyi kazi lakini wakati huo huo miradi mipya iliyopata leseni ya kuanzisha viwanda ni takribani 542 katika kipindi cha mwaka 2005 hadi 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine linahusu kuboresha vivutio kwa ajili ya uwekezaji kwenye viwanda vitakavyotumia malighafi mbalimbali zilizopo nchini vikiwemo viwanda vya nguo, ngozi, usindikaji matunda, mbogamboga na usanifu wa madini ya vito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika jitihada za kukuza uwekezaji kwenye viwanda vya kuongeza thamani katika mazao, madini ya vito na Ngozi, Wizara imeendelea kushirikiana kwa karibu na Wizara ya Fedha ili kutoa vivutio mbalimbali kwa wawekezaji. Vivutio hivyo ni pamoja na misamaha ya kodi kwa wawekezaji wanaozalisha bidhaa na kuuza nje kupitia mfumo wa *EPZ*, kuandaa maeneo na kuyawekea miundombinu ya msingi kama maji, umeme na barabara kama ilivyofanyika katika eneo la uwekezaji la Mheshimiwa Benjamin Wiliam Mkapa na kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kupunguza muda wa kusajili makampuni yanayowekeza katika maeneo ya *EPZ*, muda wa kutoa leseni na muda wa kufungua na kufunga biashara katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya *EPZ* imeendelea kubainisha maeneo ya uwekezaji ya *EPZ* na *SEZ* na kuhamasisha uwekezaji ndani ya maeneo hayo. Kwa mwaka 2012/2013, makampuni 29 yamepewa leseni za

kujenga viwanda chini ya *EPZA* na tayari makampuni matano yamekwishaanza uzalishaji. Makampuni hayo yatawekeza mtaji wa jumla ya Dola za Marekani milioni 113 na kuajiri watu 9,254. Idadi hiyo itafanya jumla ya makampuni yanayozalisha chini ya *EPZ* kufikia 70, jumla ya mtaji uliowekezwa kufikia Dola za Marekani bilioni moja na jumla ya ajira za moja kwa moja kufikia 23,000.

Vilevile, ujenzi wa miundombinu ya maji machafu katika Eneo Maalum la Uwekezaji la *Benjamin William Mkapa Special Economic Zones (BWM-SEZ)* umekamilika ambapo viwanja 18 katika eneo hilo vimetolewa kwa wawekezaji. Maeneo mapya ya *SEZ* na *EPZ* yanayoendelea kujengwa na sekta binafsi kwa mwaka 2012/2013 ni *Rusumo Falls SEZ* (Kagera) na *Kamal EPZ Industrial Park,* Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuimarisha Sekta ya Ngozi kwa kutekeleza Mkakati wa Kufufua na Kuendeleza Sekta na Viwanda vya Ngozi Nchini. Kutokana na jitihada hizo, Sekta Ndogo ya Usindikaji wa Ngozi imeongeza viwanda kutoka vitatu vya awali hadi viwanda nane mwaka 2012/2013 vyenye uwezo uliosimikwa *(installed capacity)* wa kusindika vipande vya ngozi milioni 12.4 kwa mwaka kufikia hatua ya awali *(Wetblue).* Kati ya hivyo, vipande vya ngozi za ng'ombe ni milioni 1.7 na vya mbuzi na kondoo ni milioni 10.7.

Hata hivyo, matumizi halisi ya uwezo *(capacity utilisation)* kwa mwaka 2012 ni wastani wa vipande milioni 6.6 vya ngozi vikijumuisha vipande 936,000 vya ngozi za ng'ombe na milioni 5.7 vya ngozi ya mbuzi na kondoo. Usindikaji umewezesha ongezeko la thamani ya ngozi zilizouzwa nje ya nchi kutoka Shilingi bilioni 10.6 mwaka 2011 hadi Shilingi bilioni 62.3 mwaka 2012. Vilevile, sekta hiyo imewezesha kuongezeka kwa ajira kutoka watu 1,500 mwaka 2011 hadi 2,000 mwaka 2012. Wizara kwa kushirikiana na *LAT* imewawezesha wadau wapatao 38 kushiriki Maonesho ya Saba Saba *(Dar es Salaam International Trade Fair)* na wadau 18 kushiriki Maonesho ya Nane Nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012/2013, Serikali iliongeza ushuru kwa ngozi ghafi zinazouzwa nje kutoka asilimia 40 hadi asilimia 90 au Sh. 400/= hadi Sh. 900/= kwa kilo kulingana na ni ipi kubwa. Matokeo ya hatua hiyo ni ongezeko la usindikaji wa ngozi ghafi ndani ya nchi kutoka vipande vya ngozi za ng'ombe 166,773 kati ya Januari na Juni, 2012 hadi vipande 343,860 kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2012. Usindikaji wa ngozi za mbuzi na kondoo nao uliongezeka kutoka vipande 778,023 hadi vipande 1,173,875 kwa vipindi hivyo. Hilo ni ongezeko la vipande 177,087 vya ng'ombe, sawa na asilimia 106.18 na vipande 395,852 vya mbuzi na kondoo sawa na asilimia 50.88. Thamani ya mauzo nje ya ngozi zilizosindikwa yalifikia jumla ya Shilingi bilioni 50.85 (ngozi za ng'ombe Shilingi bilioni 32.25 na ngozi za mbuzi na kondoo Shilingi bilioni 18.6) katika kipindi cha Julai, 2012 hadi Februari, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mipya ya viwanda vya ngozi inayoendelea kujengwa ni pamoja na *MERU TANNERY LIMITED* yenye uwezo wa kusindika ngozi za ng'ombe vipande 156,000 kwa mwaka na vipande vya ngozi za mbuzi 468,000 kwa mwaka. Kwa sasa ujenzi wa majengo umekamilika, usimikaji wa *drums* zipatazo 10 unaendelea na uzalishaji unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2013. Kiwanda kitaajiri wafanyakazi 30 kwa kuanzia.

Mradi mwingine ni Kiwanda cha *Xinghua Investment Co. Ltd*, kinachojengwa Mkoani Shinyanga. Kiwanda hicho ni kikubwa chenye uwezo wa kusindika ngozi za ng'ombe vipande 936,000 kwa mwaka na ngozi za mbuzi na kondoo vipande milioni 2.2 kwa mwaka. Kiwanda hicho kinaendelea na ujenzi wa majengo na usimikaji wa *drums* kubwa zipatazo 38. Ujenzi unatarajiwa kukamilika na kuanza usindikaji mwezi Agosti, 2013. Usindikaji wa ngozi utafanyika hadi hatua ya *mwisho (finished leather)* na kitaajiri wafanyakazi 500. Viwanda hivyo vikikamilika na kuanza uzalishaji kuna uhakika wa kusindika ngozi zote zinazozalishwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo

na Uvuvi na Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu, Dodoma *(Capital Development Authority-CDA)* imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari takriban 110 kwa lengo la kuanzisha na kuendeleza Vijiji vya Viwanda *(Industrial Villages).* Maeneo hayo ni maalum kwa ajili ya kuchochea na kuvutia wawekezaji katika viwanda vya bidhaa za ngozi nchini. Tayari kazi za kupima, kuweka mipaka na kuandaa michoro/ ramani ya eneo husika imefanyika na hati miliki imepatikana. Manispaa ya Singida nayo imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari 120 katika Kata ya Ng'aida kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza Kijiji cha Viwanda vya kusindika ngozi na kutengeneza bidhaa za ngozi. Upimaji wa eneo na uidhinishaji wa mchoro wa eneo husika unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau kikiwepo Kituo cha Uwekezaji nchini *(TIC)* na Mamlaka ya *EPZ* imeendelea kuandaa taarifa mbalimbali ikiwa ni pamoja na machapisho, majarida na *business profiles* pamoja na matangazo kwenye vyombo vya habari kuhusu fursa za uwekezaji katika miradi ya viwanda kwa lengo la kuhamasisha na kuvutia uwekezaji nchini. Kutokana na juhudi hizo, kwa kipindi cha Julai, 2012 hadi Machi, 2013, Kituo cha Uwekezaji nchini kilisajili jumla ya miradi ya viwanda 157 na Mamlaka ya *EPZ* ilisajili jumla ya miradi 29 na kufanya jumla ya miradi iliyosajiliwa katika Sekta ya Viwanda kuwa 186.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo na kuendeleza Programu ya Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini kwa Kutoa Ushauri, Mafunzo, Mitaji na Huduma za Kiufundi kwa Wajasiriamali, Wizara imeendelea kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Programu ya Muunganisho wa Ujasiriamali Vijijini (MUVI) inayotekelezwa kwa kuzingatia mlolongo wa thamani kwa mazao ya alizeti, mihogo, mifugo, matunda na nyanya ili kuongeza vipato vya wakulima na kupunguza umasikini. Programu hiyo inatekelezwa katika Mikoa sita ikijumuisha Wilaya 19 ambazo ni Iringa Vijijini na Kilolo, Mkoa wa Iringa; Simanjiro, Hanang na Babati, Mkoa wa Manyara; Bagamoyo, Rufiji na Mkuranga, Mkoa wa Pwani; Songea Vijijini, Namtumbo na Mbinga, Mkoa wa Ruvuma;

Sengerema, Kwimba na Ukerewe, Mkoa wa Mwanza; Muheza, Korogwe, Kilindi na Handeni, Mkoa wa Tanga; na Wilaya ya Njombe ambayo kwa sasa iko Mkoa mpya wa Njombe.

Katika mwaka 2012/2013, vyama na vikundi vya wazalishaji na wakulima 54 vimewezeshwa kuanzisha vikundi mama vya ujasiriamali. Pia, programu imewezesha upatikanaji wa pembejeo hasa mbegu za alizeti (tani 4900) na vipande milioni 2.2 vya mbegu za muhogo. Vilevile, programu imeanzisha mashamba darasa; vitalu vya miche ya maembe, michungwa na milimao yenye jumla ya miche 220,000. Shamba la majaribio ya malisho ya mifugo ekari sita limeanzishwa, wafugaji 48 wamewezeshwa kufanya safari ya mafunzo ya mbinu za kisasa za kufuga, kuchinja na kutunza malisho na mazingira. Majukwaa ya kuratibu shughuli za sekta za mazao matano yaliyochaguliwa katika ngazi ya Mkoa na Wilaya yaliendelea kukutana na kujadili mambo mbalimbali ya kuendeleza mazao husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa MUVI umewaongezea tija walengwa hususan katika uzalishaji wa mbegu bora za alizeti aina ya *RECOD* iliyobuniwa na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Mbegu hiyo imewawezesha wasindikaji kukamua lita 20 za mafuta ya alizeti kutoka katika kila kilo 50 za mbegu bora ukilinganisha na kilo 80 mpaka 90 za mbegu za zamani. Wakulima wa Hanang' wamebuni mradi wa kutengeneza mkaa wa kupikia kutokana na makapi ya mbegu za alizeti. Katika Mkoa wa Iringa tija imeongezeka kwa wakulima wa nyanya na sasa wameweza kupata kwa wastani Shilingi milioni 15 kwa ekari ya mbegu bora ya nyanya ikilinganishwa na chini ya Shilingi milioni 10 hapo awali. Vilevile, tija imeongezeka kwa wakulima wa mbegu mpya ya muhogo kutoka Mkoa wa Mwanza na sasa shina moja linatoa hadi kilo 10 za muhogo ikilinganishwa na mbegu asilia inayotoa hadi kilo nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza mchango wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo *(SMEs)* katika Pato la Taifa kutoka asilimia 33 ya *GDP* hivi sasa kufikia asilimia 40

mwaka 2015; Kama nilivyoeleza katika hotuba yangu ya mwaka 2012/2013, ilibainika kuwa mchango halisi wa sekta katika Pato la Taifa ni asilimia 27.9 badala ya makadirio ya awali ya asilimia 33. Wizara imeendelea kusimamia maendeleo ya Sekta hiyo na kuhakikisha uchangiaji wake unaongezeka kwa kuhamasisha uanzishaji wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo na kuimarisha ukuaji wa viwanda vidogo vilivyopo kupitia mikakati na programu mbalimbali ikiwemo *ODOP* na *MUVI*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya teknolojia mpya 159 zimepatikana kutoka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya matumizi ya miradi ya uzalishaji katika kipindi cha mwaka 2012/2013. *SIDO* kupitia vituo vyake vya uendelezaji wa teknolojia vilivyopo Mbeya, Arusha, Kilimanjaro, Lindi, Kigoma na Shinyanga iliwezesha utengenezaji na usambazaji kwa watumiaji mashine mpya 462 za kuongeza thamani mazao na bidhaa pamoja na vipuri 2,631.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutoa elimu na kuwajengea uwezo wakulima wa kusindika mazao kabla ya kuyauza kama vile usindikaji wa asali, utengenezaji wa mvinyo, utengenezaji wa juisi pamoja na ufungashaji wa bidhaa kwa kutumia teknolojia ya *TBS*; Wizara kwa kushirikiana na *SIDO* imekuwa ikitoa mafunzo mbalimbali kwa Wajasiriamali ili kuwaimarisha katika kuendesha na kuendeleza shughuli za biashara na miradi ya uzalishaji. Mafunzo yaliyotolewa ni pamoja na usindikaji wa nafaka na matunda kwa wajasiriamali 857 na usindikaji wa ngozi na bidhaa zake kwa wajasiriamali 1,431. Mafunzo ya ujuzi maalum pia yalitolewa kuhusu usindikaji wa mafuta ya alizeti, utengenezaji sabuni, mishumaa, chaki, utengenezaji wa mizinga ya kisasa ya usindikaji wa asali.

Vilevile, jumla ya wajasiriamali 8,382 kupitia kozi 408 wamepata mafunzo ya maarifa na stadi za kuimarisha shughuli zao za uzalishaji mali. Wizara imeendelea kuongeza mtaji wa Mfuko wa Wafanyabiashara Wananchi *(NEDF)* ili kuwawezesha wajasiriamali wadogo kupata mikopo ya kuwawezesha kuwekeza katika miradi ya kuongeza thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *SIDO*, imewaunganisha wazalishaji wadogo na makampuni makubwa na ya kati kwa nia ya kuwawezesha kupata teknolojia, ujuzi na masoko. Wajasiriamali 134 wameunganishwa na makampuni mbalimbali kwa ajili ya kuwauzia bidhaa na huduma zao.

Baadhi ya viwanda hivyo ni vya kusindika mafuta ya kupikia, bidhaa za plastiki, kuchambua pamba, saruji, bia na soda na wameunganishwa na *supermarkets* katika Mikoa ya Mbeya, Iringa, Tanga, Arusha, Dar es Salaam, Morogoro, Mwanza, Shinyanga, Singida na Manyara. Hatua hiyo imewasaidia wajasiriamali wadogo kuzalisha bidhaa zenye ubora na kukuza biashara na vipato vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuijengea uwezo kwa kuwaongezea bajeti na kuwawezesha watumishi wake kupata mafunzo mbalimbali. Katika mwaka 2012/2013, *SIDO* ilitengewa Shilingi bilioni 7.664 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 6.420 zilizotengwa mwaka 2011/2012.

Wizara pia imeiwezesha *SIDO* kupeleka watumishi 157 katika mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Jitihada nyingine ni kuendelea kuongezea mtaji Mfuko wa Wafanyabiashara Wananchi *(National Entrepreneurship Development Fund - NEDF)* na kushawishi wadau wa maendeleo kutekeleza programu zao kupitia *SIDO*, kwa mfano, programu ya *MUVI* na Usindikaji wa Mazao inayofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Korea *(KOICA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya wajasiriamali 3,567 nchini kote walipewa mikopo ya thamani ya Shilingi bilioni 3.47 kupitia Mfuko wa *NEDF* kwa ajili ya kuendeshea miradi ya uzalishaji na biashara. Kati ya mikopo hiyo, asilimia 33 ilitolewa kwa miradi ya vijijini na asilimia 51 ilitolewa kwa wanawake. Mfuko huo umetoa ajira kwa watu 7,192 wengi wao wakiwa ni wanawake sawa na asilimia 52 na umechochea ongezeko na ukuaji wa jasiriamali ndogo ambazo zimechangia kupanua wigo wa kukusanya kodi na mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara kwa kupitia *SIDO* imehamasisha wananchi kushiriki katika ujenzi wa kongano *(industrial clusters)* na ilitenga Shilingi milioni 500 katika bajeti yake ili kuanza ujenzi wa kongano katika Mikoa ya Dodoma, Kilimanjaro, Manyara, Morogoro na Singida.

Hadi mwisho wa mwezi Desemba, 2012, Shilingi milioni 80 zilikuwa zimetolewa kwa ajili ya ujenzi huo na zimewezesha kuanza ujenzi kwa hatua za awali katika Mikoa ya Dodoma na Singida. Wizara inaendelea kushirikiana na wadau wengine wakiwemo Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi katika kutenga na kuendeleza maeneo kwa ajili ya viwanda vidogo na biashara ndogo. Jumla ya maeneo 142 yametengwa na Halmashauri za Wilaya mbalimbali hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuhamasisha matumizi ya fursa za masoko ya ndani, kikanda na kimataifa zikiwemo fursa za Masoko ya *AGOA, EBA*, China, Japan, Canada na India ili kukuza biashara ya nje kwa kiwango kikubwa; katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara ilihamasisha jumuiya ya wafanyabiashara kuhusu fursa za masoko ya bidhaa na huduma zilizopatikana kupitia majadiliano ya kibiashara baina ya nchi na nchi, kikanda na kimataifa kwa kutoa taarifa hizo kwa wafanyabiashara kupitia taasisi zao. Taarifa za fursa hizo zimekuwa zikitolewa kwa njia ya mikutano ya ana kwa ana, redio, magazeti, vipeperushi, maonesho ya biashara, semina na warsha za kikanda. Matokeo yake, mauzo ya bidhaa kwenye masoko hayo ya upendeleo yamekuwa yakiongezeka kila mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauzo ya bidhaa katika Soko la Ulaya yalishuka kutoka Dola za Marekani milioni 1,382.0 mwaka 2011, na kufikia Dola za Marekani milioni 744.2 mwaka 2012. Thamani ya mauzo ya bidhaa kwenye Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika yalikuwa Dola za Marekani milioni 1,430.1 kwa mwaka 2012 ikilinganishwa na Dola za Marekani 1,158.9 mwaka 2011, hivyo kuwa na urari chanya wa Dola za Marekani 327.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania katika soko la nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki yalikuwa Dola za Marekani milioni 613.3 kwa mwaka 2012, ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 352.4 mwaka 2011, ambapo manunuzi ya bidhaa ni Dola za Marekani milioni 678.6 na kusababisha urari hasi wa biashara wa Dola za Marekani milioni 65.3. Kushuka kwa mauzo yetu kwenye Soko la *EAC* kulichangiwa na baadhi ya changamoto ikiwemo tatizo la ushindani usio wa haki ambapo baadhi ya nchi wanachama huingiza malighafi bila ushuru *(Uganda list).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu imetoa mafunzo ya mbinu mbalimbali za kuwajengea uwezo wajasiriamali ili waweze kuyafikia masoko ya nje kwa njia ya warsha na semina. Mafunzo kuhusu utayari wa biashara na mauzo ya nje *(Training for Trade and Export Readiness)* yaliyoendeshwa na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TanTrade)* kwa kushirikiana na *SIDO* na *TBS* yalitolewa kwa wajasiriamali 55 katika Mikoa ya Arusha na Dar es Salaam. Mafunzo hayo yalilenga kuwawezesha wajasiriamali kujua masharti na mahitaji ya soko hususan viwango vya ubora wa kimataifa ili kuziwezesha bidhaa kuhimili ushindani. Mafunzo mengine yalihusu namna ya kutoa taarifa kwa Shirika la Biashara la Dunia *(WTO)* juu ya mabadiliko ya sheria au hatua mbalimbali zinazochukuliwa na nchi wanachama kuhusu Sheria na Kanuni za *WTO* ili kuleta uwazi *(transparency)* katika biashara. Wadau 50 kutoka Wizara na Taasisi za Serikali walishiriki mafunzo hayo huko Bagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Uchumi kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Ulaya, nchi wanachama wa *EAC* ikiwemo Tanzania zimeendelea kunufaika na Soko la *EU* kwa kuuza bidhaa zake bila kutozwa ushuru wala kuwekewa ukomo. Vilevile, *EU* imekubali jedwali la miradi ya maendeleo *(EAC Development Matrix)* liwe sehemu ya Mkataba wa *EPA* na kuonesha nia ya kuifadhili miradi husika kwa kushirikiana na nchi wanachama wa *EAC*. Majadiliano hayo bado yanaendelea katika maeneo ya Sura ya Uasili wa Bidhaa *(Rules of Origin),* Muundo wa Kitaasisi na Utatuzi wa Migogoro,

Ruzuku katika Kilimo, Kodi kwa Mauzo ya Nje *(Export Taxes)* na suala la kutoa Upendeleo kwa Mataifa *(Most Favoured Nations – MFN).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusainiwa Itifaki ya Soko la Pamoja mwezi Novemba, 2009 na kuzinduliwa mwezi Julai, 2010, nchi wanachama zimeendelea kurazinisha sera zao ili kwenda sambamba na matakwa ya Itifaki ya Soko la Pamoja. Hatua ya Soko la Pamoja inategemewa kuongeza zaidi fursa za masoko ya biashara ya huduma, soko la mitaji, uhuru wa watu kuingia nchi wanachama na kuanzisha shughuli za kiuchumi na uhuru wa kufanya kazi popote katika nchi wanachama. Kwa kutambua fursa zitokanazo na Soko la Pamoja, Wizara kwa kushirikiana na *TCCIA, CTI, TPSF, VIBINDO* na *TAFOPA* imeendelea kuwahamasisha wafanyabiashara kuzichangamkia fursa hizo kwa lengo la kuongeza kipato na hatimaye kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kutekeleza Itifaki ya Biashara ya Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika ikiwa ni pamoja na kuendelea na majadiliano kwa lengo la kuondoa vikwazo vya kibiashara visivyokuwa vya kiushuru na ujenzi wa Vituo vya Pamoja Mipakani *(OSBP)* ili kurahisisha biashara kati ya nchi na nchi. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kufikiwa kwa punguzo la ushuru wa bidhaa mwezi Desemba, 2012 ambapo sasa bidhaa zote ziingiazo miongoni mwa nchi wanachama hazitozwi ushuru. Vilevile, nchi wanachama zimefanikiwa kukamilisha Itifaki ya Biashara ya Huduma ambayo inatoa mwanga kwa nchi wanachama kuanza kulegezeana masharti katika biashara ya huduma baada ya kukamilika kwa uondoaji ushuru wa bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara imefanya utafiti juu ya gharama za kufanya biashara nchini uliobainisha kuwepo vikwazo vya biashara visivyo vya kiushuru kati ya Tanzania na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kupendekeza njia za kuviondoa. Katika kushughulikia vikwazo hivyo, Wizara imeendelea kushiriki

vikao vya Kamati ya Kitaifa na ile ya Kikanda vyenye lengo la kupokea taarifa, kufuatilia na kuondoa vikwazo hivyo. Wizara yangu ilifanikiwa kusaini Mkataba wa Ushirikiano na Rwanda mwezi Oktoba, 2012 wenye lengo la kuondoleana vikwazo vya biashara visivyokuwa vya kiushuru na kukuza biashara kupitia mipakani *(Cross Border Trade).* Kupitia majadiliano hayo, wafanyabiashara wa Tanzania wameanza kufaidika kwa kuuza bidhaa zao Rwanda baada ya kuondolewa kwa vikwazo hivyo. Vilevile, kupitia majadiliano hayo Tanzania na Kenya mwezi Machi, 2013 zilisaini Hati ya Makubaliano *(Memorundum of Understanding)* yaliyowezesha Kenya kuondoa kikwazo kilichokuwa kinazuia bidhaa za maua kutoka Tanzania kuingia Kenya wakati wa kusafirishwa kwenda Ulaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia TanTrade ina mpango wa kuanzisha vituo vya biashara vya kanda katika Mikoa ya Arusha, Mbeya na Mwanza. *TanTrade* tayari imefanikiwa kupata jengo la kupanga *NSSF*, Mwanza kwa ajili ya kituo cha biashara Kanda ya Ziwa na taratibu zinafanyika ili kupata fedha za kulipia kodi ya pango na kupata kibali cha kuajiri watumishi kwa ajili ya Ofisi hiyo mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuhamasisha ushiriki wa wajasiriamali katika maonesho ya biashara kimataifa ndani na nje ya nchi, Wizara kupitia *TanTrade* iliendelea kuwawezesha wajasiriamali kushiriki katika Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam *(DITF)* kwa kuwatengea maeneo; kuwapa mafunzo ya ujasiriamali, mbinu za kibiashara, ufungashaji, mawasiliano; na mbinu za kupenya na kuyafikia masoko ya kimataifa. Wizara imekuwa ikiwawezesha kwa kuwatengea na kugharimia maeneo ya maonesho wajasiriamali wa Sekta ya Ngozi na Bidhaa za Ngozi kushiriki katika Maonesho ya *DITF*.

Kufuatia juhudi hizo, katika Maonesho ya *DITF* ya 36 ya mwaka 2012, washiriki wa ndani walikuwa 1,341 sawa na ongezeko la asilimia 4.41 ikilinganishwa na washiriki 900 wa mwaka 2011. Vilevile, Wizara kupitia *TanTrade* imeratibu ushiriki

wa wajasiriamali katika Maonesho ya Kimataifa ya Rwanda *(Rwanda International Trade Fair - RITF)* 2012 na ya Kimataifa ya Nairobi *(Nairobi International Trade Fair - NITF)* 2012 ambapo jumla ya wajasiriamali nane walishiriki Maonesho ya *RITF* na 23 ya *NITF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea na utafiti wa masoko kwa kufuatilia mienendo ya bei ya mazao makuu ya chakula na biashara, na bidhaa za viwandani kwa lengo la kupanua wigo wa mahitaji na kuwapatia wazalishaji bei nzuri zaidi. Bei ya mkulima kwa mazao makuu ya biashara yakiwemo kahawa aina ya arabica, chai, pamba, mkonge na korosho iliongezeka kwa viwango tofauti. Bei ya mlaji kwa mazao makuu ya chakula hususan mahindi, mchele, ngano, ulezi, mtama, maharage, uwele na sukari ziliongezeka katika msimu wa 2012/2013 ikilinganishwa na bei za msimu wa 2011/2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika imefanya utafiti kuwezesha kupata soko la tumbaku ya Tanzania nchini China na Uturuki. Wafanyabiashara kutoka China wameonesha nia ya kununua tumbaku hiyo. Wizara inafanya pia juhudi za kuwezesha tumbaku ya Tanzania kuingizwa katika orodha ya bidhaa zinazoruhusiwa kuuzwa nchini China bila ushuru na ukomo *(duty free quota free)* kupitia Mkataba Maalum wa Upendeleo *(Special Preferential Tariff Agreement).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania (*TIRDO*) na Sekta Binafsi kwa kuhusisha kikamilifu vyama vya wenye viwanda na wafanyabiashara wa Tanzania Bara na Visiwani kama vile *TPSF, CTI, TCCIA, ZNCCA, TAHA, TWCC, Tea Association of Tanzania* na *Cashewnuts Processors Association* imewezesha kuendeleza matumizi ya mfumo wa utambulisho wa kitaifa kwa bidhaa kwa kutumia Nembo za Mistari *(bar codes),* kupitia kampuni ya *GS1 (Tz) National* iliyoanza kazi rasmi Agosti, 2011. Matumizi ya mfumo huo umewezesha bidhaa za Tanzania kupenya kwa urahisi zaidi katika soko la ndani na Kimataifa. Hadi kufikia Machi, 2013, jumla ya

wazalishaji 370 wamesajiliwa na kutumia huduma hiyo na bidhaa 6,200 zimepata alama ya *GS1*. Baadhi ya viwanda vinavyotumia mfumo huo ni Kampuni ya Chai ya Kagera *(Kagera Tea Company), TBL, Konyagi Tz Ltd na SBC Company Ltd.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Sekta ya Kilimo, Sekta Binafsi, Washirika wa Maendeleo, Asasi zisizo za Kiserikali na Taasisi za Elimu ya Juu imekamilisha Mkakati wa Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo ili kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo. Waraka wa Baraza la Mawaziri kutoa taarifa ya utekelezaji wa Mkakati wa Sera ya Masoko ya Mazao na Bidhaa za Kilimo umeandaliwa na taratibu za kuridhiwa na Baraza la Mawaziri zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendeleza miundombinu ya masoko ya Mikoa na kuanzisha masoko katika vituo vya mipakani ili kukuza biashara ya ndani na kikanda, Wizara kwa kupitia Mradi *wa District Agricultural Sector Investment Project (DASIP)* inaendelea na maandalizi ya kujenga masoko saba ya mipakani katika maeneo ya Mtukula - Missenyi, Kabanga – Ngara; Nkwenda na Murongo – Karagwe; Mnanila – Buhigwe/Kasulu; Remagwe –Tarime na Busoka - Kahama. *DASIP* imeingia mikataba na Washauri Waelekezi wa kuandaa michoro na kusimamia ujenzi kwa masoko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje na Mpango Unganishi wa Biashara; Programu ya Kuendeleza Sekta ya Biashara *(Trade Sector Development Programme - TSDP)* iliandaliwa na kuwasilishwa kwa Washirika wa Maendeleo *(Development Partners - DPs)* ili kupata fedha za kuitekeleza. Majadiliano na nchi ya Sweden kupitia Shirika lake la Maendeleo ya Kimataifa *(SIDA)* ambao wameonesha nia ya kugharimia eneo la kurazinisha sheria, kanuni na taratibu za usimamizi wa viwango vya mazao ya chakula na mifugo *(Sanitary and Phytosanitary-SPS-standards)* yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuendeleza biashara ya ndani ikiwa ni pamoja na kujenga dhana ya kutumia bidhaa zilizozalishwa Tanzania (Nunua Bidhaa za Tanzania); kutokana na Serikali kutambua umuhimu wa kukuza, kuendeleza na kulinda viwanda vya ndani, kuanzia Septemba, 2012, Serikali ilifanya maamuzi kupitia Waraka wa Utumishi Na. 1 wa Mwaka 2012 kuwa Ofisi za Serikali na Taasisi zake zitanunua samani zilizotengenezwa na viwanda vya ndani kwa kutumia malighafi za hapa nchini.

Sambamba na hilo, Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi kupitia majukwaa mbalimbali kupenda na kununua bidhaa zinazotengenezwa na viwanda vya ndani kwa kutumia kaulimbiu ya 'Nunua Bidhaa za Tanzania Jenga Tanzania'. Kaulimbiu hiyo inakwenda sambamba na uboreshaji na ufungashaji wa bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali hapa nchini ambapo Wizara kupitia *TBS* imetoa mafunzo ya ubora wa bidhaa na ufungashaji kwa wajasiriamali wadogo 292 katika Mikoa ya Manyara, Mtwara, Singida na Tanga. Vilevile, sampuli za bidhaa 359 za Tanzania zilipimwa katika maabara za *TBS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kuendelea kupanua wigo wa biashara mtandao, Wizara imefanikisha mfumo wa utoaji wa taarifa zinazohusu masuala ya viwanda na biashara kwa wadau kwa wakati, katika ngazi za Wilaya, Mkoa na Taifa. Vilevile, Wizara inazingatia matumizi ya TEKNOHAMA katika kupokea, kutunza na kusambaza taarifa mbalimbali zinazohusu Sekta. Wizara inatumia mtandao wa intaneti na teknolojia ya simu za viganjani kusambaza taarifa za bei ya mazao ya kilimo na mifugo. Kwa upande wa mifugo, taarifa za bei hupatikana pia kupitia tovuti: *www.lmistz.net.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013, Wizara imeboresha Tovuti yake *(www.mit.go.tz)* ili kuongeza ufanisi katika mawasiliano na utoaji taarifa kwa njia ya mtandao. Wizara pia inaratibu uanzishwaji wa Tovuti ya Biashara ya Kitaifa - *National Business Portal* kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma (PO -

PSM) na Wakala ya Serikali Mtandao *(e-Goverment Agency - EGA).* Zoezi la kufanya upembuzi yakinifu limeanza kwa kumtumia Mtaalam Mwelekezi ambaye ameanza kazi mwezi Februari, 2013 na anatarajiwa kukamilisha kazi hiyo mwishoni mwa mwezi Mei, 2013. Kazi ya uundaji wa *National Business Portal* itaanza baada ya kukamilika kwa upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itashughulika na suala la kupanua matumizi ya simu za viganjani katika kutoa taarifa za bei ya mazao na masoko kwa wakati; aidha, kuangalia uwezekano wa kuanzisha mbao za matangazo katika ngazi ya Wilaya na Mkoa ili kutoa taarifa mbalimbali ikiwemo bei na masoko kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara katika kipindi cha mwaka 2012/2013, imekamilisha Mkakati na Mfumo Mpana na Unganishi wa Taarifa za Masoko nchini *(IMIS)* kwa kuwatumia wataalam waelekezi kutoka kampuni ya *Data Works Associates*. Mfumo huo unalenga kuimarisha mifumo iliyopo ya ukusanyaji na usambazaji wa taarifa za masoko. Hatua inayofuata ni kuufanyia majaribio mfumo huo na kuandaa Mwongozo wa Mtumiaji na Mwendeshaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha usambazaji wa taarifa za masoko nchini hasa maeneo ya vijijini, Wizara kwa kushirikiana na *SIDO* kupitia MUVI iliendesha mafunzo kwa wakusanya taarifa za masoko kutoka Mikoa yote pamoja na Wilaya 19 zinazotekeleza Mradi wa *MUVI*. Wanahabari kutoka katika vituo vya redio za kijamii *(Community Radios)* nane walishiriki. Aidha, Wizara kupitia kampuni ya Nuru *Infocom,* ilitoa mafunzo juu ya utumiaji wa simu za viganjani katika ukusanyaji wa taarifa za masoko kwa washiriki 80 yaliyofanyika mwezi Septemba, 2012.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotamka katika hotuba yangu ya mwaka 2012/2013, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TanTrade)* imeanzishwa na ilizinduliwa rasmi tarehe 1 Julai, 2011. Mamlaka hiyo inaendelea na utekelezaji wa majukumu yake ambayo ni pamoja na kuendeleza biashara ya ndani na ya nje. Mamlaka pia,

imefungua Ofisi yake huko Zanzibar na inategemea kufungua matawi huko Arusha, Mbeya na Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Bodi ya Stakabadhi ya Mazao Ghalani imetoa leseni za biashara kwa maghala 44 na waendesha maghala 21. Makampuni mawili ya ukaguzi wa maghala yamepewa leseni kwa ajili ya ukaguzi wa maghala yanayohifadhi mazao. Mfumo wa Stakabadhi za Maghala umeendelea kupanuka na unatekelezwa katika Mikoa ya Dodoma (mahindi); Kilimanjaro (mahindi, mpunga na kahawa); Lindi (korosho); Manyara (mahindi, mbaazi na pamba); Mbeya (mpunga); Morogoro (mpunga na mahindi); Mtwara (korosho); Pwani (korosho); Ruvuma (korosho); na Tanga (mahindi).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi imeendelea kutoa elimu ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani kwa wadau kwa kutumia semina, matangazo katika redio na luninga, vipeperushi na Mikutano ya ana kwa ana. Mafunzo maalum yametolewa kwa Watendaji Wakuu wa Maghala yanayosajiliwa katika mazao ya korosho, mahindi na kahawa.

Vilevile, kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Kwimba, Magu na Misungwi na Taasisi za Fedha, Bodi imepanga kuendesha mafunzo kwa wakulima ili waweze kuuza mpunga kwa kutumia mfumo wa stakabadhi katika msimu wa 2013/2014. Bodi itahamasisha matumizi ya mfumo wa stakabadhi katika Mikoa ya Katavi na Sumbawanga kwa mazao ya mahindi, mpunga, alizeti na ufuta. Tathmini ya awali ya ukaguzi wa maghala na kuangalia utayari wa wakulima imekwishafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi kwa kupitia Mradi wa *African Green Revolution Alliance (AGRA)* imeandaa mfumo wa kusajili, kutoa taarifa na udhibiti wa kumbukumbu za kiutendaji zinazohitajika kwa kila mwendesha ghala. Pamoja na hilo, Bodi inaratibu uanzishwaji wa *Electronic Warehouse Receipt System* ambao utawezesha kukusanya taarifa ikiwa ni pamoja na kuandaa daftari la kumbukumbu za wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendeleza Miundombinu ya Masoko ya Mikoa na Kuanzisha Masoko Mpakani kama vile Karagwe, Kigoma, Holili, Horohoro, Namanga, Sumbawanga, Taveta na Tarakea. Uendelezaji wa miundombinu ya masoko ya Mikoa na kuanzisha masoko ya mipakani ni kama nilivyoeleza kwa kina katika aya ya 65.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi ilianzisha Jukwaa la Wadau wa Masoko ya Mazao ya Kilimo *(National Marketing Development Forum-NMDF)* kwa lengo la kuwakutanisha wadau wa masoko ya mazao ya kilimo. Katika mwaka huu wa fedha, Wadau walifanya mkutano wa nne wa jukwaa kujadili masuala ya maendeleo ya masoko, uendeshaji, uratibu na ugharamiaji wa jukwaa hilo. Taasisi ambazo Wizara inashirikiana nazo katika kuendeleza jukwaa ni pamoja na Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania (MVIWATA), *Rural Livelihood Development Company (RLDC), Tanzania Horticulture Association (TAHA), Horticultural Development Council of Tanzania (HODECT), Agricultural Council of Tanzania (ACT), Tanzania Agricultural Market Development Trust (TAGMARK),* Bodi za Mazao na Vyama vya Ushirika.

Mafanikio ya ushirikiano huo ni pamoja na ushirikishwaji wa wadau katika kuandaliwa kwa Mkakati wa Kuendeleza Mazao ya Bustani *(Horticulture Development Strategy),* maandalizi ya Mkakati wa Masoko ya Mazao, maandalizi ya Mkakati wa Mfumo Mpana na Unganishi wa Taarifa za Masoko na mapitio ya utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha udhibiti wa bidhaa duni *(substandard goods)* kutoka nje ya nchi, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania imeendelea kuimarisha ukaguzi wa ubora wa bidhaa zinazoingia Tanzania kupitia mipaka yake. Shirika limefungua Ofisi tano katika vituo vya mipakani vya Horohoro, Sirari, Holili, Namanga na Bandari ya Tanga. Kwa sasa, tathmini inafanyika kwa ajili ya kufungua Ofisi katika vituo vya Mtambaswala, Mtukula, Rusumo na Tunduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mapitio ya utekelezaji wa mpango wa mwaka 2012/2013, Sekta ya Viwanda iliendelea na Utekelezaji wa Mkakati Unganishi wa Uendelezaji Viwanda Nchini kwa kuendeleza Uhamasishaji wa Uwekezaji na kutoa Kipaumbele kwa Viwanda Vinavyoongeza thamani ya Mazao ya Kilimo. Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati Unganishi wa Kuendeleza Viwanda Nchini *(IIDS)* ikilenga maeneo ya kipaumbele ya usindikaji wa mazao ya kilimo kama vile matunda, mbegu za mafuta, bidhaa za ngozi, madini, mbolea, kemikali, mashine na mitambo ya viwanda.

Wizara na Taasisi zake imeendelea kutoa msukumo mkubwa kwa kutekeleza miradi ya chuma cha Liganga na Maganga Matitu au Kasi Mpya; kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma na Ngaka Kusini; kuzalisha umeme kwa kutumia upepo wa Singida; kuzalisha viuadudu wa kuua viluwiluwi vya mbu waenezao malaria; uwekezaji katika miradi mikubwa ya Maeneo ya Uzalishaji kwa Mauzo Nje *(EPZ)* na Maeneo Maalum ya Kiuchumi *(SEZ);* miradi ya ushirikiano na *UNIDO* na *JICA* na utekelezaji wa Mikakati ya Kuendeleza Sekta Ndogo za Ngozi na Viwanda vya Ngozi, Nguo na Mavazi. Kufuatia juhudi hizo, jumla ya miradi ya viwanda 186 ilisajiliwa kwa kipindi cha mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara iliendelea kuhamasisha uanzishaji wa viwanda katika maeneo mbalimbali nchini hususan Kanda ya Kusini kwa sababu ya kuwa na gesi asili inayohitajika kwa matumizi ya viwanda. Viwanda hivyo ni pamoja na cha saruji cha *Dangote Cement Co. Ltd* kitakachokuwa na uwezo wa kuzalisha tani milioni tatu kwa mwaka na kuajiri jumla ya wafanyakazi 5,000.

Kiwanda hicho kitajengwa katika eneo la Mtwara Mikindani. Tayari vifaa vya awali vya ujenzi wa kiwanda hicho vimewasili Mtwara. Kiwanda kingine cha saruji katika Kanda ya Kusini ni cha *Lee Construction Materials Company Limited* (tani 300,000), Kilwa Masoko – Lindi ambacho tayari ujenzi umekamilika na *MEIS Cement Company*, Lindi ambacho ujenzi umekamilika na mitambo kusimikwa.

Miradi mingine ya viwanda vya saruji ambayo iko katika hatua mbalimbali za ujenzi ni pamoja na *Dar es Salaam Cement Company (DCC), Mbagala - Dar es Salaam; Lake Cement Company (LCC)* tani 500,000, Kimbiji - Kigamboni Dar es Salaam; *Fortune Cement Company*, Vikindu – Mkuranga - Pwani; *Athi River Cement Company,* (tani 1,500,000) Tanga; *Rhino Cement Company,* Mkuranga - Pwani chenye uwezo wa uzalishaji wa (tani 750,000) kwa mwaka na *Kisarawe Cement Company*, Kisarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kufuatilia Miradi ya *TANCOAL*, kasi mpya na umeme wa upepo (Mkoani Singida) inayoendeshwa kwa ubia kati ya Serikali kupitia *NDC* na Sekta Binafsi, kazi ya uchorongaji ili kubaini wingi na ubora wa mashapo ya chuma cha Maganga Matitu na makaa ya mawe ya Katewaka imekamilika. Taarifa ya awali inaonesha kuwepo kwa tani milioni 49.22 za chuma na tani milioni 34 za makaa ya mawe. Mradi una lengo la kuzalisha tani 330,000 za chuma ghafi *(sponge iron)* kuanzia mwishoni mwa mwaka 2014 na utazalisha tani 250,000 za chuma cha pua *(steel)* kwa mwaka. Madini ya chuma yaliyohakikiwa yanatosha kuzalisha chuma ghafi kwa muda wa miaka 78. Pia, mradi huo utazalisha umeme kiasi cha megawati 25 utakaotokana na teknolojia itakayotumika ya *Direct Reduction of Iron Ore (DRI).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha uandaaji wa Mpango Kabambe *(Master Plan)* wa Kutekeleza Mkakati Unganishi wa Kuendeleza Viwanda *(Integrated Industrial Developement Strategy - IIDS).* Mpango huo umebainisha miradi takriban 50 ya kutekeleza. Wizara itachapisha mpango huo na kuusambaza kwa wadau kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza vema mkakati wa Kuendeleza Sekta Ndogo ya Nguo na Mavazi kwa Kushirikiana na Sekta Binafsi, Wizara imeanzisha Kitengo cha Kuendeleza Sekta ya Nguo na Mavazi *(Textile Development Unit –TDU),* chenye lengo la kutatua changamoto mbalimbali zinazokabili viwanda vya nguo zikiwemo huduma za umeme,

bandari na ushuru. Kitengo hicho kimetembelea viwanda vyote vya nguo nchini na kufanya mikutano na wadau ili kutambua changamoto zinazoikabili sekta hiyo. Baadhi ya mafanikio yaliyoanza kuonekana ni kama yafuatayo:-

(a) Uhusiano kati ya wenye viwanda vikubwa na vidogo vya sekta ndogo ya nguo na mavazi nchini umeboreshwa. Hivi sasa wafumaji nguo wadogo wanaotumia *hand looms* wanaweza kupata malighafi (nyuzi) kirahisi kupitia makubaliano ambayo yamefanyika kati yao na viwanda vya *21st Century, Afritex* na *Mwatex* hali ambayo haikuwa rahisi hapo awali;

(b) Kuboresha utendaji wa viwanda kwa kushughulikia ujuzi wa kiufundi wa wafanyakazi na wasimamizi. Kiwanda cha *Mwatex* kimekubali kutumika kama kituo cha kutolea mafunzo ya ujuzi wa ufumaji *(weaving).* Utaratibu wa kuleta wataalam wakufunzi 30 kutoka nje ya nchi kuja kufundisha waendesha mitambo unaendelea;

(c) Kushauri na kuhamasisha wamiliki wa viwanda vya nguo nchini kuwekeza katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali *(product diversification)* na kuondokana na uzalishaji wa khanga na kitenge pekee. Tayari viwanda vya *Mwatex* na Karibu *Textile Mill* vimeonesha nia ya kuwekeza katika kupanua wigo wa bidhaa za nguo wanazozalisha; na

(d) Kitengo kimeunganisha viwanda ambapo kwa sasa wakuu wa viwanda wanakutana kila baada ya miezi mitatu na wameweza kuwaunganisha na vyombo vya fedha ili kuweza kupata mitaji mfano *Hero Textiles* ya Dar es Salaam na *Mbeya Knitwear Ltd.* Viwanda vya nguo nchini vimeweza kuongea kwa sauti moja matatizo yao hususan ya uingizaji nguo kutoka nje na masuala ya ukwepaji kodi. Vilevile, Kitengo kwa kushirikiana na *VETA* kinaandaa mpango wa mafunzo ya kuongeza ujuzi kwenye sekta ya nguo hasa upande wa mavazi ili kuondoa tatizo linalowafanya

wawekezaji wasite kuwekeza katika viwanda vya mavazi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea na uhamasishaji wa uanzishwaji wa viwanda vipya hasa katika Sekta Ndogo za Nguo na Mavazi, Ngozi na Viwanda vya Kusindika Mazao ya Kilimo. Wizara kwa kushirikiana na wadau ikiwemo Kituo cha Uwekezaji nchini *(TIC), BRELA* na Mamlaka ya *EPZ*, imesajili miradi mipya 186 na imeendelea kuhamasisha na kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Viwanda na Biashara. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Kituo cha Uwekezaji Nchini kilisajili jumla ya miradi ya viwanda 157, kati yake miradi miwili ni ya kuzalisha nguo na minne ya kusindika ngozi. Aidha, Mamlaka ya *EPZ* ilisajili miradi mbalimbali 29, kati yake miradi minne ni ya kuzalisha nguo na mavazi na saba ya kusindika mazao ya kilimo na mifugo. Hii inafanya jumla ya miradi ya nguo na ngozi kuwa 17, ya kuzalisha nguo ikiwa sita na usindikaji ngozi/bidhaa za ngozi 11.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kuendeleza Viwanda *(UNIDO)* inaendelea kutekeleza mradi wa kujenga uwezo wa wafanyakazi wake na wadau wakuu wa kuandaa na kuchambua sera ya viwanda na zinazohusiana ambapo mafunzo yamekuwa yanatolewa.

Kufuatia mafunzo hayo, Ripoti ya Hali ya Ushindani wa Sekta ya Viwanda nchini *(Tanzania Industrial Competitive Report)* 2012 iliandaliwa na kuzinduliwa tarehe 20 Novemba, 2012 wakati wa maadhimisho ya Siku ya Viwanda Afrika *(Africa Industrialization Day - AID).* Ripoti hiyo inatoa mapendekezo ya kuhakikisha kuwa Sekta ya Viwanda nchini inachukua nafasi yake ya kuendeleza uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *UNIDO* iliendelea kutekeleza Mradi wa *African Agribusiness and Agro-processing Development Initiative (3ADI).* Mradi huo unalenga uongezaji thamani katika mlolongo wa thamani kwa mazao ya korosho, nyama na ngozi. Kwa upande wa zao la korosho, mradi unahusisha vikundi vinane vya

wajasiriamali wadogo *(SMEs),* wengi wao wakiwa vijana na wanawake na viwanda vikubwa viwili. Mambo yaliyofanyika na kukamilika ni pamoja na kuandaa kabrasha la mafunzo *(cashewnut technical training manuals);* kufanya mafunzo, kuboresha mashine za kubangua korosho zinazotengenezwa nchini; kuhamasisha matumizi ya maeneo ya Kongano *(clusters)* ambapo vikundi vitatu kati ya vinane vya wajasiriamali wadogo vimehamia katika Kongano la *SIDO* Mtwara; na kununua mashine za kubangua korosho kwa Kikundi cha Kitama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa zao la nyama, kazi zilizofanyika ni pamoja na ripoti ya mlolongo wa thamani; usanifu wa nyumba za machinjio *(slaughter houses)* kwa miji ya Mbeya na Iringa; usanifu na ununuzi wa vifaa vya ujenzi wa mahali/meza za kuchinjia *(slaughter slabs)* kwa Mbeya na Iringa Vijijini; ununuzi wa vifaa kama kompyuta kwa Bodi ya Nyama pamoja na uandaaji wa ripoti ya fursa za malisho na mahusiano na wachinjaji. Vilevile, kwa upande wa ngozi, kazi zilizofanyika ni pamoja na ripoti ya mlolongo wa thamani wa zao la ngozi; uendeshaji wa mafunzo ya ubora; uandaaji wa *patterns* na kozi ya kutengeneza *patterns*; na ushauri wa uboreshaji wa Chuo cha Taaluma ya Ngozi cha Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *UNIDO* iliendelea kutekeleza Mradi wa *Industrial Upgrading and Modernisation*. Mafunzo kwa wakufunzi Watanzania ili waweze kutoa mafunzo kwa wanaviwanda na uchambuzi *(diagnostic analysis)* wa kubainisha matatizo ya Sekta ya Usindikaji Maziwa umekamilika kwa viwanda vitano na uchambuzi kuhusu usindikaji wa mafuta ya alizeti kwa viwanda vitano umeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Japan kupitia Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA)* inatekeleza Mradi wa Kaizen kwa ajili ya kutoa mafunzo yenye lengo la kuongeza tija, ufanisi, usimamizi wa shughuli za viwanda na kuongeza ubora wa bidhaa. Awamu ya majaribio ilikwishafanyika kwa kutoa mafunzo kwa

wajasiriamali 113 wenye viwanda vya nguo na mavazi waliopo Mkoa wa Dar es Salaam. Makubaliano kati ya Wizara na *JICA* ya kutekeleza mradi wa Kaizen yalisainiwa mwezi Oktoba, 2012 na mradi umeanza kutekelezwa mwezi Aprili, 2013. Sekta zitakazofaidika na mradi huo ni pamoja na viwanda vya usindikaji mazao ya kilimo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kushiriki katika Kuandaa Mpango Kazi wa Sera ya Viwanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na mapitio ya sera ya viwanda katika *SADC* na kufanya maboresho kulingana na mahitaji ya nchi yetu; Wizara imeshiriki ipasavyo katika kukamilisha Mpango Kazi wa Kutekeleza Sera ya Uendelezaji Viwanda kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Uhamasishaji *(sensitisation)* wa Mpango Kazi husika unaendelea sambamba na uhamasishaji Sera ya Maendeleo ya Viwanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili wadau waweze kuelewa na kuwa tayari kutekeleza.

Rasimu ya Sera ya Maendeleo ya Viwanda kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)* imekamilika na kupitishwa na Baraza la Mawaziri wa Biashara wa *SADC (CMT)* mwezi Novemba, 2012. Rasimu hiyo itawasilishwa katika Mkutano wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa *SADC* unaotarajiwa kufanyika mwezi Agosti, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kufuatilia uboreshaji wa utendaji wa Kiwanda cha Nguo cha Urafiki *(FTC)*na malimbikizo makubwa ya madeni. Hata hivyo, hali ya sasa ya uzalishaji imeimarika kutokana na juhudi zinazofanywa na uongozi wa kiwanda ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka mita milioni 2.05 mwaka 2011 hadi mita milioni sita mwezi Aprili, 2013. Ajira imeongezeka kutoka wafanyakazi 656 mwaka 2011 hadi 800 mwezi Aprili, 2013. kutokana na kiwanda kuwa na mitambo ya kizamani (1960s). Juhudi za pamoja zinafanywa ili kiwanda kiweze kupata mitambo ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekamilisha uandaaji wa Rasimu ya Sheria ya Biashara ya Chuma Chakavu baada ya kujadiliwa katika ngazi ya Makatibu Wakuu *(IMTC).* Muswada wa kutunga sheria hiyo unafanyiwa maboresho ili kuwasilishwa Baraza la Mawaziri kwa maamuzi na hatimaye Kamati ya Sheria na Katiba ili kuwasilishwa rasmi Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kuhusu kupitia na kutathimini utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo na kutoa mapendekezo kwa madhumuni ya kuhuisha; katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara ilifanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo katika eneo la watoa huduma kwa Sekta ili kubainisha aina za huduma zinazotolewa na Wizara na Taasisi za Umma, Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi. Zoezi hilo limekwishafanyika katika Mikoa ya Dar-es-Salaam, Iringa, Morogoro, Ruvuma, Tanga, Mtwara, Mwanza, Arusha, Dodoma na Mbeya na kufikia jumla ya Taasisi 150. Matokeo ya awali yanaonesha kuwa wengi wa wajasiriamali wadogo wamenufaika na huduma hizo kote mijini na vijijini ingawa watoa huduma za teknolojia bado ni wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara kwa kushirikiana na *UNWOMEN* ilifanya tathmini ya ushiriki wa wanawake wajasiriamali waishio mipakani katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki pamoja na changamoto zinazowakabili.

Tathmini hiyo ilibaini kuwa ushiriki wa wajasiriamali husika ni hafifu na changamoto kuu ni pamoja na uelewa mdogo kuhusu masuala ya Itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Uasili wa Bidhaa *(Rules Of Origin),* biashara zao kutokuwa rasmi na kuwa na uelewa mdogo wa sheria na taratibu za forodha. Wadau hao wamekubaliana kuanzisha mitandao ya wanawake wajasiriamali wa mipakani ili kuwa na sauti moja kuhusu masuala yanayohusu biashara zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *TanTrade* imeunda vikundi vya akina mama na kuanzisha madawati ya jinsia katika vituo vya mipakani vya Mutukula, Kabanga, Namanga, Rusumo na Sirari. Wizara kupitia *Tanzania Women Chambers of Commerce -TWCC* imewezesha uandaaji na ushiriki wa Mtandao wa Wafanyabiashara Wanawake wa Afrika Mashariki katika Mkutano uliofanyika Dar es Salaam, mwezi Novemba, 2012 uliolenga kupanua wigo wa masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa na wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga uwezo wa kutoa huduma za ugani katika maeneo walioko wajasiriamali hasa vijijini, Wizara kwa kushirikiana na wataalam kutoka *SIDO, BRELA, TCCIA, GS1* na *TBS*, imeendesha mafunzo yaliyolenga kuboresha bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali ili ziweze kushindana katika soko la ndani na nje hasa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na *SADC*. Mafunzo hayo yalijumuisha Wajasiriamali kutoka Mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Lindi, Shinyanga, Mara, Kagera, Geita, Simiyu, Kigoma, Iringa, Rukwa, Mtwara na Mwanza. Warsha hizo ziliwezesha kuandaa mipango ya biashara vizuri na kuitekeleza, kutengeneza bidhaa bora, utengenezaji na utunzaji wa mitambo na ujasiriamali. Jumla ya Wajasiriamali 125 na Maafisa Biashara 16 walifaidika. Warsha hizo zimewezesha wajasiriamali kuanza kutumia nembo za ubora na kuweza kuuza bidhaa zao kwenye *'Supermarkets'*. Wizara kupitia *SIDO* iliweza kutoa huduma za ugani kwa wajasiriamali 9,660 nchini kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuhamasisha Manispaa na Halmashauri za Wilaya na Miji kutenga maeneo na sekta binafsi kushiriki kujenga miundombinu hasa majengo ya uzalishaji kwa ajili ya uongezaji thamani mazao ya kilimo ndani ya maeneo yaliyotengwa. Wizara imehamasisha Watendaji wa Halmashauri za Manispaa, Kata na Vijiji umuhimu wa utengaji wa maeneo ya kufanyia kazi wajasiriamali wadogo katika eneo la Bahi, Korogwe, Kongwa, Dodoma Mjini, Muheza, Mpwapwa, Tanga Mjini na Handeni. Kutokana na jitahada

hizo, Halmashauri ya Mpwapwa imetenga eneo la kongano la karanga na Kongwa imetenga kongano la zabibu. Vilevile, Mkoa wa Tanga umetenga eneo la Mwahoka barabara ya Pangani eneo ambalo linatarajiwa kutumika na wajasiriamali kati ya 800 na 2000, eneo la Majani Mapana kwa ajili ya maduka 41 ya kuuza unga na mashine 8 za kusindika na eneo la Manundu limetenga hekta 50 kwa ajili ya uwekezaji wa Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Jitihada hizo zitaendelezwa katika mikoa mingine nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwawezesha Wajasiriamali kushiriki katika maonesho ya ndani na nje ya nchi, Wizara imeendelea kuratibu ushiriki katika maonesho ya bidhaa za wajasiriamali yaliyoandaliwa na *SIDO*. Maonesho hayo yalifanyika katika Kanda ya Kusini (Lindi), Kanda ya Ziwa (Mwanza) na Kanda ya Pwani (Morogoro). Wajasiriamali 252 walipata fursa ya kutangaza bidhaa zao kama vile vyakula vilivyosindikwa, sabuni, bidhaa za uhunzi, ngozi, nguo, chumvi, mashine na zana za kazi. Pamoja na kutangaza bidhaa, washiriki wameweza kuboresha bidhaa zao kutokana na mafunzo waliyoyapata na maoni mbalimbali ya wateja na wageni wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeratibu maonesho ya Mwezi wa Mwanamke Mjasiriamali *(Month of Woman Enterprenuer-MOWE)* yaliyofanyika katika viwanja vya Mnazi Mmoja mwezi Novemba, 2012. Maonesho hayo yalishirikisha wanawake wapatao 200 kutoka Mikoa yote ya Tanzania. Wizara ilitumia fursa hiyo kutoa mafunzo kwa washiriki kuhusu kuboresha biashara wanazozifanya kwa kutumia taasisi za *SIDO, FCC, BRELA, TBS, TCCIA* na *GS1*. Mafunzo hayo pia yaliwezesha washiriki kusajili biashara zao, kuanza michakato ya kupata viwango vya ubora na kupata nembo za utambuzi wa bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kujenga uwezo wa uzalishaji wa zana za kilimo, Wizara kupitia *SIDO* imeimarisha Vituo vya Kuendeleza Teknolojia *(Technology Development Centers – TDCs)* vilivyopo Arusha, Iringa, Kigoma, Kilimanjaro,

Lindi, Mbeya na Shinyanga ili viweze kuzalisha zana za kilimo. Mashine za kusindika mazao ya kilimo kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kuongeza thamani ya mazao ya muhogo na alizeti zilizalishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kupanua wigo wa masoko ya upendeleo kwa bidhaa zetu, mwaka 2012/2013, Wizara imeendelea kufanya majadiliano ya kibiashara na nchi za China, Japan, Malaysia, Indonesia, Korea Kusini, Uturuki, India, Czechoslovakia, Urusi, Falme za Kiarabu, Marekani, Mexico, Costarica, Ujerumani, Umoja wa Ulaya, Pakistani, Finland, Nigeria, Sudan, Sudani ya Kusini na Oman. Pia Wizara imeendelea kushiriki majadiliano ya kibiashara ya Kikanda na Kimataifa na hasa yale ya *EAC, SADC, AU, COMESA-EAC-SADC,* Ubia wa Uchumi na kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Ulaya *(EAC EU- EPA)* na yale ya Shirika la Biashara la Dunia *(WTO)* kupitia Duru la Doha *(Doha Round).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio yaliyopatikana kutokana na majadiliano hayo ni pamoja na Tanzania kusaini makubaliano ya ushirikiano wa biashara na uchumi na Uturuki yenye lengo la kukuza biashara na uwekezaji. Kupitia makubaliano hayo, tayari mwezi Desemba, 2012, Uturuki ilizindua safari za ndege kupitia Uwanja wa Ndege wa Kilimajaro, hatua ambayo imesaidia kurahisisha biashara kwa wauzaji wa maua na mboga mboga nje na hivyo kupunguza adha na gharama ya kusafirisha mizigo yao kupitia uwanja wa ndege wa Nairobi kabla ya kusafirisha kwenda nje. Makubaliano hayo pia yamesaidia kukuza Sekta ya Utalii na kuanzishwa kwa Kituo cha Wafanyabiashara kati ya Uturuki na Tanzania kiitwacho *ABITAT*, ambacho kilizinduliwa na Mheshimiwa Rais mwezi Aprili, 2013. Vilevile, China imeweza kuongeza fursa za masoko ya bidhaa za Tanzania kuingia soko la China kutoka asilimia 60 hadi 95 bila kutozwa ushuru kwa bidhaa za kilimo, uvuvi, mifugo, madini na bidhaa za viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwezi Februari, 2013, Tanzania ilisaini Mkataba wa ushirikiano wa Biashara na

Uchumi na Oman. Makubaliano hayo yanalenga kukuza ushirikiano katika Sekta za Kilimo, Ufugaji, Uvuvi, na Usafiri wa Anga. Zaidi ya makampuni 30 yameonesha nia ya kuja kuwekeza Tanzania. Majadiliano kati ya taasisi za Oman na Tanzania kuhusu namna ya kuanzisha ushirikiano kupitia sekta husika yanaendelea. Pia, majadiliano ya biashara baina ya nchi na nchi yamewezesha Korea Kusini kufungua Kituo cha Biashara jijini Dar es Salaam ili kusaidia uratibu na kupatikana taarifa za biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imefanyia mapitio Sheria ya *Anti Dumping* na *Counterveiling Measures Act, 2004* kwa nia ya kuihuisha ili kuendana na mfumo wa *WTO* kuhusu masuala ya *dumping* kwa kujumuisha wadau wote muhimu Tanzania Bara na Visiwani. Rasimu ya Mapitio ya Sheria iko tayari na Rasimu ya Waraka wa *BLM* kuhusu mapendekezo ya Marekebisho ya Sheria ya *Anti Dumping* na *Counterveiling Measures Act, 2004* imeandaliwa tayari kupelekwa *Cabinet Secretariat*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Septemba, 2012, Tanzania imeongezewa muda wa Mpango wa *AGOA* hadi mwaka 2015, ili kuzisaidia nchi za Afrika zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara ikiwemo Tanzania kuendelea kufaidika na fursa za Soko la Marekani kwa bidhaa za nguo na mavazi bila kulipa ushuru na bila kuwepo kwa ukomo *(Duty Free Quota Free Market Access).* Tanzania na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zinaendelea na majadiliano na Serikali ya Marekani yenye lengo la kuanzisha mkataba wa Ushirikiano wa Biashara na Uwekezaji *(Partnership for Trade and Investment Agreement-PATIA)* ili kukaribisha wawekezaji kutoka Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2012/2013, vituo vya Biashara vya Tanzania vya London na Dubai vimeendelea kuvutia wawekezaji wa nje ili kuwekeza Tanzania. Vilevile, Vituo vimetafuta masoko kwa ajili ya bidhaa za Tanzania katika masoko ya Ulaya na Umoja wa Falme za Kiarabu *(UAE).* Kituo cha Dubai kimewezesha wajasiriamali watano kushiriki kwenye maonesho ya Global Village ambapo jumla ya Shilingi

milioni 150 zilipatikana kutokana na mauzo ya bidhaa za sanaa za mikono, majani ya chai na kahawa. Kituo hicho vilevile kimewezesha Kampuni za Tanzania kuuza mbao aina ya mitiki *(Teak),* dhahabu, Tanzanite, mashudu, karafuu na nyama ya mbuzi katika soko la UAE vyenye thamani ya zaidi ya Shilingi bilioni 100. Pia, Kituo kilisambaza jumla ya machapisho 5,000 kutoka vituo vya utalii kama *TANAPA*, Ngorongoro, *TTB*, na Kamisheni ya Utalii Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia mafanikio yaliyopatikana kutokana na Vituo vya London na Dubai, Wizara imeanza maandalizi ya awali ikiwa ni pamoja na kutenga fedha za kuanzisha vituo vingine katika bajeti yake ya mwaka 2013/2014. Vituo hivyo vinategemewa kuanzishwa China, Ubelgiji, Afrika Kusini na Marekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *WTO* iliendesha mafunzo kuhusu uandaaji wa kutoa taarifa *(notifications)* kwa Maafisa 22 kutoka Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali. Warsha hiyo ilifanyika mwezi Novemba, 2012 huko Bagamoyo, Pwani. Lengo la warsha hiyo lilikuwa ni kujenga uwezo na uelewa wa jinsi ya kuandaa *notifications* kwa Wizara na Taasisi ambazo zinawajibika kutoa taarifa hizo *(enquiry points).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majadiliano ya kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara la Utatu *(Tripartite Free Trade Area - FTA)* linalojumuisha Kanda za *COMESA, EAC* na *SADC* lenye nchi zipatazo 26 na soko lenye wakazi wanaokadiriwa kufikia milioni 750 yalianza rasmi Septemba, 2012. Majadiliano hayo yamejikita katika maeneo ya Mtangamano wa Biashara *(Market Integration);* Maendeleo ya Miundombinu *(Infrastructure Development)* na Maendeleo ya Viwanda *(Industrial Development).*

Makubaliano yamefikiwa katika tafsiri ya Kanuni na taratibu za kuendesha mikutano ya majadiliano, mpango kazi, ratiba ya mikutano na majadiliano ya kibiashara. Vikundi Kazi vimeundwa katika maeneo ya Vigezo vya Uasili wa Bidhaa *(Rules of Origin);* Ushirikiano wa Forodha *(Customs*

*Cooperation, Documentation, Procedures and Transit related issues);* Vikwazo vya Kiufundi vya Biashara *(Technical Barriers to Trade),* Usalama wa Afya ya Binadamu, Mimea na Wanyama *(Sanitary and Phytosanitary Measures-SPS);* Vikwazo Visivyokuwa vya Kiushuru *(Non Tariff Barriers);* na Ulegezaji wa Viwango vya Ushuru *(Tariff Liberalization).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeshiriki kwenye majadiliano ya uanzishwaji wa Itifaki ya Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC Monetary Union).* Hadi sasa jumla ya vifungu sabini na saba (77) vimejadiliwa. Maeneo ambayo hayajafikiwa muafaka na yenye mvutano ni pamoja na *Macro economic Convergence Framework na Legal and Institutional Framework* ambayo yanahitaji mwongozo kutoka Baraza la Kisekta la Mawaziri wanaosimamia majadiliano ya Itifaki ya Uanzishwaji wa Umoja wa Fedha. Majadiliano kuhusu Mpango Kazi *(Road Map)* juu ya mchakato wa Uanzishwaji wa Itifaki ya Umoja wa Fedha yamekamilika. Utekelezaji wa Itifaki ya Umoja wa Fedha utaanza rasmi mara baada ya miaka kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeratibu vikao vya Kamati ya Kitaifa inayoshughulikia masuala ya Vikwazo vya Biashara Visivyo vya Ushuru kwa kuendelea kufuatilia, utoaji taarifa na mikakati ya kuondoa vikwazo vya biashara visivyokuwa vya kiushuru, *(NTBs).* Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Masuala ya Afya za Binadamu, Wanyama na Mimea *(National SPS Commitee)* ilikutana tarehe 4 Desemba, 2012 na kukubaliana kuwa na mkakati wa kuimarisha uzalishaji wa nyama ya kuku usimamiwe na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi ili sekta hiyo iweze kuhimili ushindani. Kamati za kikanda zimekuwa zikikutana na kupeana taarifa juu ya hali ya vikwazo visivyokuwa vya kiushuru na kupendekeza hatua za kuviondoa.

Baadhi ya vikwazo hivyo ambavyo vilikuwa vinalalamikiwa na wafanyabiashara ni pamoja na tozo ya Dola za Marekani 200 kwa kila gari la biashara lililokuwa linaingia Tanzania, kuongeza masaa ya kazi kuwa 24 katika vituo vya bandarini na Namanga, kuwa na Kituo Kimoja cha

Kukagua Mizigo *(One Stop Centre)* katika Bandari ya Dar es Salaam na hivyo kupunguza gharama za kufanya biashara na msongamano bandarini baada ya kujenga vituo vya bandari ya nchi kavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea na Majadiliano ya Kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa *SADC* na Kulegeza Masharti katika Sekta ya Biashara ya Huduma. Wizara imeshiriki katika majadiliano ya uanzishwaji wa Umoja wa Forodha wa Nchi za *SADC*.

Majadiliano hayo yanafanyika kulingana na mapendekezo ya tafiti mbalimbali zilizofanyika kuhusu muundo bora unaofaa wa Umoja wa Forodha wa *SADC*. Tafiti hizo zilifanyika katika maeneo manne. Maeneo hayo ni wigo wa pamoja wa kukusanya ushuru *(Common External Tariff-CET);* Ukusanyaji wa mapato; namna ya kugawana mapato na mfuko wa fidia *(Revenue Collection, Distribution, Sharing and Compensatory Fund).* Sheria na muundo utakaotumika katika utekelezaji wa Umoja wa Forodha unaotarajiwa *(Legal Administration and Institutional Framework);* na Urazinishaji wa Sera za Biashara *(Harmonization of Trade Policies).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara vilevile imeshiriki katika majadiliano ya kulegeza masharti ya Biashara ya Huduma katika sekta ndogo sita za kipaumbele ambazo ni Fedha, Uchukuzi, Utalii, Mawasiliano, Ujenzi na Nishati. Ili kutekeleza kazi hiyo, Wizara imeunda kikosi kazi cha kitaifa kuratibu majadiliano ya masuala ya biashara ya huduma. Kikosi kazi hicho kinaundwa na wataalam kutoka Wizara saba, Idara za Serikali kumi na Asasi Binafsi nne na kufanya jumla ya wajumbe wa kikosi kazi kuwa ishirini na moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003 inafanyiwa mapitio ili kuendana na mabadiliko mbalimbali yaliyojitokeza katika kipindi cha miaka tisa tangu ilipotungwa. Maoni ya wadau kupitia warsha za kikanda kwa nchi nzima ikiwemo Zanzibar yamekusanywa. Mkakati wa Kisera *(Trade Strategy Development Paper - TSDP)*

unaandaliwa ili kuwezesha kutayarisha andiko la kisekta *(Sectoral Papers)* na hivyo kuandaa rasimu ya Sera ya Taifa ya Biashara ambayo itazingatia maoni ya wadau likiwemo suala la jinsia katika utekelezaji wa Sera hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kuratibu na kukamilisha marejeo ya Sera ya Taifa ya Biashara kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania. Zoezi hilo lilifanyika chini ya Shirika la Biashara la Dunia *(WTO)* mwezi Novemba, 2012 huko Geneva Uswisi. Lengo la marejeo hayo ni pamoja na kutoa taarifa kwa wanachama wa *WTO* na wadau wa ndani na nje wakiwemo wawekezaji kuhusu Sera za Biashara na Mazingira ya Uchumi kwa ujumla katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Sekta ya Kilimo imeandaa mwongozo na kutoa elimu katika Halmashauri zote nchini kuhusu dhana ya mnyororo wa thamani, ambapo masuala ya miundombinu ya masoko yamezingatiwa kama kigezo muhimu katika kuendeleza mfumo wa masoko ya mazao wenye ufanisi. Kwa kuzingatia mwongozo huo, Halmashauri za Wilaya kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya *(DADPs)* huibua mahitaji ya miundombinu ya masoko husika kama vile masoko, maghala, minada ya mifugo, miundombinu ya usindikaji kama mashine, barabara za vijijini na *cold rooms*, na kuandaa mipango ya utekelezaji kupitia *DADPs.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara, imeanza zoezi la Ufuatiliaji na Tathmini *(M & E)* wa miundombinu ya masoko katika Wilaya zote ili kubaini hali halisi ya miundombinu na kutathmini mahitaji ya miundombinu hiyo kwa kila Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kushirikiana na Halmashauri za Kasulu, Nanyumbu na Songea Kuendeleza Masoko katika Mipaka ya Kilelema, Mtambaswala, Daraja la Mkenda mtawalia; ujenzi wa masoko katika vituo vya mipakani vya Mtambaswala Wilayani Nanyumbu, Mkenda *Bridge* Wilayani Songea Vijijini na Nyamgali Wilaya ya Kasulu/

Buhigwe unaendelea chini ya usimamizi wa Halmashauri za Wilaya hizo. Ujenzi wa masoko hayo chini ya ufadhili wa Mradi wa *TASP* unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni 2013. Kwa Wilaya ya Kasulu, awali soko lilitarajiwa kujengwa katika eneo la Kilelema lakini Halmashauri husika ilibadilisha eneo la mradi kwa kuwa soko la Kilelema litajengwa kupitia utaratibu mwingine unaoihusisha Benki ya Maendeleo ya *TIB*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza nia ya Serikali ya kufanikisha ujenzi wa Masoko ya Segera na Makambako, Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Mikoa ya Tanga na Njombe na Halmashauri za Wilaya za Handeni na Njombe imekamilisha maandalizi ya awali ambayo ni pamoja na upembuzi yakinifu, maandalizi ya Mpango Kabambe *(Master Plan),* utengaji wa maeneo ya kutosha, tathmini ya athari za kimazingira *(Environment Impact Assessment)* kupitia Baraza la Taifa la Mazingira *(NEMC)* na utoaji wa elimu kwa umma. Wizara imewakutanisha wahusika wa Mikoa ya Tanga na Njombe na Benki ya Maendeleo ya *TIB* ili kufanikisha ujenzi wa masoko hayo. Benki imetembelea maeneo husika na kufanya majadiliano na Uongozi wa Mikoa hiyo. Taratibu za kupata hati miliki za maeneo yaliyotengwa zinaendelea. Hii ni pamoja na Halmashauri kulipa fidia kwa wale waliopisha ujenzi wa masoko hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara inaendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta katika uanzishwaji wa Vituo vya Pamoja vya Mipakani *(OSBP).* Vituo vya Pamoja vinajengwa katika mipaka ifuatayo; Tanzania na Kenya (Holili/Taveta), Tanzania na Uganda (Mutukula), na Tanzania na Burundi (Kabanga/Kobero). Hadi sasa ujenzi wa kituo cha Kobero umekamilika wakati ujenzi wa *OSBP* kwa upande wa Kabanga bado haujaanza, hivyo maofisa wa Tanzania watahamia upande wa Kobero nchini Burundi mpaka pale ujenzi wa kituo kwa upande wa Tanzania utakapokamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa *OSBP* ya mpaka wa Mutukula kwa upande wa Tanzania umekamilika kwa

asilimia 85. Ujenzi wa *OSBP* ya Holili/Taveta kwa upande wa Tanzania umefikia asilimia 95 wakati kwa upande wa Kenya wapo katika hatua za awali za ujenzi wa *OSBP* ya Taveta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada za kupunguza gharama za biashara na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya umma na binafsi imeanzisha Kamati za Pamoja Mipakani *(Joint Border Committees – JBCs* katika vituo saba vya mipakani: Mtukula, Namanga, Kabanga, Rusumo, Sirari, Kasumulo, na Tunduma. Kamati za Pamoja Mpakani *(JBC)* ni Kamati zilizoanzishwa kwa lengo la kuziwezesha Taasisi za Udhibiti mipakani kufanya kazi kwa pamoja kwa lengo la kupunguza gharama za kufanya biashara kwa kurahisisha upatikanaji wa huduma zinazotolewa na Taasisi hizo. Wajumbe wa Kamati hizo hutoka sekta ya umma na binafsi na hukutana kila robo mwaka. Ili kufanikisha uendeshaji wa Kamati hizo, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeandaa mwongozo wa kuingiza na kutoa mizigo na bidhaa mipakani kwa lengo la kupunguza muda na gharama zinazotumika na wafanyabiashara na wasafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupitia Sheria Sita ili kuweka mazingira wezeshi ya upatikanaji wa masoko ya mazao na mifugo, Wizara kwa kushirikiana na wadau imefanya mapitio ya sheria za *The Agricultural Products (Control of Movement) Act* na *The Export Control Act* na kuwasilisha mapendekezo kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufuta Sheria ya *The Agricultural Products (Control of Movement) Act* na kuifanyia marekebisho Sheria ya *The Export Control Act* kulingana na mapendekezo ya wadau. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeandaa rasimu ya kanuni za kutekeleza Sheria nne za biashara ambazo zinatokana na marekebisho ya sheria mbalimbali za biashara za mwaka 2012. Sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Alama za Bidhaa *(Merchandise Marks Act, Cap 85).* Sheria ya Makampuni *(Companies Act, Cap 212),* Sheria ya Majina ya Biashara *(Business Names Act, Cap 213)* na Sheria ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(Tanzania Trade Development Authority Act, Cap 155).* Rasimu

za Kanuni hizo ziko kwa Mwasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya uhakiki kabla ya kusainiwa na Waziri wa Viwanda na Biashara ili kuanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kushirikiana na Bodi ya Stakabadhi za Maghala, Uongozi wa Mkoa wa Kagera na Vyama vya Ushirika ili kuanzisha matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi kwa zao la kahawa kwa msimu wa ununuzi wa 2013/2014, katika kuendeleza Mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani katika Mazao ya Kahawa, na Mazao Mengine Mahindi, Mpunga na Alizeti; Wizara kupitia Bodi ya Leseni za Maghala imetoa mafunzo kuwezesha kuanzishwa kwa Mfumo wa Stakabadhi kwa zao la kahawa Mkoani Kagera. Uhakiki wa maghala yanayofaa kwa kazi hiyo umefanyika na kwa kuanzia utekelezaji wa mfumo wa maghala utafanyika kwa majaribio katika Wilaya ya Ngara. Wizara imekubaliana na Mkoa wa Kagera kufanya ziara ya mafunzo kwa vitendo kwa kuwachukua wadau wa zao la kahawa kutembelea maeneo ya mfumo wa maghala (Lindi, Mtwara na Tunduru – Songea) ili kubadilishana uzoefu na kujionea jinsi mfumo unavyofanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha Rasimu ya Sera na Mkakati wa Kitaifa wa Miliki Bunifu *(National Intellectual Property Policy and Strategy)* na kazi ya kukusanya maoni ya wadau imekamilika. Mkutano wa kwanza wa wadau umefanyika Februari 2012 Mkoani Dar es Salaam kwa Kanda ya Mashariki na Mkutano wa Wadau kwa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Mkoani Mbeya umefanyika Februari, 2013, na Kanda ya Ziwa umefanyika Aprili, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na wadau imekamilisha maandalizi ya kuanzisha Soko la Bidhaa *(Commodity Exchange).* Rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri kuhusu uanzishwaji wa Soko hilo umeandaliwa na kujadiliwa katika ngazi ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Kikosi Kazi chenye Wajumbe kutoka Sekta ya Umma na Sekta binafsi kimeundwa ili kuratibu uanzishaji wa soko hilo kikisimamiwa na Kamati ya Usimamizi *(Steering Committe)* iliyoko chini ya Uenyekiti wa Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Wizara yangu inaendelea na maandalizi ya kuanzisha Soko la Bidhaa hususan kufanikisha ujenzi wa maghala chini ya utaratibu wa *PPP*, kuweka mfumo wa taarifa unaounganisha masoko na maghala, kurekebisha sheria ya *WRS* na kutoa elimu kwa wadau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Taasisi za Uwekezaji, Utafiti, Maendeleo ya Teknolojia na Mafunzo zilizo chini ya Wizara *(TIRDO, TEMDO CAMARTEC, NDC, EPZA na CBE)* zimetekeleza yafuatayo: Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania *(TIRDO).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TIRDO* limeendelea kutoa mafunzo na kuhamasisha utumiaji wa mfumo wa ufuatiliaji kwa wazalishaji viwandani na wajasiriamali ili bidhaa zao ziweze kuingia kwenye masoko kwa ushindani. Wazalishaji katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na pia Mikoa ya Kusini (Mtwara) walipatiwa mafunzo ya utekelezaji wa mfumo wa ufuatiliaji. Uhaba wa rasilimali fedha umefanya mfumo huo wa ufuatiliaji kushindwa kuwekwa kwenye mfumo wa kikompyuta *(computerised traceability system)* na kuweza kuuboresha zaidi mfumo huo wa kujaza karatasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea Kusaidia Utendaji wa Kampuni ya *GS1* kama Mshauri wa Kiufundi Chini ya Uendeshaji wa Sekta Binafsi. Shirika la *TIRDO* limeendelea kutoa ushauri wa kitaalam wa jinsi ya matumizi ya nembo za mistari *(bar-codes).* Shirika kwa kushirikiana na taasisi nyingine limeweza kuwapatia *GS1 (Tz) National Limited* Ofisi na Kampuni imeanza kazi ya kutoa nembo ya mstari *(Bar Codes)* kwa makampuni ya ndani na nje ya nchi. Hadi sasa makampuni 151 yamekuwa wanachama wa *GS1* hapa nchini na bidhaa 2,500 zimepata nembo za mstari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TIRDO* limeendelea kutoa ushauri wa kitaalam *(technical evaluation)* kupitia Benki ya Maendeleo *(TIB)* kuhusu uanzishwaji wa viwanda kwa kutumia mikopo ya *TIB*. Wawekezaji wanne (4) katika mikoa ya Pwani (Kiwanda cha kutengeneza filter za magari), Dar es Salaam (Kiwanda cha nyama/soseji) na Arusha (Kiwanda

cha kuzalisha juisi na cha kuzalisha maji) walipata ushauri wa kitaalam uliowawezesha kupata mikopo ya *TIB*. Aidha, Shirika la *TIRDO* limeendelea kutoa ushauri wa kitaalam kwa wazalishaji viwandani kuhusu uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira. Viwanda vya *ALAF, TCC*, *Tanga Cement* na, *Coca Cola* (Bara na Visiwani) vilipata ushauri huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo *(TEMDO)* katika *k*uendeleza Utoaji Huduma za Kihandisi Viwandani kwa Lengo la Kuongeza Uzalishaji, Ubora wa Bidhaa, Kuhifadhi Mazingira na Matumizi Bora ya Nishati; Utoaji wa huduma za kihandisi na mafunzo zilitolewa na *TEMDO* kwenye viwanda vya sukari *(Kilombero Sugar Company na TPC Limited),* viwanda vya vinywaji *(Tanzania Breweries Limited na Banana Investments)* na *TANALEC*. Huduma kubwa iliyotolewa katika kipindi hicho ni mafunzo ya Afya Kazini, Usalama na Mazingira *(Occupational Safety, Health and Environment – OSH&E).* Jumla ya wafanyakazi 56 walipata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TEMDO* imebuni na kuuendeleza teknolojia ya machinjio za kisasa na za kuongeza thamani ya bidhaa zitokanazo na mabaki ya mifugo mbalimbali. Kazi ya uboreshaji wa mashine na vifaa vya machinjio ya kuku umekamilika vikiwemo kifaa cha kuchinjia, kupasha joto na cha kunyonyoa kuku. Vilevile, shirika limetengeneza mashine na vifaa ambavyo hutumika kutayarisha mifupa kwa ajili ya kuondoa madini ya fluoride kwenye maji na zimefungwa katika kituo cha maji wilayani Meru. Kwa sasa ubunifu wa teknolojia ya kutengeneza gundi kutokana na mabaki ya mifugo unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea na maboresho pamoja na uhawilishaji wa teknolojia mbalimbali ikiwa ni pamoja na teknolojia ya kuteketeza taka za hospitali *(bio-medical waste incineration), TEMDO* imeendelea kuboresha kiteketezi cha kuchomea taka za hospitali na taka ngumu *(bio-medical/solid waste incinerator).* Uboreshaji uliofanyika umehusisha utengenezaji wa kiteketezi kisichotoa moshi mwingi na kisichotumia maji *(smokeless hospital solid*

*waste incinerator).* Kiteketezi hicho kimebuniwa ili kupunguza gharama za uendeshaji hasa katika matumizi ya maji. Kiteketezi cha aina hiyo kimefungwa katika hospitali za Lugalo, Bagamoyo na Babati Manyara. Kiteketezi kilicho bora zaidi kimefungwa katika hospitali ya St. Elizabeth, Arusha kwa majaribio. Vilevile, ubunifu na utengenezaji wa mtambo wa kusaga karanga ili kutengeneza siagi ya karanga (peanut butter machine) umefanyika na mashine hizo zinatumiwa na wajasiriamali wasindikaji. Mashine hizo ni za kupukuchua na kukaanga karanga na kutoa siagi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kituo cha Zana za Kilimo na Ufundi Vijijini *(CAMARTEC)* kufanya Utafiti na Uendelezaji wa Teknolojia za Kilimo na Ufundi Vijijini; Kituo kimeunda na kukamilisha majaribio ya mashine ya kuvuna mpunga inayoendeshwa na *Power tiller* ikiwa ni moja ya utafiti unaotokana na kusikiliza mahitaji halisi ya wakulima. Mashine hiyo imefanyiwa majaribio Mkoani Kilimanjaro. Kituo kimefanikiwa kutengeneza jumla ya matrekta 14, tela nne na plau nane zitakazotumiwa na trekta hilo. Awali, plau hizo zilikuwa zikiagizwa nje ya nchi.

Halikadhalika, Kituo kimezalisha mashine mbili za kusaga. Pia Kituo kimefanikiwa kuuza trekta moja kwa mkulima mkoani Katavi na kinaendelea kukamilisha viunganisho vyake kwa ajili ya kuuza pamoja na matrekta matano kwa Serikali ya mitaa Mkoni Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kimefanikiwa kujenga mitambo ya biolatrini katika shule moja ya sekondari Mkoani Dar es Salaam, moja Mkoa wa Mara na moja Mkoa wa Arusha. *CAMARTEC* kwa kutumia mafundi waliopata mafunzo yanayotolewa kwa kupitia mradi wake wa ujenzi na usambaji wa mitambo midogo imejenga mitambo 201 ya biogesi na kuisambaza katika ngazi ya Kaya katika mikoa ya Tanga, Arusha, Kilimanjaro, Manyara, Mbeya na Kagera. Kiasi hicho ni sawa na asilimia 80.4 ikilinganishwa na lengo la mitambo 250. Aidha, teknolojia hiyo inasaidia kuhifadhi mazingira na kuongeza matumizi ya mbolea bora katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kimetengeneza na kueneza majiko 2,042 yanayobana matumizi ya mkaa kwa matumizi ya kaya. Teknolojia hiyo inapunguza matumizi ya kuni na hivyo kuhifadhi mazingira. Kituo kimetengeneza mitambo nane ya kuchemshia maji kwa kutumia mionzi ya jua na kuzisambaza sita katika hospitali ya *AICC* ya mkoani Arusha na mbili kwa wakulima mkoani Arusha kwa matumizi mbalimbali. Kituo pia kimetengeneza na kusambaza mashine tatu za kukamulia mbegu za nyanya, mbili Mkoani Kilimanjaro na moja mkoani Arusha, pia kimetengeneza na kusambaza mashine mbili za kukatia malisho ya wanyama mkoani Dar es Salaam na Arusha. Kituo kimetengeneza mashine sita za kufyatua tofali za udongo-saruji na zimekamilishwa kwa asilimia 80. Mashine hizo zitasambazwa kwa watumiaji mikoani Arusha na Manyara. Vilevile, Kituo kimefanikiwa kuboresha miundombinu katika karakana na eneo la *CAMARTEC* Tawi la Nzega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza miradi ya Mchuchuma na Liganga, tafiti za kuhakiki wingi na ubora wa madini yaliyopo, kukamilisha uhakiki *(Due Diligence)* wa Mradi wa Kasi Mpya wa kuzalisha chuma ghafi *(Sponge Iron)* na kuendelea kulinda na kusimamia rasilimali zilizopo katika mashapu ya Mchuchuma na Liganga zinaendelea. Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC)* kwa kushirikiana na mbia *(Sichuan Hongda)* kupitia kampuni tanzu ya *Tanzania China International Mineral Resource Limited (TCIMRL)* inaendelea na kukamilisha ujenzi wa kambi ya makazi ya watafiti katika maeneo ya Mchuchuma na Liganga. Kazi ya uchorongaji wa uhakiki *(Confirmatory Drilling)* imekamilika katika eneo la Mchuchuma wakati *Geophysical Prospecting* imekamilika katika eneo la Liganga. Jumla ya mashimo 40 yenye kina cha zaidi ya mita 8,800 yamekwishachimbwa katika eneo la Mchuchuma. Taarifa kamili ya uchorongaji pamoja na usanifu wa mgodi *(Mine Design)* na upembuzi yakinifu kwa Mradi wa Mchuchuma unategemea kukamilika hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukamilisha ujenzi wa Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu *(biolarvicides)* kwa ajili ya Kuua Viluwiluwi kwenye mazalia ya mbu wa malaria *(TAMCO,*

Kibaha), Wizara kupitia *NDC* inatekeleza Mradi wa Kuzalisha Viuadudu *(Biolarvicides)* vya kuulia Viluwiluwi wa Mbu Wanaoeneza malaria kwa kushirikiana na Serikali ya Cuba. Ujenzi wa majengo ya kiwanda ulianza Januari 2012 na unategemewa kukamilika mwezi Oktoba 2013. Ununuzi wa mitambo ya kiwanda unaendelea na baadhi ya mitambo tayari imekwishafikishwa katika eneo la mradi. *NDC* inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya maji taka. Maji safi yamekwishafikishwa katika eneo la kiwanda na kazi ya kuunganisha umeme inaendelea. *NDC* inafanya mazungumzo na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii ili pindi uzalishaji wa viuadudu utakapoanza mwezi Novemba 2013, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii iwe mnunuzi na mratibu wa usambazaji na utumiaji wa viuadudu hivyo. Nia ni kuhakikisha kuwa viuadudu vitakavyozalishwa vinatumiwa nchini badala ya kulenga soko la nje pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imeendelea kufuatilia utekelezaji wa Mradi wa Makaa ya Mawe wa Ngaka Kusini, Songea unaotekelezwa na *Tancoal Energy Ltd* ambayo ni kampuni ya ubia kati ya *NDC* na *Intra Energy Corporation (IEC)*. Mradi huo unaendelea vizuri na hadi kufikia Januari, 2013, tani 166,775 zilikwishachimbwa, tani 71,862 zikiwa zimechimbwa kwa kipindi cha Januari, 2012 hadi Desemba, 2012. Makaa hayo huuzwa kwa viwanda vya Saruji vya Tanga na Mbeya na vya Jasi na sehemu iliuzwa nchi za Malawi, Mauritius, Kenya na Uganda. Kwa sasa, soko la makaa ya mawe bado ni dogo kwa vile uzalishaji wa umeme ambao ungetumia makaa ya mawe kwa wingi haujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za kujenga kituo cha kuzalisha umeme zinaendelea. Majadiliano kati ya *TANCOAL* na *TANESCO* kuhusu Mkataba wa Kuzalisha Umeme *(Power Production Agreement-PPA)* yanaendelea na yakihitimishwa uzalishaji wa umeme utaanza. *TANCOAL* imepanga kuzalisha umeme wa MW 120 - 200 kuanzia mwaka 2015 na kuongeza hadi MW 400 ifikapo 2016. Hata hivyo, kuanza kwa uzalishaji wa umeme kunategemea kasi ya ujenzi wa njia ya umeme wa msongo mkubwa wa Kilovoti 220 kutoka Songea hadi Makambako unaojengwa na Serikali kupitia *TANESCO* kwa

msaada wa Shirika la Maendeleo la Sweden (Sida). *TANCOAL* itajenga msongo wa umeme wa Kilovoti 220 kutoka Ngaka hadi Songea na kukamilika 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia upepo Singida unategemewa kuanza uzalishaji wa Megawati 50 mwaka 2014 na kuongezeka kwa Megawati 50 kila mwaka hadi kufikia Megawati 300 mwaka 2019. Umeme huo utaunganishwa katika Gridi ya Umeme ya Taifa kupitia kituo kikuu cha umeme *(High Voltage Substation)* kilichoko Singida. Gharama za kutekeleza mradi huo awamu ya kwanza ya MW 50 zinakadiriwa kuwa Dola za Marekani milioni 136. Wizara kupitia *NDC* na kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha inatafuta mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya *EXIM* ya Serikali ya Watu wa China. Tayari ridhaa ya Serikali *(Letter of Support)* imewasilishwa *EXIM Bank* na Wizara ya Fedha kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inaendelea kufuatilia ufufuaji wa Kiwanda cha *General Tyre (EA) Ltd (GTEA)* na Kuanza Uzalishaji wa Matairi ambapo Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* linaendelea na jitihada za kutekeleza azma ya Serikali ya kufufua kiwanda hicho kwa kushirikiana na Sekta Binafsi. Aidha, Wizara kupitia NDC imekamilisha ukarabati wa baadhi ya majengo ya Kiwanda pamoja na kuandaa Mpango wa Biashara *(Business Plan).*

Mhandisi Mshauri wa Viwanda *(Consulting Industrial Engineer)* amekamilisha uhakiki/ukaguzi wa mitambo iliyopo *(plant and equipment evaluation/audit)* katika kiwanda hicho. Vilevile, Mshauri huyo amekamilisha uchambuzi wa kina wa mahitaji na gharama ya kufufua mitambo ya kiwanda hicho ili kuvutia wawekezaji ambao watafanya upanuzi wa Kiwanda pamoja na miundombinu yake. *NDC* itaendelea kutafuta wabia wenye uwezo na uzoefu wa uzalishaji wa matairi ya magari kwa lengo la kufufua na kupanua. Wawekezaji mbalimbali kutoka Afrika ya Kusini, Jamhuri ya China, India, Taiwan, na kadhalika. wameonesha nia ya kushirikiana na *NDC* katika kufufua na kupanua kiwanda hicho. Vilevile, utaratibu wa kuhakikisha upatikanaji

wa fedha na ufumbuzi wa madeni ya kiasi cha shillingi bilioni 38 kufikia Machi, 2011, unaendelea kufuatiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukamilisha Tafiti na Kuanzisha Kiwanda cha Kuzalisha Magadi Soda (Ziwa Natron na Engaruka, Arusha), hivi sasa, *NDC* imekamilisha upembuzi yakinifu kuhusu Hydrolojia, kemia, ecology, na Resource Assessment ya Ziwa Natron ili kubaini athari katika mazingira na kuandaa hatua stahiki zitakazochukuliwa kulinda mazingira hayo. Taarifa ya upembuzi huo ambayo imetayarishwa na Mshauri Mwelekezi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, imekwishakabidhiwa *NDC*. Pia, *NDC* inakamilisha utafiti kuhusu athari kwenye Ziwa Natron, mazalia na uhamaji wa ndege aina ya Korongo unaoweza kusababishwa na mradi.

Sambamba na utafiti uliofanyika na unaoendelea kufanyika eneo la Ziwa Natron; tafiti nyingine zinafanyika katika eneo la Engaruka lililoko umbali wa kilomita 58 kutoka Ziwa Natron katika Wilaya ya Monduli kubaini upatikanaji wa magadi katika eneo hilo ili kupata chanzo kingine cha magadi mbali na kile cha Ziwa Natron. Utafiti katika eneo hilo umefikia hatua ya uchorongaji wa kina *(detailed drilling)* ili kuhakiki mashapo *(reserve)* ya malighafi hiyo na ubora wake katika viwango vya kimataifa na hatimaye kuvutia wawekezaji wa ndani na nje katika kuendeleza mradi huo. Matokeo ya uchorongaji wa awali yalionesha kuwepo kwa magadi mengi yenye makadirio ya lita za ujazo milioni 4.7. *NDC* inaendelea na utafiti wa kina kwa kuchoronga mashimo 12 ili kuweza kubaini wingi wa magadi yaliyopo katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuanzisha Viwanda vya Kusindika Nyama, Mpira na Mazao mengine ya Kilimo, *NDC* inakusudia kuanzisha mashamba makubwa ya kilimo na ufugaji kwa ajili ya viwanda vya nyama *(Meat Processing Plants)* ikiwa ni pamoja na usindikaji wa mazao yake. *NDC* inaendelea na uboreshaji wa mashamba ya mpira ya Kihuhwi na Kalunga Wilayani Muheza na Kilombero kwa kuandaa

mpango wa muda mrefu wa kuendeleza viwanda vya mazao ya mpira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kujenga Maeneo ya Viwanda *(Industrial Parks)* Sehemu za *TAMCO, KMTC*, Kange, na kadhalika, katika eneo la Viwanda la *TAMCO* Kibaha; *NDC* imekamilisha michoro *(layout design)* ya eneo la wazi lenye ukubwa wa hekta 88 kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vipya *(Industrial Estates)* katika eneo la *TAMCO* – Kibaha. Zoezi la upimaji wa viwanja na maeneo ya miundombinu *(cadastral survey)* limekamilika na kuidhinishwa na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Vilevile, *NDC* imekodisha kiwanda cha kuunganisha magari cha *TAMCO* kwa mwekezaji atakayeunganisha magari ya mizigo na mashine nyinginezo. *Detailed Design* ya miundombinu ya barabara, maji safi na maji taka umekamilika. Ujenzi wa miundombinu hiyo pamoja na usanifu wa kituo cha umeme *(Power Sub Station)* unasubiri upatikanaji wa fedha. Vilevile, uhamishaji miliki wa eneo la *TAMCO* kwenda *NDC* umekamilika. *NDC* imeingia mikataba na wawekezaji watatu ambao wamejitokeza kutaka kupata viwanja katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za kuhamisha umiliki wa eneo na Kiwanda cha Kilimanjaro *Machine Tools Company (KMTC)* kwenda *NDC* zinaendelea ikiwa ni pamoja na ulinzi na utunzaji mazingira na mali katika eneo la kiwanda. Mfumo wa maji umefanyiwa matengenezo na sasa unafanya kazi vizuri. Pia, Shirika linafanya ukaguzi wa kina *(Health Check)* katika Kiwanda cha *KMTC* kwa lengo la kuboresha uendeshaji wake. Ili kuvutia wawekezaji kwa eneo la wazi, *NDC* imeandaa hadidu za rejea kwa ajili ya kufanya *cadastral survey* na baada ya hapo ujenzi wa miundombinu ya msingi utaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, michoro ya eneo la viwanda katika eneo la Kange Tanga imekamilika na kuidhinishwa na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi ikiwa ni pamoja na kutolewa kwa hati miliki kwa viwanja husika.

Shirika pia limewasiliana na *TANESCO* kwa lengo la kuunganisha umeme katika eneo hilo. Pia, Shirika limekamilisha utaratibu wa kupata mkandarasi atakayejenga uzio na barabara za ndani katika eneo la Kange. Kazi ya kuvutia wawekezaji kwa ajili ya kuwekeza katika eneo la Kange inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Mamlaka ya *EPZ* iliendelea kuhamasisha uwekezaji wa kujenga miundombinu na kuzalisha katika Maeneo Maalum ya Uwekezaji *(EPZ/SEZ).* Kwa mwaka 2012/2013; jumla ya makampuni 29 yamepewa leseni za kujenga viwanda chini ya *EPZA* na tayari Makampuni 5 yamekwishaanza uzalishaji.

Makampuni hayo yatawekeza mtaji wa jumla ya Dola za Marekani 113 milioni na kuajiri watu 9,254. Idadi hiyo itafanya jumla ya makampuni yanayozalisha chini ya *EPZ* kufikia 70, mtaji uliowekezwa kufikia Dola za Marekani bilioni moja na jumla ya ajira za moja kwa moja *(direct employment)* kufikia 23,000. Pia katika mwaka huu wa fedha Mamlaka ya *EPZ* ilikamilisha uandaaji wa kanuni za mfumo wa *SEZ* ambao ulianza kutumika rasmi mwezi Oktoba, 2012. Mfumo huo wa *SEZ* ambao huruhusu pia wawekezaji wanaouza soko la ndani, utaleta ongezeko kubwa la wawekezaji kupitia Maeneo Maalum ya Uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Bagamoyo *SEZ* lina ukubwa wa hekta 9,000 (ekari 23,000) na litaendelezwa katika mfumo wa mji wa kisasa wa viwanda na biashara. Eneo litahusisha miundombinu ya bandari mpya katika eneo la Mbegani, ujenzi wa uwanja wa ndege, eneo la viwanda vikubwa na vidogo, eneo la biashara, utalii, teknohama, maghala, makazi na kadhalika. Katika kipindi cha mwaka 2012/2013, Wizara kupitia Mamlaka ya *EPZ* imekamilisha upembuzi yakinifu na kwa kusaidiana na Benki ya Dunia *(World Bank)* wamekamilisha uandaaji wa Mpango Kabambe *(Master Plan).* Zoezi la ulipaji wa fidia limefanyika kwa asilimia 25 ambapo hekta 1,500 kati 6,000 zilizofanyiwa uthamini tayari wamelipwa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la *Mtwara SEZ* limekuwa kivutio kikubwa kwa wawekezaji kutokana na tafiti za gesi na mafuta zinazoendelea katika pwani na ndani ya bahari ya Hindi. Makampuni ya *British Gas, Ophir, Start Oil* na *Petrobras* yanaendelea na tafiti katika eneo hilo. Kutokana na umuhimu wa eneo hilo, katika mwaka 2012/2013, Mamlaka ya *EPZ* kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari wametangaza eneo la hekta 110 kuwa eneo huru la Bandari *(Mtwara Freeport Zone)* ambapo tayari makampuni 18 ya ndani na nje yameonesha nia ya kuwekeza ndani ya eneo hilo. Aidha, Kampuni ya Solvochem (T) Ltd kutoka Lebanon inaendelea na ujenzi wa kiwanda cha vifaa vya *plastic* katika eneo la bandari kupitia *EPZA*. Kiwanda hicho kitakamilika mwishoni mwa mwaka huo na kitaajiri watu 250. Mamlaka ya *EPZ* kwa kushirikiana na Mamlaka ya Bandari wanaendelea na taratibu za kuanzisha Mtwara *SEZ* kwenye eneo la hekta 2,600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Kigoma *SEZ* ni mashuhuri kwa biashara kati ya nchi za Burundi, *DRC* na Zambia. Eneo la hekta 3,000 limetengwa kwa ajili ya *EPZ/SEZ* ambapo awamu ya kwanza ni uendelezaji wa hekta 690. Katika mwaka 2012/2013, Mamlaka ya *EPZ* kwa kushirikiana na uongozi wa Mkoa wa Kigoma wamekamilisha upembuzi yakinifu, uandaaji wa Master Plan na ulipaji wa fidia kwa nusu ya wadai ambapo Shilingi bilioni 1.5 zimelipwa. Tayari makampuni ya *City Energy, Rutale* na *Macis* yameonesha nia ya kujenga viwanda katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya eneo lililofidiwa Bagamoyo hadi sasa ni hekta 1,468. Aidha, Wizara kupitia Mamlaka ya *EPZ* imepeleka kiasi cha Sh. milioni 550 kwa Mthamini Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanya uthamini katika eneo la China Tanzania Logistic Centre. Mradi wa *Tanzania - China Logistic Centre* utatekelezwa kwa ubia baina ya China kupitia Kampuni ya *YIWU - Pan African International Investment Corporation* na Tanzania kupitia Mamlaka ya *EPZ*. Mradi utahusisha ujenzi wa eneo la biashara na viwanda vya kuunganisha vifaa *(light assembly)* na vya kuongeza thamani katika mazao kwenye eneo la ekari 60 Kurasini, Dar es Salaam.

Maandalizi ya Mkataba wa Makubaliano ya Ubia baina ya nchi mbili pia unaendelea. Kutokana na kutopatikana kwa fedha yote iliyopitishwa kwenye bajeti ya 2012/2013, fidia ya eneo lililobaki Bagamoyo, pia maeneo ya Tanga, Songea, Kigoma na Kurasini haikuweza kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Mamlaka ya *EPZ* ilikamilisha utengaji wa maeneo ya *EPZ/SEZ* katika mikoa 20 ya Tanzania Bara. *EPZA* kwa kushirikiana na Serikali za Mikoa mipya ya Simiyu, Geita, Njombe na Katavi wanaendelea na juhudi za kupata maeneo ya *EPZ* na *SEZ* katika Mikoa hiyo kupitia Sekretariati za mikoa na Halmashauri za Wilaya husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba Chuo cha *CBE* kimepata Mkuu wa Chuo *(Rector).* Katika mwaka 2012/2013, Chuo kimepitia mitaala yake katika ngazi ya astashahada, stashahada na shahada ili kuimarisha mafunzo kwa vitendo yanayolenga mahitaji ya soko la ajira. Mitaala hiyo iliwasilishwa *NACTE* na kuidhinishwa ili iweze kutumika. Chuo kwa kushirikiana na Taasisi ya Uendelezaji Utalii Zanzibar *(ZIToD)* na *NACTE* kinatekeleza mradi uitwao *"Improving the Labour Market Responsiveness of Technical Education in Tanzania"* wenye lengo la kuimarisha ubora wa utendaji wa wahitimu katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia tarehe 17 hadi 24 Machi, 2013, Chuo cha Elimu ya Biashara kikishirikiana na wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Maastricht cha Uholanzi na Chuo Kikuu cha Witwatersrand cha Afrika Kusini, kiliendesha mafunzo kwa wakufunzi wake juu ya utekelezaji wa mafunzo yenye mwelekeo wa kiutendaji. Vilevile, mitaala mipya ya shahada ya kwanza katika ujasiriamali, menejimenti ya rasilimali watu na elimu ya biashara itaandaliwa katika robo ya tatu na nne ya mwaka wa fedha. Baada ya Chuo kupitia mpango kazi na bajeti ya mwaka 2012/2013 upya, zoezi la kuandaa mitaala mipya ya shahada ya uzamili limeahirishwa hadi mwaka mpya 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo kimeendesha mafunzo ya muda mfupi mara mbili ambapo jumla ya wajasiriamali wadogo 53 walishiriki. Mafunzo yaliyotolewa yalijumuisha mbinu za kubuni biashara, namna ya kupata mtaji wa biashara na mbinu bora na endelevu za kusimamia na kuendeleza biashara; utafutaji masoko na stadi za kuimarishsa ubora wa bidhaa. Chuo kimeandaa andiko la kuandaa mpango kabambe *(Master Plan)* katika Kampasi zake tatu. Andiko hilo litatangazwa kwa kuzingatia taratibu za zabuni *(tendering process)* ili kumpatia mtaalam atakayeandaa Mpango Kabambe *(Master Plan)* wa Chuo. Chuo kimefanya ukarabati mdogo katika majengo yake katika Kampasi zake zote tatu. Maeneo yaliyofanyiwa ukarabati ni pamoja na mifumo ya umeme, maji safi na maji taka, na uboreshaji wa vyoo. Katika mwaka 2012/2013, Chuo kimewapa ruhusa ya kwenda masomoni na kulipia gharama za masomo kwa wakufunzi wanne. Kati ya hao, wakufunzi watatu wanasoma katika ngazi ya uzamivu *(PhD)* na mkufunzi mmoja anasoma katika ngazi ya uzamili *(Master Degree).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, malengo ya Wizara katika masuala ya ushindani na udhibiti wa bidhaa na huduma kupitia *TBS, TANTRADE, COSOTA , BODI YA MAGHALA, FCC, FCT* na *SIDO* yalikuwa ni kuratibu ushindani, sera, kanuni za biashara na kusimamia ubora wa bidhaa na huduma; kuthibitisha umahiri wa baadhi ya maabara, mafunzo, utafiti na maendeleo ya teknolojia na kuwezesha maabara zake kuthibitishwa umahiri wa utendaji kazi zake. Utekelezaji wa malengo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi Machi 2013, Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* kupitia kwa mawakala wake wa ukaguzi wa magari limefanikiwa kukagua magari 22,338. Vilevile, Shirika liliendelea kutekeleza mkakati wa kudhibiti bidhaa duni kutoka Nje ya Nchi. Hadi kufikia mwezi Machi 2013, Shirika lilikuwa limetoa jumla ya leseni 16,276 za ubora wa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje. Ongezeko hilo la leseni limetokana na kuanzishwa kwa utaratibu wa kuhakiki

ubora wa bidhaa kabla ya kusafirishwa kuja Tanzania *(Preshipment Verification of Conformity to Standards - PVoC)*. Ili kurahisisha utekelezaji wa mfumo wa *PVoC*, mnamo tarehe 02 Julai, 2012, Shirika lilianzisha kitengo maalum karibu na Bandari ya Dar es Salaam na Ofisi ya Forodha cha kusimamia *PVoC* kwa lengo la kuwahudumia wateja wa bidhaa zinazoingizwa nchini kwa ukaribu zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika lina maabara saba zenye vifaa vya kisasa na wataalam. Maabara hizo ni za Kemia, Uhandisi Umeme, Uhandisi Mitambo, Uhandisi Ujenzi, Chakula, Ugezi *(Metrology)* na Nguo/Ngozi/Kondomu. Kati ya maabara hizo, maabara za Ugezi, Chakula, Kemia na Nguo/Ngozi/Kondomu zina vyeti vya umahiri *(Accredited Laboratories).* Vilevile, Shirika limeendelea kutoa mafunzo kuhusu Mifumo ya Uhakiki wa Ubora (ISO 9001:2008 and ISO 17025) katika taasisi mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2013, Shirika limepima sampuli za bidhaa mbalimbali zinazofikia 6,077 katika maabara zake za Chakula, Kemia, Uhandisi, Nguo/Kondomu pamoja na Ugezi *(Metrology).* Kati ya sampuli hizo, 82 ni za Wajasiriamali Wadogo na wa Kati *(SMEs).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2013, jumla ya wajasiriamali wadogo na wa kati *(SMEs)* 219 kutoka katika Mikoa ya Arusha, Mwanza, Morogoro Iringa na Mbeya walipata mafunzo ya ufungashaji bora wa bidhaa zao. Idadi ya wajasiriamali wadogo na wakati *(SMEs)* waliopata vyeti mpaka kufikia robo ya tatu ya mwaka 2012/2013, ambavyo vitawapa uwezo wa kutumia nembo ya ubora ya *TBS* walikuwa 14 tu.

Vilevile, viwanda 60 vya wajasiriamali wadogo na wakati *(SMEs)* katika mikoa ya Ruvuma, Iringa, Kilimanjaro, Tabora, Dodoma, Rukwa, Morogoro, Kigoma, Pwani, Mwanza, Mbeya, Dar es Salaam, na Singida vilifanyiwa ukaguzi kwa lengo la kuvisaidia na kuvielekeza ili viweze kuzalisha bidhaa zenye ubora unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* wamefikia makubaliano juu ya kuoanisha *(harmonise)* viwango kwa baadhi ya bidhaa muhimu ili kuwezesha wafanyabishara wa nchi wanachama wa *SADC* kufanya biashara bila vikwazo. Hadi sasa, nchi wanachama zimekubaliana kupeleka majina ya bidhaa tano ambazo zinauzwa nje zaidi *(5 most traded goods)* katika sekretariet ya *SADC* ili kuweza kuoanisha viwango kwa bidhaa hizo na kurahisisha upatikanaji wa masoko yake. Chombo kinachosimamia uoanishaji huo kimeundwa ambacho ni *SADCSTAN*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) huendesha mafunzo kwa Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Tanzania hususan Wajasiriamali Wadogo na wa Kati *(SMEs)* ili kuwapa uwezo kupitia mafunzo na ushauri. Kwa mwaka 2012/2013, katika vipindi viwili tofauti, *TanTrade* kwa kushirikiana na Shirika la Kijerumani *GIZ* iliendesha mafunzo kwa wajasiriamali kwa awamu mbili katika Mikoa ya Dar es Salaam na Arusha. Vilevile, *TanTrade* kwa kushirikiana na *GIZ* ilifadhili na kuratibu safari ya mafunzo kwa Watanzania kumi na tano (15) kutembelea maonesho ya matunda na mbogamboga *(Fruits Logistica)* Berlin na maonesho ya bidhaa zinazozalishwa kiasili *(Biofach),* Nuremberg nchini Ujerumani kuanzia tarehe 4 hadi 17 Februari, 2013.

Mashirika hayo ni wazalishaji na wamiliki wa kampuni binafsi tisa na maofisa watano (5) kutoka Taasisi zinasosimamia masuala ya biashara. Safari hiyo ililenga kujifunza kwa kutembelea maonesho ili kuweza kuona ubora wa bidhaa zinazouzwa katika Soko la Ulaya na kujua mahitaji na vigezo vinavyohitajika katika soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, *TanTrade* kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara, Ofisi ya Waziri Mkuu kitengo cha Uboreshaji Mazingira ya Biashara na kwa msaada wa Kituo cha Biashara cha Kimataifa *(ITC),* ilifanikiwa; kuwezesha kuanzishwa kwa vikundi vitano vya wafanyabiashara wanawake, katika mipaka ya

Kabanga, Rusumo, Mutukula, Sirari na Namanga; Kutoa mafunzo katika mpaka wa Kabanga, ambapo jumla ya wajasiriamali 43 walipata mafunzo na kati yao 38 wakiwa ni wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza nia ya Serikali ya kukuza na kutafuta masoko ya bidhaa za kitanzania, *TanTrade* kwa kushirikiana na Wizara pamoja na wadau wengine iliandaa Maonesho ya 36 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam yaliyofanyika kuanzia tarehe 28 Juni, - 8 Julai, 2012 katika uwanja wa Maonesho wa Mwl. J. K. Nyerere.

Katika maonesho hayo ya kimataifa maarufu kama SabaSaba, jumla ya makampuni 1,341 ya ndani na 435 kutoka nje ya nchi walifanikiwa kuonesha bidhaa zao. Kwa upande wa biashara, ahadi za mauzo ya nje *(Export Enquiries)* zipatazo Dola za Marekani milioni 93.8 zilipatikana, vilevile mauzo ya papo kwa papo yalikuwa Dola za Marekani milioni 19.7. Ahadi za manunuzi toka nje zilikuwa ni Dola za Marekani milioni 115.3. Bidhaa zilizopata maulizo kwa wingi ni pamoja na asali, viungo *(spices)* kama iliki na tangawizi pamoja na bidhaa za mikono. Halikadhalika, bidhaa za viwandani ikiwa ni pamoja na nguo, samani za ndani na vifaa vya jikoni vilipata maulizo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuona umuhimu wa asali na bidhaa zitokanazo na nyuki kuwa ni bidhaa zinazopatikana kwa wingi Tanzania, Wizara kwa kuzishirikisha *TanTrade*, Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na wadau wengine kwenye sekta hiyo waliandaa maonesho ya Asali (1 - 7 Oktoba, 2012) ambayo yaliratibiwa na *TanTrade*. Katika maonesho hayo, Halmashauri 73 kutoka wilaya mbalimbali za Tanzania, taasisi za umma saba pamoja na washiriki binafsi 14 walishiriki. Pia, katika maonesho hayo, kulikuwa na jumla ya waoneshaji bidhaa na huduma 159 kutoka vikundi na mtu mmoja mmoja wa Halmashauri za Wilaya, makampuni, taasisi, na mashirika ya umma. Kwa upande wa biashara mauzo yaliyofanyika wakati wa maonesho hayo yanakadiriwa kuwa Shillingi milioni 89.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutafuta masoko ya nje kwa kuratibu Maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya nchi za nje; katika kuhakikisha bidhaa za Tanzania zinapata fursa za masoko ndani ya nchi, kikanda na kimataifa, *TanTrade* kupitia Kitengo cha Taarifa za Biashara inaendelea na jukumu la kupokea/kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza taarifa za biashara, takwimu na machapisho mbalimbali kutoka vyanzo mbalimbali vya nje na ndani ya nchi. Wafanyabiashara ndani na nje ya nchi wapatao 78 walipata taarifa za biashara wakiwamo wafanyabiashara binafsi, asasi mbalimbali, wakulima, watafiti, walimu wa vyuo vikuu na wanafunzi. Taarifa hizo zilisambazwa kupitia maonesho ya 36 ya *DITF* na wengine kutembelea Kitengo cha Biashara, kutumia barua pepe, kupiga simu na kutuma nukushi *(fax).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ilishiriki maonesho makubwa ya dunia yajulikanayo kama *EXPO* 2012 yaliyofanyika katika mji wa Yeosu, Korea ya Kusini kwa lengo la kutangaza bidhaa zinazozalishwa nchini. Makampuni 10 kutoka Tanzania yalishiriki katika *EXPO* 2012. Makampuni hayo yaliteuliwa na Kamati ya Maandalizi ya Kitaifa chini ya uratibu wa Wizara ya Viwanda na Biashara na *TanTrade* yaliuza bidhaa mbalibali kama vile kahawa, korosho, bidhaa za viungo, bidhaa za ngozi, bidhaa za nguo, bidhaa za mikono, bia, konyagi, mvinyo, chai, *Zanzibar Dhow* na *Zanzibar Door (Miniature).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa hizo zilikuwa kivutio kikubwa kwa watu wengi na kuwezesha kupatikana kwa miradi mitano (5) ikiwemo ya ununuzi wa korosho kutoka nchi ya Armenia, Ununuzi wa korosho na iliki kutoka Dubai, Ununuzi wa viungo kutoka Tajakistan na India na Ununuzi wa kahawa kutoka Korea ambapo hawa wote waliunganishwa na wauzaji wa Tanzania moja kwa moja. Katika maonesho hayo, miradi mbalimbali iliwasilishwa kwenye *EXPO* 2012 na kutafutiwa wabia. Miradi hiyo ni Zanzibar *Intergrated Community Maniculture Development Project-ZNZ* wenye lengo la kuhifadhi mazingira ya bahari na ufukwe ili kupunguza uvuvi holela pamoja na shughuli mbadala za

kuongeza kipato cha wananchi; Pemba Sustainable *Aquaculture Development Project-PSTZ* unaolenga kuhifadhi mazingira pamoja na ufugaji wa samaki aina ya kaa na kilimo cha mwani; na *Community Capacity Enhacement to alternative Enviromental Conservation Project – MECA* unaolenga kuhifadhi ufukwe kwa upandaji wa mikoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Leseni za Maghala *(TWLB)* imetoa leseni za biashara kwa maghala 44 na waendesha maghala 21 katika msimu wa 2012/2013. Halikadhalika, jumla ya kampuni mbili za wakaguzi zimepewa leseni kwa ajili ya ukaguzi katika maghala yanayohifadhi mazao na wastani wa vitabu 160 vya stakabadhi vimethibitishwa na kutolewa katika msimu wa 2012/2013. Vilevile, Bodi iliendelea kusimamia leseni zinazotolewa na imeanza mchakato wa kuwapeleka Mahakamani waendesha maghala waliopoteza mazao ya wakulima katika maghala. Upotevu huo ni ule unaozidi kiwango cha unyaufu kilichokubaliwa. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika tunaangalia jinsi ya kupunguza kero kwa wakulima kwa kufanya mapitio ya sheria na kanuni za Mfumo wa Stakabadhi za Maghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ilisimamia utekelezaji wa mfumo wa stakabadhi kwa msimu wa mwaka 2012/2013. Pia, bodi ilitembelea mikoa ya Lindi na Mtwara kwa ajili ya kuangalia na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mfumo hususan ununuzi na uuzaji wa korosho. Gineri ya *KNCU* na Chama cha Ushirika cha Oridoy (Babati) kilitembelewa kutathmini matumizi ya mfumo kwenye zao la Pamba. Vilevile, Bodi kwa ushirikiano wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, na Viwanda na Biashara, imeanza kuanisha maeneo yanayohitaji marekebisho katika Sheria Na. 10 ya mwaka 2005 na kanuni zake za mwaka 2006.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi inaandaa Mpango Mkakati wa Bodi wa miaka mitano na kutekeleza mpango wa kujengea uwezo wadau ikiwemo wakulima vijijini kuhusu mfumo wa Stakabadhi na kuhamasisha matumizi ya mfumo

na faida zake. Bodi imeendelea kutoa elimu kwa wadau wengine kwa nyakati tofauti kwa kutumia matangazo katika redio na luninga, vipeperushi na mikutano ya ana kwa ana. Mafunzo maalum yametolewa kwa Watendaji Wakuu wa Maghala yanayosajiliwa katika mazao ya korosho, mahindi na kahawa.

Vilevile, kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya za Kwimba, Magu na Misungwi na Taasisi za Fedha, Bodi itaendesha mafunzo kwa wakulima ili waweze kuuza mpunga kwa kutumia mfumo wa stakabadhi katika msimu wa 2012/2013. Ukaguzi wa Maghala husika umekwishafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi imejipanga kufanya uhamasishaji wa kina katika mikoa ya Katavi na Sumbawanga ili kuanzisha matumizi ya mfumo kwa zao la mahindi, mpunga, alizeti na ufuta. Tathmini ya awali ya ukaguzi wa maghala na kuangalia utayari wa wakulima imeshafanyika. Katika maeneo mengine ambako mfumo unatumika kwa muda mrefu sasa wameendelea pia kupata elimu ya mfumo ili kuongeza tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Hakimiliki *Tanzania (COSOTA)* kimeimarisha ofisi zake za kanda za Ofisi za Dar es Salaam na Mbeya, kwa kuajiri Afisa Leseni atakae simamia ukusanyaji wa mirabaha. Hadi kufikia Februari 2013, *COSOTA* imekusanya mirabaha ya jumla ya Shilingi milioni 98.8. Kati ya hizo, Shilingi millioni 88.0 ziligawiwa mwezi wa Machi 2013 zikiwa ni makusanyo ya Julai- Desemba, 2012 na zilizobaki zitaingia katika mgao wa Julai, 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jitihada dhidi ya uharamia wa kazi za sanaa, *COSOTA* imeendelea na zoezi la ukaguzi, ukamataji wa kanda na *CD* bandia na kuwafungulia kesi za jinai watuhumiwa mbalimbali. Hadi kufikia Januari 2013, *COSOTA* imepokea na kusikiliza kesi na kusimamia mashitaka yanayohusiana na ulipaji wa mirabaha. Jumla ya mashitaka yaliyopokelewa ni 26 dhidi

ya kazi za hakimiliki na kushughulikia migogoro 23 ya wasanii mbalimbali na migogoro 14 imepatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *COSOTA* imefanya kampeni ya uhamasishaji wa masuala ya hakimiliki kupitia vyombo vya habari, mikutano, na kutoa mafunzo kwa maafisa ugani na maafisa leseni na kutoa elimu kwa watafiti mbalimbali kuhusu hakimiliki na hakishiriki. *COSOTA* imesajili wasanii wa muziki 403 na kazi zao 9,839; wasanii wa filamu 22 na kazi zao 737 pamoja na wasanii wa kazi za maandishi 51 na kazi zao 1,437. Hadi kufikia Februari, 2013, *COSOTA* imekusanya jumla ya Shilingi milioni 9.32 kama ada ya usajili wa wanachama na ada za mwaka za wanachama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Vipimo *(WMA),* imekuwa ikifanya ukaguzi wa vipimo mbalimbali vitumikavyo katika biashara ikiwemo mizani itumikayo katika ununuzi wa mazao ya wakulima. Kwa mwaka 2012/2013, jumla ya vipimo 576,744 vilikaguliwa ikilinganishwa na Vipimo 545,506 vilivyokaguliwa mwaka 2011/2012. Wamiliki 5,627 walitozwa faini kwa makosa mbalimbali waliyofanya kuhusiana na vipimo ikilinganishwa na wamiliki 5,503 waliotozwa faini kwa mwaka 2011/2012, na wafanyabiashara 10 walifikishwa mahakamani kwa makosa mbalimbali yanayohusu vipimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo, imeendelea kuwapa mafunzo watumishi wake. Kwa mwaka 2012/2013, watumishi 193 walipata mafunzo ya aina mbalimbali ili kuwaongezea weledi katika kazi. Vilevile, wakala ilipanga kununua magari 20 kwa mwaka 2012/2013 na hadi kufikia Machi 2013, magari 11 yalikwisha nunuliwa na kusambazwa mikoani. Magari tisa yaliyobaki yatanunuliwa katika robo ya nne ya mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kaguzi na uhakiki wa vipimo, Wakala imeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari (Magazeti, Redio na Televisheni) pia kuzitumia vyema fursa kama vile za maonesho ili kuelimisha umma. Wakala imeshiriki katika maonesho sita

(6) ya biashara *(DITF), MOWE*, NaneNane, *SIDO*, Maonesho ya Nyanda za Juu Kusini ya *SMEs* na Maonesho ya Ufunguzi wa Mkoa Mpya wa Katavi. Vipindi vitano (5) vya redio na vipindi vitatu (3) vya luninga vilitayarishwa na kurushwa hewani. Makala zaidi ya 30 zilitayarishwa na kuchapishwa kwenye magazeti. Machapisho ya vipeperushi mbalimbali yapatayo 9,000 yalifanyika na kusambazwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Wakala wa Vipimo, inalo jukumu la kusimamia matumizi sahihi ya vipimo katika Sekta ya Mafuta na Gesi ili kuepuka udanganyifu na matumizi yasiyo sahihi ya vipimo. Vipimo vilivyo sahihi huwezesha Serikali kupata mapato yake sahihi na watumiaji wa mafuta na gesi kupata bidhaa hiyo kwa thamani ya fedha yao. Katika kuimarisha kitengo hicho, Wakala imeendelea kutoa mafunzo kwa watumishi wake wa bandari na kwa mwaka 2012/2013 mtumishi mmoja amekwishapata mafunzo maalum ya usimamiaji wa usahihi wa vipimo bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Vipimo katika kudhibiti usahihi wa vipimo vitumikavyo katika gesi asilia na ile itokanayo na mafuta ya petroli; kwa kushirikiana na wadau wake inaandaa rasimu ya kanuni za gesi aina ya *LPG (Liquefied Petroleum Gas)* ili kusimamia kiasi cha gesi inayojazwa kwenye mitungi na kwa hali hiyo, kumlinda mlaji na vipimo visivyo sahihi. Vilevile, Wakala imeendelea kufanya utafiti na uchambuzi wa mfumo wa vipimo vinavyotumika katika usambazaji wa gesi asili *(Natural Gas-NG)* nchini ili kuweza kupata taarifa sahihi ya vipimo hivyo vinavyotumika kwenye mfumo huo. Kwa kufanya hivyo, itasaidia mchakato wa kuandaa rasimu ya kanuni ya gesi asili itakayokidhi usimamizi wa matumizi sahihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukamilishaji wa sheria mpya ya vipimo unaendelea na kwamba tarehe 28/11/2012 mapendekezo ya sheria hiyo kupitia Waraka wa Baraza la Mawaziri ilijadiliwa na *IMTC* na kutoa ushauri wa kuboresha waraka huo. Kwa sasa Wizara kwa kushirikiana na Wakala

wa Vipimo, inafanya maboresho ili uweze kuwasilishwa Baraza la Mawaziri kwa hatua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA),* katika kuboresha utoaji wa huduma za Wakala, hadidu za rejea za kumpata mshauri mwelekezi wa kuandaa mifumo ya kiteknolojia ya kuwezesha upatikanaji wa taarifa na huduma kupitia mtandao wa kompyuta *(online registration system)* zimeandaliwa. Wakala inakamilisha taratibu za kuwezesha wateja kulipia ada za huduma za usajili kupitia Benki za *NMB* na *CRDB*. Ili kufanikisha uanzishaji wa *online registration*, Sheria ya Ushahidi *(the Evidence Act),* inatakiwa kufanyiwa marekebisho ili kuruhusu nyaraka za mitandao kutumika kwenye ushahidi. Pia wakala inapaswa kuwa na jengo linalofaa kufunga mitambo ya kiteknologia na ukamilishwaji wa mifumo ya *ICT* ili masijala zote ziweze kuwasiliana kwa njia ya kielektroniki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uboreshwaji *(digitisation)* wa Masijala ya Taarifa za Makampuni na Majina ya Biashara, Hataza *(patent)* na Leseni za Viwanda umekamilika. Wakala inaendelea na maboresho ya masijala ya Alama za Biashara na Huduma *(Trade and Service Marks)* ili kuanzisha mfumo wa masijala ujulikanao kama *Intellectual Property Automation System- IPAS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na marekebisho ya Sheria za Makampuni na Majina ya Biashara kupitishwa na Bunge Mwezi Aprili, 2012, Wizara kwa kushirikiana na *BRELA*, na wadau wengine imeandaa Kanuni za kutekeleza Sheria hiyo na kuwasilishwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa uhakiki kabla ya kupitishwa na Waziri wa Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala imeendelea kutoa elimu kwa njia ya semina, na maonesho mbalimbali yanayofanyika nchini. Katika maonesho yote na semina, Wakala hutoa huduma ya usajili papo kwa hapo. Wakala imewaelimisha watendaji wa *TCCIA* Tanzania nzima ili

waweze kutoa huduma ambazo sio za kisheria kwa wananchi ikiwa ni pamoja na elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala imenunua kiwanja No. 24 eneo la *Ada Estate,* Kinondoni, na taratibu za kumpata mtaalam wa usanifu majengo na kusimamia ujenzi zimefikia hatua za mwisho za tathimini. Inategemewa ifikapo mwezi Mei mwishoni 2013, mtaalam atakayechora na kusimamia jengo hilo atakuwa amepatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Ushindani *(FCC)* ilikamata na kuadhibu waagizaji bidhaa bandia themanini na mbili (82) kwa kukiuka Sheria ya Alama za Bidhaa. Katika kaguzi hizo, Tume ya Ushindani pia ilifanikiwa kukamata bidhaa mbalimbali kama vifaa vya kompyuta *(computer accessories),* mipira ya ndani ya pikipiki *(vee-rubber),* taulo za usafi za wanawake *(always),* simu za mkononi *(Samsung),* maandishi ya luninga *(Eurostar),* miswaki, na vifaa mbalimbali vya umeme na ujenzi ambazo zimehifadhiwa katika maghala ya Serikali zikisubiri utaratibu wa kuharibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai mpaka Desemba 2012 , Tume imefanya uchunguzi wa awali katika makampuni mbalimbali na mgogoro wa bidhaa za mafuta ya petroli. Tume imefanya uchunguzi katika muungano wa makampuni na taarifa itatolewa utakapokamilika. Vilevile, Tume iliangalia muungano wa makampuni *(mergers)* mbalimbali ili kuona yanaleta tija na ufanisi katika soko. Jumla ya maombi nane yaliwasilishwa kwa Tume na kufanyiwa kazi, kati ya hayo makampuni matano, maombi yao yalikubaliwa na kupitishwa bila masharti na mengine matatu yaliyobakia yako katika hatua ya uthibitisho na uchunguzi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO)* limetafuta, kuzifanyia marekebisho na kutoa teknolojia mbalimbali kwa wajasiriamali kutoka ndani na nje ya nchi. Shirika linasimamia vituo vya maendeleo ya teknolojia ndani ya mitaa ya viwanda vidogo vilivyoanzishwa ili viweze kubuni, kutengeneza na hatimaye

kuuza bidhaa na mashine mbalimbali kwa wananchi, na kuwaelekeza namna nzuri ya kuzitumia kuanzisha miradi. Vituo hivyo pamoja na teknolojia zinazozalishwa ni:- Arusha (mashine za kukamua miwa na zana za kilimo), Iringa (mashine za mbao na usindikaji wa mtama), Kigoma (mashine za kusindika mawese na mazao ya mchikichi), Kilimanjaro (mashine za kutengeneza chaki na bidhaa za ujenzi), Lindi (mashine za kusindika korosho na mihogo), Mbeya (mashine za usindikaji wa maziwa na zana zinazolenga kupunguza uharibifu wa mazingira) na Shinyanga (mashine za kusindika ngozi na kutengenezea bidhaa za ngozi). Huduma zilizotolewa zimewezesha uzalishaji na hatimaye upatikanaji wa bidhaa mbalimbali za viwanda vidogo mijini na vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *SIDO* inatekeleza Mkakati wa Zao Moja kwa Wilaya Moja *(ODOP),* imewezesha wajasiriamali nchini kote kuzalisha bidhaa kutokana na malighafi zinazopatikana katika sehemu husika na kuchangia maendeleo ya viwanda vidogo vijijini. Mkakati huo umewezesha kutengenezwa na kusambaza mashine mpya za aina mbalimbali 462 kupitia vituo vya kuendeleza teknolojia vilivyopo mikoa ya Arusha, Iringa, Kigoma, Kilimanjaro, Lindi, Mbeya na Shinyanga. Kati ya teknolojia mpya zilizosambazwa ni pamoja na za usindikaji mkonge, muhogo, viungo, asali ukamuaji mafuta ya kula na usindikaji ngozi. Huduma zilizotolewa zimewezesha uanzishwaji wa viwanda vidogo 80 vilivyozalisha nafasi za kazi 582.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya kujenga miundombinu ya kongano za alizeti yanaendelea kukamilishwa katika mikoa ya Dodoma, Singida na Manyara. Uhamasishaji wa sekta binafsi kushiriki kujenga miundombinu hasa majengo ya uzalishaji ndani ya maeneo yaliyotengwa na Halmashauri za Wilaya na Miji unaendelea. Taratibu za kutayarisha michoro, kutafuta vibali vya ujenzi, kujenga miundombinu kwenye maeneo, kuweka maji, umeme na kukamilisha taratibu za manunuzi ya huduma kwa kuwapata wakandarasi watakaoshiriki katika ujenzi wa majengo ya mfano zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huduma ya viatamizi inakusudia kuwawezesha wajasiriamali wenye mawazo ya ubunifu kuyatumia kutengeneza bidhaa au mfumo wa uzalishaji wenye tija. Bidhaa au mifumo hiyo mipya baadaye huwa msingi wa kuanzisha viwanda vidogo na kuongeza uzalishaji, biashara, kuongeza kipato, kuleta ajira na kujenga uchumi. Programu hiyo iliendelea kutekelezwa katika mikoa ya Dar-es-Salaam, Mbeya, Mwanza, Rukwa na Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuandaa mafunzo ya aina mbalimbali ni kuwawezesha wajasirimali kupata ufahamu na stadi zinazowawezesha kuanzisha na kuendesha miradi yao vyema. Mafunzo yaliyotolewa yaliendeshwa katika Mikoa yote na wajasiriamali 4,766 walinufaika. Mafunzo hayo yalilenga kutoa uelewa na ujuzi wa kiufundi katika uzalishaji mali kama usindikaji wa mafuta ya kupikia, ngozi, ubanguaji korosho, kuhifadhi na kusindika vyakula vya aina mbalimbali.

Mafunzo hayo pia yalielekezwa katika kujenga na kuimarisha mbinu za kibiashara na uendeshaji wa miradi ya kiuchumi kwa walengwa hasa uongozi, masoko, ubora wa bidhaa, mbinu za uzalishaji mali, utunzaji wa vitabu, uendeshaji na utunzaji mashine na uongozi wa vikundi na vyama. Kwa ujumla, mafunzo yamewawezesha wajasiriamali kupata maarifa na stadi za kuimarisha shughuli zao za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa Ofisi ya *SIDO* Mkoa wa Manyara umekamilika na jengo limekwisha anza kutumika rasmi. Vyuo vya mafunzo na uzalishaji vilianzishwa katika mikoa mbalimbali ili kuwa chimbuko la kutoa stadi za kazi kwa mazao na bidhaa maalum kwa maeneo hayo. Tafiti hufanywa ili kubaini fursa za maarifa na ujuzi vinavyohitajika ambavyo hufuatiwa na kuandaliwa mafunzo maalum kuziba mianya hiyo. Katika kipindi hicho cha mwaka, mafunzo ya ujuzi maalum yalitolewa na vyuo vya Njombe (usindikaji wa vyakula), Dar es Salaam (uzalishaji wa bidhaa zitokanazo na kamba za asili) na Tanga (bidhaa zitokanazo na makumbi ya nazi). Jumla ya wajasiriamali 220 walishiriki katika mafunzo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, maonesho matatu ya bidhaa zilizozalishwa na wajasiriamali nchini ya vyakula vilivyosindikwa, sabuni, bidhaa za wahunzi, bidhaa za ngozi, nguo, chumvi, mashine na zana za kazi yalifanyika katika Kanda ya Kusini (Lindi) na kuwashirikisha wajasiriamali 197 ambapo mauzo ya bidhaa zao yenye thamani ya Shilingi milioni 45 yalifanyika. Maonesho ya Kanda ya Ziwa (Mwanza) na kuwashirikisha wajasiriamali 264 ambapo mauzo ya bidhaa zao yenye thamani ya Shilingi milioni 182 yalifanyika. Pamoja na kufanya mauzo ya bidhaa zao, walibadilishana mawazo, kujifunza kutoka kwa wenzao na kujenga msingi wa masoko mapya. Maonesho ya tatu yalihusisha Kanda ya Pwani (Morogoro) na kuwashirikisha wajasiriamali 200 ambapo mauzo ya bidhaa zao yenye thamani ya Shilingi milioni 60 yalifanyika. Pamoja na kufanya mauzo ya bidhaa zao, walibadilishana mawazo, kujifunza kutoka kwa wenzao na kujenga msingi wa masoko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa huduma kwenye vituo 20 vya habari unaendelea vizuri na kwa kipindi cha mwaka 2012/2013, jumla ya wajasiriamali 3,620 wametumia huduma za vituo hivyo kufanikisha miradi na biashara zao. Vituo hivyo hutoa taarifa mbalimbali kuhusu uendelezaji wa ujasiriamali yakiwemo masoko. Ofisi zote za mikoa isipokuwa ya Mkoa wa Pwani zina vituo vya habari ambapo wajasiriamali hupata habari zote zinazohusiana na uanzishaji na uendelezaji wa miradi ya uzalishaji na biashara ikiwa ni pamoja na teknolojia, mafunzo na masoko. Vituo hivyo vinapaswa kuwa na sehemu ambako wajasiriamali wanaweza kuweka sampuli za bidhaa zao ili wananchi waweze kuona. Hadi sasa mikoa ya Dodoma na Rukwa ndiyo iliyo na sehemu za wajasiriamali za kuoneshea bidhaa zao *(display facility)* ambazo zimejidhihirisha vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Julai mpaka Desemba, 2012, jumla ya kesi nne zilisikilizwa na kutolewa maamuzi na kesi tano zinaendelea na mchakato wa kusikilizwa. Pia, Baraza la Ushindani *(FCT)* liliweza kukamilisha Mpango Mkakati mpya wa kipindi cha 2012/2013 – 2015/2016. Rasimu ya Mpango Mkakati huo ilijadiliwa

kwenye kikao cha wadau wote muhimu wa Baraza tarehe 28/09/2012. Uidhinishaji rasmi wa Mpango Mkakati huo unatarajiwa kufanyika mwaka 2013. Baraza limefanya mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wake ili kuwajengea uwezo zaidi katika maeneo yao ya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza limefanya mapitio ya Sheria ya Ushindani na kubainisha upungufu kadhaa unaohitaji kufanyiwa marekebisho. Upungufu huo ni pamoja na kukosekana kwa Makamu wa Mwenyekiti na muda wa Wajumbe kukoma kwa pamoja. Baraza kwa kushirikiana na Tume ya Ushindani limefikisha mapendekezo ya marekebisho ya sheria Wizarani ili mchakato wa kuyafikisha Bungeni uanze. Mapendekezo hayo yameandikiwa Waraka wa Baraza la Mawaziri ambao kwa sasa uko katika hatua ya kujadiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji *(NCAC)* linasimamia maslahi ya mlaji kwa kupeleka maoni yake kwenye Tume ya Ushindani, Mamlaka za Udhibiti na Serikali kwa ujumla. Katika mwaka 2012/2013, Baraza limeendelea kupokea na kusambaza taarifa na maoni yenye maslahi kwa mlaji; Kuanzisha Kamati za Mlaji za Mikoa na Sekta na kushauriana na Kamati hizo; wenye viwanda, Serikali na jumuiya nyingine za walaji katika mambo yenye maslahi kwa mlaji. Ili kumlinda mlaji, elimu kwa mlaji imetolewa kwa kuanzia katika mikoa ya Mwanza, Morogoro na Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Biashara Nje ya Nchi. Kituo cha Biashara cha Tanzania Dubai (*TTC*-Dubai) Kwa mwaka 2012/2013, Kituo kimeendelea kuvutia wawekezaji wa nje ili kuwekeza Tanzania na kutafuta masoko kwa ajili ya bidhaa za Tanzania katika Umoja wa Falme za Kiarabu *(United Arab Emirates – UAE).* Juhudi zilizofanyika kwa mwaka huo ni kama zifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutafuta masoko ya bidhaa za Tanzania, Kituo kimeratibu na kuwezesha ushiriki wa wajasiriamali watano wa Tanzania kwenye maonesho ya *Global Village* yaliyofanyika Dubai kwa miezi sita. Kituo

kimewezesha kampuni za Tanzania kuuza mbao aina ya *Teak*, dhahabu, *Tanzanite*, karafuu, mashudu na nyama ya mbuzi katika soko la Umoja wa Falme za Kiarabu, ambapo mauzo ya zaidi ya Shilingi bilioni 100 yamefanyika.

Vilevile, Kituo kimewezesha Kampuni ya *Ms Faisal Oils* kuwekeza katika usambazaji wa vilainishi *(lubricants)* nchini kwa lengo la kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha biashara hiyo kwa nchi zote za Afrika Mashariki na Kusini. Mauzo yao kwa sasa wamefikia zaidi ya Shilingi billioni 10. Baadaye, wanakusudia kujenga kiwanda cha kutengeneza vilainishi hivyo nchini. Aidha, Kampuni ya *ISSG Group* ya Dubai, imewekeza katika uchimbaji wa dhahabu eneo la Morogoro. Uzalishaji wa majaribio tayari umekwishaanza na jumla ya Shilingi bilioni 2 zinatarajia kuwekezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kimendelea kuwa kitovu cha habari za utalii na kuwasilisha machapisho ya utalii kwa mawakala wa utalii na wanajumuiya wa *UAE*. Jumla ya machapisho 5,000 kutoka *TANAPA*, Ngorongoro, *Tanzania Tourist Board-TTB*, Kamisheni ya Utalii Zanzaibar na kampuni binafsi ya *Bobby Tours* ya Arusha yamesambazwa. Pia, Kituo kiliratibu ushiriki wa Tanzania kwenye *World Route Development Forum* ambapo washiriki kutoka viwanja vya ndege vya *JNIA*, Mwanza, mashirika ya *TCAA, TAA, KADCO* na *TTB* walishiriki na kuweza kuvitangaza viwanja vyetu na vivutio vyetu vya utalii. Shirika la Ndege la Uturuki lilisaini makubaliano na *KADCO* ya kutumia Uwanja wa KIA kwa ndege zake za abiria. Aidha, Tovuti za mawakala wa utalii wa Tanzania, Kampuni ya *Bobby Tours* ya Arusha na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* waliunganishwa na Tovuti ya Kituo cha Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukuza biashara, Kituo cha Biashara cha Tanzania Londoni *(TTC-London)* kimefanya utafiti wa bidhaa zenye sifa ya kupata masoko nje katika Maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam na Nanenane (Dodoma) ambapo utafiti wa makampuni yenye bidhaa zenye sifa ya kupata masoko nje ulifanyika na sampuli za bidhaa 12 kukusanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maonesho ya Bidhaa za Chakula yalifanyika London na makampuni sita ya *Market Research and Export Agent ya Dar es Salaam, Amir Hamza (T) Ltd* ya Bukoba, *KYM'S Enterprises* ya Kibaha, *Kagera Tea Blenders Ltd* ya Kagera, *Nature Ripe Kilimanjaro Ltd* ya Dar es Salaam, na *TanTrade (Zanzibar)* yalishiriki. Kongamano la kiuchumi kati ya Afrika na Ireland lilifanyika tarehe 22 Oktoba, 2012 mjini Dublin ambapo fursa za kibiashara na uwekezaji zilizopo kati ya Afrika na Ireland zilijadiliwa na mikakati ya kuimarisha mahusiano hayo iliwekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kituo kiliendelea kuvutia uwekezaji kama vile usafiri wa reli ambapo Kituo kiliwezesha Kampuni ya *SMH RAIL* ya Malaysia kufanya mawasiliano na kampuni ya *TAZARA* na walifanikisha kusaini mkataba wa ushirikiano mwezi Oktoba 2012. Kituo kilishiriki katika mkutano wa masuala ya gesi na mafuta uliohusu nchi za Afrika Mashariki ambapo wadau 150 wakiwa ni wawekezaji, waandishi na maafisa balozi na Serikali za Ethiopia, Somalia, Kenya, Msumbiji, Uganda na Tanzania walishiriki. Kutokana na mkutano huo, wawekezaji kutoka Kampuni ya *Chicago Bridge and Iron Company (CBI)* walitembelea Kituo kwa ushauri wa mipango ya ziara nchini Tanzania ambayo yalifanyika tarehe 16 Oktoba 2012 ili kudadisi fursa za uwekezaji katika Sekta ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utangazaji wa fursa za uwekezaji kupitia chapisho la *International Investor* ulifanyika ambapo sera, mikakati na fursa za biashara na uwekezaji Tanzania vilitangazwa.

Aidha, vivutio vilivyoko nchini Tanzania vilitangazwa kupitia semina ya Utalii - *Redditch*, maonesho ya Utalii ya *(WTM)* London yaliyofanyika mwezi Novemba 2012, ambapo Makampuni 60 ya Tanzania yalishiriki. Vilevile, Kituo kiliendeleza mahusiano ya Kimataifa kwa kushiriki Mkutano Mkuu wa mwaka wa *Britain Tanzania Society* katika mkutano wa shirika la mkonge, Mkutano wa Shirika la Sukari, Mkutano wa Shirika la wataalamu wa kilimo *(CABI)* ambao Wajumbe wake ni wanachama wote wa Jumuiya ya Madola

*(Commonwealth Agricultural Bureau International)* na Mkutano wa Shirika la Nafaka *(International Grain Council).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu maendeleo ya Rasilimali Watu. Wizara ina Watumishi 232 wa kada mbalimbali. Kwa mwaka 2012/2013, imejaza nafasi 32 zilizowazi na imepandisha vyeo watumishi 28. Kwa upande wa kuwajengea uwezo watumishi, Wizara imewezesha kuwapeleka jumla ya watumishi 48 katika mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Awamu ya Pili ya Programu ya Kuboresha Utumishi wa Umma ya miaka mitano kuanzia mwaka 2008 hadi 2012, ambayo inalenga kuimarisha utendaji unaojali matokeo na kuimarisha uwajibikaji katika Utumishi wa umma, katika mwaka 2012/ 2013, watumishi wote wamesaini Mikataba ya Kazi kwa Mfumo wa Wazi wa Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi – MWAMTUKA, *(OPRAS).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2012/2013, Wizara imeunda Kamati ambayo ni Dawati la Kushughulikia Malalamiko na Kero za wadau wa ndani na nje. Kamati hiyo imejumuisha Wajumbe kutoka kila Idara na Vitengo. Kamati imeweka utaratibu wa kupokea, kukusanya, kufuatilia na kutafuta ufumbuzi wa malalamiko na kero na kuwasilisha taarifa kwenye Menejimenti ya Wizara. Umewekwa muda maalum wa wiki moja kushughulikia malalamiko na kero na kutoa mrejesho kwa wadau ndani ya muda maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala mtambuka, kwa upande wa kupambana na Rushwa, Wizara imeendelea na jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa watumishi wake kwa kutoa mafunzo ya Sheria mbalimbali za kazi, zikiwemo Sheria Na. 8 ya mwaka 2002 ya Utumishi wa Umma, na Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sheria ya Fedha ili kuwawezesha kufanya kazi na kutoa maamuzi kwa kuzingatia matakwa ya sheria tajwa. Ili kuweza kutoa huduma bora zinazokidhi viwango vilivyoainishwa katika Mkataba wa Huduma kwa Mteja, Wizara imetoa mafunzo

ya elimu ya huduma kwa mteja kwa watumishi wa Wizara ili kuwapatia mbinu mbalimbali za kuhudumia wateja. Wizara pia, ilitoa mafunzo kuhusu maadili ya utendaji katika Utumishi wa Umma na kuwakabidhi vijitabu hivyo kwa mujibu wa Kanuni Na. 66 (1) ya Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mazingira, Wizara kwa kushirikiana na *NEMC* na wadau mbalimbali imeendelea kutekeleza mikakati inayohusu utunzaji wa mazingira pamoja na programu ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi na Utunzaji wa Mazingira. Wizara imehamasisha miradi mipya itakayoanzishwa kutimiza masharti ya uzalishaji salama viwandani na kuhimiza miradi ya zamani ambayo haikuwa na mifumo salama kwa mazingira ijenge mifumo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupambana na UKIMWI/VVU, Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya kujikinga na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na kuhamasisha upimaji wa afya za wafanyakazi kwa hiari.

Pia, Wizara imeendelea na jitihada za kuwawezesha watumishi waliojitokeza na watakaojitokeza wanaoishi na virusi vya UKIMWI kupata huduma ya virutubisho, lishe na usafiri. Waelimishaji rika walipewa mafunzo upya ya kuwawezesha kupata mbinu mpya ambazo zimewezesha kuwaelimisha watumishi wenzao na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kujumuisha Masuala ya Jinsia katika Sera, Mikakati, Programu na Bajeti ya Wizara na Kutoa Mafunzo kwa Wataalam katika Masuala ya Jinsia, Mwongozo wa Taifa wa kuratibu masuala ya Jinsia katika Utumishi wa Umma unaelekeza uanzishwaji wa programu ya masuala ya jinsia ya kisekta, Dawati na Kamati ya Kuratibu Maendeleo ya Jinsia katika sekta. Wizara imetoa mafunzo kwa maafisa 50 kutoka Idara na Taasisi chini ya Wizara kuhusiana na uchambuzi wa masuala ya jinsia katika Sekta ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za Sheria, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria wa Serikali, inaendelea kupitia sheria, mikataba na mashauri mbalimbali ya Wizara na Taasisi kwa lengo la kuboresha utekelezaji wake na kulinda maslahi ya nchi. Pia, Wizara inazingatia matumizi ya njia za amani katika kutatua migogoro inayohusu sekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya jukumu la Wizara ni kutoa taarifa zinazohusu masuala ya Viwanda na Biashara kwa wadau na kwa wakati. Wizara inazingatia matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano - *TEHAMA* katika kupokea, kutunza na kusambaza taarifa mbalimbali zinazohusu Sekta. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara imeboresha Tovuti yake *(www.mit.go.tz)* ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu yake. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma *(POPSM)* na Wakala ya Serikali Mtandao *(eGA)* inaratibu uanzishwaji wa Tovuti ya Biashara ya Kitaifa *(National Business Portal).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuimarisha usimamizi wa Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kuhakikisha kwamba Sheria/ Kanuni na taratibu za fedha,zinazingatiwa. Kwa mwaka 2012/2013, Wizara imefanya ukaguzi wa kawaida na kutoa taarifa za kila robo mwaka katika Kamati ya Ukaguzi ya Wizara. Ukaguzi maalum ulikuwa ukifanyika pale ambapo kuna hitaji la kufanya hivyo.

Pia, Wizara imekuwa ikitekeleza ushauri unaotolewa katika taarifa za ukaguzi ili kuhakikisha kwamba mapungufu yaliyobainishwa yanarekebishwa; imeratibu na kusimamia vikao vya Kamati ya Ukaguzi na Kamati ya Kusimamia na Kudhibiti Mapato na Matumizi ya Serikali na kuwasilisha taarifa ngazi husika kwa wakati. Wizara imesimamia na kujibu Hoja za Ukaguzi wa nje na kushiriki katika vikao vya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC);* imeandaa na kuwasilisha taarifa za mwaka za mapato na matumizi kwa kufuata mfumo wa IPSAs na imeratibu na kuandaa taarifa za mapato na matumizi  na kuziwasilisha kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Sheria ya Ununuzi wa Umma Na. 21 ya Mwaka 2004 na Kanuni zake za mwaka 2005, Wizara imeandaa Mpango wa Manunuzi wa Mwaka 2012/2013 kulingana na Sheria hiyo na kusimamia utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa malengo ya kisekta, Wizara na Taasisi zilizo chini yake zilikabiliwa na changamoto mbalimbali. Moja kati ya changamoto hizo ni uhaba wa rasilimali fedha ambao umepunguza kasi ya Wizara katika kuendeleza viwanda, biashara, masoko na viwanda vidogo na biashara ndogo nchini. Kwa mfano, Wizara bado haijapata fedha za kutosha hususan za kulipia fidia katika maeneo huru ya Bagamoyo, *Tanzania-China Logistic Centre* (Kurasini) pamoja na ulipaji fidia kwa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya *EPZ* katika mikoa ya Tanga, Ruvuma na Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda pia imekabiliwa na mlolongo mkubwa wa kodi, ushuru na tozo wanazotozwa wenye viwanda. Hivi sasa viwanda vinatozwa kodi na tozo mbalimbali zipatazo 25. Vilevile, kumekuwa na changamoto ya gharama kubwa za kufanya biashara *(cost of doing bussiness)* na uwekezaji kutokana na kuongezeka kwa bei ya umeme na maji; kukatika mara kwa mara kwa umeme kunakosababisha uharibifu wa mitambo pamoja na bidhaa zilizoko kwenye mtiririko wa uzalishaji; Kushuka kwa thamani ya Shilingi; Mitambo chakavu na teknolojia duni za uzalishaji na Upungufu wa wataalam wenye umahiri katika fani mbalimbali viwandani *(specialised industrial skills, e.g. leather and textiles technologists etc.).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushindani usio wa haki kutokana na bidhaa zinazoagizwa nje ya nchi kutolipiwa ushuru stahiki kwa kukwepa kodi au kutaja thamani ndogo ya bidhaa husika *(under invoincing and under declaration)* umeendelea kuwa changamoto kubwa. Changamoto nyingine ni ukosefu wa maeneo ya uwekezaji wa viwanda pamoja na ukosefu wa mitaji ya kuanzisha viwanda vya kuendeleza biashara. Aidha, uendelezaji wa usindikaji wa zao

la korosho na pamba kwa ukamilifu wake katika uchumi wetu bado ni changamoto kubwa kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto na kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara, Wizara na Taasisi zake zimechukua hatua zifuatazo: Kutayarisha maandiko mbalimbali yatakayosaidia sekta hiyo kunufaika na mikopo ya kibenki pamoja na Mpango wa Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi - *Public Private Partnership (PPP).* Pia tuliendelea kushirikiana na Taasisi nyingine zinazohusika na maendeleo ya teknolojia kama vile *COSTECH* katika kuwawezesha na kuendeleza ubunifu wa taasisi za *TIRDO, CAMARTEC* na *TEMDO* ambazo zimefaidika na fedha za Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia.

Vilevile, tumeshirikiana na sekta nyingine katika kuboresha mazingira ya biashara na kusaidia kupunguza gharama za kufanya biashara. Jitihada hizo zinajumuisha kurahisisha taratibu za usajili wa Makampuni kupitia *BRELA* kwa kuweka fomu zote za maombi ya usajili mbalimbali kwenye tovuti yake na kufupisha muda wa kusajili kutoka siku tano hadi kufikia siku tatu. Pia *SIDO* inahamasisha ujasiriamali na kuelimisha umma kuhusu kufanya shughuli rasmi na katika vikundi ili kuondokana na mtizamo hasi katika kufanya biashara na shughuli nyingine za kiuchumi.

Aidha, Wizara kupitia taasisi zake za *FCC, CBE, COSOTA, SIDO, TBS, WMA, TWLB* na *TANTRADE* zinashirikiana ili kumsaidia mwananchi katika kupata elimu ya biashara, mbinu za kufanya biashara kiushindani, kumlinda mlaji dhidi ya bidhaa bandia pamoja na manyanyaso ya soko na pia kusimamia matumizi sahihi ya vipimo na viwango katika biashara.

Vilevile, wananchi wanafahamishwa kuhusu fursa mbalimbali za masoko na matumizi yake yakiwemo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC),* Jumuiya ya Uchumi Kusini mwa Afrika *(SADC),* masoko ya upendeleo na masoko maalum kama AGOA, India na China. Kuendelea kutekeleza miradi muhimu ya maendeleo kupitia *NDC, EPZA, SIDO,*

*CAMARTEC, TEMDO, TIRDO* na kuendeleza majadiliano na washirika wa Maendeleo *(Sector Dialogue)* ambao wanasaidia sekta hii hususan nchi rafiki na taasisi za kimataifa ili kushirikiana na kupata teknolojia inayohitajika kuendeleza sekta hii ya kipaumbele cha Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya mwaka 2013/2014, imelenga kutatua changamoto zilizotajwa, kuongeza ubunifu katika utendaji wetu, kuongeza ushirikiano na sekta binafsi kwa kupitia mfumo wa *PPP*, kutafuta fedha zaidi na hivyo kuendeleza sekta hiyo, ili itoe mchango wake kama inavyotegemewa katika mpango wa miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka 2013/2014, Sekta ya Viwanda ina malengo yafuatayo:-

(i) Kuendelea na utekelezaji wa Mkakati Unganishi wa Uendelezaji Viwanda nchini kwa kuendeleza uhamasishaji wa uwekezaji na kutoa kipaumbele kwa viwanda vinavyoongeza thamani ya mazao ya kilimo;

(ii) Kufuatilia miradi ya *TANCOAL*, Kasi mpya Mchuchuma na Liganga na Umeme wa Upepo (Mkoani Singida) inayoendeshwa kwa ubia kati ya Serikali kupitia *NDC* na Sekta Binafsi. Mradi wa kiwanda cha kuzalisha viuadudu vya mazalia ya mbu waenezao malaria TAMKO, Kibaha;

(iii) Kusimamia utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Kuendeleza Viwanda (*Master Plan);*

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa miradi ya Mchuchuma na Liganga unaoendeshwa kwa ubia kati ya Serikali ya Tanzania na Kampuni ya Sichuang Hongda ya nchini China;

(v) Kuendelea kutoa mafunzo ya kuongeza tija, ufanisi pamoja na ubora wa bidhaa kwa wenye viwanda kupitia program ya Kaizen kwa kushirikiana na Shirika la Misaada la Japan *(JICA)* pamoja na *UNIDO*;

(vi) Kuendelea kushiriki katika uhamasishaji wa utekelezaji wa Mpango Kazi wa Sera ya Viwanda ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na ukamilishaji wa Sera ya Viwanda kwa nchi za *SADC* na kufanya maboresho kulingana na mahitaji ya nchi yetu;

(vii) Kufuatilia ufufuaji wa viwanda vilivyobinafsishwa ambavyo havifanyi kazi, ufufuaji wa *General Tyre* na Urafiki;

(viii) Kukamilisha sheria na kuandaa Kanuni za biashara ya chuma chakavu;

(ix) Kuendeleza utekelezaji wa Mkakati wa Kuendeleza Viwanda vya Ngozi na Bidhaa za Ngozi; na Mkakati wa Viwanda vya nguo na mavazi;.

(x) Kuendelea kuhamasisha, kuhifadhi na kulinda mazingira katika shughuli zote za uzalishaji viwandani;

(xi) Kufuatilia uendelezaji na uwekezaji katika maeneo ya *EPZ* na *SEZ* ikiwemo ulipaji wa fidia kwa maeneo husika; na

(xii) Kufanya tathmini ya maendeleo ya Viwanda ili kubaini changamoto zinazokabili sekta na kuzitafutia Ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka 2013/2014, Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo ina malengo yafuatayo:-

(a) Kupitia na kutathimini utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo na kutoa mapendekezo kwa madhumuni ya kuhuisha;

(b) Kujenga uwezo wa kutoa huduma za ugani katika maeneo walioko wajasiriamali hasa vijijini;

(c) Kuhakikisha teknolojia zinazofaa zinatafutiwa utaratibu wa kuzalishwa kwa wingi na kusambazwa kwa watumiaji;

(d) Kujenga misingi ya kusaidia uzalishaji wa bidhaa mpya kutokana na ubunifu wa wajasiriamali;

(e) Kuhamasisha Halmashauri na kuandaa mwongozo utakaosaidia Halmashauri kutenga maeneo yanayohamasisha sekta kupanuka;

(f) Kuratibu utoaji wa mikopo kupitia Mfuko wa *NEDF*;

(g) Kuwawezesha wajasiriamali kushiriki katika maonesho ya ndani na nje ya nchi; na

(h) Kuwezesha uzalishaji wa zana za kuongeza thamani mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka 2013/2014, Sekta ya Biashara ina malengo yafuatayo:-

(i) Kuendeleza majadiliano kati ya nchi na nchi, Kikanda na Kimataifa kwa lengo la kupanua wigo wa fursa za masoko yenye masharti nafuu na kuvutia wawekezaji;

(ii) Kuendeleza majadiliano ya Mkataba wa Ubia wa Uchumi kati ya Jumuiya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Ulaya *(EAC - EU - EPA Negotiations)* kwa lengo la kupata misaada ya kifedha na kiufundi ambazo zitasaidia kupunguza changamoto za uzalishaji duni;

(iii) Kuendeleza majadiliano ya kuanzishwa kwa Eneo Huru la Biashara la Utatu *(Tripartite Free Trade Area - FTA)* linalojumuisha Kanda za *COMESA - EAC* na *SADC* ili kupanua wigo zaidi wa fursa za masoko ya bidhaa zetu;

(iv) Kuendelea na majadiliano ya kuanzisha Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC Monetary Union)* kwa lengo la kurahisisha biashara;

(v) Kuendelea kuimarisha Kamati ya Kitaifa inayoshughulikia ufuatiliaji, utoaji taarifa na utekelezaji wa mikakati ya kuondoa Vikwazo Visivyo vya Kiushuru (NTBs) kwa lengo la kurahisisha biashara;

(vi) Kuendelea na majadiliano ya kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa *SADC (SADC-Customs Union)* na kulegezeana masharti katika sekta ya Biashara ya Huduma *(Trade in Services Liberalization)* ili kupanua wigo wa Biashara ya bidhaa na huduma;

(vii) Kuimarisha vituo vya biashara vilivyopo London na Dubai ili kuendelea kutangaza masoko ya bidhaa za Tanzania na fursa mbalimbali na kuvutia wawekezaji na watalii nchini;

(viii) Kuanzisha vituo vipya vya biashara kwa kuanzia nchini China na Afrika Kusini na pia kupeleka Waambata wa Biashara nchini Marekani na Ubelgiji kwa lengo la kuitangaza Tanzania na kuunganisha wafanyabiashara wa Tanzania na masoko ya nje;

(ix) Kutekeleza Mkakati wa Kukuza Mauzo Nje ambao umelenga mazao, bidhaa za huduma za kipaumbele zenye fursa na uwezekano wa kuendelezwa kwa haraka na kutoa matokeo ya haraka –*(Quick Wins)* na Mpango Unganishi wa Biashara ya Tanzania.*(Tanzania Trade Integration Strategy-TTIS);*

(x) Kuendelea kushiriki majadiliano ya Duru la Doha kwa lengo la kutetea maslahi ya Tanzania katika majadiliano yanayoendelea;

(xi) Kuhamasisha Jumuiya za Wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla juu ya fursa mbalimbali za masoko ya bidhaa na huduma zitokanazo na majadiliano mbalimbali;

(xii) Kukamilisha zoezi la Mapitio ya Sera ya Taifa ya Biashara ya mwaka 2003; na

(xiii) Kushiriki kikamilifu katika majadiliano kati ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Marekani *(EAC-US Trade and Investment Partnership)* yenye lengo la kukuza biashara na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka 2013/2014, malengo ya Sekta ya Masoko ni yafuatayo:-

(i) Kuendelea kushirikiana na wadau kuendeleza miundombinu ya masoko nchini;

(ii) Kuendelea kushirikiana na wadau katika kuendeleza Vituo vya Ukaguzi wa Pamoja Mipakani *(One Stop Border Post - OSBP) ;*

(iii) Kuimarisha Kamati za Kufanya Kazi Pamoja Mipakani *(Joint Border Committees – JBCs)* ili kuboresha mazingira ya kufanya biashara mipakani;

(iv) Kukamilisha marekebisho ya sheria zinazokinzana na uboreshaji wa mazingira ya biashara;

(v) Kuandaa Sera ya Walaji *(consumer policy);*

(vi) Kushirikiana na wadau kukamilisha maandalizi ya kuanzisha Soko la Mazao na Bidhaa *(Commodity Exchange);*

(vii) Kuendeleza mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani ili uweze kutumika katika uanzishaji wa Soko la Mazao na Bidhaa;

(viii) Kukusanya, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza taarifa za masoko kwa wadau kwa wakati;

(ix) Kuhamasisha matumizi ya fursa za masoko ya mipakani, kikanda na kimataifa; na

(x) Kutangaza bidhaa za Tanzania katika masoko ya ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya *EPZA* kwa mwaka 2013/2014 ni yafuatayo:-

(i) Kukamilisha ulipaji wa fidia katika eneo *EPZ* Bagamoyo;

(ii) Kuanza uendelezaji wa miundombinu ya msingi (barabara, umeme, maji safi na maji taka) pia ujenzi wa Bandari mpya katika eneo la Mbegani kwa kushirikiana na sekta binafsi;

(iii) Kukamilisha mikataba ya ubia na kuanza uendelezaji wa mradi wa *Tanzania China Logistic Centre;*

(iv) Kupima na kufanya tathmini katika maeneo ya *EPZ* Mikoani Arusha na Mwanza na kuandaa *Master Plans* kwa maeneo ya *EPZ/SEZ* ya Mtwara, Mara, Tanga, Songea na Manyara;

(v) Kukamilisha ulipaji fidia katika maeneo ya Ruvuma, Tanga na Kigoma;

(vi) Kuanzisha viwanda vipya vya uzalishaji 35 katika maeneo ya *EPZ* na *SEZ*; na

(vii) Kuanzisha mradi wa uwezeshaji wajasiriamali (EPZ *Incubator*) kwa ajili ya kuwapa uwezo wa kuwekeza kupitia mifumo ya *EPZ* na *SEZ*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* katika mwaka 2013/2014 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuendeleza utekelezaji wa miradi ya makaa ya mawe ya Mchuchuma na chuma cha Liganga;

(ii) Kukamilisha ujenzi wa Kiwanda cha Kuzalisha Viuadudu *(biolarvicides*) vya kuua viluwiluwi wa mbu waenezao malaria katika eneo la *TAMCO*, Kibaha;

(iii) Kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe ya Ngaka Kusini, Songea;

(iv) Kukamilisha upatikanaji wa mkopo wa mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia upepo Singida na kuanza ujenzi;

(v) Kukarabati Kiwanda cha *General Tyre*, Arusha ili kukifufua na kuanza uzalishaji wa matairi;

(vi) Kukamilisha tafiti na kuanzisha kiwanda cha kuzalisha magadi soda eneo la Ziwa Natron na Engaruka, Arusha;

(vii) Kuanzisha viwanda vya kusindika nyama, mpira na mazao mengine ya Kilimo;

(viii) Kuendeleza utekelezaji wa mradi wa Kasi Mpya wa kuzalisha chuma ghafi;

(ix) Kujenga maeneo ya viwanda *(Industrial parks*) sehemu za *TAMCO, KMTC* na Kange;

(x) Kujengea uwezo wananchi wa maeneo husika kufaidi miradi inayotekelezwa na *NDC*; na

(xi) Kuratibu uendelezaji wa kanda za maendeleo za Mtwara, Tanga, Kati na Uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya *CAMARTEC* kwa mwaka 2013/2014 ni yafuatayo:-

(i) Kuunda zana za kilimo hifadhi zitakazotumika kwenye trekta lililoundwa *CAMARTEC*;

(ii) Kukamilisha uundaji wa mashine ya kuvuna, kupura na kupepeta mpunga na kuifanyia majaribio kwenye mikoa ya Kilimanjaro na Mororgoro;

(iii) Kuunda mashine ya kufunga majani kwa ajili ya kuboresha matumizi ya malisho kwa kuongeza muda wa kukaa rafuni;

(iv) Kuendelea kujenga mitambo mikubwa ya biogesi kwa ajili ya kufua umeme kwenye shule na taasisi nchini kwa kuanzia na mikoa ya Manyara, Mara, Kagera na Mwanza;

(v) Kuendeleza uundaji wa mashine kukatakata malisho ya wanyama zinazoendeshwa kwa injini;

(vi) Kueneza vifaa vya matumizi ya nishati ya biogesi (*biogas appliances*) katika maeneo kulikojengwa mitambo ya biogesi ili kuifanya teknolojia hiyo kuwa endelevu;

(vii) Kutoa mafunzo kwa wajasiriamali juu ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na usanifu wa mitambo ya biogesi; na

(viii) Kutoa mafunzo kwa watumiaji wa zana za kilimo ili kuongeza tija katika kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya *TEMDO* kwa mwaka 2013/2014 ni yafuatayo:-

(i) Kutoa huduma ya ushauri wa kihandisi pamoja na mafunzo katika viwanda kumi vya kati na vikubwa kwa lengo la kuongeza uzalishaji, ubora wa bidhaa, faida, kuhifadhi mazingira na matumizi bora ya nishati;

(ii) Kuboresha miundombinu ya kiatamizi na kutoa huduma kwa wajasiriamali watengenezaji wa mashine na vifaa kwa matumizi ya viwanda vya kati *(machinery and equipment for light industries*). Lengo ni

kuwezesha wajasiriamali wawili kufikia uwezo wa kuendesha viwanda vya kati;

(iii) Kubuni, kuendeleza na kuhamasisha utengenezaji wa mtambo mdogo wa kuzalisha umeme kutokana na nguvu ya maji *(Mini Hydro Power Plant)* kwa matumizi ya uzalishaji wa umeme vijijini pamoja na mtambo mdogo wa kurejesha maji *(Small Scale Water Recycling Plant)* mijini;

(iv) Kuendeleza na kuboresha chasili *(prototype development*) cha mtambo wa kurejesha taka za plastiki na mtambo wa kuzalisha umeme kutokana na mabaki ya mimea *(generation of electricity from biomass and municipal solid wastes);* na

(v) Kuendelea na maboresho pamoja na uhawilishaji wa teknolojia mbalimbali ikiwa ni pamoja na teknolojia ya kuteketeza taka za hospitali (bio-medical waste incineration), teknolojia ya machinjio na kuongeza thamani katika mabaki ya mazao ya mifugo na teknolojia ya vifaa vya hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya *TIRDO* kwa mwaka 2013/2014 ni ifuatavyo:-

(i) Kufanya tafiti zenye lengo la kupata teknolojia za kuongeza thamani kwenye mazao ya kilimo *(Value addition on Agro products);*

(ii) Kutoa huduma za kitaalam viwandani zenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora bila kuchafua mazingira pia zinazolenga matumizi bora ya nishati;

(iii) Kuendelea kutekeleza mkakati wa kuimarisha sekta ya ngozi na viwanda vya ngozi ili kupunguza uharibifu wa mazingira kwa kurejesha taka za ngozi ili kutengeneza bidhaa kama *Leather Boards*;

(iv) Kukamilisha mchakato wa kuhakiki *(Accreditation)* na kuboresha maabara ya mazingira na ya vifaa vya kihandisi ili ziweze kufikia viwango vya kimataifa na kuweza kutoa huduma bora kwa wazalishaji viwandani;

(v) Kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji wa mazao *(traceability)* kwa kutumia teknohama na pia kusaidia utendaji wa kampuni *ya GS1 (Tz) National Ltd*. kama mshauri wa kiufundi;

(vi) Kutoa huduma za kitaalam kwa wawekezaji wanaotaka kuanzisha viwanda vikubwa na vidogo katika sekta ya uzalishaji bidhaa zitokanazo na mazao ya kilimo *(agro-processing, industries)* kupitia benki ya rasilimali *(TIB);*

(vii) Kujenga tovuti ili kusaidia wazalishaji wadogo na kati kutangaza bidhaa zao waweze kupata masoko ya ndani na nje ya nchi;

(viii) Kuendelea kukusanya maoni ya wadau kuhusu kurejea Sheria ya Bunge Na. 5 ya mwaka 1979 iliyoanzisha *TIRDO* ili Shirika liweze kufanya utafiti kuendana na mabadiliko yanayoendelea duniani; na

(ix) Kukamilisha mchakato wa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya *TIRDO (land use Plan)* ili kuzuia uvamizi na kuainisha matumizi yanayolenga kuleta tija kwa shirika na viwanda kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya Shirika la Viwango kwa mwaka 2013/2014 ni yafuatayo:-

(i) Kuendeleza utekelezaji wa utaratibu wa kupima ubora wa bidhaa zote mahali zinapotoka kabla ya kuingia nchini *(Preshipment Verification of Conformity to Standards – PVoC);*

(ii) Kuendelea kuimarisha utaratibu wa kukagua ubora wa bidhaa zilizo sokoni ukiwemo ukaguzi wa magari kabla ya kuingia nchini;

(iii) Kuendeleza juhudi za kutoa elimu na kuhakikisha kwamba maabara zote za Shirika zinapata vyeti vya umahiri *(laboratory accreditation)* ili kuwezesha kukubalika kwa bidhaa nyingi zaidi za Tanzania katika soko la ndani na nje;

(iv) Kushirikiana kwa karibu na vyombo vingine vya Serikali kama Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA),* Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania *(TFDA),* Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji *(EWURA),* Tume ya Ushindani Halali *(FCC),* Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)* ili kuhakikisha kuwa bidhaa zinazoingia nchini ni zenye ubora unaokubalika;

(v) Kuongeza idadi ya leseni kutoka leseni 120 kwa mwaka kufikia leseni 150 katika mwaka 2012/2013;

(vi) Kuongezeka idadi ya upimaji sampuli kutoka 9,300 kwa mwaka hadi kufikia 10,900 katika mwaka 2012/ 2013;

(vii) Kutayarisha viwango vya taifa vinavyofikia 150 vikiwemo viwango vya sekta ya huduma katika mwaka 2012/ 2013; na

(viii) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali nchini kote kuhusu viwango vya udhibiti wa ubora wa bidhaa na kuongeza vyeti vya ubora wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014, Baraza la Ushindani litatekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kusikiliza kesi za rufaa zinazotokana na mchakato wa Udhibiti na ushindani wa Biashara kwenye soko;

(ii) Kujenga uwezo zaidi wa Baraza katika kushugulikia kesi hizo kwa kuimarisha rasilimali watu na Wajumbe wa Baraza;

(iii) Kutoa elimu kwa umma juu ya kazi za Baraza na umuhimu wake katika uchumi; na

(iv) Kuanza taratibu za kununua kiwanja kwa ajili ya ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Baraza kwa kuwa kwa sasa Baraza lipo kwenye jengo la kupanga (Ubungo Plaza).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA).* Malengo ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni kwa mwaka 2013/2014 ni yafuatayo:-

(i) Kuendelea na maandalizi ya utaratibu wa kuweka mifumo ya kiteknolojia itakayowawezesha wadau kupata taarifa na huduma kwenye mifumo ya kompyuta *(On line registration systems)* kwa wakati;

(ii) Kuboresha usajili wa makampuni na majina ya biashara kwa kutumia mfumo na mashine za kisasa *'special machine readable certificates';*

(iii) Kufanya marejeo ya sheria zinazosimamiwa na Wakala ili ziweze kwenda na wakati;

(iv) Kuboresha mifumo ya uwekaji na utunzaji wa Masijala tano za kisheria zinazosimamiwa na Wakala ili kuweza kushabihiana na mifumo ya kitekinolojia na hatimaye kurahisisha utoaji huduma;

(v) Kuendelea kuelimisha umma kuhusu shughuli za Wakala na umuhimu wa kusajili biashara;

(vi) Kuendeleza watumishi na kuwawekea mazingira mazuri ya utendaji kazi ili kuongeza tija na uwajibikaji;

(vii) Kuendeleza mahusiano na mashirika ya kimataifa ambayo Tanzania ni Mwanachama;

(viii) Kuanza kwa ujenzi wa Jengo la *BRELA* kwa ajili ya Ofisi na Masijala;

(ix) Kutoa huduma za usajili kwa wateja wa *BRELA* kwa mtindo wa papo kwa papo katika maonesho mbalimbali kama Sabasaba, Nanenane, Wiki ya Utumishi wa Umma, makongamano na katika warsha zinazoandaliwa na Wakala au Wadau wengine kama *SIDO*, MKURABITA na wengineo fursa zinapotokea; na

(x) Kuendeleza na kuimarisha mahusiano mazuri na ushirikiano na taasisi mbalimbali za ndani ya nchi katika kufanikisha shughuli za Wakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka wa 2013/2014, Tume ya Ushindani *(FCC)* imepanga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kudhibiti na kupambana na uingizaji na uzalishaji wa bidhaa bandia;

(ii) Uchunguzi na usikilizaji wa kesi za ushindani;

(iii) Utafiti wa masoko ili kubaini matatizo ya ushindani usio wa haki wa masoko husika na hatua za kurekebisha; na

(iv) Kumlinda na kumwelimisha mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika kipindi cha mwaka 2013/2014, Baraza la Taifa la Utetezi wa Mlaji litatekeleza yafuatayo:-

(i) Kusimamia maslahi ya mlaji kwa kupeleka maoni yake kwenye Tume ya Ushindani, Mamlaka za Udhibiti na Serikali kwa ujumla;

(ii) Kuendelea kupokea na kusambaza taarifa na maoni yenye maslahi kwa mlaji; na

(iii) Kuanzisha Kamati za Mlaji za Mikoa na Sekta na kushauriana na Kamati hizo; wenye viwanda, Serikali na jumuiya nyingine za walaji katika mambo yenye maslahi kwa mlaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka 2013/2014, Bodi ya Leseni ya Maghala *(TWLB)* itatekeleza yafuatayo:-

(i) Kusimamia utekelezaji wa Mfumo wa Stakabadhi za Maghala katika maeneo yote yanayotekeleza mfumo huo hapa nchini;

(ii) Kutoa elimu ya Mfumo kwa wadau hususani wakulima waishio vijijini;

(iii) Kujenga uwezo kwa wakulima na wadau wengine wa mfumo kwa kuwapa mafunzo ya mfumo wa Stakabadhi za mazao ghalani;

(iv) Kuratibu shughuli za wadau wa Mfumo wa Stakabadhi za maghala;

(v) Kuwaunganisha wakulima na taasisi za fedha kupitia Vikundi na Vyama vya Ushirika ili waweze kujipatia mikopo; na

(vi) Kuiwakilisha Serikali kwenye mikutano na makongamano ya kitaifa na kimataifa yanayojadili maswala yanayohusiana na mfumo wa stakabadhi za maghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo. Malengo ya *SIDO* kwa mwaka 2013/2014 ni yafuatayo:-

(i) Kuimarisha uwezo wa kuzalisha na kusambaza mashine ndogo ndogo za kusindika mazao;

(ii) Kuwezesha usambazaji wa teknolojia vijijini kwa kupitia programu ya Wilaya Moja bidhaa Moja *(ODOP);*

(iii) Kusaidia uanzishwaji wa kongano za viwanda vidogo vya kusindika alizeti;

(iv) Kusaidia shughuli za ubunifu na utengenezaji wa bidhaa mpya kupitia programu ya kiatamizi;

(v) Kujenga chumba cha kufundishia cha Kituo cha mafunzo ya ngozi cha Dodoma;

(vi) Kuanzisha vituo vidogo vya kuuzia bidhaa za wajasiriamali hasa mazao ya shamba katika barabara kuu;

(vii) Kuhakikisha upatikanaji wa vifungashio kwa bidhaa za wajasiriamali wadogo;

(viii) Kuhawilisha teknolojia zilizobuniwa na kujaribiwa ili ziweze kupatikana kwa wingi na kutumika kuzalishia mali;

(ix) Kutoa elimu ya ujasiriamali, uongozi wa biashara, usindikaji wa vyakula na kuzingatia ubora wa bidhaa;

(x) Kujenga Ofisi ya *SIDO* ya Mkoa wa Pwani;

(xi) Kuwezesha vyuo vya mafunzo na uzalishaji vya *SIDO* kufanya kazi;

(xii) Kuchangia kukamilisha ujenzi wa vituo vya mafunzo na uzalishaji wa vyakula vya Morogoro na Dar es Salaam;

(xiii) Kuwezesha wazalishaji wadogo kupata masoko ya bidhaa na huduma zao, kwa kutengeneza miundombinu ya kupokea na kusambazia habari za kibiashara, kutengeneza sehemu ya kuonyeshea bidhaa za wazalishaji wadogo; na

(xiv) Kutoa huduma za kifedha ikiwa ni pamoja na ushauri na mikopo pale itakapojidhihirisha kuhitajika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Hakimiliki Tanzania *(COSOTA);* malengo ya *COSOTA* kwa mwaka 2013/ 2014 ni yafuatayo:-

(i) Kufungua Ofisi ya Kanda ya Hakimiliki mjini Arusha kwa ajili ya Kanda ya Kaskazini na mjini Dodoma kwa ajili ya Kanda ya Kati na Magharibi;

(ii) Kukamilisha marejeo ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki ya mwaka 1999;

(iii) Kuanza utaratibu wa kusambaza stika (Hakigram) wasambaziji wote wa kazi za muziki na filamu;

(iv) Kuhamasisha wanunuzi wa *CD*, kanda za miziki na filamu kununua kanda na *CD* zenye Hakigram; na

(v) Kuingia mkataba na makampuni binafsi kwa lengo la kukusanya mirabaha na kufanya operesheni dhidi ya kazi bandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2013/2014, Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* kinalenga kutekeleza yafuatayo:-

(i) Kuimarisha mafunzo yenye mwelekeo wa kiutendaji katika nyanja za biashara yaani: Menejimenti ya Ununuzi na Ugavi, Utawala na Uongozi wa Biashara, Uhasibu, Menejimenti ya Masoko, Taaluma ya Mizani na Vipimo, Taaluma ya Habari na Mawasiliano na Taaluma nyingine zinazohusiana na hizo katika ngazi za astashahada, stashahada, shahada na stashahada ya uzamili;

(ii) Kuandaa mitaala mipya ya shahada ya kwanza katika Ujasiriamali, Menejimenti ya Rasilimali Watu na Elimu ya Biashara. Vile vile Chuo kitaandaa mitaala ya shahada ya uzamili;

(iii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wajasiriamali wadogo wadogo na wakati ili kuwasadia wafanye biashara zao kwa ustawi mkubwa zaidi;

(iv) Kufanya utafiti na kutoa machapisho;

(v) Kuandaa mpango kabambe wa Chuo *(Master Plan)* katika Kampasi zake tatu yaani: Dar es Salaam,Dodoma na Mwanza;

(vi) Kununua ardhi ekari 500 kwa ajili ya upanuzi wa shughuli za kampasi ya Dar es Salaam; na

(vii) Kukarabati majengo ya Chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TanTrade)* kwa mwaka 2013/2014 ni yafuatayo:-

(i) Kuwajengea uwezo wajasiriamali ili waweze kuzijua fursa na changamoto za masoko ya ndani na nje na jinsi ya kuzimudu;

(ii) Kuwawezesha wanawake wafanyabiashra kwenye sekta isiyo rasmi katika mipaka ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki, ambayo ni mipaka ya Kabanga, Mutukula, Sirari na Namanga;

(iii) Kukuza Biashara na Kutafuta Masoko ya Ndani kwa kuratibu Maonesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam *(DITF,2013);*

(iv) Kutafuta masoko ya nje kwa kuratibu maonesho ya Biashara ya Kimataifa ya nchi za nje;

(v) Kuwaunganisha wafanyabiashara na wadau wengine na fursa mbalimbali zikiwemo masoko ya ndani na nje ya nchi, kuwapa uelewa wa mwenendo wa bei za bidhaa kitaifa na kimataifa;

(vi) Kuendeleza soko la ndani kwa Kusisimua maendeleo ya biashara katika Sekta muhimu za kiuchumi;

(vii) Kutoa huduma ya taarifa za kibiashara;

(viii) Kushiriki katika kuboresha mfumo na sera za biashara; na

(ix) Kuimarisha Ofisi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya Wakala wa Vipimo (WMA) kwa mwaka 2013/2014 ni yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuimarisha usimamizi wa matumizi ya vipimo vilivyo sahihi nchini kupitia uimarishwaji wa uhakiki na ukaguzi wa vipimo hivyo kwa lengo kuu la kumlinda mlaji;

(ii) Kuendelea kuongeza mbinu za utoaji wa elimu ya matumizi ya vipimo hivyo kwa umma ili kuongeza uelewa wa matumizi yake na ufungashaji wa bidhaa kwa kiasi sahihi ili mnunuzi aweze kupata bidhaa hiyo kulingana na thamani ya fedha yake;

(iii) Kuendelea kuimarisha Kitengo cha Vipimo Bandarini *(WMA Ports Unit)* chenye jukumu la kusimamia, kuhakiki na kukagua usahihi wa vipimo vitumikavyo kupimia kiasi cha mafuta yaingiayo hapa nchini ili kiweze kutoa huduma hiyo kwa ufanisi;

(iv) Kukamilisha kazi ya utafiti na uchambuzi wa mfumo wa vipimo vitumikavyo katika usambazaji wa gesi asilia *(Natural Gas)* ilikuweza kukamilisha zoezi la utengenezaji wa kanuni za gesi hiyo itakayokidhi usimamizi wa matumizi sahihi ya vipimo hivyo;

(v) Kuendelea na zoezi la kuandaa kanuni mpya ya ufungashaji wa gesi kwenye mitungi itokanayo na mafuta ya petroli *(LPG)* kwa kuwashirikisha zaidi wadau ili kuwezesha usimamizi wa usahihi wa kiasi cha gesi inayowekwa kwenye mitungi hiyo;

(vi) Kuendelea na kazi ya ujenzi wa kituo cha kupimia magari yanayosafirisha mafuta katika eneo la Misugusugu, pwani, kituo cha Mwanza na Iringa;

(vii) Kuendelea na taratibu za kukamilisha utungaji wa Sheria mpya ya Vipimo *(Legal Metrology Act)* ili kukidhi matakwa ya sasa ya biashara na pia kuzingatia maridhiano yaliyofikiwa na nchi kikanda na kimataifa kuhusu masuala ya vipimo; na

(viii) Kuendelea kuboresha mazingira ya kazi kwa kuongeza vitendea kazi ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kitaalam na vyombo vya usafiri imara na vya kutosha kwa ofisi zote ili kuhakikisha huduma za Wakala zinazowafikia walaji/wadau wengi zaidi, kwa haraka na ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya Kituo cha Biashara cha Tanzania Dubai-*(TTC-Dubai)* Kwa mwaka 2013/ 2014 ni yafuatayo:-

(i) Kuongeza msukumo kwenye kuongeza mauzo ya nyama ya mbuzi na kondoo hususan baada ya kukamilika kwa ujenzi wa machinjio ya Ruvu na ya mwekezaji binafsi mkoani Kagera na bidhaa za majini *(sea food)*, kwa kusaidia Makampuni ya sekta hiyo kushiriki katika maonesho maalum yatakayofanyika Dubai mwezi Novemba, 2013;

(ii) Kuandaa kongamano la uwekezaji kwenye Sekta ya Ngozi nchini India kwa nia ya kupata wawekezaji toka India kuwekeza kwenye usindikaji na kuongeza thamani mazao ya sekta ya ngozi;

(iii) Kutoa msukumo wa kutangaza fursa za uwekezaji kwenye sekta ya *Real Estate Development* hususan katika mji mpya wa Kigamboni; na Maeneo ya *Special Economic Zone – SEZ* ya Bagamoyo; na.

(iv) Kufuatilia mapendekezo yaliyotolewa na kituo kuhusu juhudi zinazohitajika kuwekwa ili kuongeza mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenye soko la Dubai hususan kwa

mazao kama mananasi, kakao, viungo, korosho na maparachichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malengo ya Kituo cha Biashara cha Tanzania London - *(TTC-London)* kwa mwaka 2013/2014 ni yafuatayo:-

(i) Kukuza biashara kwa kushiriki katika maadhimisho ya miaka 50 ya Shirika la Kimataifa la kahawa *(ICO)* yatakayofanyika nchini Brazil mwezi wa Septemba, 2013;

(ii) Kuandaa Mkutano kwa kushirikiana na Ubalozi na wadau wengine kuhusu Kuvutia uwekezaji katika sekta mbalimbali hasa katika kilimo, miundombinu na huduma;

(iii) Kutangaza vivutio vya Utalii vya Tanzania kupitia maonyesho mbalimbali ya utalii yatakayofanyika katika miji mikubwa ya Uingereza; na

(iv) Kukuza Diplomasia ya Uchumi kwa kushiriki katika shughuli za mashirika ya Kimataifa ili kubaini fursa za kibiashara na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na maendeleo ya rasilimali watu, kwa mwaka 2013/2014, Wizara inatarajia kuajiri watumishi wapya 72, kupandisha vyeo watumishi 61, kuthibitisha kazini watumishi 11 na kuwapeleka mafunzo ya muda mfupi na mrefu watumishi 70. Aidha, Wizara itaendelea kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na UKIMWI/VVU waliojitokeza kwa mujibu wa Waraka Namba Moja wa mwaka 2004, kutoka Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masuala mtambuka; Wizara itaendelea na jitihada za kupambana na kudhibiti rushwa kwa watumishi wake kwa kutoa mafunzo ya Sheria mbalimbali za kazi zikiwemo Sheria Na. 8 ya mwaka 2002 Utumishi wa Umma, Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sheria ya

Fedha ili kuwawezesha kufanya kazi na kutoa maamuzi kwa kuzingatia matakwa ya sheria husika. Ili kuweza kutoa huduma bora zinazokidhi viwango vilivyoainishwa katika Mkataba wa Huduma kwa Mteja, Wizara itaendesha mafunzo ya elimu ya huduma kwa mteja kwa watumishi 50 ili kuwapatia mbinu mbalimbali za kuhudumia wateja.

Vilevile, Wizara inatarajia kuimarisha dawati la kushughulikia malalamiko ya Sekta ya Viwanda na Biashara ili kuweza kutatua kero mbalimbali za wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa mwaka 2013/2014, Wizara itaendelea na jitihada za kuwawezesha watumishi waliojitokeza na watakaojitokeza wanaoishi na virusi vya UKIMWI kupata huduma ya virutubisho, lishe na usafiri. Pia, Wizara itaendelea kutoa mafunzo ya kujikinga na maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI na kuhamasisha upimaji wa afya za wafanyakazi kwa hiari.

Aidha, waelimishaji rika watapewa mafunzo ili kuwawezesha kupata mbinu mpya ambazo zitawawezesha kuwaelimisha watumishi wenzao na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia, inatarajia kuendelea na kutoa huduma kwa Watumishi na wanaoishi na virusi vya UKIMWI waliojitokeza ili kuweza kutoa mchango wao kwa Wizara na Taifa kwa ujumla; kuajiri watumishi wapya 72; kupandisha vyeo watumishi 61; kuthibitisha kazini watumishi 11 na kuwapeleka mafunzo ya muda mfupi na mrefu watumishi 70.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na *NEMC* na wadau mbalimbali itaendelea kutekeleza mikakati inayohusu utunzaji wa mazingira pamoja na programu ya utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi na Utunzaji wa Mazingira. Wizara itahamasisha miradi mipya itakayoanzishwa kutimiza masharti ya uzalishaji salama Viwandani na kuhimiza miradi ya zamani ambayo haikuwa na mifumo salama kwa mazingira ijenge mifumo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara itaendelea kuzingatia masuala ya jinsia katika kupanga na kutekeleza sera, mikakati na mipango mbalimbali ya kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani. Naomba uniruhusu kuwashukuru kwa dhati nchi rafiki na Mashirika ya Kimataifa ambayo yamekuwa yakitoa na yanaendelea kutoa misaada mbalimbali kusaidia Sekta ya Viwanda na Biashara. Misaada na michango hiyo imekuwa chachu na nyenzo muhimu kwa Wizara yangu kuweza kutekeleza majukumu yake. Nchi rafiki ni pamoja na Austria, Canada, China, Denmark, Finland, India, Ireland, Japan, Korea ya Kusini, Marekani, Norway, Sweden, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani na Uswisi. Mashirika ya Kimataifa ni pamoja na: Benki ya Dunia, *DANIDA, CFC, ARIPO, DFID, EU, FAO, IFAD, JICA*, Jumuiya ya Madola, *KOICA*, Sida, *UNCTAD, UNDP, UNIDO, USAID, WTO* na *WIPO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maombi ya Fedha Katika Mwaka 2013/2014. Katika mwaka 2013/2014, Wizara inatarajia kukusanya Shilingi 40,330,000 kutokana na uuzaji wa nyaraka za tenda, faini kwa kukiuka sheria ya leseni, pamoja na makusanyo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katika mwaka wa 2013/2014, Wizara ya Viwanda na Biashara na Taasisi zilizo chini yake inaomba kutengewa jumla ya Sh. 78,502,631,820/= kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya kuiendeleza Sekta ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo. Kati ya fedha hizo, Sh. 29,665,989,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kiasi cha Sh. 48,836,642,820/= zimeombwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matumizi ya Kawaida. Katika fedha za matumizi ya kawaida ya Sh. 29,665,989,000/=, Sh. 22,225,249,000/= zimetengwa kwa ajili ya mishahara *(PE)* na Sh. 7,440,740,000/= zimetengwa kwa ajili ya Matumizi Mengine *(OC).* Aidha, kati ya Fedha za mishahara *(PE),* Sh. 2,296,161,000/= zimetengwa kwa ajili ya mishahara ya Wizara na Sh.19,929,088,000/= zimetengwa kwa ajili ya mishahara ya Taasisi.

Vilevile, katika Sh. 7,440,740,000 zilizotengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, Sh. 5,976,859,000/= zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya Wizara na kiasi cha Sh. 1,463,881,000/= zimetengwa kwa ajili ya Taasisi zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sh. 48,836,642,820/= zilizotengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo, Sh. 42,100,000,000/= ni fedha za ndani na Sh. 6,736,642,820/= ni fedha za nje zitakazotokana na Washirika wa Maendeleo. Aidha, katika fedha za ndani zilizotengwa, Sh. 40,900,000,000/= ni mahsusi kwa maeneo ya kimkakati inayohusu maendeleo ya miradi chini ya *EPZA* (*SEZ* Bagamoyo na Tanzania – *China Logistic Centre*); *NDC* (Liganga, Mchuchuma, Mradi wa kuzalisha viuadudu vya kuua viluwiluwi wa mbu waenezao malaria - Kibaha*, General Tyre (EA) Ltd,* Mradi wa Magadi Soda wa Ziwa Natron/Engaruka, Mradi wa Kufua Umeme kwa Upepo - Singida) na *SIDO (SMES Industrial Infrastructure Expansion & Capacity Building).* Pia Sh. 1,200,000,000/= ni kugharamia miradi na mipango mingine muhimu ya maendeleo kwa Wizara na Taasisi nyingine 15 zilizo chini ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sh. 6,736,642,820/= fedha za nje za maendeleo zitakazotokana na Washirika wa Maendeleo, Sh. 3,024,594,076/= ni za mradi wa MUVI utakaogharimia kuboresha mlolongo wa thamani kwa mazao yaliyochaguliwa na Mkoa husika, upatikanaji wa mbegu bora na masoko. Sh. 547,581,904/= ni za mradi wa *ASDP* zitagharimia kuimarisha Mfumo wa Taarifa za Masoko, kuboresha na kukamilisha Mkakati wa kukuza mfumo wa Stakabadhi za Mazao Ghalani, kuanzisha Soko la Mazao na Bidhaa nchini *(Commodity Exchange);* Kuratibu, kufuatilia na kutathmini uendelezaji wa miundombinu ya usindikaji ili kuongeza thamani mazao ya kilimo - Tanzania Bara na Kuendelea kushirikiana na wadau kuendeleza miundombinu ya masoko nchini.

Aidha Sh. 1,583,000,000/= za mradi wa *Support for Trade Mainstreaming* zitatumika kujenga uwezo wa Taasisi

mbalimbali zinazochangia kuendeleza biashara kwa kutoa mafunzo kwa wataalam wa Taasisi.

Pia mradi wa *Support for Gender Mainstreaming in Trade Sector na Micro and Small Enterprise Development Strategy* wenye Sh. 337,179,000/= zitatumika kufanya uchambuzi wa sera za Sekta ya Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo kwa lengo la kuhusisha masuala ya jinsia katika sera na mikakati ya Wizara. Sh. 816,100,000/= za mradi wa *Integrated Industrial Development Programme* ni za kutekeleza Programu za *UNIDO* zinazojumuisha Mradi wa *Accelerated Agribusiness and Agro-processing Development Initiative (3ADI)* unaolenga uongezaji thamani mazao ya kilimo na *Industrial Upgrading and Modernisation* ambao unalenga kuboresha ufanisi wa viwanda hasa viwanda vidogo na vya kati ambavyo vinahitaji msaada kidogo ili kuzalisha bidhaa zenye ubora na zinazoweza kuingia katika masoko ya nje. Sh. 428,187,840/= ni za mradi wa *Strenthening TWLB Capacity for efficiency in Warehouse Receipt System (WRS) service provision in Tanzania* zitagharimia kuimarisha uwezo wa *TWLB* ili kuleta ufanisi kwa kutoa mafunzo, kununua vifaa, kuimarisha ukaguzi, na kuandaa *database* ya mazao yanayohifadhiwa ghalani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kukushukuru tena wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Wizara www.mit.go.tz. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kusoma kwa umakini sana. Sasa namwita Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Mgimwa.

**MHE. MAHMOUD H. MGIMWA – MWENYEKITI KAMATI YA UCHUMI, VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44) kwa Mwaka 2012/2013 na Makadirio ya Bajeti ya Mwaka 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipata fursa ya kupitia majukumu, mafanikio na changamoto za utekelezaji wa shughuli za Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na kupokea Taarifa kuhusu Utekelezaji wa Shughuli za Uendelezaji wa Sekta Viwanda, Sekta ya Viwanda vidogo na Biashara ndogo, Sekta ya Masoko na Sekta ya Biashara. Kamati ilijadili taarifa hizo kwa kina ikiwemo ile ya Makadirio ya Bajeti ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2013/2014 na hatimaye kuishauri Wizara hiyo ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo changamoto mbalimbali, Kamati inaridhishwa na mafanikio yanayopatikana katika sekta hizi kwa kutumia rasilimali ndogo za Serikali na kupanga vipaumbele ndani ya vipaumbele ili kuleta matokeo ya haraka yanayokusudiwa ya kisekta. Aidha, mafanikio yaliyopatikana yanatokana na kuzingatia na kutekeleza maagizo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda imeweza kuongeza uzalishaji wa bidhaa viwandani ambao umechangia ukuaji wa Sekta ya Viwanda kufikia asilimia 9.9 mwaka 2008, kutoka asilimia 8.5 mwaka 2006 na katika mwaka 2011 sekta hii imechangia asilimia 7.8. Katika mwaka 2012 uzalishaji viwandani umeendelea kuimarika na hivyo kuchangia ukuaji wa asilimia 8.2. Aidha, mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa nao umeendelea kuongezeka kutoka asilimia 8.9 mwaka 2005 na kufikia asilimia 9.4 mwaka 2008 na mwaka 2011 ulikuwa asilimia 9.74. Mwaka 2012 sekta hii imechangia asilimia 9.85 kwenye Pato la Taifa, bado ongezeko hili lipo chini ya malengo

tuliyojiwekea la asilimia 15 lililoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo zimetoa mchango mkubwa katika ajira takribani 5,000,000 sawa na asilimia 23.4. Sekta hii imechangia asiliamia 27.9 kwenye pato la Taifa. Aidha, mchango katika Sekta ya Biashara ulikua kwa asilimia 8.1 mwaka 2011 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 8.2 kwa mwaka 2010. Katika kipindi cha mwaka 2012 sekta hii imekua kwa asilimia 7.7. Kwa upande wa Pato la Taifa sekta hii ilichangia asilimia 12.2 mwaka 2011 ikilinganishwa na asilimia 12.1 mwaka 2010. Kwa mwaka 2012 imechangia asilimia 12.3. Ongezeko la ukuaji na uchangiaji huu umetokana na kuongezeka kwa fursa mbalimbali za masoko kwa bidhaa na uboreshaji wa mazingira ya kibiashara katika masoko ya ndani na nje ya nchi, yaani *EAC, SADC, EU,* Asia, Marekani na mashariki ya mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Sekta ya Masoko, kumekuwa na ongezeko la bei ya mazao makuu ya chakula hali inayopelekea kuwepo na mfumuko wa bei mara kwa mara. Hata hivyo, Serikali imeendelea na jitihada ya kukabiliana na tatizo hili pamoja na kujenga masoko yanayokidhi viwango vya kimataifa katika maeneo mbalimbali nchini. Pia uanzishwaji wa mfumo wa stakabadhi za mazao ghalani kumesaidia wakulima kuwa na uhakika wa bei za mazao wanayoyalima. Hata hivyo, utekelezaji wa mfumo huu unahitaji usimamizi wa karibu kuhakikisha wakulima wote wanafaidika na mfumo huu, hivyo Kamati inaiagiza Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika kuhakikisha inafanyia marekebisho Sheria ya Stakabadhi Ghalani na kuileta Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika Sekta ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2012/2013, takwimu zinaonyesha kuwa, Serikali ilitenga kiasi cha Shilingi bilioni 52.0 kwa ajili ya Mradi wa Mchuchuma na Liganga lengo ikiwa ni kuimarisha barabara za Itoni – Mkiu - Mchuchuma na Mkiu - Liganga

pamoja na kuongeza ujuzi wa wataalam. Hata hivyo, utekelezaji wake upo kwenye ngazi ya upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mradi wa Kiwanda cha Viuadudu - Kibaha, Pwani, Serikali ilitenga kiasi cha Shilingi bilioni 3.26 kwa ajili ya malipo ya Mhandisi Mshauri, kutoa mafunzo kwa wataalam, ujenzi wa mfumo wa maji safi na majitaka na usanifu wa kituo cha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa eneo la *TAMCO* – Kibaha limekusudiwa kuwa eneo la viwanda vidogo na kati. Serikali imeweza kukamilisha michoro ya eneo, upimaji wa viwanja na usanifu wa miundombinu ya barabara, maji safi na taka. Hata hivyo, mpaka sasa bado miundombinu hususan barabara za uhakika kwa ajili ya wawekezaji hazijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huu kwa upande wa majengo ya kiwanda na usanifu wa mitambo umekamilika. Kwa upande wa mradi wa Magadi Soda- Bonde la Engaruka, Serikali ilitenga kiasi cha Shilingi milioni 700 kwa ajili ya upembuzi akinifu na kuchimba visima12. Hata hivyo, mpaka sasa utafiti wa uwingi wa magadi umekamilika na bado inaendelea kutafuta taarifa za uwekezaji kwenye mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kuwa Serikali ilitenga kiasi cha Shilingi bilioni 50.2 kwa ajili ya kukamilisha ulipaji wa fidia katika maeneo maalum ya uwekezaji- *Export Processing Zones (EPZ)* kwa Bagamoyo na Kigoma ingawa tathmini ya fidia inaonyesha kuwa eneo la Bagamoyo thamani yake ni Shilingi bilioni 58.8 na eneo la Kigoma thamani yake ni Shilingi bilioni 2.8. Kwa upande wa utekelezaji kiasi cha Shilingi bilioni 16.9 zimelipwa kwa eneo la Bagamoyo, yaani hekta 1,600 kati ya hekta 5,700. Kwa upande wa eneo la Kigoma kwa mwaka huu wa fedha hakuna malipo yoyote yaliyofanyika hadi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuwa mstari wa mbele katika kuandaa na kusimamia miradi ya

Maendeleo kama ilivyoainishwa kwenye Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kila mwaka, Kamati inashangazwa na utekelezaji wa kusuasua wa miradi hii ya kimkakati ambayo ni kipaumbele cha Serikali katika kukuza uchumi wa nchi. Kiasi cha fedha kilichopokelewa kwenye miradi hii mpaka sasa ni kidogo mno na hivyo hakitoi taswira halisi ya uwajibikaji wa Serikali kama kweli ni Mipango ya Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa Malengo ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kipindi cha mwaka 2012/2013, Kamati ilielezwa kuwa kwa upande wa mafanikio, Wizara imeweza kutekeleza mambo ya msingi yafuatayo:-

(i) Wizara imeweza kusimamia na kuratibu Sekta ya Viwanda na hivyo kuendelea kuongeza uzalishaji wa bidhaa viwandani na kukua kwa asilimia 8.2. Mfano, usindikaji wa ngozi umeongezeka kutoka futi za mraba 6,038,00 mwaka 2005 hadi futi za mraba 37,305,215 mwaka 2009 kwa kiwango cha *wet-blue*; kuna viwanda vya nguo 22 hadi sasa ikilinganishwa na viwanda 17 vilivyokuwepo mwaka 2006; viwanda vya bidhaa na ujenzi vimeongezeka vikiwemo vile vya chuma, cement, vinywaji na chakula, maziwa na viwanda vya madawa ya binadamu;

(ii) Imeendelea kufufua na kuendeleza viwanda vilivyobinafsishwa, kuanzisha viwanda vipya pamoja na uendelezaji wa viwanda katika maeneo maalum ya *EPZ*;

(iii) Wizara kupitia Mamlaka ya Maeneo Maalum ya Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje *(EPZA)* na Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* imeendelea kutenga maeneo maalum ya uwekezaji katika Mikoa yote nchini;

(iv) Sekta ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo imeendelea kukua na kuchangia kiasi cha asilimia 27.9 katika pato la Taifa na kuajiri kiasi cha Watanzania milioni 5.2 ikihusisha wajasiamali milioni tatu;

(v) Thamani ya mauzo ya bidhaa za nje iliongezeka hadi Dola za Kimarekani milioni 5,098.8 mwaka 2011 ikilinganishwa na Dola milioni 4,323.1 mwaka 2010;

(vi) Wizara imeendelea kuboresha Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani na hivyo kuongeza ushindani wa manunuzi ya mazao na hatimaye kuongeza bei ya mazao ya mkulima;

(vii) Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta kufanikisha ujenzi wa masoko na miundombinu ikiwemo yale masoko ya mipakani;

(viii) Wizara kwa kushirikiana na *TIRDO*, imewezesha sekta binafsi kutumia mfumo wa utambuzi wa bidhaa kwa kutumia nembo za mistari *(Bar Code);* na

(ix) Imeendelea kuboresha mazingira ya kufanya biashara ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilielezwa kuwa pamoja na baadhi ya mafanikio haya, bado Wizara inakabiliwa na changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa majukumu yake:-

(i) Upungufu wa Bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara, na fedha kutofika kwa wakati uliopangwa;

(ii) Uhaba wa umeme na maji kwa ajili ya shughuli za uzalishaji viwandani;

(iv) Ushindani usio wa haki katika masuala ya biashara na ukosefu wa masoko ya uhakika kwa bidhaa zinazozalishwa hapa nchini;

(iv) Miundombinu hafifu na isiyo na tija inayoathiri sekta shindani ya Viwanda;

(v) Ukosefu wa wataalamu na teknolojia duni; na

(vi) Uingizaji wa bidhaa dhaifu katika soko la ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na changamoto za kisekta, Wizara imejitahidi kuchukua hatua mbalimbali zikiwemo kuzingatia ushauri wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara ambayo imekua ikitoa michango, ushauri na maelekezo mbalimbali ambayo yamelenga kuimarisha sera na mifumo mizuri ya ukuzaji wa sekta ya viwanda na uzalishaji viwandani, kufanya biashara pamoja na kutafuta masoko ya uhakika ya ndani na nje ya nchi. Aidha, Kamati imeendelea kutoa msisitizo wa kuboresha mazingira wezeshi ya kufanya biashara ndani na nje ya nchi na hivyo kuvutia wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda na Biashara imeendelea kuchangia uchumi hasa katika shughuli za uzalishaji, usindikaji usambazaji na masoko. Sekta hizi bado zina nafasi kubwa ya kuliwezesha Taifa kuondokana na umasikini na kulifikisha katika kiwango cha uchumi wa kati wa Viwanda. Haya yote yanawezekana ikiwa Serikali itaweza kusimamia ipasavyo na kuratibu shughuli zote za msingi zinazohusu sekta hizi na kukabiliana na changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2012/2013 Wizara ilitengewa na kuidhinishiwa na Bunge kiasi cha Sh. 170,199,842,000/=; kati ya fedha hizo Sh. 38,819,055,000/= zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Sh. 131,380,787,000/= zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Maombi haya ya fedha yaliidhinishwa na Bunge baada ya kuridhika na mchanganuo wa shughuli zilizohitajika kutekelezwa na Wizara hii kwa kipindi hicho. Hata hivyo, mchanganuo unaonyesha kuwa hadi kufikia mwezi Februari, 2013 Wizara ilikuwa imepokea asilimia 23 tu ya fedha

iliyopitishwa na Bunge, na hadi kufikia mwezi huu wa Mei, Serikali haijatekeleza ahadi yake ya kumalizia fedha zilizobaki. Kwa mwenendo huu wa ufinyu wa bajeti kwa Wizara na fedha kuchelewa kufika kwa wakati, ni dhahiri:-

(i) Serikali haitaweza kufikia malengo yake iliyojiwekea ya kuleta mabadiliko ya uchumi kutoka kiwango cha uchumi wa chini unaotegemea kilimo kufikia kiwango cha uchumi wa kati unaotegemea viwanda;

(ii) Wizara imeshindwa kutekeleza majukumu yake ya msingi hivyo matatizo ya kiuchumi yanayoikabili nchi yetu kama vile ukosefu wa ajira, umaskini wa kipato, ufinyu wa wigo wa kodi, na thamani hafifu kwenye mazao ya kilimo na maliasili yataendelea kuwepo;

(iii) Kuendelea kuwepo usimamizi hafifu wa kuboresha upatikanji wa huduma za kuendeleza Sekta za Viwanda, Biashara, Masoko na Viwanda Vidogo; na

(iv) Fedha kwa ajili ya matumizi mengine *(OC)* imeendelea kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inajiuliza kuwa, kama Bunge limeidhinisha fedha kwenda kwenye Wizara husika, ni nani mwenye mamlaka ya kupinga maamuzi ya Bunge? Kwa staili kama hii: Je, tutaweza kweli kutimiza malengo yetu tuliyojiwekea kwenye utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa?

Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu lihakikishe fedha zote zilizoidhinishwa kutolewa kwa Wizara hii zipatikane ili iweze kukamilisha majukumu yake ya msingi iliyojiwekea hasa kwa upande wa miradi ya maendeleo. *(Makofi)*

Jedwali. Na 1. Bajeti ya mwaka 2012/2013 iliyopitishwa kwa Wizara ya Viwanda na Biashara ikiwianishwa na fedha iliyokwisha tolewa hadi mwezi Februari 2013.

| | Maelezo | Bajeti iliyopitishwa 2012/2013 | Fedha iliyokwishatolewa hadi mwezi Feb.2013 | % ya Bajeti iliyopitishwa 2012/13 vs Fedha iliyo-kwishatolewa hadi Februari 2013 |
|---|---|---|---|---|
| **Matumizi ya kawaida** | Mishahara | 31,378,315,000 | 15,814,856,107 | 50% |
| | Matumizi mengine | 7,440,740,000 | 3,729,029,500 | 50% |
| | Jumla | 38,819,055,000 | 19,543,885,607 | 50% |
| **Bajeti ya Maendeleo** | Fedha za Ndani | 123,713,139,000 | 16,807,814,775 | 14% |
| | Fedha za Nje | 7,667,648,000 | 2,673,307,987 | 35% |
| | Jumla | 131,380,787,000 | 19,481,122,762 | 15% |
| | Jumla Kuu | 170,199,842,000 | 39,025,008,369 | 23% |

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia *Exporting Processing Zones (EPZ)* imeendelea kuhamasisha uwekezaji pamoja na ujenzi wa baadhi ya miundombinu katika maeneo ya *EPZ/SEZ.* Pia imeendelea kutoa fidia katika maeneo maalum ya uwekezaji, mfano eneo la Kurasini ili kutekeleza mradi wa *Tanzania - China Logistics Centre* na eneo la mradi wa *EPZ* – Bagamoyo. Maeneo haya ni ya kimkakati yaliyopewa kipaumbele kwenye utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2012/2013 ambayo yanategemewa kuongeza ajira, soko la malighafi nchini pamoja na kuvutia uwekezaji na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa zoezi hili la ulipaji wa fidia umekuwa wa kusuasua na hivyo kuondoa ile dhana kuwa ni kweli Miradi ya Kimkakati. Mfano, katika Bajeti

ya mwaka 2012/2013 Wizara iliomba na kuidhinishiwa na Bunge kiasi cha Shilingi bilioni 60 kwa ajili ya kulipa fidia ya eneo la Kurasini na wadau wetu wa maendeleo (China) wangetoa Shilingi bilioni 600 hii ikiwa na maana ya uchangiaji ulikuwa wa uwiano wa 1:10 ili kutekeleza mradi huu ambao unatoa ajira takribani 25,000. Hata hivyo, mpaka sasa Serikali imekwishatoa kiasi cha Shilingi milioni 550 tu kati ya Shilingi bilioni 60 na kwa upande wa mradi wa *EPZ* - Bagamoyo *(Tanzania Mini Tiger Plan),* Serikali imekwishatoa kiasi cha Shilingi bilioni 10.9 tu, kati ya Shilingi bilioni 50.2. Maombi haya ya fedha yalikuwa Maalum na yalitakiwa yatoke kwa mkupuo mmoja yaani *ringfenced.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaona kuwa kwa mwenendo kama huu wa utoaji hafifu wa fedha kwenye miradi tuliyoipa kipaumbele kwenye Mpango wa Maendeleo ya Taifa kamwe hatutaweza kuimaliza kama tulivyopanga. Pia kuna hatari kubwa ya kupoteza wahisani/wadau wa maendeleo kwenye miradi mikubwa kama hii ambayo tuliwahihikishia kushirikiana nao ipasavyo.

Serikali inabidi ielewe kuwa Dunia ya sasa ni ya kiushindani na kibiashara na muda haupo upande wetu, kila nchi inapenda kupata fursa za kuingia ubia kama hizi za kwetu na zinajitahidi kuweka mazingira wezeshi ya kupata wawekezaji. Sisi fursa kama hizi tunazichezea tu na hapaonekani mahali ambapo tumekuwa *serious* kwenye miradi kama hii na kuona matokeo *(impact)* bora. Kwa kuwa maombi ya fedha hizi yalikuwa *ringfenced* na Serikali ilikwishayatolea uamuzi, Kamati inaiagiza Serikali kuhakikisha inatoa fedha zote zilizobaki kabla ya mwaka mpya wa fedha haujaanza, ili miradi hii itekelezeke mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu unatuonyesha kuwa nchi nyingi duniani zinalinda viwanda vyao vya ndani pamoja ya kuwa kuna ushindani. Lazima tuhakikishe viwanda vyetu vinazalisha na kutosheleza soko la ndani na la nje kwa kutumia malighafi tunayozalisha nchini. Kwa kuzingatia haya, Kamati inatoa ushauri ufuatao:-

(i) Serikali iongeze jitihada za kufufua Kiwanda cha *General Tyre (EA) Ltd* ikiwemo upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kulipa madeni yote. Hii itasaidia kuongeza ajira, wigo wa ukusanyaji mapato yatokanayo na kodi na pia kusaidia kukuza uchumi;

(ii) Miradi yote inayotekelezwa kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC),* yaani mradi wa makaa ya mawe wa Mchuchuma na wa Chuma cha Liganga, mradi wa kuzalisha umeme wa Ngaka, mradi wa kuzalisha umeme wa upepo na mradi wa kutengeneza Viuadudu *(Biolarvicides)* vya kuua viluwiluwi vya mbu wa malaria na ule wa uchimbaji wa magadi (*Soda Ash*) –Ziwa Natron; isimamiwe na kuratibiwa vizuri ili ikamilike kwa wakati uliopangwa. Kukamilika kwa miradi hii sambamba na kujenga uwezo wa Wizara wa kuandaa Sera ya Maendeleo ya Viwanda na Kuboresha Utendaji wa Viwanda kutasaidia kupatikana kwa umeme wa uhakika, ajira na kuongeza mapato na hivyo kusaidia kukuza uchumi kupitia sekta ya viwanda.

(iii) Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kusimamia ipasavyo ujenzi wa Viwanda vipya vya Saruji na hivyo kuongeza uwezo wa uzalishaji na upatikanaji wa ajira mpya. Mfano, *Tanzania Portland Cement Co. Ltd* kimeongeza uwezo wa uzalishaji kutoka tani 700,000 mwaka 2008 hadi 1,400,000 mwaka 2011; *Tanga Cement* kutoka tani 500,000 hadi tani 1,200,000; na *Mbeya Cement* kutoka tani 250,000 hadi 350,000 katika kipindi hicho.

Hivyo kutoka mwaka 2006 hadi 2011 uwezo wa uzalishaji wa saruji kwa viwanda vyote vitatu uliongezeka kwa wastani wa asilimia 95.4 (kutoka tani 1,514,073 hadi tani 2,959,164). Kukamilika kwa ujenzi wa viwanda vipya vya saruji, yaani *Athi River Cement Co. – Tanga, Mbagala Cement Co. - Dar es Salaam na Arusha Cement Co. - Arusha* kutasaidia upatikanaji zaidi wa saruji na hivyo kuachana na tabia ya kuagiza saruji toka nje inayouzwa kwa bei ya chini kutokana na ruzuku inayotolewa kwa viwanda vyao na hivyo kupelekea viwanda vyetu kujiendesha katika ushindani usio wa haki. Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua za kutoza

kodi au ushuru kwenye saruji inayoagizwa toka nje ili kulinda uzalishaji wa ndani. *(Makofi)*

(iv) Viwanda vya sukari vilivyopo nchini pamoja na vile vidogo kwa ujumla vinazalisha takribani tani 304,000 na mahitaji yetu ni tani 400,000. Jitihada za makusudi zinahitajika kuongeza uzalishaji ili kuweza kukidhi mahitaji ya ndani. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaongeza ujenzi wa viwanda vipya vya sukari sambamba na kongeza kilimo cha miwa ili kutosheleza mahitaji na kulinda bei za walaji na hivyo kuondokana na utaratibu wa kuagiza sukari toka nchi za nje.

(v) Serikali inahitaji kufanya jitihada zaidi katika kuhamasisha kilimo cha mazao yanayozalisha mafuta ya kula kama vile alizeti, karanga na mawese. Takwimu zinaonyesha kuwa bado hatujajitosheleza katika uzalishaji wa mbegu zinazotoa mafuta. Tunazalisha tani 320,000 za mbegu zinazotoa tani 90,000 tu za mafuta wakati mahitaji yetu ni tani 350 hadi 450,000 za mafuta ya kula na hivyo kutosheleza asilimia 40 ya mahitaji yetu. Jitihada hizi ziendane na udhibiti wa viwanda vinavyoagiza mafuta toka nje viagize mafuta yasiyosafishwa *(crude oil)* ili yasafishwe hapa nchini. Pia Serikali ifuatilie malalamiko yanayotolewa na wananchi kuhusu uwepo wa Bandari bubu zinazotumika kupitisha bidhaa mbalimbali ikiwemo ya mafuta ya kula, na watakaobainika kuhusika na tuhuma hizo wachukuliwe hatua kali kwani ni wahujumu wa uchumi na wanaikosesha Serikali mapato. *(Makofi)*

(vi) Kwa upande wa viwanda vya korosho bado vimeshindwa kuhimili ushindani wa soko na vingine vimeshindwa kufanya kazi. Hii imetokana na viwango vikubwa vya kodi zinazotozwa kwenye vipuri na vifungashio, bei kubwa ya korosho ghafi kwa wabanguaji wa ndani kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani ukilinganisha na wanunuzi kutoka nje ambao hupewa ruzuku ya asilimia 30 na nchi zao na pia ukosefu wa umeme wa uhakika na mitaji ya kuendeshea viwanda. Kamati inaitaka Serikali kutafuta

suluhisho la matatizo haya ili kusaidia wakulima wa korosho na wamiliki wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwango la Taifa *(TBS)* limekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha linadhibiti uingizaji wa bidhaa zisizo bora na hivyo kukuza matumizi ya viwango na hivyo kulinda afya ya walaji, usalama wa walaji na kulinda mazingira ya nchi yetu. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa pamoja na juhudi hizi, Shirika linakabiliwa na upungufu wa wafanyakazi. Idadi ya sasa ni wafanyakazi 197 tu ambao wanatakiwa kufanya kazi na kuzunguka Tanzania nzima kuhakikisha kuwa bidhaa zenye ubora unaokubalika tu ndio zinatengenezwa au kuingizwa nchini na zinakidhi viwango vya kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika *(TBS)* hili limekuwa likilalamikiwa mara kwa mara kwamba halifanyi kazi yake ipasavyo. Ukweli ni kwamba shughuli za kiuchumi zimeongezeka na hivyo shughuli za Shirika zimeongezeka na haziendi sanjari na idadi ya wafanyakazi waliopo hivyo linashindwa kufanya kazi kwa ufanisi kutokana na upungufu wa wafanyakazi. Mfano, mwaka 2010/2011 Shirika liliomba kibali cha kuajiri wafanyakazi 35 lakini Serikali ilitoa kibali cha kuajiri wafanyakazi 18 tu. Hata hivyo, kibali hicho hakikutekelezwa kwa sababu Serikali ilisitisha ajira. Mwaka uliofuata wa 2011/2012 Shirika liliomba nyongeza ya wafanyakazi 15 tu. Ombi hili halikufikiriwa.

Mwaka 2012/2013, Shirika liliomba tena wafanyakazi 62 lakini Serikali ilitoa kibali cha kuajiri wafanyakazi 32 tu. Hata hivyo, ajira zilisitishwa tena mwezi Februari mwaka 2013. Kwa takwimu hizi ni dhahiri Shirika *(TBS)* haliwezi kufikia malengo yake iliyojiwekea; mfano, Shirika la Viwango la Kenya *(KEBS)* lina wafanyakazi zaidi ya 1000 na lina ofisi za kanda zikiwemo Mombasa, Kisumu, Garisa, Nyeri, Nakuru na katika *entry points* mbalimbali za mipakani. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatoa kibali cha ajira ya watu 62 iliyoomba mwaka 2012/2013 ili Shirika hili liweze kutekeleza majukumu yake ikiwemo kufungua ofisi za kanda na vituo vya mipakani na hivyo kusogeza huduma zake karibu zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo inahusisha sekta zote za uchumi ambazo zimejikita katika jasiriamali za kuzalisha (asilimia 13.6), kununua na kuuza (asilimia 55), huduma (asilimia 30) na nyinginezo (asilimia 1). Sekta hii imeajiri Watanzania takribani milioni 5.2 na mchango wa sekta hii katika Pato la Taifa kwa sasa umefikia asilimia 27.9. Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hii inayohusisha wajasiriamali wa viwango na kada mbalimbali za mtaji na elimu, Kamati inashauri kama ifuatavyo:-

(i) Serikali ikamilishe ahadi yake iliyoitoa kwenye bajeti ya Mwaka 2012/2013 ya kuwapa *SIDO* kiasi cha Shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kuratibu na kuendeleza programu mbalimbali za Wajasiriamali. Wizara mpaka sasa haijapokea fedha hizo licha ya kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu alisisitiza *SIDO* wapewe hizo fedha;

(ii) Kwa kuwa shughuli nyingi za sekta hii ziko katika sekta isiyo rasmi, basi Serikali haina budi kufanya mchakato wa kurasimisha sekta hizi ili iweze kupata mapato yake yatokanayo na kodi;

(iv) Serikali iongeze juhudi ya kutoa elimu ya uendeshaji wa miradi ambayo ina uhusiano wa moja kwa moja na ukuaji wa biashara;

(iv) Serikali iboreshe fursa ya kupatikana mikopo yenye riba nafuu kwa wajasiriamali pamoja na kuendeleza programu mbalimbali zinazosimamia na kuboresha shughuli za wajasiriamali; na

(v) Serikali iendelee kuweka vivutio vya kuhamasisha na kuwezesha sekta hii ya wajasiriamali kuchangia uchumi wa nchi yetu kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chini ya mfumo wa '*PPP*', Serikali lazima iongeze jitihada za kukuza uwekezaji wa viwanda kupitia Sekta Binafsi pamoja na kuimarisha na kuboresha mazingira mazuri ya kuendesha viwanda. Jukumu

hili lazima liambatane na kuweka mazingira wezeshi kwa Sekta Binafsi kufanya biashara na hivyo kuwa mhimili mkuu wa ukuaji wa uchumi. Hatua hizi zitatusaidia kufikia malengo yetu ya kujenga uchumi imara kupitia viwanda utakaohimili ushindani wa ndani na nje ya nchi na hivyo kufikia lengo la kuiwezesha Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati kama inavyoelekezwa kwenye Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025, Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2011/2012 - 2015/2016 na Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa inayoandaliwa na Benki ya Dunia, *'Doing Business 2013';* kati ya nchi 185 duniani, Tanzania ni nchi ya 134 katika kurahisisha mazingira wezeshi ya ufanyaji biashara *(Ease of doing business).* Kamati bado inaitaka Serikali kuhakikisha inapitia na kufanya marekebisho ya Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali zinazokinzana na kuleta urasimu mkubwa katika kufanya shughuli za biashara, kufanyia tathmini Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji nchini pamoja na kuondoa tatizo la ucheleweshaji au kutokutoa maamuzi kwa wakati. Ni dhahiri kuwa hatutaweza kuendelea bila ya kuwa na msukumo wa hali ya juu wa kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuwekeza ili kuongeza kasi ya kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Marekebisho haya yatatoa fursa ya kushiriki kikamilifu katika mahusiano ya kibiashara baina ya nchi na nchi *(Bilateral Trade);* Makubaliano ya Kibiashara ya Kikanda *(Regional Trading Agreements – RTAs)*; Mpango wa Mtangamano wa Utatu *(COMESA – EAC - SADC Tripartite Free Trade Area Arrangements);* na Soko la Pamoja la Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* juu ya Uhuru wa Biashara ya Bidhaa *(Free Movements of Goods),* Uhuru wa Biashara ya Huduma *(Free Movement of Services)* na Uhuru wa Kuhamisha Mitaji *(Free Movement of Capital).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda ni mojawapo ya sekta iliyopewa kipaumbele chini ya Sheria ya Uwekezaji ya Mwaka 1997 *(TIC Act, 1997).* Pamoja na kuwa

kodi ni muhimu katika kugharamia shughuli za Serikali, nafuu katika kodi ni muhimu kwa ajili ya kutengeneza mazingira mazuri kwa ukuaji wa uchumi na hivyo kuwa na wigo imara wa kodi kwa siku za usoni. Unafuu wa kodi unaotolewa kwenye sekta hii ambao hutegemeana na aina ya mradi ni pamoja na Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha sifuri, misamaha ya kodi chini ya maeneo ya maalum ya uzalishaji kwa ajili ya kuuza nje *(EPZ)* kama vile misamaha kwenye kodi ya mapato kwa miaka 10 *(Tax Holiday)* na nyingine.

Kamati inatoa wito kwa wenye viwanda kujiandikisha kwenye kituo cha uwekezaji na maeneo ya *EPZ* ili kutumia fursa hizi kupata unafuu katika uzalishaji na kuongeza ushindani. Matatizo ya wenye viwanda hayatokani sana na mfumo wa kodi bali yanatokana na matatizo ya upatikanaji wa umeme wa uhakika, miundombinu hafifu, teknolojia duni, ujuzi wa kusimamia biashara katika mazingira ya kisasa ya ushindani. Hali hii inasababisha hasara kubwa kwa wenye viwanda kutokana na gharama kubwa za uzalishaji na pia kupunguza fursa za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kusimamia mchakato wa kuendeleza Sekta ya Viwanda na Biashara ili kuwezesha nchi kufikia uchumi wa kati wa viwanda ifikapo mwaka 2025. Pamoja na malengo mazuri ya Serikali, Kamati inatoa angalizo lifuatalo ili malengo hayo yatimie:-

(i) Sekta ya viwanda na biashara mafanikio yake yanategemea sana uwepo wa miundombinu bora ya bandari, reli na barabara ili kuwezesha usafirishaji wa malighafi na bidhaa ndani na nje ya nchi. Kuna hatari kubwa viwanda vyetu kufungwa kutokana na kutokuweza kusafirisha bidhaa walizozalisha kwa kutumia barabara kwa sababu inaharibiwa na magari yaliyobeba mizigo mizito kuliko ustahimilivu wa barabara.

Hivyo, Serikali itilie mkazo ufufuaji wa reli kwa ajili ya usafirishaji wa bidhaa na mizigo.

(ii) Bado kuna urasimu mkubwa katika kusimamia kuingiza na kusafirisha mizigo kupitia Bandari ya Dar es Salaam, pia Serikali haijatoa kipaumbele katika upanuzi wa Bandari ya Dar es Salaam, Tanga au Mtwara, hivyo kuna hatari mizigo mingi kupitia bandari za nchi ya Kenya (Mombasa, Lamu), Msumbiji, Angola au Namibia ambazo zote zipo kwenye programu za upanuzi na zinaunganishwa na miundombinu bora ya barabara na reli.

(iii) Serikali iendelee kuhamasisha uwekezaji katika viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu kupitia uimarishaji wa viwanda vilivyopo na uanzishwaji wa viwanda vipya vya usindikaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo maalum ya uwekezaji *'Export Processing Zones' (EPZ)* na *'Special Economic Zones' (SEZ)* ni maeneo muhimu ya kukuza viwanda, kuongeza ajira, kukuza teknolojia, kukuza mauzo ya nje na kuhamasisha uongezaji wa thamani. Mifumo kama hii imesaidia kukuza uchumi kupitia viwanda kwa nchi za Ireland, China, Vietnam, Jordan, Afrika ya Kusini na kadhalika, ili kuzalisha ajira kwa wingi kupitia viwanda, Serikali ilikwishatoa agizo kuwa kila Mkoa utenge maeneo maalum ya uwekezaji. Kamati imeona kuwa agizo hili ni zuri kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Hata hivyo inatoa angalizo kuwa:-

(i) Serikali ijiandae kulipa fidia kwa Mikoa 20 ambayo imekwishatenga maeneo hayo, ucheleweshaji wa malipo haya kwa wakati unakuwa mzigo mkubwa wa malipo kwa Serikali kwa sababu thamani ya ardhi inakuwa imepanda;

(ii) Maeneo yaliyotengwa yaendelezwe kwa hatua kutokana na vipaumbele vilivyopo na misaada tunayopata; na

(iii) Maeneo yaliyotengwa yatengenezewe Mpango *Mpana (Master Plan).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Tawi la Yanga hapa Bungeni, napenda kuipongeza *Young Africans* kwa ubingwa waliotwaa. Tawi la Yanga Bungeni linamwagiza Rais wa Yanga ndugu Yusuf Manji kwamba ubingwa ule hautanoga kama tarehe 18 hawatawapa kipigo wapinzani wao wa jadi Simba na hii itasaidia kuboresha safari ya mtani wetu Mwenyekiti Mheshimiwa Aden Rage. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kumshukuru Waziri wa Viwanda na Biashara - Mheshimiwa Dkt. Abdallah O. Kigoda, Naibu Waziri - Mhe Gregory Teu, Katibu Mkuu, pamoja na Wataalamu wa Wizara na Taasisi zilizochini ya Wizara kwa kuwa tayari kutoa ufafanuzi na kupokea maoni na ushauri wa Wajumbe wa Kamati wakati wote wa mjadala wa makadirio haya. Ni matarajio ya Kamati kuwa ushirikiano huu utaendelea katika mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee kabisa, napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Uchumi, Viwanda na Biashara ambao wameweza kutoa maoni na michango ya mawazo yao mbalimbali katika kuboresha makadirio haya ili hatimaye yaletwe mbele ya Bunge hili Tukufu. Naomba nitumie nafasi hii kuwatambua Wajumbe wote kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mahmoud Hassan Mgimwa - Mwenyekiti, Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula - Makamu Mwenyekiti na Wajumbe ni Mheshimiwa Margareth Agness Mkanga, Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mheshimiwa Ester Lukago Minza Midimu, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Dkt. Titus Mlengeya Kamani, Mheshimiwa Joyce John Mukya, Mheshimiwa David Zakaria Kafulila, Mheshimiwa Shawana Bukhet Hassan, Mheshimiwa Said Mussa Zubeir, Mheshimiwa Vicky Pascal Kamata, Mheshimiwa Naomi Ami Mwakyoma Kaihula, Mheshimiwa Khatibu Said Haji, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Josephine Jonson

Genzabuke, Mheshimiwa Eng. Habib Juma Mnyaa na Mheshimiwa Mohamed Hamis Misanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru sana wewe mwenyewe binafsi na Mheshimiwa Naibu Spika kwa kutupatia maelekezo mbalimbali kwa Kamati yetu ambayo wakati wote yamefanikisha kazi za Kamati. Aidha, napenda pia kumshukuru na kumpongeza Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas D. Kashililah, Katibu wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara Ndugu Michael Kadebe kwa kuratibu shughuli za Kamati hadi taarifa hii kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara (Fungu 44), kama alivyowasilisha mtoa hoja muda mfupi uliopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa nimwite Msemaji wa Kambi ya Upinzani Wizara ya Viwanda na Biashara.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusoma hotuba ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu mapitio ya utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2012/2013 na mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2013/2014 kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge toleo la mwaka 2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninaposoma hotuba hii ni takribani miaka 15 tangu tuingie rasmi kwenye Sera ya Ubinafsishaji na ambayo kiuhalisia imefeli na Wizara hii ya Viwanda na Biashara inatoa tathimini nzuri zaidi kuonyesha jinsi ambavyo sera hiyo imeshindwa katika utekelezaji wake, ni bahati kuwa leo waziri aliyesimamia jukumu la kubinafsisha viwanda vyetu ambavyo leo kila mmoja analia kuwa

vimekufa, mashine na mitambo yake zinauzwa kama chuma chakavu ndio huyo huyo aliyepewa jukumu la kuvisimamia na au kuvifufua viwanda vilivyouawa na sera hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji imeshindwa na sasa ni wakati muafaka wa kufanya tathimini kama Taifa na tujipange upya kwa maslahi ya nchi yetu sasa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda ilipanuka katika karne ya 19 hadi katikati ya karne ya 20 katika nchi zilizoendelea karibu nusu ya wafanyakazi wote walijikita katika sekta hiyo. Nusu ya pili ya karne ya 20, sekta ya tatu na ya nne, yaani biashara na huduma zilianza kuwa na wafanyakazi wengi zaidi. Tanzania iliwahi kuwa na viwanda vingi vya uzalishaji mali, kwa sababu viwanda vinaweza kuinua uchumi wa Taifa na kuondoka katika daraja la kuwa nchi maskini duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwasisi wa nchi yetu tayari alikwishatufikisha katika hatua ambayo tayari tulikuwa tunakaribia kutoka gizani na kuanza kuona nuru *(First, it is important to be persistent. It will always be dark before we can see good days)* kwani viwanda alivyoviasisi kwa nia njema ya kuimarisha uchumi wa nchi hii, lakini madaktari na maprofesa wa uchumi waliona Mwalimu alikosea na wakaviuza viwanda vyetu badala ya kuvitafutia tiba ya kuvifanya viwe na tija zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kupiga hatua za kimaendeleo, Serikali na sekta binafsi inaanzisha mpango kabambe wa kufufua baadhi ya viwanda vilivyouawa na baadhi ya viongozi. Hakuna asiyefahamu kama Tanzania ina malighafi za kutosha ambazo zinaweza kutumika kutengeneza bidhaa viwandani na kuuzwa ndani na nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malighafi hizo zinazopotea kutokana na viongozi kutoweka mikakati ya kuwasaidia

wananchi kwa kuwapa elimu na namna ya kuanzisha viwanda vidogo na vikubwa vya kutosha vya kusindika na kutengeneza bidhaa mbalimbali ili kuinua uchumi. Ukweli ni kwamba kuna viwanda vingi ambavyo havifanyi kazi kutokana na ukosefu wa mitambo imara na hivyo kusababisha uzalishaji wa bidhaa kuwa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezji wa bajeti ya mwaka 2012/2013 na mipango ya mwaka 2013/2014; hadi kufikia Februari, 2013 Wizara hii ilikuwa imepokea kiasi cha asilimia 23 tu ya fedha yote ya bajeti iliyokuwa imeidhinishwa na Bunge, kwa upande wa fedha za maendeleo ni kiasi cha Shilingi bilioni 16.807 ya fedha za ndani sawa na asilimia 14 ndiyo kilikuwa kimetolewa na Hazina, wakati fedha za maendeleo kutoka nje zilipokelewa asilimia 35. Kambi Rasmi ya Upinzani, inaona kuwa Serikali haina nia wala mpango wa kukuza viwanda vyetu na ndiyo maana haitoi fedha ambazo zimepitishwa na kuidhinishwa na Bunge hili kwa ajili ya sekta hii muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. Tunataka majibu, nini kilipelekea mgawanyo huu wa bajeti kuwa kiasi kidogo hivyo? Je, tuna uhakika gani kuwa bajeti ya mwaka huu itatekelezwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha uliopita kilitengwa kiasi cha Shilingi bilioni 60 kwa ajili ya kulipia fidia eneo la Kurasini ili kupisha ujenzi wa kituo cha Biashara kati ya Tanzania na China *(Tanzania – China Logistic Centre),* jambo la kushangaza ni kuwa kwa mwaka huu wa fedha zimetengwa Shilingi bilioni moja tu kwa ajili ya *EPZ.* Pamoja na marekebisho yaliyowasilishwa na Waziri wa Fedha, ambayo nimeyaona yamewasilishwa Mezani, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kujua ni kwanini mwaka huu wa fedha zimetengwa fedha kidogo kiasi hicho, wakati tunatumia Shilingi bilioni 60 kulipa fidia? Mbona hatutengi fedha kwa ajili ya kuendeleza mradi kama lengo ni kuondoa utegemezi wa *EPZ* kwa Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Serikali iliendelea na ahadi yake kuwa itakifufua Kiwanda cha Matairi cha *General Tyre* cha Arusha, na mpaka

mwezi Machi, 2011 kiwanda hiki kilikuwa kinadaiwa jumla ya Shilingi bilioni 38.

Aidha, mpaka sasa Serikali haijaweza kumpata mbia mwingine kwa ajili ya kuendeleza kiwanda hicho kutokana na ukweli kuwa bado Serikali haijakamilisha utaratibu wa kuachana na mwanahisa mwenza, Kampuni ya *Continental AG*.

Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kupata majibu ni taratibu gani zinazokwamisha Serikali katika kuachana na mbia mweza ili uzalishaji uweze kuanza kwa kumtafuta mbia mpya?

Aidha, ni kwanini Serikali isitenge fedha za kutosha kulipa hayo madeni inayodaiwa ili kiwanda hiki kiweze kuanza uzalishaji? Ni kiasi gani cha mtaji kinachohitajika kwa ajili ya kufufua kiwanda hicho, ikiwa tayari mhandisi mshauri wa viwanda ameshakamilisha taarifa yake kuhusiana na uchambuzi wa kina wa mahitaji ya gharama ya kufufua kiwanda hicho? Je, kiasi cha Shilingi bilioni 6.3 kilichotengwa mwaka huu wa fedha 2013/2014 kinatosha katika kufufua kiwanda hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa waraka wa Utumishi Na.1 wa mwaka 2012 ambao ulitoa mwongozo kuhusu utaratibu wa kununua samani za ofisi za Serikali kutoka kwa wazalishaji wa ndani na malighafi za samani hizo ziwe zimezalishwa humu nchini, na utekelezaji wa waraka huo ulianza tarehe 01 Oktoba, 2012.

Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata majibu ya kina juu ya utekelezaji wa waraka huo na ni hatua gani zitachukuliwa dhidi ya Afisa maduhuli ambaye atakiuka waraka huo na kununua samani za ofisi kutoka nje ya nchi? Aidha, tangu kuanza kutekelezwa kwa waraka huo, ni Idara ngapi za Serikali zimetii na kuutekeleza kikamilifu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* limepata ridhaa ya Serikali kuratibu utekelezaji wa

miradi mbalimbali kama vile uzalishaji wa umeme na usafirishaji wake, mawasiliano, madini, kilimo, misitu na uvuvi na miundombinu ya barabara inayotekelezwa chini ya kinachoitwa Mtwara *Development Corridor.* Upembuzi yakinifu kwa baadhi ya miradi hiyo tayari umekwishakamilika. Aidha, utekelezaji wake unafanyika chini ya mpango mpana wa *SADC*.

Aidha, kuanzisha na kuendeleza maeneo huru ya uzalishaji na uanzishaji wa bandari huru. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge katika miradi hiyo hadi sasa ni miradi gani ambayo imekwishakamilika na uendeshaji wake ukoje?

(a) Ushirika kati ya *NDC* na *Intra Energy Ltd:*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa inamiliki asilimia 30 katika kampuni ya *TanCoal*. Kampuni hiyo inayojishughulisha na uchimbaji wa makaa ya mawe kwa sasa inatarajia kuanza kuzalisha umeme wa 400MW, na kati ya hizo 200MW zinatarajiwa kuzalishwa mwaka 2014 hadi kufikia mwaka 2017 uzalishaji wa 400MW nyingine utakuwa umekamilika.

Aidha, hazina ya makaa ya mawe ya tani 38,039 ilikuwa imehifadhiwa mpaka mwezi Januari 2013, hii inatokana na ukweli kuwa uzalishaji mkubwa wa umeme kutokana na makaa ya mawe bado haujaanza kutekelezwa kikamilifu na hii inatokana na majadiliano ya muda mrefu kati ya *TANCOAL* na *TANESCO* kwa ajili ya mkataba wa kuzalisha umeme – *PPA*.

Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kujua ni lini majadiliano hayo yataweza kufikia ukomo ili tuanze kuzalisha umeme kwa kutumia makaa ya mawe na hatimaye tuweze kuondokana na umeme ghali wa kutumia nishati ya mafuta hapa nchini?

(b) Mradi wa kuzalisha umeme wa upepo – Singida:

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ambao unashirikisha Shirika la Maendeleo la Taifa na Kampuni binafsi inayoitwa *Power Pool East Africa Ltd* kwenye mradi wa nishati umeme kwa nguvu za upepo, ambao upo takriban kilometa 12 mashariki mwa Halmashauri ya Singida.

Mradi unatarajiwa kuzalisha jumla ya Megawati 300, lakini mradi huo unatarajia kuanza kuzalisha Megawati 50, kwa mujibu wa *Power System Master Plan (PSMP)* mradi ulitarajiwa kuanza rasmi mwaka 2012/2013.

Aidha, kwa mujibu wa randama ya Wizara ukurasa wa 55 inasema kuwa nanukuu: "Wizara inaendelea kushughulikia upatikanaji wa fedha Dola za Marekani milioni 136 kutoka *EXIM Bank* ya China ambayo imekubali kutoa mkopo wenye masharti nafuu na tayari ridhaa ya Serikali *(Letter of Support)* imewasilishwa *EXIM Bank* na Wizara ya Fedha."

Kambi Rasmi ya Upinzani, inataka kujua Kampuni ya *Power Pool EA* iliwezaje kupata ubia huu na *NDC* na ni kwa nini *NDC* kwa kushirikiana na Serikali ndiyo imekwenda kutafuta fedha za mradi huu kwa kutumia *guarantee* ya Serikali? Waziri aweke wazi wamiliki wa *Power Pool EA* maana habari za kuaminika zinaonyesha kuwa wamiliki wa mradi huu ni ndugu na jamaa wa Wabunge na Mawaziri wa CCM ambao ni Maswa Kagoswe, Isaac Joseph Mwamanga, Emmanuel Kasyanju, Prosper Tesha, Lennard Tennende na Athuman Ngwilizi, na hivyo wametumia ushawishi wao Serikalini kupata ubia huu ili kufaidika kifedha. *(Makofi)*

Aidha, tunataka kujua kama Serikali ilifanya uchunguzi wa kina *(vetting)* juu ya wamiliki, uwezo na uhalali wa kampuni hii ya *Power Pool EA* katika kuzalisha umeme kabla ya kutoa ridhaa ya Serikali juu ya mkopo huo mkubwa ili

isijekuwa hii nayo ni *"Richmond"* nyingine, na kama iliwahi kufanya mradi mwingine popote wa kuzalisha umeme kwa njia ya upepo.

(c) *Mradi wa uyeyushaji chuma ghafi uliopo Ludewa:*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika hili la *NDC* liko kwenye ubia na kampuni ya *MM Steel Resources Public Limited Company (MMSR PLC*), ambapo kampuni ya ubia inayoitwa *"Maganga Matitu Resource Development Limited (MMRDL)"* iliyopo Wilaya ya Ludewa kwa ajili ya matumizi ya chuma ghafi kutoka eneo la maganga matitu ambalo ni sehemu ya machimbo ya Liganga na Katewaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2012/2013 ilitengewa Shilingi bilioni 7.9 kwa ajili ya miradi yote, na mradi wa mchuchuma Sh. 1,779,763,501/=.

Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, *NDC* imetengewa Shilingi bilioni mbili kwa ajili ya mradi wa Mchuchuma wa kufua umeme kwa kutumia makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi ya Upinzani inataka kujua uwezo wa kiutawala *(Managerial and Technical Aspect)* kwa Shirika hili kuweza kushiriki mchakato mzima wa utendaji kwa Makampuni haya yote ambayo Shirika lina mikataba kwa kufungua Kampuni za ubia, kutokana na ukweli kwamba Serikali ndiyo inayowekeza fedha za walipa kodi kwa mujibu wa vitabu vya Randama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba Serikali imekuwa ikipoteza fedha nyingi kutokana na kutokuwemo kwenye utawala na uendeshaji kwa kampuni tulizo na hisa, kutokana na kukosekana kwa usimamizi dhabiti wa hisa zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogovidogo (*SIDO*). *SIDO* imekuwa ni taasisi yenye msaada mkubwa kwa wajasiriamali wadogo na wa kati hapa nchini, inafanya nini katika kuingia ubia na wananchi katika kuanzisha viwanda vya kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, (ushirikiano na wakulima kama vile miwa, Morogoro, Manyara, Mbinga, Tanga na kadhalika), alizeti, matunda na kadhalika badala ya *SIDO* kutafuta fedha au Serikali kuwekeza katika viwanda vidogo na vya kati).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, *SIDO* imeweka malengo mengi baadhi yake ni yafuatayo: kuimarisha uwezo wa kuzalisha na kusambaza mashine ndogondogo za kusindika mazao, kuwezesha usambazaji wa teknolojia vijijini kwa kupitia program ya Wilaya moja kwa moja, kuwezesha wazalishaji wadogo kupata masoko ya bidhaa na huduma zao, kwa ktengeneza miundombinu ya kupokea na kusambazia habari za kibiashara na kutengeneza sehemu za kuonyeshea bidhaa za wazalishaji wadogo, kutoa huduma za kifedha ikiwa ni pamoja na ushauri na mikopo pale itakapojidhihirisha kuhitajika, kutoa elimu ya ujasiriamali, uongozi wa biashara, usindikaji wa vyakula na kuzingatia ubora wa bidhaa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa malengo haya muhimu sio jambo jepesi kama kweli tunahitaji tija ipatikane kwa Watanzania. Hivyo basi kwa bajeti ya maendeleo ambayo imetengwa ya jumla ya kiasi cha shilingi 6,224,594,000/=, kati ya fedha hizo za ndani ni shilingi 3,000,000,000/-, huu ni mzaha kwa nchi inayojipanga upya kuanzisha viwanda vya msingi katika uongezaji thamani kwa mazao ya kilimo. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuliangalia upya suala la mgawo wa fedha za ndani kwa *SIDO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa taasisi hii mbali ya kutoa huduma kwa wajasiriamali wadogo bali pia ni taasisi inayofanya biashara, hivyo basi, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutumia uzoefu wa *SIDO* badala ya kuwa

Mshauri Mwelekezi katika uanzishwaji wa viwanda vidogo bali kuingia ubia na vikundi na wajasiriamali mbalimbali kuwekeza katika viwanda vidogovidogo. Tunaamini kabisa kwa njia hii kuwa ushauri wanaoutoa utakuwa ni endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwango la Taifa – *TBS*. Shirika hili ndilo lenye jukumu la msingi la kuhakikisha bidhaa zote zinazozalishwa nchini au kuingizwa nchini toka nje zinakuwa na ubora unaoridhisha kabla havijaingizwa kwenye soko letu la ndani. Kwa bahati mbaya ni kwamba kumetokea malalamiko makubwa toka kwa watumiaji wa bidhaa kuwa baadhi ya bidhaa zinakuwa hazina ubora unaohitajika, miongoni mwa bidhaa hizo ni zile zinazohusu pembejeo za kilimo ambapo watumiaji wake wamepata hasara kutokana na kutumia pembejeo hizo, *"Serikali imezinyang'anya leseni ya uagizaji na usambazaji wa mbolea nchini kampuni ya Mohamed Enterprises Ltd na Staco kutokana na kusambaza mbolea feki. Aidha, alibainisha kuwa kutokana na uchunguzi uliofanywa asilimia 80 ya mbolea iliyosambazwa katika Mkoa wa Ruvuma ni feki." Kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbolea kwa wakulima ni maisha, hivyo uzembe wowote wa wahusika kutokutimiza wajibu wao maana yake ni hujuma kwa wakulima. Kwa kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuwa 80% ya mbolea iliyosambazwa Mkoani Ruvuma ilikuwa ni feki, maana yake ni kwamba *TBS* hawakufanyakazi yao ya msingi na hivyo kwa vyovyote wanatakiwa wawajibike kwa hasara waliyoipata wakulima na pili suala la kunyang'anywa leseni kwa Kampuni zilizokuwa zinaingiza na kusambaza mbolea haitoshi, bali wanatakiwa wafunguliwe mashtaka ya kuhujumu uchumi na kulipa fidia kwa wakulima wa Mkoa wa Ruvuma. Uswahiba wa wafanyabiashara na CCM, rushwa na ufisadi, ndio vinavyoiua nchi hii. Kambi Rasmi ya Upinzani inataka Serikali ieleze hatua zilizokwishachukuliwa kwa sakata hilo la mbolea feki kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu gazeti la

Mtanzania la Jumanne, Machi 05, 2013 "*Dkt. Kigoda alitoa agizo hilo Dar es Salaam jana, alipokuwa akizindua bodi mpya ya Shirika hilo, baada ya kuvunja bodi ya zamani kwa kutokuridhishwa na utendaji wake. Dkt. Kigoda alikiri kuwa hivi sasa bidhaa bandia zimezagaa kwa kiasi kikubwa sokoni, hivyo akataka bodi hiyo mpya kuhakikisha bidhaa zote zenye ubora hafifu zinatokomezwa".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kauli hiyo ya Waziri ni dhahiri walaji wamekwishapata madhara makubwa sana kutokana na kununua bidhaa zisizo na ubora unaokubalika. Hoja ni kwa vipi wale ambao madhara yamekuwa ni makubwa mno watakavyofidiwa na *TBS*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa randama ni kwamba *TBS* imeweka malengo ambayo ni pamoja na kuendeleza utekelezaji wa utaratibu wa kupima ubora wa bidhaa zote mahali zinapotoka kabla ya kuingia nchini, kuimarisha utaratibu wa kukagua ubora wa bidhaa ukiwemo ukaguzi wa magari kabla ya kuingia nchini, kutayarisha viwango vya Taifa vinavyofikia 150 vikiwemo viwango vya sekta ya huduma katika mwaka 2012/2013.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi cha shilingi 1,865,148,000/- kilichoombwa na *TBS* kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 kwa kazi zinazohitajika kutekeleza malengo yake, inawezekana zikawa ni chache kutokana na hali halisi ilivyo kama alivyodokeza Mheshimiwa Waziri kuwa bidhaa zenye ubora hafifu zimejaa sokoni na hivyo ni jukumu la *TBS* kuhakikisha vinaondolewa sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS* na ukaguzi wa magari nje ya nchi. Shirika la Viwango Tanzania limekuwa na utaratibu wa kukagua bidhaa mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuweza kubaini ubora wake na kutoa hati maalum za ubora kabla ya bidhaa hizo kuruhusiwa kuingia kwenye soko la nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na uwepo wa kitengo maalum kwa ajili ya kufanikisha kazi hiyo, Shirika hili

limeonyesha udhaifu mkubwa sana katika kufanya ukaguzi wa magari unaofanywa na kampuni mbalimbali nje ya nchi kwani waliopewa kazi hiyo ni makampuni ambayo hayana uwezo wala sifa ya kuweza kuifanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata majibu ni kiasi gani cha fedha ambacho mnunuzi wa gari anatakiwa kutoa kama ada ya ukaguzi wa gari pindi anaponunua, kwani kwa mujibu wa taarifa ya Serikali ni kuwa ni dola za Marekani 150 kwa gari, ila uhalisia ni kuwa ukiagiza gari unatakiwa kulipia kati ya dola za Marekani 300 hadi 450 kama ada ya ukaguzi wa gari. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na viwango hivi vya ada ya ukaguzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa zilizotolewa na Serikali ni kuwa tangu mwaka 2002 ni kuwa kiasi cha dola 18 milioni kiliweza kutumika kama ada ya ukaguzi wa magari na fedha zilizoingia nchini ni kiasi cha dola 2.2 milioni tu. Kambi ya Upinzani, inataka kujua ni kwa nini Serikali ilipata kiasi kidogo namna hiyo cha fedha na kuna utaratibu gani wa kuhakikisha kuwa tunaweza kukusanya mapato zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo makampuni ambayo yalifungiwa na *TBS* kufanya kazi ya ukaguzi kutokana na makampuni hayo kutokufikisha fedha Serikalini, makampuni hayo ni pamoja na *Jaffer Al Garage (Dubai), Planet Automotive (Singapore), Quality Gerage (Hong Kong)* na *WTM* ya (Uingereza). Kambi ya Upinzani, inataka kupata majibu ni hatua gani zaidi zimechukuliwa dhidi ya makampuni hayo na fedha kiasi gani zimerejeshwa? Vilevile ni kiasi gani cha fedha kilichokusanywa kutokana na faini wanazopigwa wamiliki wa magari ambao wanaingiza magari yao bila kukaguliwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRA* na uuzaji wa magari. Kumekuwepo na malalamiko mengi kutoka kwa watu na wafanyabiashara wanaoagiza magari toka nje kwa kutozwa ushuru ambao ni tofauti kulingana na bei halisi ya kununulia

magari yao kama inavyooneshwa na nyaraka za *“bill of lading”.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malalamiko hayo yanatokana na kile kinachosemekana kuwa *TRA* wanakuwa na orodha za bei za kununulia magari ya aina mbalimbali kutoka nchi mbalimbali ofisini kwao. Hivyo kufanya bei inayoonyeshwa na nyaraka za ununuzi kukataliwa na Maofisa wake na kutoza ushuru kwa kuangalia bei walizonazo ofisini kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwaeleza Watanzania ni lini *TRA* imeanza kujihusisha na biashara ya kuuza magari badala ya kukusanya ushuru? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume ya Ushindani wa Kibiashara - *Fair Competition Commission.* Kama ilivyokuwa kwa *TBS*, Tume hii nayo inahusika moja kwa moja katika kuliokoa Taifa letu kuwa jalala la kutupia bidhaa zisizo na ubora na viwango jambo linalosababisha bidhaa zinazozalishwa hapa nchini kuonekana zina bei kubwa kulinganishwa na bidhaa zinazotoka nje. Bidhaa nyingine zinazalishwa hapahapa nchini na kuwekwa nembo kuwa zinatoka nje ya nchi na kuingizwa kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhara ni makubwa kwa viwanda vya ndani na uharamia huu sio kama haujulikani na vyombo na mamlaka husika, kwa mfano mdogo ni kama nilivyoeleza hapo juu, Waheshimiwa Wabunge walipopata nafasi kutembelea viwanda vilivyojificha kwenye maeneo ambayo hayakutengwa rasmi kuwa ya viwanda na bidhaa zake kuingizwa sokoni kinyemela. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza Tume hii iko wapi wakati hayo yakifanyika na kuonekana kuwa bidhaa za ndani sio shindani kwa mlaji wa mwisho wakati bidhaa feki ndizo zinanunuliwa kutokana na bei kuwa ya chini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Utafiti, Mafunzo na Maendeleo ya Teknolololoji. Taasisi hizo kwa kiwango kikubwa

ni kwa ajili ya kutoa usaidizi wa kuibadilisha sekta nzima ya viwanda ili iweze kuleta tija kwa Watanzania kwa kuwa kichocheo kikuu katika ukuzwaji wa uchumi kwenye sekta nyingine za uzalishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa taasisi hizi za utafiti, bado Serikali hii ya CCM haioni haja ya kuwekeza fedha za kutosha kwa ajili ya kuzifanya ziweze kutimiza majukumu yake kikamilifu pamoja na badhi ya taasisi kama *CAMARTEC* kuweza kuzalisha trekta ililobuni yenyewe kwa kutumia teknolojia ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kwa mwaka huu wa fedha taasisi ya *TIRDO* imetengewa kiasi cha shilingi 130,000,000 tu kwa ajili ya kufanya utafiti na kusambaza teknolojia zilizohakikiwa, kutekeleza mfumo wa ufuatiliaji mazao kwa kutumia teknolojia na kuhakiki maabara ya mazingira na vifaa vya kihandisi. Aidha, taasisi ya *CAMARTEC* imetengewa kiasi cha shilingi 200,000,000 kwa ajili ya kujenga ukuta kuzungukia eneo lake, kuendeleza uzalishaji wa trekta lililobuniwa na *CAMARTEC*, kununua na kufunga jenereta la dharura ili kukabiliana na kukatika kwa umeme, kuendeleza utafiti na uendelezaji wa teknolojia mbalimbali za zana za kilimo. Kambi Rasmi ya Upinzani, haikubaliani na mgawanyo huu wa rasilimali katika Fungu la Maendeleo na hasa kwenye maeneo ya utafiti kutokutengewa fedha za kutosha ni dhahiri kuwa hatuna nia ya dhati ya kuimarisha sekta hii ya viwanda hapa nchini. Tunataka maelezo ya kina ni kwa nini Wizara hii haioni umuhimu wa kuwekeza kwenye utafiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chama cha Hakimiliki Tanzania – *COSOTA*. Kwa mujibu wa Sheria ya Hakimiliki, Namba 7 ya mwaka 1999 *(Copyright Act No.7 ya 1999) inasema kuwa kazi za cha pamoja na zingine Kifungu cha 47(a) kinasema kuwa "to promote and protect the interests of authors, performers, translators, producers of sound recordings, broadcasters, publishers, and, in particular, to collect and distribute any royalties or other remuneration accorded to them in respect of their rights provided for in this Act"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Chama cha Hakimiliki Tanzania *(COSOTA),* ndio chombo chenye mamlaka ya kusimamia, kuendeleza na kulinda haki za wasanii. Moja ya haki ya msanii ni mapato halali kutokana na kazi yake ya kisanii. Hivi sasa wasanii wengi nchini na hasa wasanii vijana wa muziki wananyonywa na makampuni makubwa yenye nguvu kwa sababu *COSOTA* haina dhamira kutetea na kulinda kazi za wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza kuwa *COSOTA* itoe kanuni kudhibiti biashara ya nyimbo za wasanii kama miito *(ring tones).* Nchini Marekani miito ya simu ni kazi za kisanaa na wasanii *(content creators)* hulipwa si chini ya asilimia kumi (10%) ya mapato kutoka kwenye mitandao ya simu *(network providers)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nchini hakuna kanuni za kuongoza biashara hii ambayo imetokana na maendeleo ya teknolojia. Wasanii wetu wamekuwa wananyonywa kwa sababu ya kukosekana kwa kanuni hizi na hivyo biashara hii kuwa na usiri mkubwa jambo linalopelekea haki kukosekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka uwepo uwazi katika biashara ya *Ringtones* na tunataka vijana wetu wapate malipo halali. Haisadii kuendelea kuwatumia wasanii kuimba kwenye majukwaa ya kisiasa na kuwatosa badala ya kuwasaidia kupata haki zao. Tunataka uwazi na haki katika biashara hii na *ring tones* na ijulikane kiasi gani cha Kodi kinapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Taarifa Rasmi za Bunge, ni kwamba Kambi Rasmi ya Upinzani imekuwa ikitoa mapendekezo kadhaa kuhusiana na kuimarisha COSOTA, kama vile *"Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kuwa Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki Na.7 ya mwaka 1999 ifanyiwe marekebisho kwa lengo la kuipa meno zaidi ya kulinda haki na kuhakikisha wasanii wananufaika na kazi zao. Moja ya mapendekezo ni kuifanya COSOTA kuwa chombo chenye nguvu zaidi katika*

*kulinda kazi za Wasanii kuliko ilivyo hivi sasa. Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo katika sehemu ya marekebisho tunayopendekeza, Kambi Rasmi ya Upinzani tunataka Sura Na. 218 ya Sheria ya Hakimiliki na Hakishiriki, ifanyiwe marekebisho ili kuunda Mamlaka ya Hakimiliki Tanzania (Copyright Regulatory Authority of Tanzania (CORATA) badala ya kuiacha COSOTA kama ilivyo hivi sasa". Hansard ya tarehe 11.8.2011.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu ulitokana na ukweli kwamba *COSOTA* ipo kisheria lakini haina nguvu kisheria au meno kupambana na uharamia ulipo katika tasnia ya hakimiliki jambo linaloinyima nchi na wasanii haki zao stahiki kutokana na kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, *Hansard* 18 Juni,2012 inaonyesha kuwa *"Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo, Serikali mwaka 2006 kupitia Gazeti la Serikali Na. 18 la tarehe 10 mwezi wa Februari, ilianzisha utaratibu wa HAKIGRAM kama stiker maalumu za kazi halali za wasanii zinazotolewa na COSOTA. Kambi ya Upinzani tunapendekeza utaratibu huo uendelee na Mamlaka ya Mapato (TRA), ihusike kukusanya mapato kwa ajili ya kazi hiyo na COSOTA wataratibu utoaji wa HAKIGRAM. Hii itaenda sambasamba na kuzuia uchakachuaji wa HAKIGRAM hizo ili kutopoteza lengo la kuweka mfumo huo. Stiker zisitolewe na TRA bali zitolewe na COSOTA na TRA isimamie eneo la mapato tu. Hii itasaidia kwani stiker hizi hazitatumika kupata mapato pekee bali pia kuweka kumbukumbu muhimu za kazi za wasanii".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba juhudi hizo zote zimeshindwa kuwanufaisha wasanii na Serikali, kwani bado kuna wajanja wachache wanaochukua *"lion share"* katika biashara nzima ya sanaa na kuacha wasanii katika mlolongo mzima wa kazi za sanaa kukosa wanachostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inataka kupata taarifa kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Uhuru

wa bidhaa iliyopitishwa na Bunge kwa shinikizo la Wabunge wa Upinzani. Sheria ile inataka kila kazi ya sanaa inayouzwa nchini kama *CD, DVD* na kadhalika iwe na *stamp* za *TRA*. Tunapenda kujua kuwa atakayepewa *stamp* hizo ni nani? Msanii au Msambazaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uelewa wa mnyororo wa thamani *(value chain)* wa biashara hii ni muhimu sana. Wasanii wetu huuza haki zao kwa wasambazaji kwa sababu ya umaskini, ni vizuri kuhakikisha kuwa hakimiliki inabakia kwa msanii na msambazaji azuiwe kikanuni *(Fair Competition Regulation)* kuwa mzalishaji *(producer).* Hii itasaidia sana *"authors"* na *"producers"* kubakia na hakimiliki na msambazaji auziwe na *producers/authors* haki ya kusambaza tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ni muhimu sana *stamp* zitolewe kwa msanii na mzalishaji tu *(producers)* na sio *distributors*. Hii itatoa nguvu kwa wasanii na itakata unyonyaji wa wasambazaji kwa wasanii wetu ambao hivi sasa wamegeuzwa waajiriwa wa makampuni ya usambazaji wa kazi za sanaa. *COSOTA* na *FCC* wasikwepe wajibu wao wa kusimamia tasnia na kudhibiti ushindani ili wasanii wa Tanzania wafaidi jasho lao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya viwanda. Ukuaji wa sekta ya viwanda kwa mwaka 2011/2012 ulikua kwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.9 mwaka wa fedha 2010/2011 na mchango wake katika Pato la Taifa uliongezeka kutoka asilimia 9.6 mwaka 2010/2011 na kufikia asilimia 9.7 mwaka 2011/2012. Ongezeko dogo la mchango wa sekta hii haukuweza kumnufaisha mwananchi moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2008, idadi ya viwanda vilivyokuwa vinafanyakazi kwa upande wa Tanzania Bara ni 729. Kati ya idadi hiyo ya viwanda, vilivyokuwa katika Mkoa wa Dar es Salaam ni (383), Arusha (51), Mwanza (39), Singida (27), Tanga (27), Kagera (26) na

Kilimanjaro (24). Kati ya viwanda hivyo vilivyokuwepo mwaka 2008, viwanda 643 vinamilikiwa na watu binafsi na viwanda 72 vinamilikiwa na Serikali na vilivyobaki 14 vinamilikiwa kwa pamoja kati ya Serikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kuwa viwanda 549 vinamilikiwa kwa asilimia mia moja na wazawa na viwanda 121 vinamilikiwa na wageni toka nje ya nchi na vilivyobaki takriban viwanda 59 vinamilikiwa kwa ubia kati ya Serikali na watu binafsi au wageni na wazawa. Aidha, kati ya viwanda 729 vilivyokuwepo mwaka 2008, asilimia 93 au viwanda 680 ni viwanda vya uzalishaji bidhaa, kati ya hivyo asilimia 93, viwanda 240 vinajihusisha na uzalishaji bidhaa za chakula, vinywaji na tumbaku na mashine za kusaga nafaka 61.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu walioajiriwa katika viwanda hivyo walikuwa ni watu 117,622 na kati ya hao 107,388 wako katika viwanda vya uzalishaji, viwanda vilivyo Dar es Salaam vimetoa ajira kwa wafanyakazi 34,554 au asilimia 29. Viwanda binafsi 643 vimeajiri jumla ya watu 103,237 ikilinganishwa na jumla ya watu 12,394 waliokuwa wanafanyakazi kwenye viwanda 72 vinavyomilikiwa na Serikali. Viwanda vilivyokuwa vinamilikiwa na wazawa viliajiri jumla ya watu 53,950 kwa kulinganisha na watu 42,192 walioajiriwa na viwanda vinavyomilikiwa na wageni. Aidha, walioajiriwa na viwanda vinavyomilikiwa kwa pamoja kati ya Serikali, watu binafsi (wageni, wazawa na nchi za nje) ni 21,515, hii ni kwa mujibu wa *Annual Survey of Industrial Production, 2008*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mpango wa maendeleo wa miaka mitano, mwaka huu wa fedha vipaumbele kwa Wizara hii ya Viwanda na Biashara ni kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya uwekezaji, hasa katika maeneo maalum ya uwekezaji *(EPZ/SEZs),* kuendelea na utekelezaji wa mradi wa Kituo cha Biashara na Uwekezaji Kurasini *(Kurasini Logistical Trade Hub),* utekelezaji wa miradi ya makaa ya Mawe Mchuchuma na Liganga pamoja na

magadi katika Bonde la Engaruka. Aidha, ni uendelezaji wa viwanda vinavyotumia rasilimali zinazopatikana hapa nchini kama vile usindikaji wa bidhaa za kilimo, nguo, makaa ya mawe, gesi asilia na chuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchunguzi uliofanywa na gazeti la Raia Mwema ulibaini kampuni kadhaa kubwa na maarufu nchini zinazojihusisha na biashara ya chuma chakavu katika mfumo unaoikosesha nchi mapato kupitia kodi. Moja ya kampuni hiyo ni ile iliyopata kuuziwa na Serikali baadhi ya viwanda vya nguo, pamoja na mashamba ya mkonge na chai, ambayo badala ya kuwekeza imekuwa ikiuza mitambo waliyokuta katika viwanda hivyo kama chuma chakavu, bila kuzingatia utaratibu na mikataba ya mauziano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyakati tofauti nyaraka za mauzo zinaonyesha kuwa wamekwishauza mitambo mbalimbali kwa jumla ya Sh. 438,184,000. Mitambo iliyouzwa ni ile ya viwanda walivyouziwa na Serikali katika Mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam na Mara, Mjini Musoma. Mauzo kwa mitambo ya viwanda walivyonunua vilivyopo Dar es Salaam kwa awamu ya kwanza yalifanyika Februari 15, mwaka 2010 (Sh. Milioni 8.6), mauzo ya awali ya pili ni Agosti 12, mwaka 2010 (Sh. 108,625,000). Uuzaji mwingine wa mitambo ya moja ya viwanda vilivyonunuliwa na kampuni hiyo Mkoani Morogoro ulifanyika Februari 22, 2010, kwa mauzo ya Sh.72,500,000. Mkoani Musoma mauzo ya mitambo kama chuma chakavu yalifanyika Aprili 24, mwaka jana, kwa thamani ya Sh.248,359,000. Mmiliki wa viwanda hivyo anajulikana na mwanaye ni Mbunge katika Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali, kuwaeleza Watanzania ni kwa vipi viwanda vitafufuliwa wakati waliobinafsishiwa viwanda hivyo wanang'oa mitambo na kuuza kama chuma chakavu na viwanda vinabaki kuwa maghala kwa maana kwamba mashine zilizong'olewa zilikuwa zinafanyakazi kwa asilimia mia na kufanya kiwanda kuhimili kiasi kikubwa cha pamba

iliyozalishwa hapa nchini, lakini mashine zilizoletwa zinafanyakazi kwa asilimia kumi tu? Tutawezaje kukuza ajira kama viwanda vyetu vinauwawa makusudi, mitambo inang'olewa na kuuzwa kama chuma chakavu na Serikali ipo, inaona na haichukui hatua yoyote? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi imekuwa ikisema mara zote kuwa mambo haya yanatokea kutokana na ukweli kwamba waliobinafsishiwa viwanda ni washirika wa Karibu na CCM. Jambo hilo limepelekea kutokuchukuliwa kwa hatua zozote kwa watu hao ambao wanakiuka mikataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkazo wa uendelezaji wa viwanda hasa vinavyotumia malighafi za kilimo utapelekea kubadilika kwa mfumo ambao umezoeleka wa kilimo kuwa ndio sekta inayotoa ajira zaidi na sekta ya viwanda kuwa ndio mhimili mkuu katika utoaji wa ajira. Ili kufikia hapo ushirikiano kati Serikali na sekta binafsi ni muhimu sana ili kufufua sekta ya viwanda upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ndogo ya nguo. Ukuaji wa uchumi usiozalisha ajira ndiyo moja ya sifa za uchumi wa Tanzania katika kipindi cha muongo mmoja (2001 – 2011). Taarifa ya hali ya umasikini nchini (*PHDR* 2011) kwa kukata tamaa kabisa, imesema licha ya kasi ya ukuaji wa uchumi wa Tanzania kuwa kubwa na ya kuridhisha, uzalishaji wa kazi (ajira) umekuwa ni wa kukatisha tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha katika kila Watanzania 650,000 wanaoingia katika soko la ajira kila mwaka 610,000 wanakosa ajira. Uchumi unashindwa kuzalisha ajira za kutosheleza vijana wanaoingia kwenye soko la ajira. Hata vijana wasomi waliosoma kwa fedha za walipa kodi nao wanahangaika mitaani bila kazi kwa kipindi kirefu mara baada ya kuhitimu masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imekamilisha uandaaji wa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ndogo ya Nguo na Mavazi. Mkakati huo umeandaliwa kwa ushirikiano na

*Gatsby Charitable Foundation (GCF)* ya Uingereza na Tanzania *Gatsby Trust (TGT).* Madhumuni ya Mkakati huu ni kufufua na kundeleza sekta ndogo ya nguo na mavazi ambapo itaanza na uanzishaji wa Kitengo cha Kusimamia mradi husika *(Textile Development Unit –TDU).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vyetu vya nguo vinaweza kuwa na ushindani kutokana na gharama ndogo za wafanyakazi (Tanzania US$ 0.4 kwa saa), ikilinganishwa na India (0.75), China (0.9) Turkey (4 USD), Misri (0.9), Italy (24 USD) na umeme. Changamoto inayokabili sekta hii ni ukosefu wa umeme wa uhakika; gharama kubwa za upatikanaji mitaji – riba: Tanzania (16-17 %), USA (4%), China (6%), Italy (4%); mashine nyingi za zamani ambapo (90%) ya mashine zina zaidi ya miaka kumi na 50% zina zaidi ya miaka 20 na kumekuwa na uwekezaji mdogo. Viwanda vya mavazi vimeshindwa kujiendesha kutokana na gharama kubwa za kodi ya pango, umeme usio wa uhakika, viwanda kujikita katika utengenezaji wa khanga na vitenge tu, viwango vidogo vya kuingiza mbinu za uhandisi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyabiashara, Wakulima na Wenyeviwanda *(TCCIA)* katika Mkoa wa Dar es Salaam, Ndg. Edgar Nkunda, katika ushuhuda wake kuhusu uongezaji thamani bidhaa za pamba, kwani alipata kuwa ni mmiliki wa kiwanda cha nguo kwenye hatua fulani ya mchakato wa kutengeneza nguo. Alikuwa akinunua nyuzi (*yarn*) kutoka kwenye viwanda vikubwa na kutengeneza vitambaa (*fabrik*) baada ya mchakato wa usokotaji (*weaving*) kama ilivyo kwenye mnyororo wa kuongeza thamani wa sekta ya nguo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *"Kiwanda chake kidogo kilitoa ajira kwa watu 40. Mwaka 2007 na 2008 tatizo la mgawo wa umeme likayumbisha biashara yake".* Mwaka 2008 na 2009 mdororo wa uchumi duniani ulitikisa sio wateja wake tu bali sekta nzima ya pamba. Haya mambo mawili, mgawo wa umeme na kukosa soko la bidhaa zake, yalimfanya afunge biashara, akang'oa mashine za kiwanda chake na kuuza

kama chuma chakavu. Vijana wenzake 40 wakakosa kazi na yeye akaingia katika biashara ya kutengeneza batiki anayofanya hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani kote sekta ya nguo ndio hutumika kutoa ajira nyingi sana kwa wananchi na hasa wanawake. Sekta ya nguo ni sekta mkakati ya kukuza ajira nchini, sekta ya nguo pekee inaweza kutengeneza ajira 100,000 hapa nchini kwa kiwango cha sasa cha uzalishaji wa pamba. Uzalishaji wa pamba nchini ukiongezeka maradufu na kufikia angalau marobota milioni 1.5, sekta ya nguo itaweza kuzalisha ajira mpaka 250,000 kupitia kwenye uchambuzi (*ginneries*), nyuzi (*spinning*), vitambaa (*weaving*) na nguo (*garments*). Hii ni kwa mujibu wa Raia Mwema, Toleo la 271, tarehe 5 Desemba, 2012, Tunahitaji uamuzi mgumu kisiasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misingi hii ya ajira sio kwamba haikuwapo. Waasisi wa taifa waliona umuhimu huu na ndio maana wakati mwaka 1967 hapakuwa na chembe ya pamba ya Tanzania iliyokuwa ikifanyiwa mchakato ili kupata nguo (kwa maana ya kuongeza thamani hapa hapa nchini), mwaka 1975 kulikuwa na viwanda vinane vya nguo. Utafiti unaonyesha kuwa mahitaji ya matumizi ya nguo hapa nchini ni sawa na marobota milioni mbili kwa mwaka. Kwa hiyo, pamba tunayoiuza nje kama '*yarn'* hurudi nchini kama vitambaa au nguo zilizokamili. Hivyo kazi nyingi sana zinakuwa zimepelekwa nje kwa kuuza pamba ghafi nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka tunaanza mchakato wa ubinafsishaji kulikuwa na viwanda takribani 12 vya nguo, ikiwa ni pamoja na kiwanda kikubwa cha nyuzi Tabora. Watanzania kwa maelfu waliajiriwa kwenye viwanda vya nguo. Hivi sasa ni viwanda vichache kati ya vilivyouzwa kwa wawekezaji binafsi vinafanya kazi. Vingi ukiondoa kiwanda cha *21st Century* cha Morogoro na A to Z cha Arusha, vinatumia malighafi kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suluhisho la kujinasua na

balaa hili kwa sasa ni sekta ya viwanda vidogovidogo kupata msaada mkubwa toka ndani na nje kama kweli Serikali ina dhamira ya kweli kuwasaidia wadau katika sekta hii kuwekeza katika eneo la *weaving* na *garments*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyaraka za Wizara zinasema kuwa, "… kati ya viwanda vya zamani vilivyokarabatiwa na kufanyiwa upanuzi ni pamoja na Kiwanda cha Zana za Kilimo (UFI) ambacho sasa kinaitwa *Tanzania Steel Pipes (TSP)*, Dar es Salaam". Nini hatma ya uzalishwaji wa zana za kilimo kwani kiwanda cha UFI kimebadilishwa na kuwa kiwanda cha kuzalisha mabomba na kiwanda cha ZZK Mbeya limekuwa ni ghala la kiwanda cha bia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mwekezaji aliyenunua UFI alikuwa na mtaji wa kutosha ni kwa nini asiendelee kuzalisha zana za kilimo na uzalishaji wa mabomba uwepo? Uagizaji wa zana za kilimo toka nje ya nchi ni mkubwa sana kwa sasa kutokana na msukumo wa Serikali kwenye kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri wa Viwanda, Biashara na Masoko, Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi (Mb), akiwasilisha Bungeni makadirio ya matumizi ya fedha kwa mwaka 2006/2007, alisema nanukuu: *"Kwa ujumla uwekezaji katika viwanda unaendelea kuongezeka na kutoa nafasi za ajira. Kati ya viwanda vipya vilivyoanzishwa ni pamoja na China Paper Corporation cha Kilimanjaro (ajira 60), Kahama Ginnery and Oil Mill Ltd cha Shinyanga (ajira 120) na Merchandise Products Group cha Kibaha (ajira 20) na viwanda vingine vya kusindika samaki katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa. Aidha, kati ya viwanda vya zamani vilivyokarabatiwa na kufanyiwa upanuzi ni pamoja na Kiwanda cha Zana za Kilimo (UFI) ambacho sasa kinaitwa Tanzania Steel Pipes (TSP), Dar es Salaam; Kiwanda cha Nyuzi Tabora (TABOTEX); Tanzania Dairy Ltd, cha Tanga; Tanganyika Instant Coffee (TANICA), Kagera na Tanzania Pharmaceutical Industries Ltd (TPI), Arusha".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wa Mbunge wa Jimbo la Uchaguzi la Tabora Kaskazini hapo

tarehe 26 July 2012 alisema kwamba *"Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna Kiwanda cha Nyuzi New TABOTEX, imedhihirika kuwa kiwanda hiki hakitumiki ipasavyo, tayari wakulima wamelima pamba jinsi ilivyoahidiwa na uongozi wa kiwanda hicho, lakini mpaka sasa haijanunuliwa na kiwanda hicho, jambo ambalo limeleta usumbufu mkubwa kwa wakulima wa pamba".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kauli hizo mbili, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuna tatizo juu ya utendaji wa Kiwanda cha Nyuzi-Tabora, kwani Serikali ilitoa kauli hiyo mwaka 2006 na ushuhuda wa Mbunge ulitolewa mwaka 2012. Inawezekana kabisa Kiwanda cha Nyuzi cha Tabora baada ya kuuzwa kinafanya kazi ambayo ni tofauti au hailingani na iliyokuwepo kama ilivyo kwa kiwanda cha Ufi cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inataka kupata majibu ya kina kuhusu mafao ya kustaafu kwa waliokuwa wafanyakazi 834 wa kiwanda cha nguo cha Mutex, kwani Serikali iliwapelekea mafao yao kiwango cha kiasi cha shilingi elfu themanini na tatu (83,000) tu kila mmoja, kwa watu ambao walifanya kazi kwa zaidi ya miaka 20 sio tu kwamba ni dharau, bali ni dhihaka kubwa kwa wastaafu hawa na ndio maana walikataa kupokea kiasi hicho cha fedha ambacho hakitoshi hata nauli ya kumsafirisha mtu mmoja kwenda nyumbani kwake achilia mbali kusafirisha familia. Tunaitaka Serikali kama imeshindwa kulipa haki zao ama iwaachie nyumba za kiwanda walizokuwa wanaishi ama wauze nyumba hizo kwa wafanyakazi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vidogo vidogo na vya kati- *(SMEs).* Kwa mwaka wa fedha 2011/2012, sekta ya viwanda na biashara ndogondogo ilichangia takriban asilimia 28 katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba katika nchi nyingi zinazoendelea kuna sehemu kubwa ya biashara

ambayo kwa njia moja au nyingi haikidhi vigezo vya kuifanya kuwa rasmi na hivyo kuingia kwenye mfumo rasmi wa uchumi. Kuna kila dalili kuwa hazijafanyika juhudi za kutosha za kuhamasisha na kutoa mafunzo ya kutosha kwa wahusika ili kuingia kwenye mfumo wa rasmi wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tafiti zilizofanywa na *"The Tanzania Private Sector Foundation, FinScope na Esaurp"* kwa kutumia vigezo tofauti lakini walifikia mwafaka kuwa hapa Tanzania kuna kati ya viwanda milioni 2.5 na 3 ambavyo havijarasimishwa *(backyard production),* lakini vinafanya kazi. Aidha, inakadiriwa kwamba asilimia 48 ya uchumi wa Tanzania upo kwenye sekta isiyo rasmi. Hii ni kwa mujibu wa kitabu cha *"Transforming the Informal sector, how to overcome the challenge"* kilichotolewa na taasisi ya *ESAURP*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa safari za Kamati ya kudumu ya Bunge yenye jukumu la kusimamia sekta ya viwanda ilijionea ni jinsi gani viwanda vingi vya raia wa kigeni vinavyozalisha bidhaa mbalimbali katika mazingira ambayo sio mwafaka kwa uzalishaji na bidhaa zao zinaingizwa kwenye soko kwa nembo ya *made in China* au India wakati zinazalishwa Tanzania. Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kabisa hadi Waheshimiwa Wabunge wanapelekwa kutembelea maeneo hayo, ni dhahiri Serikali na vyombo vyake vya dola inafahamu, hoja ni kwa nini hatua hazichukuliwi ili kuhakikisha Serikali inapata inachostahili na mazingira stahili kwa wafanyakazi katika viwanda hivyo yanaboreshwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kitabu hicho cha *ESAURP* kilichonukuu taarifa ya *Intergrated Labour Force Survey (ILFS)* ya mwaka 2006, ulinganisho wa sekta isiyo rasmi kati ya mwaka 2001 na mwaka 2006 inaonyesha kuwa watu walio kwenye sekta isiyo rasmi ilizidi kuongezeka kutoka watu 2,013,832 na kufikia watu 3,312,774, ambalo ni ongezeko la takriban asilimia 65 kwa kipindi cha miaka mitano. Watu wengi wanaojihusisha na sekta ndogo ya biashara ya

wachuuzi ndio wanaoongezeka, sawa na asilimia 57 ya sekta nzima isiyorasmi. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni kwa nini sekta hii isiyo rasmi inazidi kuwa kubwa wakati bajeti kwa taasisi husika za kuhakikisha urasimishaji wa shughuli za kiuchumi zinatolewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi za Fedha na Uwezeshaji wa Viwanda. Sekta ya viwanda vidogo na biashara ndogo kwa mujibu wa taarifa rasmi za Serikali kwa Waheshimiwa Wabunge (Randama ya Wizara), ilichangia takribani asilimia 28 katika pato la Taifa kwa mwaka wa fedha 2012 na kutoa ajira kwa Watanzania milioni 5.2 huku ikihusisha wajasiriamali milioni tatu. Kitabu cha Mpango wa Maendeleo ya miaka mitano, uk. 71, unaonyesha kuwa sekta ya viwanda kwa mwaka 2011 ilikuwa imeajiri watu 120,000 na ilitarajiwa kuajiri jumla ya watu 221,000 ifikapo mwaka wa fedha 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapenda kupata taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge, takwimu za hao Watanzania walioajiriwa na sekta ndogo ya viwanda na biashara zina ukweli kwa kiasi gani, kulinganisha na takwimu zilizopo katika Mpango wa Maendeleo kama nilivyozinukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa mwaka wa fedha 2012/2013 alitoa ahadi kuwa Serikali itaanza kulifanyia kazi eneo hili na kutoa mapendekezo ya kuboresha mchakato wa ujenzi wa viwanda katika uchumi wetu. Nchi zote zilizofikia hadhi ya nchi za kipato cha kati zimekuwa zikitekeleza na kuzingatia mikakati ya jinsi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ahadi hiyo ya Mheshimiwa Waziri inaonyesha dhahiri kuwa Serikali haina mpango wa kuvirudisha viwanda vilivyobinafsishwa ambapo wahusika walishindwa kutimiza/walivunja masharti au matakwa ya mkataba au kufufua viwanda visivyofanya kazi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hadi

sasa viwanda vilivyobinafsishwa kama vile vinavyojihusisha na uchakataji wa mazao ya kilimo hasa korosho, pamba na matunda ikoje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika viwanda vipya hapa kwetu, hasa kwa Watanzania ni kazi ngumu sana kutokana na ukweli kwamba, sekta ya benki bado haijakua kiasi cha kufanya uwekezaji mkubwa na wa muda mrefu. Hivyo ingekuwa ni bora zaidi kwa viwanda vilivyokuwepo kuvifanyia ukarabati wa kuondoa mashine ambazo zimepitwa na wakati kiteknolojia na kuweka mashine/ mitambo mipya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo chochote cha uanzishaji wa viwanda ambacho hakitahusisha umiliki wa wananchi, ni dhahiri kuwa kosa lililofanyika wakati wa uanzishwaji wa Mashirika ya Umma ambayo hatimaye ilikuja sera ya ubinafsishwaji litakuja kujirudia na hapo ndipo uhalali wa uwepo wa Serikali ileile utaanza kuhojiwa, “kutenda kosa si kosa bali kosa ni kurudia kosa”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Randama ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2011/2012 ilieleza kwamba Serikali ililenga kuongeza mtaji wa shilingi bilioni 500 kwa *TIB* katika kipindi cha miaka mitano kuanzia 2010 na hadi mwaka wa fedha 2012/2013, Serikali ilikuwa imeweka shilingi bilioni 60. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge na wananchi, je, hizo shilingi bilioni 500 ni kwa ajili ya uanzishwaji wa viwanda tu au ndio fedha hizo kwa ajili ya uwekezaji katika sekta mbalimbali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mkakati Unganishi na Mpango Kabambe wa Sekta ya Viwanda (*Integrated Industrial Development Strategy and Master Plan)* unalenga Mwambao wa Pwani kuwa Kitovu cha Kuendeleza Viwanda na Kukuza Mauzo Nje *(Water Front Industrial and Export Frontiers*). Mkakati huo unalenga kufanya usindikaji wa mwanzo (*primary processing*) Mikoani, usindikaji wa kati na usindikaji kwa ajili ya mauzo nje kufanyika katika maeneo ya

Mwambao wa Pwani ambao utakuwa kitovu cha kuendeleza viwanda na kukuza mauzo nje. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona dhana hii inaweza kuwa na mapungufu kutokana na ukweli kwamba viwanda vya usindikaji wa mwanzo vinatakiwa viwekwe maeneo ya uzalishaji na kila kona ya Tanzania kuna uzalishaji wa zao moja muhimu ambalo ni tofauti na eneo lingine, hivyo kuweka viwanda hivyo katika ukanda wa Mwambao wa Pwani ni kosa la kiufundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masoko. Ukubwa au udogo wa soko una mahusiano ya moja kwa moja na tija katika uzalishaji viwandani. Kwa mahusiano haya ya soko na uanzishwaji wa viwanda na ukuaji wa uchumi yana athari za moja kwa moja katika uwekezaji katika sekta ya viwanda. Kwa nchi inayohitaji kujikamua katika lindi la umaskini kuanzisha viwanda bila ya kuwepo kwa mkakati makini wa kuhakikisha kuwa bidhaa zitakazozalishwa zinapata soko inaweza kuwa ni msingi wa kuua viwanda hivyo kutokana na ushindani wa bidhaa ambazo tayari ziko sokoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vingi nchini Tanzania vinazalisha kwa ajili ya soko la ndani na wastani wa asilimia 22.6 ya bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu ndizo zinazouzwa katika masoko ya nje ya nchi na mauzo ya bidhaa nje ya nchi yanajumuisha tumbaku, bidhaa za karatasi, nguo na vyakula vilivyosindikwa. Bado viwanda vingi vya Tanzania havijatoa msukumo wa kutosha katika kutangaza bidhaa zake na kutumia vizuri fursa za masoko ya kikanda. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni mkakati gani wa makusudi imeuweka ili bidhaa za viwanda vyetu hasa vile vidogo na vya kati viweze kupata masoko nje ya nchi? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuweka hadharani aina ya bidhaa zitakazozalishwa na masoko yake ili tathmini ya uanzishwaji huo ifanyike vyema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Kiwia. Sasa Waheshimiwa Wabunge tuna wachangiaji sita na tunaanza na Mheshimiwa Deogratias Ntukamazina na Mheshimiwa Said Mussa Zubeir ajiandae.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona. Nianze kwa kuunga mkono hoja na kwa kweli hotuba ya Waziri imeleta matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninachangia hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara mwaka juzi, nilizungumza kwa masikitiko makubwa sana nikieleza jinsi viwanda vyetu vilivyouwawa kutokana na Sera ya wakubwa wawili ambao wote sasa hivi ni marehemu. Marehemu Ronald Reagan aliyekuwa Rais wa Marekani pamoja na Magreth Thatcher akiyekuwa Waziri Mkuu. Wao walikuja na Sera ya sekta binafsi kuwa mhimili wa uchumi na wakasema kuwa sekta ya Umma haifai. Kwa hiyo, baada ya hapo tukaanza kuuza viwanda vyetu kwa bei powa na kwa wawekezajia ambao wengine walikuwa ni matapeli na hawakuweza kuendeleza viwanda hivyo na wakageuza hata matumizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niliwahi kusimamia viwanda vyote na Mashirika yote kwa miaka sita kuanzia 1986-1991, nimekuwa nikisononeka sana na hata ilipokuja Dira yetu ya Maendeleo *(Vision 2025)* kwamba ifikapo mwaka 2025 tutakuwa ni nchi yenye uchumi wa kati na yenye viwanda vingi, mimi niliendelea kuwa *pessimistic,* niliona kuwa haiwezekani kwa sababu viwanda vingi vimeuwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nikiri kwamba baada ya kufanya utafiti na kuzungumza na watu wa *NDC* na kujua kazi nzuri inayofanywa na *NDC* na imeelezwa hata katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri, nimeanza kuwa na matumaini kuwa ifikapo mwaka 2025, tunaweza kuwa na viwanda vingi. *NDC* tumeambiwa ifikapo mwaka 2016 itakuwa imeshaanzisha kiwanda cha *Soda Ash*, Chuma cha Liganga

pamoja na Makaa ya Mawe ya Mchuchuma wameshapata mwekezaji, Makaa ya Mawe ya Ngaka wanaendelea vizuri na wanaweza ku-*export.* Nimefurahi kuwa *NDC* wamekabidhiwa *General Tyre* na watazalisha sasa matairi yenye uhakika, pia *NDC* wamekabidhiwa wafufue ile *Kilimanjaro Machine Tools,* wamekabidhiwa mambo mengi na wanafanya kazi nzuri, nimezungumza nao na wanasimamia ile *Wind Power* ya Singida lakini nimesikitika kuwa hawawezi kufufua kiwanda cha *Mangula Mechanical Machine Tools* kwa sababu mitambo yake ilishauzwa na mtu mmoja anakabidhiwa aanzishe shule, hiyo imenisikitisha sana ingawa nimemsikia Waziri anasema watafufua Kiwanda cha Mungula nitashukuru sana kama itakuwa hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuihimiza *NDC* ifufue viwanda vya nguo. Wameagizwa na Rais wafufue viwanda vya nguo na watasaidia pia kuanzisha viwanda vya *Agri-business* au *Agro-industries* ili kuongeza thamani ya mazao yetu ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, naomba sana UFI, *Ubungo Farm Impliments* iliuzwa kwa mtu ambaye aligeuza matumizi, anazalisha mambomba lakini hatuwezi kuendelea bila kuwa na kiwanda kinachozalisha zana za kilimo. Naomba tuanzishe kiwanda cha aina ya *Ubungo Farm Impliments* na tufufue kiwanda cha Mangula. Naiomba Wizara ya Nishati na Madini pamoja na Wizara ya Maji, waharakishe miundombinu ya umeme na maji ili kusaidia viwanda hivi ambavyo vinaanzishwa kwa haraka ili tuweze kuwa nchi yenye viwanda vingi ifikapo 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye *SIDO, SIDO* ndiyo tegemeo la wananchi wa kawaida. Naiomba Serikali isaidie *SIDO* waeneze viwanda vidogo, Ngara, Kibondo, Pangani na kila mahali. Tutaweza kufaidika na viwanda vya *SIDO* iwapo tutapata umeme wa gridi huko vijijini. Kwa hiyo, Serikali ni moja wafanye kazi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie *TBS. TBS* haifanyi kazi yake vizuri. Tumeona majengo yanavyoporomoka kutokana na uhafifu wa vifaa vya ujenzi lakini mnavyoona majengo yanaporomoka hivyohivyo ndivyo watu wavyokufa kutokana na vyakula vya ajabu vinavyokuwa *imported.* Siku hizi hata watoto wadogo wanapata kisukari, wanakuwa *high pertensive,* shauri ya hivyo vyakula kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye suala la sera ya uzawa. Mimi kama *senior citizen* ni lazima nisisitize sera ya uzawa. Tumejifunza kutoka Malaysia mbinu ya kusimamia utekelezaji wa miradi muhimu, inaitwa *Big Results Now* au ile *Presidential Delivery Bureau*. Tumejifunza, hicho ni kitu kizuri lakini ngoja niwakumbushe kwamba kama tumejifunza hivyo tujue kwamba Malyasia ilivyo sasa ni kutokana na sera yao ya uzawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye miaka ya themanini, Waziri Mkuu aliyekuwepo Mahadhir Muhammad aliwaeleza Wachina waliokuwa wanamiliki uchumi wa Malaysia, akawaambia kwamba tusipowashirikisha wazawa wa Malyasia, *indigenous Malays,* watawachinja. Baada ya hapo, wakaanzisha sera za upendeleo na sasa hivi wazawa wa Malaysia wanashindana kibiashara pamoja na Wachina ambao sasa hivi wazawa wameinuliwa sana kiuchumi. Hili Baraza la Uwezeshaji ni kitu kidogo sana, wanasaidia VICOBA, wanasaidia *SACCOS*, sisi tunataka tuwe na akina Mengi wengi, tuweze kumiliki uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati najifunza mambo ya *Marxism-Leninism*, nilipenda sana dhana ya *superstructure versus economic base*. Sisi Watanzania wazawa tupo kwenye siasa tu, *we are not in control* ya *economic base*. Kwa hiyo, ni lazima tufikie huo wakati ambao tunakuwa kwenye *economic base. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka sana kabla sijaishiwa na muda, kabla sijaenda Ngara, namkumbuka aliyekuwa Waziri wa Viwanda, Iddi Simba. Mheshimiwa Iddi

Simba alifanya kazi nzuri sana ya uzawa. Aliorodhesha biashara ndogondogo ambazo zinatakiwa zifanywe na wazawa lakini sasa hivi zinafanywa na Wachina na Wakorea kule Kariakoo. Ni lazima sasa tuwafikirie wazawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna nchi kama Ethiopia, mimi nimekaa Ethiopia miaka kumi nikiwa *consultant* kwenye *African Union,* yale majengo yote na viwanda vyote ni vya Wahabeshi. Kenya pia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa!

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** *Ooh my Goodness*!

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Sijazungumzia suala la Ngara.

**MWENYEKITI:** Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Said Mussa Zubeir.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nimshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na mwenye kurehemu, kwa kunipa nafasi hii leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Waziri ila nasikitika kwamba Wizara hii haikutendewa haki, Wizara hii ni kubwa tofauti na muda iliyopewa. Mimi ninasema imepewa nusu siku, maana yake hata siku haijatimia, sasa hivi saa sita, ikifika saa saba tunakwenda *lunch* tukirudi Waziri anakuja ku-*wind up*. Hii Wizara ni kubwa, tunapozungumzia viwanda na kama tunahitaji maendeleo ya nchi hii yapo kwenye viwanda.

Kama watazungumza watu wanne na nina hakika Wabunge wengi wanataka kuongea, sidhani kama tutafikia mahali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee haraka haraka kuhusu suala la fedha za maendeleo za bajeti iliyopita. Leo tunazungumzia bajeti ya mwaka 2013/2014, mimi nirudi mwaka 2012/13. Fedha za ndani za maendeleo, hapa panashangaza sana na inabidi mtu ufike mahali ujiulize maswali mengi. Hivi *are we serious*? Ni lazima tujiulize kweli sisi tuna uhakika wa tunachokizungumza kwamba tutakifanya na kitakuwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za ndani ziliidhinishwa na nilifurahi sana kwa sababu zilikuwa zinatosheleza, karibu shilingi bilioni 123 kwa ajili ya maendeleo kwenye Wizara hii. Ukiziangalia fedha zenyewe zilikuwa zinaelekea kwenye maeneo mawili muhimu au matatu lakini moja unaweza ukasema kwamba linaweza likasubiri. Ukiangalia katika maeneo hayo mawili muhimu yaliyokusudiwa hizi fedha ziende, mpaka leo tunazungumza kwamba hiyo bajeti ambayo ndiyo tunaipa mgongo, kulikuwa na *minitiger* ambayo ilikuwa imetengewa shilingi bilioni 50.2 katika hizo shilingi bilioni 123. Kulikuwa na *Logistic Center Tanzania and China*, wao vilevile walikuwa wanahitaji shilingi bilioni sitini. Cha kushangaza au jambo la kutia aibu ni kwamba mpaka hivi leo, hawa wengine wamepewa shilingi bilioni 10.9, hawa wengine unaweza ukasema wamepewa shilingi milioni mia tano hamsini na tano Watanzania wakasikia wamepata kasoro labda shilingi bilioni tano kumbe siyo shilingi bilioni ni shilingi milioni mia tano yaani nusu bilioni. Leo tunamaliza mwaka hakuna chochote kilichotendeka, hivi kweli tunahitaji mabadiliko ya nchi hii? Hili ni swali tunatakiwa tukae tujiulize.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni afadhali tuwe na jambo moja la kufanya kuliko ku-*disperse* pesa ambapo baadaye kunakuwa hakuna kitu chochote kilichofanyika, kama vile tuna *mark time*. Hili halitusaidii kugeuza Bunge hili kama labda nyumba ya Ibada, kwa sababu nyumba ya Ibada ndiyo watu

hukaa wakagawana sadaka. Sadaka ile inaweza isimsaidie mtu kushiba wala kumwondoshea hamu, ndivyo tunavyo fanya lakini ni afadhali tukatenga fedha kidogo lakini tukahakikisha kwamba hizi fedha zimefikia mahali...

**TAARIFA**

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa!

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nimpe taarifa mchangiaji kwamba nyumba ya Ibada huwa hawagawani sadaka. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa endelea.

**MHE. SAID MUSSA ZUBEIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia, inawezekana ya kwake yeye, ya kwetu sisi tunagawana sadaka na aghalabu hupata waumini wote na pengine isisaidie chochote ikawa mtu kapata tu sadaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata leo *memo* kwamba kuna uwezekano wa kupelekwa shilingi bilioni 25. Namshukuru Waziri wa Fedha kwa kufanya utaratibu huu haraka lakini bado ninasema tumechelewa. Katika shilingi bilioni 25 hizi ningeomba basi zielekezwe upande mmoja angalau zipelekwe kwenye *Logistic Center* ambapo bado zitakuwa hazijafanya kazi, tunahitaji zingine karibuni shilingi bilioni 35, sasa Waziri atakapokuja ku-*wind up* hili atatuelezaje? Tufanye kitu kimoja kikamilike kuliko kuzitawanya na hizi shilingi bilioni 25 ambazo tunasikia leo imefanyika *transaction* na zitakuwa zimeingia Wizarani. Naipongeza Serikali kwa hili lakini nauliza, je, shilingi bilioni 35 zitakwenda kwa muda gain?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati hapa mbele yangu, nimepokea marekebisho kuna fedha ambazo zinategemewa kwenda na zitakuja kwenye *Appropriation*

*Bill* mwezi wa Saba. Ni sahihi, zikiongezwa hizi, bado pia tutakuwa hatujafikia mahali maana yake 25 na zile 550 ukiongeza na hizi 31 ambayo moja ndiyo tulikuwa tunakuja nayo kwenye bajeti hii, ndiyo kwanza hizo sitini hazijatimia, tupo kwenye 56, hatujafikia hata sitini. Yote tisa, kumi hata hizo sitini sasa hivi siyo sitini tena sasa hivi zipo 94. Sijui atakapokuja Waziri atatuthibishiaje kwamba tusije tukawa tuna *dump* na hizi sasa halafu tukakaa miaka miwili kuja kutafuta hizo 34 zitakazokuwa zimebaki au karibuni 40 hazitakuwa tena 34 zitakuwa tena ni mia moja. Sisi kazi yetu itakuwa ni ku-*mark time* tu. Ninaomba sana kama kweli tunataka kuwasaidia vijana karibu elfu ishirini na tano kuweza kupata ajira kwenye *Logistic Centre* hili suala lifanyike haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi si ajira za watu 25,000 ni ajira karibu za watu laki moja mpaka laki mbili. Kivipi? Ajira ya moja kwa moja ni watu 25,000 lakini hili jengo kwanza wale Wachina pale wao watawekeza karibuni shilingi bilioni 600, ni fedha nyingi sana. Wakiwekeza pale chochote kitakachotokea kile kitega uchumi kitakuwa bado kipo Tanzania kitatusaidia tu. Hii ni faida ya kwanza. Faida ya pili tutatoa ajira nyingine zitakazokuja ambazo zitakuwa ni *indirect* ni nyingi tu. Kuna *hotel* ambazo zitapata watu wengi sana kwa sababu watu watakuja, kwa sababu hii itakuwa ni kitovu katika Afrika, hii itakuwa ni sehemu kubwa sana katika Tanzania yetu na Afrika Mashariki na Kati kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili tunalozungumza ni sahihi kuna ajira ambazo sisi hatujaziona, hizi za *indirect* ni nyingi sana zitakazojitokeza, kuanzia mahoteli, magari hata uwanja wa ndege kwa sababu watakuwa wanamiminika, hawa watakoleta hizi bidhaa na watakaokuja kufuata hizi bidhaa pamoja na Tanzania yenyewe kunufaika. Tanzania itanufaika vipi? Ni lazima tutakapokuwa na ukubwa wa *investment* kama hii, viwanda vitapanuka *automatic* kwa sababu kuna bidhaa ambazo zitakuwa zinahitajika, kwa hiyo kuna viwanda ambavyo havipo sasa hivi vitakuwepo.

Tutakuwa tuna uhakika wa soko kwamba tunalo hapahapa. Hata malalamiko ya watu wa korosho, watu wa pamba haya yote yataondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningeomba Serikali ijitahidi sana na hili suala...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru Mheshimiwa Said Mussa, sasa namwita Mheshimiwa Msigwa ajiandae Mheshimiwa Eustace Katagira.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nisiwe mbali na mchangiaji aliyepita kuhusiana na muda mfupi ambao tumepewa kama Wabunge kuijadili Wizara hii ambayo kimsingi ni Wizara nyeti, ni Wizara muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna idadi kubwa sana ya watu ambao hawajaajiriwa, watu ambao hawana kazi, watu ambao hawawezi kujikimu. Kwa hiyo, naomba sijui ni Waziri au Bunge, kwa kweli *next time* tusingefurahi sana kupewa muda mfupi wa watu wachache wachache kuchangia, ninaamini Wabunge wana mawazo mengi sana, hata wale watu wa Kamati wana mawazo mazuri sana ambayo yangesaidia kuiboresha Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema Taifa letu lina watu wengi sana ambao hawajaajiriwa na sera mbovu zimetufikisha hapa tulipofika. Ukiangalia mikataba ambayo Serikali ilikuwa imesaini au ilikuwa imejiandaa katika MKUKUTA I, ni kwa kukubaliana na masharti ya wafadhili wa nje ambao wlaiitaka Serikali isifanye *production,* ifanye *service* tu. Kwa

hiyo, matokeo yake viwanda vingi vikawa vimekufa, watu waliopewa umiliki wa viwanda hivyo wamejikuta wanageuza yanakuwa magodauni na idadi kubwa ya wananchi hasa vijana wamekosa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamheshimu sana Mheshimiwa Waziri na nina uhakika kabisa na weledi wako. Naamini kwamba Wizara hii unaweza ukai-*transform*. Kuna msemo mmoja wanasema *if the only tool you have in your hands is a hummer you tend to treat every problem as a nail*. Kama kifaa pekee ulichonacho mkononi mwako ni nyundo, utafikiri matatizo yote ni msumari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? Napenda nijikite kwenye eneo la Wamachinga ambao wapo wengi katika Taifa letu hususani hata katika Manispaa yangu ya Iringa Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wamachinga wamekuwa wanapuuzwa, Wamachinga wamekuwa wakidharauliwa na kwenye hotuba yako kidogo umezungumzia kuhusu biashara ndogo. Ni idadi kubwa sana ya wananchi wa Tanzania hawa watu ambao ni *voiceless*, hawa watu ambao ni maskini, ambayo ni *unprivileged*, lakini kila mahali wanafukuzwa kama digidigi kwenye nchi yao wenyewe. Nchi ambayo tuna watu ambao wana weledi wanaweza wakakaa, wakafikiri namna gani ya kutatua tatizo la Wamachinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jamii yetu Wamachinga wameonekana ni watu ambao wanaleta kero, hasa kwa viongozi wanasiasa na wafanyabishara wakubwa. Wanaonekana wanatutinga katika maisha yetu, wanatuvuruga, hatujakaa chini kama Taifa kuona ni namna gani tutatue tatizo la Wamachinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Polisi wamekuwa wakitumika kuwapiga Wamachinga. Kwa bahati mbaya Serikali iliyoko madarakani inadhani kutatua matatizo tunayokabiliana nayo ni kupiga watu virungu. Likitokea tatizo

la Wamachinga wanapigwa, maandamano wanapigwa, *as if tool* tuliyonayo ni nyundo tu. Fundi mzuri ana vifaa mbalimbali, kuna sehemu unahitaji *sellotape*, sehemu nyingine unahitaji bisibisi, sehemu nyingine unahitaji waya, lakini *solution* ya kuwapiga tu hawa watu, tunawaonea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hili kwa uchungu mkubwa sana na ninataka ni-*site* eneo la Iringa ambako tumekuwa na matatizo ya Wamachinga na Tanzania nzima, kwa nini hatuna *model* ambayo itatusaidia wananchi wote Tanzania tuepukane na tatizo hili, tukakaa chini kutatua tatizo hili badala ya kuona ni kero. Suala la Wamachinga haliko Tanzania tu, tumeona Wamachinga wanatengewa maeneo Ulaya, ukienda Marekani, ukienda South Afrika kule nimekaa Durban miaka mitano, Johannesburg, Cape Town, kuna mitaa inafungwa Wamachinga wanafanyakazi zao vizuri na wanapata chakula. Hawa ni watu maskini kabisa wa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wanasiasa wote tuwe wakweli katika maisha yetu, tunawatumia sana vijana hawa wakati wa kura, *we just using them* kama *stepping stone*. Nitoe mfano mmoja, mimi nilikuwa sina hela wakati wa kampeni, akina mama wanaouza ndizi walikuwa na imani na mimi, vijana ambao ni Machinga wanauza soksi kuna mwingine mpaka alinipa zawadi ya soksi, mama alinipa ndizi akasema Msigwa nina imani na wewe, naomba ukatutetee tunanyanyasika. Huyu mama alikuwa mjamzito kwenye Jimbo langu, akasema mtoto huyu nikijifungua kwa sababu naamini utashinda nitampa jina la Peter Msigwa au jina la mke wako Victoria. Alipojifungua yule mama amempa jina yule mtoto anaitwa Peter Junior lakini yule mama anakimbizwa kama swala kwenye nchi yake mwenyewe. Mtaa mmoja unaweza ukafunguwa kwa siku moja ya Jumapili watu wakafanya biashara zao, wakafanya usafi na uchumi wetu ukakua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba ni kipindi kimefika sasa, *Leaders are problems*

*solvers*, ni *solution* gani tunayo-*offer?* Naomba katika majibu yako nijue *solution* gani tunayo-*offer* kwa ajili ya kutatua tatizo hili la Wamachinga ambalo ni kubwa. Ni kwa nini Wamachinga wa Mwanza wanaweza wakakaa na Mkuu wa Mkoa Mwanza *Hotel,* wakala naye chakula halafu wamachinga wa Iringa wakakimbizwa na Polisi. Kwa nini Polisi watumike kuwapiga Wamachinga wakati siyo kazi yao, mpaka nao wa-*riot* ndiyo Mkuu wa Mkoa anawaita. Nasikitika kitendo cha juzi Iringa, Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Meya wamekusanyika wamewa-*deploy* Polisi kutoka Mafinga wamejazana wanawapiga vijana ambao hawana hatia, siyo majambazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Waziri, suala hili halipo Mkoa wa Iringa tu, kwa nini tusichukue mifano ya Mwanza, tusichukue mifano ya Mbeya, tuchukue mifano ya Moshi tukahakikisha tunairasimisha sekta hii, hawa watu waishi vizuri katika nchi yao, tuwatafutie utaratibu mzuri wa kuondokana kero hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema tusipokuwa makini, haya matatizo ya kuzalisha watu ambao hawana ajira ni kutokana na mipango mibovu ya MKUKUTA I ambayo imefeli. Sasa hivi tumekuja na neno lingine tena tunasema *Big Results Now*, lakini tusipokuwa waangalifu, yatakuwa ni maneno maana tuna Mpango wa Miaka Mitano, tuna *Big Result Now*, tuna Kilimo Kwanza, tuna MKUKUTA vyote vinashindikana, tunakuja na maneno. Ninaomba tujipange vizuri, tutafute *solution, leaders are problem solvers*. Changamoto zitakuja tu kama Taifa, lakini badala ya kujipanga vizuri, kutumia Polisi kila wakati *Police brutality,* tunawafanya vijana hawa wachukie Serikali yao. Tunatengeneza Taifa lenye chuki, tunatengeneza watu wazoeane na mabomu ya Polisi bila sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuomba Mheshimiwa Waziri, nina imani na wewe, ni mtu mwenye busara, ni mtu ambaye ni hazina katika Taifa letu, wewe kama wewe lakini siyo Chama chako. Una hazina kubwa, ninaamini hili suala

likikaa kwako, utalijadili vizuri, tukae pamoja mezani tujadiliane tuliondoe tatizo la Wamachinga. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa *quotation* ya Jim Rohn anasema; *Don't wish it were easier; wish you were better.* Kama Viongozi tutapata changamoto kubwa lakini hebu tukae katika *position* nzuri. Anamalizia kwa kusema, *don't wish for less problems; wish for more skills*. Naiomba Wizara yako itafute *skills* nyingi tofauti ambazo hata upande wa pili huku ziko, tukae pamoja, tutoe mawazo yetu, tutatue tatizo hili la Wamachinga ambalo kimsingi linaua Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake aelezee suala hili la Wamachanga. Mimi sitaunga mkono hoja hii mpaka kwanza Waziri aniambie suala la Wamachinga litatatuliwa namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nashukuru. Sasa namwita Mheshimiwa Eustace Katagira na Mheshimiwa Nimrod Mkono ajiandae.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniruhusu na mimi nichangie katika hoja hii ya Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitangulie kusema kwamba Waziri ambaye ni hazina katika nchi, anatokana na Chama ambacho ni hazina katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee suala la usafirishaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi. Nitangulie kwa kusema kwamba mimi ni mdau katika usafirishaji wa mazao ya kilimo nje ya nchi hususani kahawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii katika nchi zote ambazo zinahitaji maendeleo, mtu au shirika ambalo linasafirisha mazao nje yaani *exporter,* huwa wanaangaliwa

kwa jicho zuri kabisa. Huwa wanaonekana kwamba ni watu au ni jamii au kampuni ambayo inaleta na kujenga uchumi wa nchi. Inaingiza pesa za kigeni katika nchi na inasaidia katika kuendeleza nchi kwelikweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nidiriki kusema kwamba leo hii kama utajaribu kusafirisha kahawa nje ya nchi, umetafuta soko, unataka kwenda kuuza nje ya nchi, zao ni la wakulima, hutaweza kusafirisha kahawa hiyo mpaka umelipa ushuru ambao unaitwa *export permit fee.* Ninachotaka kueleza hapa, hii *export permit fee* siyo kusema kwamba ni leseni ya kawaida, unakuwa umeshakata leseni ya kawaida ya kusafirisha zao la mwananchi, zao la mkulima, lakini kwa kilo ambayo unataka kuisafirisha kuipeleka nje kuiuza kwa niaba ya mkulima, itabidi kila kilo uilipie kitu kinaitwa *export permit fee* na kama kweli hujalipa hiyo *export permit fee,* kahawa yako haitatoka bandarini kwenda kwa mnunuzi nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninapendekeza kwamba hii *charge* kwa mkulima isiwepo, iondolewe. Nasema hivyo kwa sababu mnaweza mkafikiria kwamba hii ni pesa ndogo, hii siyo ndogo. Katika mwaka huu kwa mfano, wakulima wa Wilaya mbili za Kyerwa na Karagwe wamelipa si chini ya shilingi milioni 200 kama *export permit fee* ya kupeleka zao kwenda kuuzwa katika masoko ya nje. Mkulima wa kahawa anakuwa ameshapata makato makubwa mengine, ameshalipa *levy,* ameshalipa ushuru wa utafiti na makato mengine. Kwa hiyo, mimi nadhani hii pesa ingemrudia akaweza kumaliza mahitaji yake ya kawaida, kama kusomesha watoto, kama kuchangia maendeleo katika Wilaya yake na katika Kijiji chake. Naomba waungane Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika wahakikishe kwamba hii kitu ya *export permit fee* mkulima anaondolewa na anaweza kubaki nayo imsaidie katika shughuli zake za kuendesha maisha na kuchangia maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi sina shida na ninatambua kazi nzuri inayofanywa na Bodi za Mazao kama

Bodi ya Kahawa lakini ni muhimu mkulima aangaliwe vizuri lakini pia aweze kupata pesa inayomfaa ambayo inakuwa faraja kwake, ambayo itamfanya aweze kuendelea kupata mapato mazuri tusije tukaingia katika matatizo waliyonayo *Zone* ya Korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, siongelei Wilaya ya Kyerwa na Wilaya ya Karagwe peke yake, naongelea Kagera nzima, naongelea Kigoma, naongelea Mara naongelea wakulima wote wa zao la kahawa ambalo linauzwa nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda. Mheshimiwa Waziri amekuja na maneno mazuri leo akiongelea viwanda ambavyo vitaanzishwa, viwanda vya saruji, viwanda vya kusindika mafuta lakini nazidi kusisitiza kwamba ni muhimu tuangalie jinsi mwananchi atakavyo-*participate* katika mtiririko huu wa uanzishwaji viwanda. Isije wakaja wageni peke yao wakaanzisha viwanda, kama ilivyokwishaelezwa, lakini na wananchi waweze ku-*participate*, mwisho wa siku na wananchi waweze kusema tuko katika nchi yetu na sisi tumo katika mtiririko wa maendeleo yanayojitokeza katika sekta ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ameongelea habari ya *financing* ambayo itapatikana. Hii ipatikane kwa ajili ya wananchi na wenyewe kuwa wabia na ku-*participate* katika sekta ya viwanda. Zipatikane *soft loans* lakini pia zenye riba pungufu, nikimaanisha kwamba hiyo 5% ambayo itakuwa inasaidia katika kulainisha gharama ya *financing* kwa wananchi wanao-*participate* katika viwanda, haitatosha. Kwa sababu bado kutakuwa kuna riba kubwa ya kubeba katika uendelezaji wa viwanda. Ningependekeza kwamba hiyo riba ipungue zaidi ya msamaha wa *five percent* peke yake. Pia, hizi *soft loans* ziwe na *grace period* ambayo ni nzuri ya kusaidia wananchi waweze ku-*participate* wenyewe mwisho wa siku waseme kwamba tumo katika nchi yetu. Tunakwenda pamoja na mabadiliko yanayotekea na tunaweza mwisho wa siku tukasema kwamba na sisi tumefaidika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namuasa Mheshimiwa Waziri, ahakikishe kwamba pesa hizo kwenye dirisha maalum, zisije zikawa ni maneno na maandishi peke yake lakini zikachomolewa zikaenda katika maeneo mengine. Zikaenda kujenga maghorofa ya kupangisha, zikaenda kwenye maeneo mengine ambayo siyo *intended* kwa shughuli hiyo. Nawaasa wenzangu hata Wakaguzi wa Mfuko huo, wawe wanahakikisha mwisho wa siku kwamba pamoja na mengine yote ambayo wanayakagua na kuyaangalia na kuyatolea taarifa, waseme pia wamekagua hizo *funds,* hizo *financings* na kwamba zimetumika jinsi zilivyopangwa na jinsi ilivyotarajiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara na nchi jirani. Yako masoko yanapangwa kujengwa katika maeneo ya mpakani hususan kule kwangu katika eneo la Murongo na katika eneo la Nkwenda. Tunaomba na ninapendekeza na ninashauri masoko haya yajengwe haraka, yasibaki kwenye michoro, yasibaki kwenye karatasi yasibaki kwenye maneno ili wananchi waweze kuyatumia na waweze kuweka ushindani na nchi jirani ambao tunafanya biashara nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazidi kupendekeza kwamba hapo kwenye masoko haya ya mpakani na ambayo sasa hivi yako, Serikali ihakikishe kwamba zile sera za ushuru, zile sera za malipo pale mpakani ziwekwe wazi kabisa. Nachotaka kumaanisha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa nashukuru, ni kengele yako ya pili.

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Mheshimiwa Nimrod Mkono na Mheshimiwa Asaa Hamad ajiandae.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii Wizara ina matatizo makubwa mno. Wizara ya Viwanda na Biashara. Naanza kwa kusema kwa nini kuna matatizo ndani ya Wizara hii. Nini maana ya biashara? Utakuwa na kiwanda lakini kiwanda chako ni lazima kizalishe mali ambayo inauzika. Anayepima kwamba mali inauzika ni kwamba unasajili, unapata cheti cha kuonyesha kwamba hizi bidhaa zako zinaweza kuuzika na zinafaa. Ndani ya Wizara hii kuna Kitengo maalum kinaitwa *BRELA*. *BRELA* ilianzishwa mwaka 1999 na sababu ya kuanzishwa kwake ilikuwa ni kuhakikisha kwamba kazi inakwenda haraka iwezekanavyo. Ofisi yao iko pale Lumumba lakini hata kiti cha kukaa hakuna. Mafaili yamepangwa mpaka kwenye choo kuna faili pale. Hiyo ndiyo *BRELA* iliyoko pale. Wanafanya nini? Wanasajili Hatimiliki za alama za biashara yaani *trade mark and service mark. BRELA* inasajili alama za *patents* au mnaita hataza, yaani siku hizi Kiswahili *patents* inaitwa hataza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ni *member* wa *Africa Region Industrial Property Office* ambayo iko Harare. Nadhani nchi za Afrika zinafanya muungano kwamba washirikiane katika kusajili hizi Hatimiliki ama *patent and trade mark services*, wana *common registration.* Sheria hii, ingawa sisi ni *members* mpaka sasa hatushiriki, hiyo ni Wizara ya Viwanda na Biashara. Sasa mwekezaji anakuja kuwekeza hapa, azalishe mali, aziuze hapa na pia azipeleke nje ya nchi. Kama bidhaa hizi hazifai ama ni *inferior* ama ni feki, hawezi kupata ushindani maalum au ushindani bora. Maana mwekezaji atakuwa anaogopa nikiwekeza Tanzania, kule hawalindi mali ama hawalindi bidhaa hizi na kuna nyingi ambazo ni feki zinauzwa mitaani, je, anaweza kuwekeza nchini ama la? Mimi nasema haiwezekani mpaka kuwe kuna *level plain field.* Wenzetu Kenya wana *registry* nzuri ambayo inafanya kazi, wenzetu Burundi wanayo, Tanzania hapana, ofisi imeoza. Ushauri wangu ni nini? Nasema tufumue *BRELA*, fumua upya kabisa, leta wataalamm waunde chombo ambacho kinafanya kazi kuweza kusaidia hapa Tanzania

tupate uwekezaji unaofaa vinginevyo hatuwezi kuingia kwenye ushindani unaofanya kazi. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kwamba kama umepata *production,* ni muda gani inakuchukua wewe kufanya *registration* ya *patent* kwa mfano, ama *service mark*? Nchi jirani zinachukua miezi mitatu, hapa inachukua miaka miwili ama miaka mitatu kusajili *patent* moja. Hii *registry* inafanya kazi ama ni usanii uko pale? Nataka nipate majibu, vinginevyo sitaunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, kama kuna ushindani labda *trade mark* yako iko-*infringed,* unapeleka maombi yako kwamba upate usuluhishi ama uende Mahakamani, inakuchukua muda gani kufanya hivyo. Utakuta ndani ya Wizara ya Viwanda na Biashara, Kitengo hiki kiko *very weak,* hakifanyi kazi. Vijana wanaofanya kazi pale, wako chini ya hamsini, ni wachache sana lakini alama zinazokuja kuandikishwa pale ni maelfu na maelfu ya alama, kwa hiyo, inachukua mwaka mzima ama miaka mitatu kusajili, tutafika wapi katika ushindani wa leo? Ushauri wangu, vunja Kitengo cha *BRELA* kiundwe upya ili kitoe huduma ambacho kilitakiwa kifanye vinginevyo haina maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi ya kusema maana mambo mengi nimeyasema kwa maandishi. Naomba usome kwa karibu kabisa uone ni jinsi gani ya kujinasua na tatizo tulilonalo katika Wizara ya Viwanda na Biashara. Ahsante sana. Siungi mkono mpaka nipate jibu la msingi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Mkono. Sasa namwita Mheshimiwa Asaa Othman Hamad na ajiandaye Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema.

**MHE. ASAA OTHMAN HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, nianze kwa kusema kwamba uwezo wa Mwenyezi Mungu ni mkubwa na tumwombe Mwenyezi Mungu asije akamrejesha Baba wa Taifa leo akaja akatuona hivi tulivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa katuachia rasilimali ya viwanda ndani ya Tanzania na alifanya hivyo kwa kuamini kwamba Mtanzania ataweza kukomboka kiuchumi kwa kupitia rasilimali hii ya viwanda. Sekta ya viwanda miaka ya 1970, 1978, 1979, Tanzania ilikuwa kwenye chati ya dunia kwa nchi zinazoendelea. Leo tukiitazama BUKOP, TANICA Kagera, Tanga, Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro na kwingineko, Watanzania wako hoi bin taabani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wengi wao walikuwa wanamudu chakula cha siku moja na hii ilikuwa inatokana na ajira ya viwanda. Tumeviua viwanda vyote kwa Sera ya Ubinafsishaji. Ubinafsishaji huu hatukufanya upembuzi yakinifu kama tulivyozoea. Hatukusema kwamba sasa tunahitaji utafiti wa kina. Walipokuja waliokuja tukaita wawekezaji, tukawauzia kwa bei poa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inaliza leo kama siyo kusikitisha, Morogoro na kwingineko, unakwenda pale ma-*godown* badala ya kuzalisha bidhaa ya ngozi, wanaita ni ma-*godown* ya kuweka tumbaku. Cha kusikitisha zaidi wawekezaji hawa ambao mimi nawaita wababaishaji, wengine tumewapa viwanda na fedha tumewapa kutoka kwenye taasisi zetu za fedha humu ndani. Hivi tujiulize kwa nini ikawa hivi? Kama tulikuwa na fedha za kuwakopesha wawekezaji kutoka nje, tulishindwaje leo kuiendeleza *SIDO*? *SIDO* ilikuwa ndiyo mkombozi pia kwa viwanda vidogovidogo. Biashara ambazo akina mama vijijini nao wangemudu kuziendesha lakini tunawapapatikia watu, hatuwajui miguu, hatujui kichwa, tunakamata tumbo, tunawaita wawekezaji, tumewajaza mapesa hatima ya viwanda vya Tanzania leo ni hapa tulipofikia. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu yangu Dkt. Kigoda, nitakuomba sana katika huo mchakato, leo hebu useme neno kwa ndugu zetu wa Kusini ya Tanzania, viwanda vyao vya korosho. Mwenzako mmoja aliwaambia viwanda hivi ni

mufilisi, vimeshauzwa kabisa. Sasa leo wape neno wapate matumaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitakusaidia kwenye uwanja mmoja, kwenye kilimo na bidhaa zake. Kitabu cha Waziri kimezungumzia viwanda vya saruji na kadhalika lakini *Agricultural Industrial Relation* ndicho kitakachoweza kuwa mkombozi kwa nchi hii ya Tanzania. *Agriculture* hii ya pamba, korosho, katani, tumbaku bila kusahau matunda na mazao mengine mfano mbogamboga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akina mama wetu hizi shughuli wanazimudu, hebu Serikali ielekeze nguvu huko. Leo viwanda tumeshaviua, wazee wale waliokuwa wanategemea waume zao na watoto wao kwenye ajira ile, ndiyo wale leo wanahangaika na mabeseni ya mbogamboga na Mgambo virungu juu. Sasa hali hii tutawatendeaje haki watu hawa ikiwa bughudha ndani ya nchi yao waliozaliwa ni hii? *(Makofi)*

Mwisho Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya viwanda na biashara ni pamoja na ndugu yangu kataja Wamachinga. Hawa nao hawana raha, maneno ya kwetu hawana buraha, Mheshimiwa Kigoda ameelewa. Hebu tuwapeni nafasi. Nchi ni yao, nchi hii ni yetu sote na wao wana haki kama vile alivyo nayo Mtanzania mwingine. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *EPZ* na mimi niuguse, kuna dhuluma kubwa inayotendeka hivi sasa na unaelewa wazi kwamba dhuluma haidumu na ikidumu ni nakama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa wamezuiliwa maeneo yao. Serikali hadi sasa haijawafanyia chochote, mradi umekwama, maeneo hayaendelezwi, hatma yao hawaijui, wanaumia ilhali chao wanacho. Kuwafanyia hivi, ni kuwadhulumu na dhuluma, nasema tena Mwenyezi Mungu hatakubaliana nayo, tutakuja kutafuta mchawi lakini ni sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira imepotea kwenye viwanda ambapo ni mamilioni ya Watanzania leo wangekuwa wako huko. Hebu Mheshimiwa Dkt. Kigoda, utakapokuja hapa kufanya *summary,* waeleze kidogo Watanzania wapate matumaini, juu ya Mradi wa *Kurasini Logistic Centre. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ambao kama Serikali, maana tunajishauri kwa mambo ambayo tayari Mwenyezi Mungu keshayaweka mikononi mwetu, hebu fanyeni hiki tunashauriana. Tunashauriana kwa haya yaliyokuwa ni ya heri tayari yameshapatiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la Kurasini, ajira zilizokuwa zimeelekezwa kwa kuanzia ni 25,000. Kwa Dar-es-Salaam leo, tusingekuwa na sababu ya kufukuzana na Wamachinga wale. Hatima yake tumesema kwamba kuna mradi wa Boda-Boda. Viongozi wa Serikali wanakwenda kufungua mradi wa Boda-Boda, hebu Serikali na ikae sasa kwa harakaharaka ione ni gharama kiasi gani inaingia ya tiba kwa wale wanaopata maumivu, ni wangapi wanaokufa kwa mwezi, lakini ni wangapi wanaoibiwa kupitia Boda-Boda hizi? Mradi wa Boda-Boda si suluhisho. Suluhisho la Tanzania ni kurudisha viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Ndugu yangu Waziri Kigoda, Mheshimiwa Rais katamka ufufuaji wa viwanda na kuvijenga vipya; nitakuomba utueleze ni mikakati gani ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kabisa, sekta ya viwanda Tanzania utairejesha kama vile Mwalimu mwenyewe alivyokusudia kabla ya kuondoka kwake Duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naheshimu muda wako, nakutakia kila la kheri Waziri Kiogoda, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Hamad, sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Mrema.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi nimpongeze sana Waziri wa Biashara na Viwanda, Mheshimiwa Dkt. Kigoda na Msaidizi wake kwa kazi nzuri. Kazi wanayoifanya kule kwenye Jimbo la Vunjo, kazi wanayoifanya kule Himo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua ni nia ya Serikali kwamba wanataka kuujenga ule Mji wa Himo, licha tu kwamba baadaye tutaomba uwe Makao Makuu ya Wilaya ya Moshi Vijijini badala ya kuwa kule Manispaa ya Moshi, lakini kazi wanayoifanya pale ni nzuri sana. Kwanza, ni suala la kujenga masoko ya kimataifa, biashara za kitaifa na viwanda. Maswali kwamba mbogamboga, mambo ya ndizi, vitunguu, nyanya, vitapata masoko ya kimataifa. Biashara ya utalii sasa itafanyika Himo badala ya kufanyika Moshi na Arusha peke yake. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba, ninaomba Serikali haya mawazo mazuri ya kupendeza, ya kufanya Mji wa Himo uwe Kituo Kikubwa cha Utalii muendelee nayo, namshukuru sana Waziri wa Viwanda na Biashara na Msaidizi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nitakuwa mwizi wa fadhila kama sitamshukuru sana Mheshimiwa Rais Jakaya Kikwete kwa sababu alifika pale na ndiye aliyetoa ushauri kwamba tuwe na masoko mawili, soko la ndizi na soko la nafaka. Pia nimshukuru sana Waziri Mkuu, uliniahidi, ile ahadi ni deni kwamba, utakuja kukagua ile kazi; nakukumbusha, nashukuru umeniambia utakuja. Kwa hiyo, ni matumaini yangu Waziri Mkuu utazunguka nchi nzima kuona namna gani mtaujenga Mji wa Himo uwe ni Kituo Kikubwa cha Viawanda, utalii na biashara za Kimataifa watu wa Kenya, Uganda, Ethiopia, Somalia, waweze kuja kununua bidhaa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wetu Mheshimiwa Waziri wa Viwanda ni kwamba, Mkoa wa Kilimanjaro, Mkuu wa Mkoa wetu, tena nilikuwa namwomba Waziri Mkuu, yule Mkuu wa MKoa usimwondoe mapema mpaka amalize kazi hii mliyompa pamoja na Sekretarieti yake. Kazi ya kujenga ule Mji wa Himo, yale masoko mawili ya Kimataifa, soko la ndizi na mbogamboga Njia Panda na Soko

la Nafaka kule Lokolova inaendelea. Tumeshapima yale masoko na Hati tunayo. Pilli, tumeshaandika andiko linaloonesha ni kazi gani zinatakiwa zifanyike pale na lile soko la ndizi tumeshapeleka barabara pamoja na kujenga vyoo na kadhalika. Namshukuru sana Waziri Mkuu kwa kuwa karibu na mimi. Kila nikikutana na wewe lazima nikukumbushe habari ya Soko la Lokolova pamoja na la ndizi pale Njia Panda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Kilimanjaro tumeshapiga hatua. Tumeshaandika *Memorandum of Understanding,* Mkuu wa Mkoa wetu na Sekretarieti ya Mkoa, Benki ya *TIB* wamekubali kwamba watawekeza. Mwaka jana mwezi Oktoba walishafanya makubaliano kwamba wako tayari kutoa shilingi bilioni 10 kwa ajili ya hayo masoko mawili. Nawashukuru sana kwa sababu hiyo inawezekana kwa sababu Serikali, mmekubali kutoa *Bank Guarantee* la sivyo wasingekubali hivihivi. Halafu pia watu wa *TIB* mwaka huu mwezi wa Aprili, wameshafika pale na kuangalia *Master Plan* na michoro kuona yale masoko yataendelea namna gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilichokuwa nataka ni kuishukuru sana Serikali, kwa sababu nitakuwa mwizi wa fadhila, nyie mnanitendea mema, halafu mimi nikose shukrani; hiyo sitafanya. Nitaendelea kuwaunga mkono *so long as* na mimi mnanisaidia, *you scratch my back I scratch yours,* kama mnavyofanya. Kwa hiyo, hongera sana Waziri Mkuu, hongera sana Rais wangu, hongera sana Waziri na juzi ulimtuma Naibu Waziri wako kule kukagua ile kazi. Hizo ndio kazi zinatakiwa zifanyike. Kwa hiyo, hilo la kwanza, nilitaka niwashukuru sana, mkinikamilishia kazi ile na mimi kazi yangu ya Ubunge itakuwa imeeleweka vizuri. *(Kicheko/ Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu ujenzi wa viwanda katika makazi ya watu. Pale nina mgogoro mkubwa sana na ninamshukuru sana Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Iko barua yake hapa nzuri sana *CE.91/329/01/E87* ya terehe 27 Januari mwaka huu. Anamwandikia Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya

Wilaya ya Moshi. Ni kuhusu malalmiko ya ujenzi wa kiwanda katika makazi ya watu, Kiwanja Namba 16, Kitalu F, Himo. Naomba Waziri wa Biashara na Viwanda, nikusomee ili msije mkaji-*contradict,* Serikali ni moja Wizara hii inakuwa na msimamo halafu Wizara nyingine inatofautiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkurugenzi wa Mipango Miji amepokea barua ya malalamiko yenye kumbukumbu namba hiyo, ilikuwa ni barua yangu ya tarehe 9/1/2013, kutoka kwa Mbunge wa Jimbo la Vunjo, aliyomwandikia Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inayohusu somo hilo hapo. Ninakushukuru Waziri, unavyopokea barua yangu, unanijibu sawia. Anasema Wananchi wa Kijiji cha Njia Panda, Himo, wanalalmika kuwa kuna mtu anajenga kiwanda cha maji, biskuti na vinywaji ndani ya eneo la makazi. Maelezo na vielelezo viambatanishwa kwenye barua hiyo, vinaonesha kuwa kiwanda hicho kinajengwa kwenye Kiwanja Namba 16, Kitalu F, Himo, ndani ya eneo la makazi. Pili, maeneo ya jirani yaliyotengwa kwa ajili ya huduma ya kuabudia na matumizi ya umma, yameongezewa kwenye kiwanja hicho na kubadilisha matumizi bila idhini ya Mkurugenzi wa Mipango Miji, kama ilivyoainishwa kwenye Kifungu Namba 6(1)(k) na 30(1) yakisomwa kwa pamoja na Sheria ya Mipango Miji ya Mwaka 2007. Waziri anasema kwamba ni kweli katika upangaji wa miji, maeneo ya viwanda hutengwa mbali na makazi ya watu kwa sababu ni matumizi yanayokinzana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barua kutoka Wizara ya Ardhi inasema kwa kuzingatia malalamiko hayo ya wananchi, Wizara inakutaka yaani Mkurugenzi Mtendaji anaambiwa, kufuatilia malalamiko hayo kwa undani na kuhakikisha kuwa kiwanda hicho hakijengwi na kama kimeanza kujengwa uagize kusimamishwa ujenzi huo. Mara moja peleka Mthamini wa kupata thamani ya maendeleo yaliyokwishakufanyika na umtake mwendelezaji kulipa faini kama ilivyoainishwa kwenye Kifungu cha Sheria 34(1) cha Sheria ya Mipango Miji ya Mwaka 2007 na kwa kiwango kilichoidhinishwa kwenye Kanuni za Adhabu za Sheria ya Ardhi ya Mwaka 1999 zilizopo kwenye Tangazo la Serikali Namba

84 la mwaka 2001 kwa kosa la kujenga bila kibali cha kubadili matumizi kutoka kwa Mkurugenzi Mipango Miji. Kasaini Linus Shayo, Mkurugenzi Mipango Miji na Vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimeamua kuileta hii barua hapa kwa sababu kule kuna mgogoro mkubwa. Watu wanatumia ubabe, wanatumia madaraka, unakwenda kujenga kiwanda kwenye makazi ya watu. Nashukuru Wizara ya Ardhi kwa kuwa na msimamo ulionyooka. Nimeangalia, ni wewe peke yako, Wizara ya Ardhi mmethubutu kuchukua msimamo huo. Sasa naomba na Wizara ya Biashara na Viwanda, tusaidiane kwa sababu ule Mji wa Himo umeshaharibika. Nitamngoja Waziri wa Ardhi wakati wake kwa sababu ule Mji wa Himo ukienda kuuliza eneo la viwanda liko wapi? Hawakutenga, wamejenga kila mahali. Yale maeneo ya wazi yote yamejengwa. Kwa hiyo na sisi tunasema Mji wa Himo utakuwa Mji Mkuu wa Wilaya ya Moshi Vijijini. Sasa ni Mji gani huo hauna maeneo, hakuna viwanja vya michezo, hakuna makaburi, hakuna maeneo ya viwanda. Kwa hiyo, mimi ninachotaka kuomba hapa, nitakuomba Waziri Mkuu unisaidie kwa sababu kama mnafanya kazi takatifu, kazi nzuri hiyo ya kuwekeza kwenye Mji ule wa Himo, kupanua utalii na haya masoko ya Kimataifa, halafu ule Mji unajengwa kienyeji bila kuzingatia masharti ya Mipango Miji, tutakuwa tumefanya makosa makubwa sana.

Mheshimiwa mwenyekiti, namalizia kwa kusema kwamba, kwanza naishukuru tena Serikali. Namshukuru Rais wangu, namshukuru Waziri Mkuu, namshukuru Waziri wa Viwanda na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Pili, namshukuru Mkuu wa Mkoa na Sekretarieti yake kwa kazi nzuri wanayofanya kule Himo, kujenga ule Mji uwe wa kisasa. Hizo dosari ndogondogo nitaongea na Waziri wa Ardhi, aweze kunisaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamejenga nyumba, halafu eti Mipango Miji ya Wilaya ya Moshi wanasema tuwaache waendelee; nyie Dar-es-Salaam mnabomoa nyumba ambazo zimejengwa katika maeneo yasiyostahili, kule kwangu hakuna mtu anayenisaidia yabomolewe yale

majengo ambayo yataharibu mandhari ya ule Mji wa Himo. Kwa hiyo, ninachosema Waziri wa Ardhi, unisaidie. Nitakuja kwako tujenge kamji kadogo kazuri kakisasa pale Himo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mchangiaji wetu wa mwisho, ni Mheshimiwa Kayombo.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya Mheshimiwa Waziri kusoma hotuba yake, nilikuwa nimeamua kutounga mkono, lakini nilipoyaona haya ambayo ameyaongea nakiri kusema kwamba nimeridhika, namtakia kila baraka za Mwenyezi Mungu aweze kufanikiwa katika kazi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge waliokwishazungumza juu ya ufinyu wa bajeti katika Wizara hii. Hii haioneshi dhamira ya kweli ya Serikali ya kuinua viwanda lakini mahsusi ningependa kuona *SIDO* wanasaidiwa zaidi na kile kituo chetu cha *China Logistic Centre* kinaweza kupewa fedha zaidi na *TBS* inawezeshwa kwa kupewa wafanyakazi zaidi ili waweze kuangalia afya zetu kupitia vipimo wanavyopima katika bidhaa mbalimbali zinaingia nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninalotaka kujikita zaidi ni mradi wa Ngaka. Waheshimiwa Wabunge yapo matatizo ya umeme nchini na hapa tulipitisha umeme wa dharura miaka miwili iliyopita lakini hakuna mafanikio, suluhisho liko hapa kwenye makaa ya mawe. Sasa Serikali, mimi sioni ina kigugumizi gani kwa nini huu mradi haiuwekei kipaumbele. Kwa nini kwenye miradi mingine Serikali inaweka fedha; kwenye mradi wa makaa ya mawe Ngaka, Mbinga, Kijiji cha Ntunduwaro, Serikali inalala usingizi, haiweki fedha na haitaki kuweka fedha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika aliunda Kamati Ndogo ya kuangalia mradi wa makaa ya mawe na Mheshimiwa Mgimwa, ambaye sasa ni Waziri wa Fedha, alikuwa kwenye Kamati hiyo; yapo mapendekezo lakini bado hayo mapendekezo hayatiliwi mkazo na wala hayatiliwi maanani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme ambao unatumika sasa *TANESCO* inaununua kwa senti za Dola ya Marekani 42. Umeme wa makaa ya mawe ni senti 12 tu. Kkwa nini mnawatesa wananchi wa Tanzania kwa kuwapa umeme ghali wakati wanaweza kupata umeme ulio nafuu zaidi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunaacha hao wawekezaji wenyewe tu waweze kujenga mtabo huu, kwa nini tusiweze kutafuta fedha za ndani za kujenga mtambo wa kufua umeme wa makaa ya mawe? Kwa nini *TANESCO* isishiriki katika ujenzi huu wa makaa ya mawe kwa ajili ya usalama wa nchi yetu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo tatizo la mazingira. Yale makaa ya mawe yanasafirishwa kwa malori. Mimi naamini kwamba kabla ya kuanza huu mradi, tathmni ya mazingira ilifanyika. Sasa kwa nini Serikali, iruhusu huu mradi kuanza na kusafirisha kwa malori ambayo yanasababisha vumbi na wananchi wote wa kutoka kule Ntunduwaro, Rwanda, Paradiso, Amani Makoro, wote wanakohoa sasa hivi. Namwomba Mheshimiwa Waziri afanye analoweza kwa kushirikiana na wawekezaji na Serikali yetu kuona kwamba barabara ya kutoka Kitai kwenda Rwanda mpaka Litui inajengwa kwa kiwango cha lami ili kuwapunguzia adha ya vumbi hawa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko tatizo la fidia na hili ni tatizo kubwa. Hivi juzijuzi mlituona kwenye *TV* tuko pale kwenye eneo la mgodi na wananchi walikuwa wakali sana. Baadhi ya viongozi wa *NDC,* wanasema Mbunge alikuwa anashirikiana na wananchi kuwashawishi wagome. Mimi siko hapa kuiwakilisha Serikali, mimi kazi yangu ni kuwawakilisha

wananchi na nitaendelea kuwawakilisha wale wananchi vizuri wa Kata na Vijiji vyote katika Jimbo la Mbinga Mashariki, Serikali timizeni wajibu wenu. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** *Yes!*

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Kwanza kwa nini Mheshimiwa Waziri mradi huu ulianza kabla ya kumaliza kero za fidia kwa wananchi? Hili ni kosa la msingi. Kwa nini mpaka sasa wenzetu wa Shirika la *NDC* hawaoni hali hii na wala hawahangaiki. Hata pale ambapo Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa alituita Viongozi kwenye mkutano wa dharura ili kuangalia baada ya mgodi kufungwa, *NDC* hawakutuma mwakilishi. Mheshimiwa Waziri hii ilikuwa dharau nafikiri kwa Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa. Mimi naomba wenzetu wa *NDC* wajifunze kushirikiana na Serikali ya Mkoa na Serikali ya Wilaya. Kila linalotokea pale Wilayani, Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya, Mheshimiwa *DED,* Mheshimiwa Mwenyekiti wa Halmashauri, Mbunge na Diwani ndio wanahangaika kila siku kwenda Ntunduwaro. Kwa nini mnaacha hii kazi kwa *Local Government* peke yake wakati nyie ndio wenye mradi na sisi hatupati chochote?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba Shirika la *NDC,* kwa mradi huu pia lifikirie kutoa *share* angalau kwa kiwango fulani kwa Kijiji cha Ntunduwaro, ili na wao waweze kuona mafanikio ya mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Serikali imeji-*committ* kulipa fidia kwa wananchi wale ifikapo tarehe 15 Juni, mwaka huu. Naiomba Serikali itimize ahadi hii. Nimeshamwandikia Mheshimiwa Waziri Mkuu tarehe 24 mwezi uliopita juu ya jambo hili. Hatutaki kuona tena vurugu zinatokea katika Kijiji kile wala mimi sipendi kuona ule mgodi unasimamishwa kwa sababu tu ya tatizo la fidia wakati ambapo tuna muda mrefu wa kutatua tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata taarifa ya Serikali juu ya hatma ya Kiwanda cha *Tanganyika Packers* kilichopo katika Jimbo la Kawe Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufilisi wa Kiwanda hiki ulifanyika tarehe 19 Aprili, 2002. Mali za Kiwanda husika zilikabidhiwa/uzwa kwa Kampuni ya *Al-Ghurair Investiment* L.L.C ya Falme za Kiarabu ili wazitumie katika kujenga vitega uchumi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji husika haukufanyika kama ilivyotarajiwa, hali iliyopelekea Serikali kuanza mchakato wa kukirudisha ndani ya miliki yake. Kauli ya mwisho ya Serikali hapa Bungeni ilibainisha kwamba wako kwenye majadiliano na mwekezaji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoeleweka katika eneo husika kuna shughuli mbalimbali za kibinadamu zinazoendelea. Kuchelewa kwa Serikali kufanya maamuzi kunaweza kupelekea kuibuka kwa mgogoro mwingine kati ya watumiaji na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata majibu juu ya hatma ya eneo hili. Kama majadiliano baina ya pande mbili, Serikali na mwekezaji yalifanyika, walikubaliana nini? Je, mchakato wa utekelezaji wa makubaliano hayo unaanza lini?

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusu mradi wa China *Logistic Centre.* Katika bajeti ya mwaka 2012/2013, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi bilioni 60 kwa ajili ya kulipa fidia wananchi maeneo ambapo mradi utafanyika. Jambo la kusikitisha, hadi mwaka unamalizika ni shilingi milioni 550 tu ndizo zilizotolewa. Je, Serikali inatuambia nini kuhusiana na mradi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni muhimu sana kwa nchi yetu. Mradi huu ungeinufaisha nchi yetu kiuchumi kwani nchi nyingi za Afrika Mashariki na *SADC* zingetengemea uzalishaji wa bidhaa katika maeneo haya lakini pia mradi huu unategemewa kutoa ajira kwa Watanzania 25,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kuwa mradi huu pia unatakiwa na nchi nyingi za Afrika na sisi tunauchezea na kupoteza fursa za kiuchumi na kijamii (ajira). Haya yanaweza kuja kuwa majuto na wazee walisema majuto ni mjukuu. Hivyo, Serikali inashindwa nini kutoa kiasi hicho cha fedha kwa ajili ya watu wake?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iliangalie suala hili kwa makini sana vinginevyo hatutakuwa pamoja. Kwa hiyo, Serikali iangalie uwezekano wa kumalizia pesa zilizobakia kwa ajili ya maendeleo ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vya zao la pareto. Hadi sasa Tanzania kuna kiwanda kimoja tu cha zao la pareto kilichopo Mafinga cha *PCT* kinachoshirikiana na Kampuni ya Marekani ijulikanayo kama *MGL*. Kampuni hii inatumia fursa hii kuwapunja wananchi kwa kununua pareto kwa bei ya chini sana. Tunaomba Serikali itafute wawekezaji wengine wakubwa ili kuleta ushindani katika sekta hii ya zao la pareto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi kuna wanunuzi wadogo wadogo wananunua pareto na uwepo wao umeongeza tija sana kwa wananchi kwani bei ya pareto imeogezeka kutoka shilingi 1700 kwa kilo moja hadi shilingi 2400 kwa kilo moja. Huyu mwekezaji mkubwa wa Marekani anawapiga vita hawa wawekezaji wadogo ili abaki peke yake. Tunaomba Serikali iwasaidie wawekezaji wazalendo

kwa kuwapa ruzuku ili waanzishe kiwanda cha pareto kitakachotoa ushindani kwa kiwanda hiki cha *PCT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya viwanda ni muhimu sana kwa ustawi wa Taifa hapa nchini. Hakuna Taifa ambalo litakuwa na maendeleo yoyote yale bila viwanda. Ni vyema Serikali ije na mpango kabambe wa kufufua viwanda ambavyo havifanyi kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uanzishwaji wa viwanda vipya hasa vya kusindika mazao ambayo yanazalishwa hapa nchini. Tukifanya hivyo, tutakuza uchumi katika nchi hii na ukizingatia unapokuwa umeongeza thamani ya mazao umewasaidia wananchi walio wengi hasa wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri sana Serikali ijenge kiwanda cha kusindika tumbaku katika Mkoa wa Tabora. Kiwanda hiki kama kitajengwa katika Mkoa huo kitasaidia sana kupandisha thamani ya zao hilo kwa Mikoa ya Tabora, Shinyanga, Mbeya, Kigoma na Katavi. Mikoa hii ni jirani na yote inazalisha zao la tumbaku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vya kukoboa korosho; ni vyema Serikali ikajenga viwanda vipya na vile vya zamani ambavyo havifanyi kazi vifufuliwe ili viweze kufanya kazi. Tukisaidia kuimarisha viwanda ambavyo vina mahusiano ya moja kwa moja na mazao ya wakulima, tutaimarisha uchumi kwa kiwango kikubwa na kukuza uchumi kwa matabaka ya wananchi wanaoishi Mijiji na Vijijini. Naomba Serikali ije na tamko litakalosaidia sana kutatua tatizo la ukosefu wa viwanda vinavyohusiana na mazao ya wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vya mbolea; ili tuweze kuwa na uzalishaji wa chakula cha kutosha nchini na mazao ya biashara, ni lazima Serikali ijenge kiwanda cha mbolea. Kiwanda hiki kikijengwa kitapunguza gharama

kubwa zinazotumiwa na Serikali kwa ajili ya kuagiza mbolea kutoka nje na kuifanya Serikali kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kununulia pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu masoko; Serikali ifanye jitihada za kuandaa mipango ya kutafuta masoko yatakayowasaidia Watanzania kuuza mali zao ambazo zitakuwa sio malighafi. Kama tunataka kuiandalia nchi yetu mfano mzuri lazima Wizara ijikite kwa dhati kuwatafutia masoko wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuendelee lazima Serikali iwekeze katika miundombinu ya umeme wa uhakika hasa vijijini. Umeme vijijini ni muhimu sana kwa ajili ya kuondoa umaskini hasa wa wananchi waishio vijijini. Naomba Wizara ihakikishe imewekeza kwenye makaa ya mawe ili tupate umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SHAFFIN A. SUMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kwa sasa imesheheni bidhaa feki, *TBS* wanatakiwa kujiimarisha kwa kuwa na watu wengi wa kufuatilia kazi za kila siku. Leo kila Mtanzania anapata hasara kwa kuuziwa bidhaa feki. Ni aibu kwa Taifa letu. Pia majengo yanaugua na hata kuporomoka kutokana na matumizi ya bidhaa feki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna Mikoa na Wilaya ambapo maeneo ya *EPZ* hayajatengwa. Je, Wizara inakusudia kuwachukulia hatua gani viongozi kama hawa kwa kuwa wanachelewesha mpango wa Serikali na maendeleo ya wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya Waziri katika bajeti yanatia matumaini. Kama uwekezaji ukifanyika, je, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha vijana wetu wanapata

ajira kwani uzoefu umeonyesha kuwa siku hizi hapa Tanzania kazi za Wamachinga zinanyonywa na wageni hasa Wachina huko Kariakoo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali iandae kijitabu ambacho kitaonyesha kila Mkoa na maeneo ya *EPZ* na fursa zilizopo katika eneo husika kwa maana ya kwamba kama mwekezaji anataka kuanzisha kiwanda cha matunda basi apate taarifa ya kutosha kuhusu Mikoa iliyo na fursa ya kuwekeza.

**MHE. RACHEL M. ROBERT**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia mambo kadhaa katika hotuba ya Wizara hii nyeti katika kuinua uchumi wa kipato cha Mtanzania mmoja mmoja au kikundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya viwanda. Pamoja na sekta hii kukua kwa asilimia 8.2 mwaka huu 2012/2013 bado kuna changamoto nyingi sana. Ni Sekta ambayo inaendelea kuliongeza pato la Taifa kila mwaka. Ni vema Serikali ione sasa umuhimu wa kuongeza viwanda vingi vikiwemo vya nguo hata katika Mikoa inayolima sana zao hili ukiwemo Mkoa wa Shinyanga na Simiyu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukosekana kwa viwanda hivi katika maeneo haya kunawafanya wakulima wa zao la pamba kukata tama. Mbali na kukosa soko la uhakika, bei ya pamba bado hairidhishi na kuendelea kushuka kila mara. Serikali inatambua kuwa zao la pamba ni muhimu sana na linaongoza kulipatia Taifa pato kubwa sasa. Kwa nini Serikali isijenge viwanda vya nguo na mafuta kuliko kutegemea viwanda vya watu binafsi ambavyo baadhi ya viwanda na kama si vyote vina tabia ya kulalia wakulima. Serikali ione umuhimu wa kujenga kiwanda cha kusindika mafuta, kuchambua pamba na nguo hata kimoja katika Kanda ambako kuna wakulima wengi wa pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uzalishaji wa nyavu za uvuvi ni zuri sana kwani kuna ongezeko kubwa la uzalishaji wa nyavu kutoka tani 165 mwaka 2011 hadi tani 295 mwaka

2012. Serikali inadhibiti vipi ubora wa nyavu hizi? Tumekuwa tukijionea jinsi wavuvi wetu wanavyonyang'anywa nyavu hivi lakini wazalishaji wa nyavu hizo wakiendelea kutengeneza nyavu hizo zisizo na viwango. Naomba Serikali iangalie upya na kwa umakini viwango vya nyavu za uvuvi katika viwanda vinavyozalisha ili wavuvi wasipate hasara wanapozinunua na kwenda kuzitumia *thereafter* wanakamatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ongezeko la bei ya mifungo mfano ng'ombe, mbuzi na kondoo, bado wafugaji hawanufaiki kwani kumekuwa na tabia ya wafanyabiashara kwenda vijijini na hasa wakati wa njaa na kuwapangia bei wafugaji ambapo mwisho wa siku mfanyabiashara ndio anapata faida. Naomba Serikali ije na bei rasmi ya mifugo hiyo ili kumnusuru mfugaji huyo anayetegemea mifugo yake ili ainue uchumi wa maisha yake na jamii inayomzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali kwa kuanza kujenga kiwanda cha ngozi cha *Xinghua Investment Co. Ltd* Mkoani Shinyanga. Naomba sasa Serikali isimamie kwa karibu kiwanda hiki kiishe kwa wakati ili wananchi wapate ajira na wafanyabiashara wa ngozi waweze kupata soko lakini pia Serikali iangalie kwa umakini zaidi maslahi ya wafanyakazi watakaoajiriwa katika kiwanda hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa Kiwanda cha *TRIPLE S* cha kusindika nyama kilichopo Shinyanga, Serikali ihakikishe kinakamilika na kuanza kazi mara moja. Uwepo wa viwanda hivyo Mkoani Shinyanga/Simiyu kutaleta hamasa kwa wafugaji wengi kufuga kitaalamu na kisasa zaidi ili waweze kupata soko katika viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya masoko, katika kitabu cha Hotuba ya Waziri nimeona kuna mkakati wa sera ya masoko ya mazao na bidhaa za kilimo. Ni vyema sasa sera hii iharakishwe ili iweze kuwakomboa wakulima hasa wa mazao ya pamba na korosho ambapo bei zake zimekuwa hazitabiriki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuwa na mpango kabambe wa kufufua viwanda pamoja na kujenga viwanda vipya lakini huu ujengaji wa viwanda uende sambamba na miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asilimia 80 ya wananchi wako vijijini na wengi wamejielekeza kwenye kilimo, wenye kulima matunda, alizeti, korosho na kadhalika na wako tayari kuongeza kilimo kwenye mazao hayo. Tatizo kubwa huko vijijini hakuna kiwanda cha kubangua korosho, kutengeneza mafuta, kutengeneza *juice* kutokana na matunda, pamoja na jitihada waliyokuwa nayo, wakulima hawa hawawezi kuondokana na umaskini kutokana na kuwa mapato wanayopata ni madogo, kutokana na kuwa hawana viwanda vya kutosha huko vijijini. Zao la korosho limeshamiri huko vijijini lakini wakulima wanauza bei ndogo kutokana na kwamba hazijakobolewa, inabidi zisafirishwe nje kwenda kukobolewa halafu zinarudi hapahapa Tanzania kwa bei kubwa, zao tunalima hapa nchini lakini wanaonufaika ni nchi za nje. Kwa kuwa Serikali imejipanga kujenga hivi viwanda, naomba itekelezwe azma yao kwa vitendo na kwa namna hiyo Serikali itaweza kuongeza mapato nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kwa yale maeneo ambayo wanataka kujenga viwanda na ikiwa wananchi ambao wamevunjiwa maeneo yao, walipwe kwa haraka ili kuepukana na migogoro inayojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uingizaji wa bidhaa feki bado unaendelea nchini licha ya jitihada ya Serikali kuweka sheria. Naiomba Serikali iangalie upya sheria hii ili iweze kwenda na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kisungura kidogo, naiomba Serikali itoe pesa zote ambazo zimekuwa *budgeted* kwenye Wizara hii ili miradi hii iweze kutekelezwa.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya vifaa vya ujenzi. Najua Serikali haijihusishi na biashara au uendeshaji wa viwanda. Hata hivyo, najua kwamba ni jukumu la Serikali kusimamia au kuweka misingi ya sera za bei. Inashangaza kuona bei ya saruji inayotengenezwa/ inayozalishwa Mbeya ina bei kubwa Mkoani Mbeya kuliko bei ya saruji hiyohiyo katika Mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam na kadhalika. Hali hii haikubaliki na tunaomba Serikali kupitia Wizara iingilie kati jambo hili. Wote tunajua malighafi nyingi inayotumika kwa ajili ya uzalishaji saruji inapatikana katika Mkoa wa Mbeya; sasa iweje wananchi wasifaidike na kiwanda hicho? Nini faida ya kuwa na kiwanda katika Mkoa huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za bati na nondo pia zipo juu sana, zinakatisha tamaa! Hali hii inapunguza kasi ya wananchi kujijengea nyumba bora. Naomba Serikali pia iingilie kati ili kuhakikisha kwamba bei ya vifaa hivyo inadhibitiwa ili kuwapa wananchi nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, napenda pia kujua ni lini kiwanda cha nyama cha Mbeya *(Tanganyika Packers)* kitaanza uzalishaji wa nyama baada ya kusimama kwa muda mrefu sana. Nashauri Serikali ilitolee jambo hili maelezo ya kina kwa sababu kukiacha kiwanda hicho katika hali ya sasa ni sawa na kufukia mamilioni ya hela ardhini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha.

**MHE. MCH. LUCKSON N. MWANJALE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nampongeza Mheshimiwa Dkt. Abdallah Kigoda, Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na timu yake kwa juhudi zao za kulifanya Taifa hili kuwa la viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa tulilokuwa nalo hapa Tanzania, ni ubora wa bidhaa zetu, lazima uangaliwe kwa makini ili tuweze kushindana na nchi zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la ubora pia na vifungashio ni tatizo kubwa *(Packing).* Ili kuepuka matatizo hayo ni vizuri *TBS* iongeze nguvu kuongeza watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kwa ajili ya kuuza bidhaa ambayo ni bora kwa matumizi ya hapa hapa nchini kwetu ni muhimu na hata nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha nguo cha *Mbeya Textile* kimefungwa na hakifanyi kazi na mitambo inazidi kuondolewa na wananchi walifanya maandamano makubwa ya kupinga ung'oaji wa mitambo. Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya Kiwanda hicho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba naunga mkono hoja hii lakini naomba jibu hasa la Kiwanda hiki cha nguo.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii na kuileta hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ndogo inayopangwa kwenye Wizara hii na fedha kidogo sana inayotolewa kwa Wizara hii ni kikwazo kikubwa kuwezesha Wizara hii kutekeleza malengo yake na kazi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawezaje kutoa Taifa hili kutoka kwenye uchumi wa biashara ndogo ndogo na kwenda kwenye uchumi wa kutegemea viwanda wakati Serikali haiwekezi kwenye maendeleo na viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwanda Vidogo Vidogo *(SIDO)* lina wataalam wazuri wenye uwezo mzuri. *SIDO* ina uwezo wa kuajiri vijana wengi sana wanaotoka Vyuo

vya *VETA*. *SIDO* inaweza kuinua kilimo chetu kutoka kwenye kilimo cha mkono kwa kutengeneza *Power tillers* na *tractor* ndogo ndogo. *SIDO* wanaweza kabisa kuwezesha uwepo wa viwanda vidogo/mashine za kuchakata mazao mfano, kukamua mafuta ya karanga, ufuta, alizeti, matunda na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* iwezeshwe kupata fedha za kutosha kuinua kipato cha Taifa na Watanzania wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumekuwa soko la bidhaa mbalimbali kutoka nchi jirani kama vile, Kenya, South Africa, Zambia, Zimbabwe na kadhalika. Hata kwa bidhaa ambazo zinaweza kutengenezwa hapa nchini. Ni kwa nini tumefungua milango wazi kuruhusu kila kitu kuletwa hapa bila kuweka viwango ili kuviwezesha viwanda vyetu kupata soko kwa bidhaa za ndani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao vijana wengi mitaani hawana kazi, hivi kweli tunaingiza *(import)* hata *toothpick, cotton buds,* viberiti, hii ni aibu kwa Taifa hili. Tuna mbao tuna *cotton* tumeshindwa nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilieleze Bunge ni kwa nini hakuna viwango *(standards)* vya Taifa vya ubora unaotakiwa kwa bidhaa zinazotoka nje ya nchi. Tanzania imekuwa sehemu ya kuleta chochote hata kama hakifai. Bidhaa za Kichina zipo dunia nzima, lakini bidhaa ya Kichina zinazoletwa hapa nchini ni zile dhaifu zisizokuwa na viwango na Serikali imeruhusu haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bidhaa feki ni tatizo kubwa hapa nchini na wananchi wamepata hasara kubwa kwa kununua bidhaa feki.

(i) Vifaa vya umeme vingi madukani ni feki na wanaouza wanajua na Serikali inajua.

(ii) Vyakula vinavyoingia kutoka nje vingi ni feki, watu wanakula vitu feki, wanaathirika kiafya.

(iii) Madawa feki yanaingizwa madukani, watu wanatumia badala ya kutibu maradhi, tunapata magonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwa *TBS Management* imebadilishwa bado hatujaona mabadiliko kuhusiana na utendaji kudhibiti bidhaa feki. Vinaingiaje hadi vinauzwa madukani wakati tunayo taasisi inayoshughulikia viwango?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vyote vilivyobinafsishwa na wawekezaji wameshindwa kuviendeleza au wamebadilisha matumizi nini hatma yake?

(i) Nini hatma ya Kiwanda cha Nyuzi Tabora ambacho kinaozea pale na baadhi ya mashine zimeanza kung'olewa kwa wizi kinyemela huku Serikali iko kimya?

(ii) Kiwanda cha Urafiki – Ubungo tumeingia ubia na Mchina, nini kinaendelea pale. Tulikuwa tunazalisha kanga na vitenge vya ubora mkubwa *from* Urafiki, leo hakuna, Serikali inatuambia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wa Kiwanda cha Karatasi, Mgololo *(SPM)* wamekuwa wanalalamika kwa miaka mingi kuhusu mwekezaji wa kiwanda hicho na Serikali imeshindwa kuwasaidia.

(i) Mwekezaji wa kiwanda hicho aliponunua kiwanda hicho 2005 mkataba wake ulikuwa kuwalipa wafanyakazi waliokuwepo kwanza kabla ya kuwapa ajira mpya.

(ii) Mpaka leo hakulipa chochote kwa wafanyakazi wale na wengine wamedai mpaka wamekufa, amegoma kulipa. Ni lini wafanyakazi hao watalipwa madai yao? Wanaodai mpaka leo ni 750 na wengine wamekufa bila kulipwa.

(iii) Mwekezaji analipa mshahara kwa wafanyakazi baada ya siku 60 (miezi miwili) anatumia sheria gani?

(iv) Mwekezaji anakata makato mengi kwenye mshahara wa wafanyakazi wanabakiwa na fedha kidogo sana kwa nini?

**MHE. NYAMBARI C. M. NYANGWINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuwapongeza viongozi wa Wizara hii; Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wengine. Pamoja na pongezi hizi napenda kutoa mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ubunifu ni muhimu sana katika kuendesha sekta ya viwanda hapa nchini. Kwa mfano, ili Kilimo Kwanza kifanikiwe katika nchi yetu lazima sekta ya viwanda ipewe kipaumbele kwa kubuni viwanda vya kila aina kulingana na mazao yanayozalishwa katika eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)*; napenda kuchukua nafasi hii kutoa ushauri kwa Wizara kuwa ipitie upya mtaala wanaoutumia kutolea elimu katika Vyuo vya Elimu ya Biashara *(CBE)* kwani ni wa zamani na umepitwa na wakati na hivyo ni ngumu kuhimili ushindani kwa wahitimu wa vyuo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtaala unaotumika kwa sasa kwa vyuo vingi hasa vinavyotoa Shahada ni mfumo wa Umilisi yaani *Competency syllabus*. Ni mfumo unaoruhusu ujifunzaji Shirikishi na unaofikirisha zaidi. Pia nashauri *co-subject* kwa wanafunzi wote toka Stashahada/Cheti hadi Digrii (Shahada) liwe la Ujasiriamali ili kuwafanya wanafunzi wetu wanaohitimu katika vyuo hivi wawe wajasiriamali badala ya kutangatanga barabarani kwa kutafuta ajira za maofisini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *EPZ* limekuwa ni kama wimbo ambao hauna wasikilizaji. Naomba kuuliza maswali yafuatayo kuhusu *EPZ*.

(i) Tangu mpango huu ubuniwe, umeleta mafanikio yapi hapa nchini?

(ii) Wananchi waliotwaliwa maeneo yao hasa wale wa Bagamoyo, Songea, Tanga, Kigoma, Bunda wamelipwa fidia halali?

(iii) Kwa nini *EPZ* isiwe kwa kila Wilaya?

(iv) Hasara na faida za *EPZ* ni zipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya viwanda vilibinafsishwa kwa wawekezaji uchwara, lakini hadi sasa hakuna mafanikio yoyote au vimebadilishwa matumizi. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu viwanda vya aina hiyo? Kwani Serikali haiwezi kuvifufua viwanda hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Viwanda vya Nguo; napenda kuishauri Wizara kufanya yafuatayo ili kuweza kujenga na kuimarisha Viwanda vya Nguo hapa nchini:-

(i) Angalau kila Mkoa/Kanda iwe na kiwanda kimoja cha nguo.

(ii) Pamba ya hapa nchini itumike kuzalisha nguo katika viwanda hivyo.

(iii) Serikali na taasisi zake kama vile Jeshi, Polisi, wanafunzi na wafanyakazi wengine walazimishwe kushona nguo katika viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unyanyasaji na ubaguzi wa wafanyakazi; kuna madai kuwa baadhi ya viwanda hasa vile vinavyomilikiwa na Wahindi na Waarabu hapa nchini huwabagua kimishahara, posho na marupurupu mengineyo na pia kuwadhalilisha na kuwadharau wafanyakazi weusi (wazawa).

(i) Je, Wizara inalifahamu tatizo hilo?

(ii) Ni hatua zipi zinachukuliwa na Wizara kulinda maslahi ya wafanyakazi katika viwanda hivyo?

(iii) Serikali ina mpango gani wa kuwawezesha wazawa kuanzisha viwanda vyao hapa nchini?

(iv) Viwanda vya kuchapa/uchapishaji hapa nchini Tanzania vinakabiliwa na matatizo gani. Je, Serikali imejiandaaje kutatua matatizo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali mengine yanayohitaji utatuzi; Wizara inasaidiaje wafanyabiashara wadogo wanaokwenda katika nchi za China, Dubai, Turkey, Thailand, India, *South Africa* kwa kuwaongezea mitaji isiyo na riba? Je, Serikali inafahamu kuwa wafanyabiashara hao hunyanyasika sana kwa kudhulumiwa katika nchi hizo? Hata kama ni soko huria, kwa nini hatuna Tume ya Bei hapa nchini? Ni lini Tume hii itaanzishwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanga ni kuchagua; ni sababu zipi za msingi zilizopelekea *TBS* kuweka utaratibu wa kukagua magari yaliyotumika toka nje ya nchi katika nchi za Dubai, Japan na Hong Kong? Je, nchi zingine zenye huduma hiyo ni zipi? Kwa nini kama kupanga ni kuchagua, tusikague magari hayo hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuisemea Tarime; Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuufanya ukanda wa Sirari, Wilayani Tarime kuwa ukanda maalum wa kibiashara?

(i) Je, Wizara imejipanga vipi kujenga masoko ya kisasa na yenye hadhi katika mipaka ya nchi hususani eneo la Sirari, Wilayani Tarime.

(ii) Je, wizara imejipanga vipi kuanzisha viwanda vya kusindika mazao ya aina mbalimbali Wilayani Tarime?

(iii) Ni lini wataalam wa Wizara hii ya Viwanda na Biashara watafika Wilayani Tarime kutoa elimu ya Ujasiriamali kwa wananchi wa Tarime?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali ya fikra na utafiti; malighafi, nguvu ya umeme, rasilimali watu, mtaji, masoko

ya uhakika, sera za Serikali, historia ya nchi na uimara wa Serikali, ni baadhi ya mambo yanayoweza kushawishi ustawi wa viwanda hapa nchini. Je, Wizara imefanya utafiti wowote kuhusu suala hili na kama bado kwa nini haijafanya? Kama imefanya inatoa au inakuja na nadharia gani kuhusu sekta ya viwanda hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Nguo hapa Tanzania vinakabiliwa na matatizo haya: uzalishaji ni ghali sana, ukosefu wa masoko ya uhakika, ubunifu mdogo, ufundi duni, miundombinu mibovu, rushwa na kukosekana kwa haki na mtaji duni, tatizo la umeme. Je, Serikali kupitia Wizara hii inawashauri nini wamiliki wa Viwanda vya Nguo hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Viwanda na Biashara inaishauri nini Serikali kuhusu uanzishwaji wa viwanda vya kusafisha malighafi ya madini kama vile dhahabu hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda vya Samaki hapa nchini hasa Kanda ya Ziwa vinasaidiaje kukuza uchumi wa nchi hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mbao nyingi zinazozalishwa kienyeji hapa nchini. Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha *Heavy Duty Timber Industries* kwa kila mkoa hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Wizara hii imejipanga vipi kuzalisha vitu/vifaa vinavyopendwa sana na watalii hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda ni muhimu sana ili kuinua pato la Taifa na la mtu mmoja mmoja. Sayansi na Teknolojia ni muhimu ili kufanikisha suala la ukuaji wa viwanda hapa nchini. Je, mpango wa maendeleo katika nchi yetu, umehusishaje sekta ya viwanda/ *Science and Technology* ili kuinua pato la Mtanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naunga mkono hoja.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *COSOTA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni za utekelezaji wa sheria ya *COSOTA* zinasema waziwazi kwamba, vituo vya televisheni na redio wanapaswa kulipa mirabaha kwa wasanii kupitia *COSOTA*. Tatizo lililopo ni kwamba *TCRA* hawatoi ushirikiano kwa *COSOTA* katika kutoa taarifa.

Suala hili Waziri alipeleke Wizara ya Mawasiliano ili *TCRA* waagizwe kutoa taarifa za mapato ghafi kwa vituo vya redio na televisheni kwa *COSOTA*. *TCRA* kugoma kutoa taarifa ni uhalifu na kutenda kosa. *COSOTA* mara moja watangaze zabuni kupata kampuni ya kufanya *monitoring* ya *airtime*. Kuanzia tarehe 1 Julai, 2013 mirabaha ya televisheni na redio ianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, agizo la Waziri la kufanya mabadiliko ya kanuni za *COSOTA Act* litekelezwe mara moja ili kuhakikisha kuwa biashara ya miito ya simu *(RBT)* inaendeshwa kwa haki na mikataba ya wasanii isimamiwe na *COSOTA* na mapato halali yapatikane kwa wasanii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Sticker* za *TRA* zitolewe kwa Wasanii na *Producers* na sio kwa *distributors*. *FCC* izuie ukiritimba dhidi ya wasanii unaofanywa na *distributors*. *Distributors* kamwe asiwe *Producer*. Tuangalie sheria zetu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile mapato yakusanywayo na *TRA* kutoka kwenye *stickers* asilimia 50% ielekezwe *COSOTA* ili kuisaidia *COSOTA* kusimamia masuala ya Hakimiliki. Hakuna haja ya *sticker* mbili i.e Hakigram na *TRA ones*. *TRA* waelezwe lengo la *sticker* sio mapato tu bali kupambana na uharamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya *COSOTA* iundwe haraka sana ili kuweza kusimamia vema masuala ya *copyright*. Wajumbe wa Bodi wawe watu makini sana wenye nia ya dhati ya kuisaidia tasnia ya hakimiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kigoma.

(i) Soko la mpaka wa Kapunga (Tanzania/ Burundi).

(ii) Kigoma SEZ nayo sijaona kipaumbele chake.

*(iii)* *Focus:* Viwanda vidogo vya usindikaji.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri na timu yake yote kwa uwasilishaji wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Sekta ya Viwanda; ukisoma ukurasa wa nane wa kitabu cha hotuba unazungumzia kuhusu hali ya viwanda vyetu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali halisi ya viwanda vyetu nchini inasikitisha sana kwa kuwa pamoja na Serikali kuonesha kuwa imekua, lakini katika uhalisia wake ni mbaya. Kwa nini Serikali imebinafsisha viwanda, lakini haifuatilii kama kweli wawekezaji wanafanya biashara waliyokubaliana nayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wawekezaji wetu kwenye sekta hii ya viwanda *either* ni matapeli au madalali kwa sababu kuna baadhi ya viwanda vyetu toka vimechukuliwa na wawekezaji ama vimefungwa kwa muda mrefu bila kufanyika chochote au mitambo imefunguliwa wawekezaji wanabadilisha kabisa matumizi na viwanda vingine vimegeuzwa maghala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nijue kama Serikali inatambua na kama ilishawahi kuchukua hatua yoyote kwa wawekezaji wa aina hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mpango gani umewekwa kwa ajili ya kuwasaidia wafanyakazi wanaouza bia ma-*barmaids* ambao wamekuwa hawana mikataba, wanapata matatizo makubwa katika kazi zao wakati wao ni kama maajenti wa kuuza bia, kinywaji ambacho

kimekuwa kikichangisha mapato makubwa sana katika nchi yetu, tumeshuhudia wenyewe waajiri wao wakiwanyanyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maeneo ya *EPZA*; Serikali ilijitahidi kuhamisha na kutenga maeneo maalum kwa ajili ya uwekezaji, lakini maeneo hayo mengi yalikuwa yanamilikiwa na watu binafsi yanahitaji fidia ili yaweze kutumika kama ilivyokusudiwa. Kwa mfano, eneo lililotengwa katika Mkoa wetu wa Iringa lililopo katika Wilaya ya Kilolo limetengwa muda mrefu sana. Eneo hili mpaka leo linawanyima fursa wananchi wa Iringa, eneo hilo kuwekeza na kutengeneza ajira kwa wananchi wanaozunguka eneo hilo. Nilipoleta swali Bungeni kuhusiana na jambo hilo niliambiwa tatizo ni eneo hilo linahitaji fidia. Je, lini sasa maeneo hayo wananchi watapewa fidia ili yaweze kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao wawekezaji mbalimbali ambao wamekuwa wakiwekeza wanafanya biashara katika sekta mbalimbali. Serikali ina mpango gani wa kuweka sheria ili watoe asilimia fulani ziweze kusaidia jamii?

**MHE. STEPHEN M. WASIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoani Mara kuna *EPZ* ambayo ardhi imelipiwa fidia ambayo imegharimu zaidi ya shilingi bilioni mbili. Baada ya kulipa fidia pale Bunda, hakuna hatua yoyote inayoendelea. Bila kuchukua hatua za kuendeleza ardhi, watu wanaozunguka eneo hilo wataanza kurejea kwa kuvamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* inahitajika sana kufanya kazi kama zamani. Tunao vijana wengi hawana kazi. Viwanda vidogo vinaweza kuwa suluhu. Tunaomba huduma ya *SIDO* katika Wilaya ya Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye jitihada kufufua viwanda ambavyo vilibinafsishwa lakini vikaachwa. Mfano wa viwanda hivyo ni Viwanda vya Korosho, Ngozi, Nguo, Nyuzi na kadhalika. Hata vinavyofanya kazi chini ya uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha na pia naunga mkono hoja.

**MHE. NAOMI A.M. KAIHULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kwanza nioneshe masikitiko yangu makubwa kwa wahusika wa ratiba kuipangia Wizara nyeti kama hii siku ya kujadiliana kuipa siku moja tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli hawa watungaji wa hii ratiba wanaitakia nchi hii heri, maana sekta hii inagusa masuala ya wananchi mfano:-

(1) Ajira nyingi sana zinazalishwa kwenye biashara.

(2) Masuala ya uchumi kama viwanda vikubwa na vidogo viko huko.

(3) *SIDO* inayowasaidia wanyonge hasa wanawake.

(4) Viwanda ni chanzo cha uzalishaji wa vifaa vya kilimo kwanza.

(5) Fedha za kigeni na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hili suala limetendeka, sasa iwe mwisho safari ijayo ni zaidi ya siku moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo lingezungumzwa kama muda ungekuwepo ni hili la ukosefu wa maono ya Serikali yetu hii. Badala ya kuweka Wizara hii kipaumbele cha kwanza ili i-*generate* (izalishe ajira, vifaa vya mkulima, umeme, maji, mavazi na kadhalika) sisi hapa tunakubaliana na bajeti finyu inayopewa, hiki nini? Tunakuwa kama vile ni Mataahira. Tafadhali sana ongezeni uchokozi huko mnakokwenda kudai maana watu hawaelewi wanafikiri huenda nyie watu wa Wizara ndiyo hamjui kupanga mipango na kutengeneza (*projects* michanganuo).

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kusahau mambo yanayopaswa kufuatilia ambayo hayahitaji fedha bali usimamizi imara na msukumo wa dola ni hili la Chuo cha

Biashara, *Campus* ya Dar es Salaam mpaka sasa ahueni imepatikana. Shukrani lakini jambo muhimu sana kwa ajili ya lengo la kupata elimu ili yasijetokea yale yaliyotokea kwenye Baraza la Mitihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachohitajika ni majengo na *facilities* zinazoendana na *level*, hadhi ya chuo hicho na hili litawezekana pale ambapo mipaka ya chuo itarejeshwa toka mikono ya mafisadi ambao ndiyo wanashikilia maeneo ya chuo hicho. Mmoja anaendesha kiwanda ndani ya maeneo ya chuo. Mwingine anaendesha *bar* na kadhalika ndani ya mazingira ya chuo. Inashindikana kwa ajili ya wahusika wengine waliotoa na kupokea rushwa. Jambo hili lishughulikiwe mara moja. Uongozi uliopo sasa naamini unaweza kazi hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitangulize haya machache kwanza.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja.

(i) Kuanzisha Kiwanda cha Kusokota Nyuzi za Pamba. Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania itaendelea kuwatesa wakulima wa pamba nchini kama haitaweka mkakati wa kuwajengea kiwanda tajwa hapo juu hasa Kanda ya Ziwa. Ni nini kikwazo? Ushauri wangu kwa Serikali ni kujenga kiwanda hicho ili tujitegemee na hapo hapo pamba ya Tanzania kupata thamani.

(ii) Kiwanda cha Saruji, Kanda ya Ziwa. Sipingi mahali viwanda vya saruji, hapa nchini vilipojengwa hivi sasa, lakini ni lini ukanda wa ziwa utapata pia Kiwanda cha Saruji? Kiwanda cha Tanga kiko mbali cha Dar es Salaam na pia Mbeya ni mbali sana. Ushauri wangu ni baada ya Mtwara iwe Mwanza.

(iii) *MWATEX*, swali nauliza, je, Kiwanda tajwa hapo juu kimeuzwa kwa mwekezaji? Je, kama kiliuzwa, wafanyakazi walioachishwa kazi nyakati hizi stahili zao

zililipwa zote? Ushauri wangu kwa Serikali ni Serikali kuwa makini sana kuvibinafsisha viwanda nchini kwa sababu wawekezaji wengine hawana uwezo wa kuviendesha kiendelevu.

(iv) Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi hili liitwalo Machinga ni kubwa kwa wingi wao kila mmoja wetu tunawajua. Je, kama jamii tu inawafahamu, je Serikali inasema nini juu ya kukosa kwao ajira au kujiajiri? Ushauri wangu ni Serikali kujipanga vizuri, ni jinsi gani uamuzi uliofikiwa wa kuwajengea *Machinga Complex* ili waweze kuyatumia maeneo hayo vizuri kwa mpangilio wa kitija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nawasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMANZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuunga mkono hoja na kumpongeza Waziri kwa hoja yenye matumaini. Wizara ya Viwanda na Biashara ni Wizara ambayo tunaitegemea sana kutufikisha kwenye nchi ya ahadi, nchi yenye uchumi wa kati *A semi industrialized Economy*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara itoe *support* kubwa kwa *NDC* ambayo naiona iko *serious* katika kuanzisha na kufufua viwanda vilivyokufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuma cha Liganga na Makaa ya Mawe ya Mchuchuma ni rasilimali muhimu sana. Ni ukombozi mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba usimamie vizuri *TBS,* lazima *TBS* ifanye kazi yake kwa uadilifu na uzalendo. Nchi yetu haiwezi kuendelea kuwa *a dumping place* ya bidhaa hafifu na hasa vyakula. Tunapukutika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* kama nilivyosema kwenye mchango wangu wa kauli ndiyo tegemeo la wananchi wa kawaida. Tusambaze viwanda vidogo huko vijijini huko Ngara na kwingineko. Nishaiomba *SIDO* kuja

Ngara kutoa elimu ya ujasiriamali na ikiwezekana itusaidie mizinga ya kisasa tuweze kufuga nyuki kisasa. Hii ni katika ule utaratibu wa zao moja kwenye kila Wilaya. Ngara ina zao la Kahawa lakini eneo ninalotoka la Rulenge, sisi hatulimi kahawa, lakini tunaweza kufuga nyuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kwa kuanzisha mchakato wa Soko la Kimataifa la Kabanga huko Ngara. Najua soko hili linajengwa na Mradi wa *DASIP* kwa ufadhili wa *ADB,* lakini najua Wizara ya Viwanda na Biashara inahusika na mchakato huu pia. Naiomba Wizara isaidie kuanzisha masoko ya mpakani ya Murusagamba na Rusumo Wilayani Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Ngara inayopakana na nchi za Rwanda na Burundi na haiko mbali na nchi ya Kongo – Kinshasa, inafaa sana kama mahali pa kuanzisha utaratibu wa *EPZ* au *Special Economic Zone*. Naomba mtaalam aje Ngara kuona hali ilivyo. Ni muhimu pia kuiwezesha Ngara kufanya biashara na Rwanda na Burundi.

(i) Naiomba Wizara ianzishe Kiwanda cha Kuzalisha Zana za Kilimo aina ya *UFI* au kumnyang'anya Kiwanda cha *UFI* Mwekezaji aliyebadilisha matumizi kwa kuzalisha mabomba.

(ii) Kiwanda cha Mangula kilikuwa kinazalisha *spare parts* kwa ajili ya Viwanda vya Sukari pamoja na *Landrovers*. Kwa nini tusinunue mitambo tena na kukifufua badala ya kumwachia mtu majengo kuanzisha shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, Hotuba yako inaleta matumaini isiwe ni *intentions* tu. Tutumie mbinu ya *Big Results Now*. Tutekeleze huo mpango wako wa kuanzisha viwanda. Watumishi ambao hawawezi kubadilisha *mindset* wawe *fired*. Muwekeane *(performance contracts),* mikataba ya utendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu la kuwawezesha wazawa kumiliki viwanda ni muhimu sana. Wazawa

(Watanzania weusi) hawawezi kuendelea kuwa Manamba kwenye nchi yao. Lazima wawe na *BIG Stake* kwenye uchumi wao siyo kuishia kupiga siasa *(Superstructure)* bila kumiliki *Economic Base*. Viwanda vyetu ndivyo vitakavyotoa ajira ya uhakika kwa vijana wetu.

**MHE. AMINA M. MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa masikitiko makubwa sana na kubwa linalonihuzunisha ni kwa nini Wizara nyeti na muhimu kama hii ambayo lengo lake kuu ni kukuza uchumi na kuongeza pato la Taifa na kuondosha umaskini wa kipato kwa wananchi, inapewa siku moja ya kuijadili bajeti yake. Kwa kweli hii si haki hata kidogo kwani inatunyima haki ya msingi ya kuijadili Wizara hii na kutoa maoni yatakayopelekea kuisaidia Wizara, kwa njia moja au nyingine. Kwa siku moja hii ni kama vile funika kombe mwanaharamu apite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kubwa ni upungufu wa bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara na hata hizo chache zinazotengwa pia hazifiki kwa wakati, ukiangalia mpaka Februari, 2013 Wizara imepokea asilimia 23 tu ya fedha zilizotengwa, hii ni aibu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwendo huu wa kusuasua na ufinyu wa bajeti kwa Wizara na fedha kuchelewa kufika kwa wakati. Hii inaonesha wazi kabisa kuwa Serikali haina nia ya dhati ya mabadiliko wanayoyaongea ya kutoka katika uchumi wa chini wa kutegemea kilimo na kwenda kwenye uchumi wa kati wa viwanda na biashara. Kusema ukweli kwa mwendo huu wa bajeti, hii itakuwa ni ndoto za alinacha hazitakamilika abadani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, tuna miradi ya kimkakati mikubwa kabisa ya *Tanzania China Logistic Centre* na Bagamoyo *EPZ,* pesa zinazotakiwa kwa fidia tangu mwaka 2010 ni bilioni 60 na bilioni 50, mpaka leo Serikali bado imelala. Nampa pole sana Mheshimiwa Waziri kwani hata uwe na *degree* sita za uchumi kama huna fedha kwenye Wizara yako hutaweza kufanya chochote. Ni lazima Serikali itoe pesa hizi kama ilivyokwishaahidi kwani hatuko tayari

kuwapoteza hawa wadau, kuna nchi kibao zinaukodolea macho huu mradi wa *logistic centre* ni kama vile tunachezea shilingi chooni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo yaliyotengwa kwenye baadhi ya mikoa kwa ajili ya uwekezaji *EPZ/SEZ* kama Tanga – neema, Mtwara, Kigoma na mikoa mingine. Tathmini ya maeneo hayo imefanyika tangu 2008/2009 kwa Tanga ilikuwa ni bilioni 42.3, pesa ya fidia kwa kipindi hicho mpaka leo lazima itakuwa imeongezeka. Lakini wasiwasi mkubwa ni lini hasa watalipwa hawa watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri suala hili linatugusa sana kwani wananchi waliohamishwa maeneo hayo wameathirika kisaikolojia na wamerudi nyuma kimaendeleo. Niiombe Serikali isiwahamishe watu tena kama hawajajipanga kwani ni hasara kubwa kwa Serikali na wananchi kwa ujumla. Najua kwenye Wizara yako kuna wataalam wazuri kabisa, lakini tatizo kubwa ni fedha, hivyo Serikali lazima kutekeleza wajibu wake ili kuweza kufikia malengo yaliyowekwa kwenye Wizara.

**MHE. HAJI KHATIB KAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote duniani hutegemea kukuza uchumi wake kwenye sekta ya viwanda, lakini pia nchi yoyote duniani hupanua ajira kwa wananchi wake kwenye sekta hiyo hiyo ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nchi yetu ikiwa na vijana wengi ambao hawana ajira, Bajeti ya mwaka 2012/2013, iliidhinisha Shilingi Bilioni 60 kwa ajili ya kulipia fidia ya makazi ya wananchi kwenye eneo la Kurasini, eneo ambalo linatarajiwa kujengwa mji wa viwanda *China – Logistic Center*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko hadi mwaka wa fedha umekwisha, Serikali iliipatia Wizara kiasi cha Shilingi Milioni 550 tu katika bajeti hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwekezaji akifuatilia kwa Serikali au Wizarani kujua kwamba tayari wamekamilisha

kulipa fidia eneo hilo la mradi, tukumbuke kwamba zipo nchi ambazo zinaunyemelea mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo Serikali itashindwa kutoa fedha hizo kwa wakati, mwisho mwekezaji huyo bila shaka mradi huo ataupeleka kwa wengine wanaounyemelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo mradi huu ambao unatarajiwa kutoa ajira zaidi ya 25,000 kwa Watanzania, basi dunia itatucheka, lakini pia Watanzania watafahamu kwamba Serikali yao imekuwa ikiwafurahisha kwa maneno mazuri, lakini haina nia ya dhati kuwasaidia na kuwakomboa kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikiwa Serikali hadi sasa imeshindwa kukamilishwa kulipa fidia ya Bilioni 60 na kwa kuwa fidia hiyo hadi sasa imeongezeka na imefikia Bilioni 94. Je, Serikali kweli itaweza kulipa nyongeza hiyo ya thamani iliyoongezeka na je! Serikali iko *serious* na mradi huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 *TBS* ilipata shutuma na lawama nchi nzima hadi kupelekea aliyekuwa Mkurugenzi wake Charles Ekerege kusimamishwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shutuma hizo na lawama kwa upande mmoja sawa lakini kwa upande mwingine shutuma hizo na lawama zinafaa zielekezwe moja kwa moja kwa Serikali iliyoko madarakani, kwa sababu haiingii akilini na wala haifanani nchi kama Tanzania yenye watu zaidi ya Milioni 40 badala yake *TBS* iwe na wafanyakazi 197 na iweze kudhibiti bidhaa zenye ubora nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na upungufu wa wafanyakazi mwaka 2010/2011, Shirika liliomba kibali cha kuajiri wafanyakazi 35, lakini Serikali ilitoa kibali cha kuajiri wafanyakazi 18 tu. Hata hivyo, kibali hicho hakikutekelezwa, Serikali ilisitisha ajira, mwaka uliofuata shirika liliomba nyongeza ya wafanyakazi 15. Ombi hilo halikufikiriwa kabisa na mwaka wa bajeti 2012/2013, Shirika liliomba tena kibali

cha kuajiri wafanyakazi 32 tu. Hata hivyo, kibali hicho hakikutekelezwa kwa sababu Serikali ilisitisha ajira mwezi Februari mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitamwomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya majumuisho atuambie ni lini sasa Shirika la *TBS* litapatiwa wafanyakazi wa kutosha ili wasilalamike kila wakati?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiona jinsi Shirika linavyofanya kazi, lakini hata hivyo linashindwa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kutokana na upungufu huo. Ni muhimu sasa Serikali kuipatia *TBS* rasilimali watu ya kutosha ili wafanye kazi yao kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majirani zetu Kenya wamefanikiwa sana kwenye Shirika lao la Viwango *KEBS*, kwa nini wamefanikiwa, Serikali ya Kenya imeliwezesha Shirika lake kwa kulipatia wafanyakazi zaidi ya 1,000. Vile vile Kenya imefanikiwa sana na mfumo wa sheria ya *PVOC*. Mheshimiwa Mwenyekiti, nini maana ya PVOC? *PVOC* ni mpango wa udhibiti ubora ambao hutumika kuthibitisha kuwa bidhaa zinazoingizwa nchini kutoka nchi mbalimbali zinakidhi matakwa ya viwango kabla ya kusafirishwa kwenda nchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri na niseme kuiga jambo jema si dhambi. Kwa hiyo, tuangalie ikiwa Kenya utaratibu wanaotumia wa kukagua bidhaa zinapofika nchini unawasaidia, tofauti na sisi bidhaa zinazokaguliwa nje ya nchi, basi tuige, kuiga jambo jema si dhambi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimetoa ushauri huo, nimetoa ushauri huo kwa kuzingatia kauli ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara hapa Bungeni alipokuwa akijibu swali aliposema Mawakala wetu wanaokagua bidhaa nje ya nchi sio waaminifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kuhusiana na maendeleo ya viwanda. Mheshimiwa Waziri

Mkuu hivi karibuni alizungumza kwamba, nchi yetu iko kwenye mapinduzi ya viwanda. Viwanda vyetu vidogo vidogo vimekuwa vikiathiriwa sana katika uzalishaji wake na tatizo la umeme, umeme limekuwa ni tatizo kwa sababu umeme umekuwa ukikatikakatika kila baada ya masaa kadhaa, kutokana na tatizo hilo, viwanda vimekuwa vikisimamisha utendaji wake wa kazi kwa muda unaotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mapendekezo yangu kwa Wizara kushirikiana na Wizara ya Nishati kutatua tatizo la umeme ili kuweza kuvikomboa viwanda vyetu vidogo vidogo. Vile vile Serikali ilitamka wazi kuwa imeandaa mkakati wa kuendeleza sekta ya nguo na mavazi ili kuboresha teknolojia ya viwanda vya nguo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mradi huo uweze kufikia malengo yake ni lazima Serikali ifanye juhudi za makusudi za miradi ya makaa ya mawe, lakini kwa umeme huu huu wa kukatikakatika kila wakati malengo haya hayatafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango na mikakati hii ambayo utekelezaji wake unahitaji mambo mengi kufanyika kwa kutegemea eneo lingine basi mashirikiano katika kufanikisha hili uwekewe mkazo zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishukuru Serikali na Wizara hii husika kwa kufanikisha ununuzi wa mashine za uchimbaji makaa ya mawe. Hii inaweza kutusaidia na pengine kuelekea mahali ambako Watanzania wangependa tuwe. Nashukuru.

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kupata nafasi hii ya kuchangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko ya mwaka 2013/ 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa Hotuba yake ya Bajeti nzuri na yenye kutekelezeka. Hakika kwa mipango hii Serikali

itatatua matatizo yaliyopo katika sekta hizi muhimu na ikumbukwe sekta hii ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuanza kuchangia hoja hii iliyokuwa mbele yetu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alituahidi kujenga soko la kisasa Mlandizi na Kiwanda cha Kusindika Nyanya, lakini mpaka leo hakuna utekelezaji wa aina yoyote. Tunaomba maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na masoko atuambie hizi ahadi za Mheshimiwa Rais zitatekelezeka lini, kwani ni muda mrefu sasa na wananchi wa Kibaha Vijijini bado wanaendelea kupata hasara kwa kukosa mahali pa kusindikia mazao yao kipindi chote hiki. Pamoja na uhitaji wa soko hilo, kwani ikumbukwe kwamba tunapochelewesha miradi hii tunapoteza mapato ambayo yangetokana na ushuru ambao ungetozwa kutokana na miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali yetu kufanya juhudi kubwa katika sekta hii lakini bado inakabiliwa na changamoto nyingi, changamoto zote hizo zinafanya bidhaa zetu kuwa na bei kubwa hivyo kumuumiza sana mwananchi wa kawaida. Pia kuporomoka kwa sarafu yetu katika soko la dunia limekuwa kikwazo kikubwa, pia ifahamike kwamba matumizi ya fedha za kigeni yanaathiri sana uchumi wetu na watu wetu pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itilie mkazo na kusimamia hilo na kukataza biashara ndani ya nchi zifanyike kwa fedha za kigeni na badala yake shilingi yetu ndio itumike katika matumizi yote. Kufanya hivyo kutaleta heshima ya sarafu yetu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile gharama kubwa ya malighafi na vipuri toka nje, kupanda kwa bei za mafuta yaani bidhaa za *petrol*, hapa kuna changamoto nyingi sana kwani kwa nchi yetu imekuwa kawaida kwa mwaka mmoja, bei hizi za mafuta kubadilika kila mara bila kuwa na sababu

za msingi, ikilinganishwa na baadhi ya nchi jirani ambazo hawana bandari na wanakuja kuchukua mzigo wa mafuta hapa kwetu, lakini wamekuwa wakisimamia bei moja ya nishati hii ya mafuta kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni changamoto kubwa na napenda kuishauri Serikali iweke mikakati madhubuti, kwanza ya kuzuia hii milipuko ya bei na zaidi kushirikisha wadau wote kutafuta mbinu za kuwezesha kutatua matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi ambazo ziko juu kiuchumi zilifanya juhudi kubwa kuwa na sera nzuri ya viwanda, kuwekeza katika viwanda na kuboresha sekta hiyo, siku zote viwanda huleta faida nyingi ukiachilia mbali kukuza ajira kwa watu wake, lakini kikubwa ni ukuaji wa uchumi wa nchi, viwanda vyetu vingi vimekufa yamebakia magofu tu, lakini tuna uwezo wa kutafuta wawekezaji kuja nchini kuwekeza katika viwanda. Ifike mahali kama Taifa tuwe na mkakati maalum wa kukuza viwanda nchini na utiliwe mkazo mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuikumbusha Serikali kutokuwasahau wenye viwanda vidogo vidogo tena kuwawezesha ili wainuke. Miaka ya hivi karibuni kumetokea wabunifu wengi ambao ubunifu wao unahusu zaidi viwanda, lakini tumeishia tu kuwasifu na kuwaacha kama walivyo. Naishauri Serikali kuwajali na ikiwezekana katika Bajeti ya Viwanda, Biashara na Masoko watengewe bajeti yao ili tupate wataalam wetu wenyewe katika fani ya kugundua vitu na kutengeneza. Hii itailetea sifa nchi yetu na kuzidi kututangaza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Kibaha Vijijini tuna upungufu wa viwanda, viko vichache, tunaiomba Serikali kuangalia hilo, pale panapotokea mwekezaji kuja kuwekeza kwenye sekta ya viwanda, basi Serikali iwaelekeze Kibaha kwani tuna maeneo makubwa na ya kutosha kujengwa viwanda vikubwa na itasaidia upatikanaji wa ajira ambao ndio kilio cha vijana nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile tunaiomba Serikali kutujengea Chuo cha Ufundi katika Kata ya Kwala au Magindu ili kuweka mazingira yatakayowezesha vijana kupata mafunzo na kuanzisha viwanda vidogo vidogo vitakavyotumia rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie suala la mazingira, hapa nagusia zaidi viwanda vyetu nchini ambavyo havifuati Sheria ya Mazingira nchini. Kufanya hivyo ni kutotii mamlaka na Sheria zilizopo, naomba Serikali kutilia mkazo kwenye hilo kwani Sheria zipo na wasimamizi wa mazingira wapo pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, wafanyakazi wanaofanya kazi katika sekta ya viwanda wamekuwa wakilalamikia suala la kufanya kazi bila vitendea kazi maalum ambapo baadaye hupata maradhi ama kuathirika na kuishia kutelekezwa na waajiri wao pasipo msaada wowote huku hao wamiliki wa viwanda hivyo wakijua kabisa kutokumpatia mfanyakazi vifaa maalum (*safety equipments*) ni kosa. Naishauri Serikali kufanya ukaguzi wa kila mara kwenye viwanda hivi na adhabu kali kutolewa kwa wote watakaobainika kutenda makosa kama hayo ili kuwalinda watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumalizia kuikumbusha Serikali kuwa katika Bunge lililopita nilizungumzia kuhusu Serikali kutenga eneo maalum la kuegeshea magari yote yanayoingia nchini hata yale ya *transit* sehemu moja ili kuwezesha Serikali kuingiza mapato kupitia mradi huo. Nilipendekeza mradi huo ujengwe Kibaha kwani sisi tuna maeneo ya kutosha na pia itasaidia kupunguza msongamano wa sehemu za kuuzia magari mjini, kwani hivi sasa imekuwa kero, kila baada ya kilomita mbili utakutana na *yard* ya magari zilizozagaa mjini na kusababisha mandhari mabaya ya miji yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza pia aina hiyo ya uuzaji magari mitaani uwekwe katika mfumo huu wa kuyatengea sehemu moja kama wafanyavyo nchi nyingine,

hii itasaidia pia kuliingizia pato Taifa kwani kupitia mradi huo ambao utakuwa chini ya Serikali wadau watakuwa wakilipia gharama na hivyo kupata fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara. Maendeleo ya kiuchumi yoyote duniani yanategemea kwa kiwango kikubwa uwekezaji katika sekta ya viwanda sambamba na uwekezaji wa hali ya juu katika uzalishaji wa nishati ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana nchi yetu kwa kipindi kirefu imekuwa haitilii maanani katika uwekezaji wa viwanda nchini baada ya viwanda vingi vilivyoanzishwa baada ya nchi yetu kupata uhuru kuwa vimekufa na kubinafsishwa, viwanda vilivyokuwa vinamilikiwa na umma wa Watanzania. Baada ya nchi yetu kuruhusu na hatimaye kufungua milango tayari kwa kuondokana na mfumo wa uchumi hodhi na kuingia katika mfumo wa soko huria hapa nchini, mambo yamebadilika kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki tumeshuhudia changamoto mbalimbali ikiwemo ujio wa wawekezaji kutoka nje ya nchi wenye shahada za kuwekeza katika sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwemo sekta ya viwanda, madini, kilimo na sekta za ujenzi. Sekta ya viwanda na biashara inategemea sana maendeleo katika sekta zingine kama vile maendeleo ya sekta za usafirishaji za reli, bandari, barabara, mabenki, huduma za bima, maendeleo ya rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza kwa dhati Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kuchukua hatua na kuanza utekelezaji wa mradi wa uchimbaji wa makaa ya mawe na hatimaye kuanza kwa shughuli za uzalishaji wa chuma huko Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano baina ya Shirika la Maendeleo la Taifa la *NDC* na wawekezaji wa Kampuni ya Kichina, hatua hii ni hatua sahihi na ya kupigiwa mfano, kwani Mwenyezi Mungu katujaalia madini haya muhimu ya makaa ya mawe na madini ya chuma. Makaa ya mawe jumlisha madini ya chuma sawasawa na chuma cha pua na umeme. Kwa lugha nyepesi ni kwamba, uchenjuaji wa madini ya chuma unategemea sana uwepo wa makaa ya mawe ambapo tunapata vyote katika eneo moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupatikana kwa chuma kutasaidia sana mapinduzi katika sekta ya viwanda na kusaidia ujenzi wa miundombinu ya reli na madaraja na bandari, pia majengo na vipuri vya mitambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MHONGA S. RUHWANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TBS* na *TFDA; TBS* iko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara wakati *TFDA* iko Wizara ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS* kazi yake ni kuhakikisha ubora wa vifaa na bidhaa mbalimbali ikiwemo chakula hasa *packed food* za ndani na nje ya nchi ili kulinda afya ya walaji na usalama wa walaji na kulinda mazingira ya nchi yetu. *TFDA* inafanya kazi ya kusimamia na kudhibiti usalama na ubora wa dawa na chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maoni yangu vyombo hivi vilivyo chini ya Wizara tofauti vifanye kazi pamoja, hivyo Wizara hii ya viwanda na biashara wakae na Wizara ya Afya ili *TFDA* iwe Idara mojawapo katika Wizara ya Viwanda ikiwa chini ya *TBS* iwe chini yake kwa sababu kazi zake ni moja zinafanana. Hiyo itasaidia ufanisi wa kazi kwani vyombo hivi vitakuwa pamoja kudhibiti ubora na usalama wa bidhaa za nchini na zitokazo nje ya nchi, kwani yapo pia malalamiko kuwa *TBS* haifanyi kazi yake ipasavyo kwani sababu ni upungufu wa wafanyakazi na Serikali ilikuwa imesitisha zoezi la utoaji vibali vya ajira 2010/2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shirika liliomba kibali cha kuajiri wafanyakazi 18 hawakutekelezwa, 2011/2012 shirika liliomba wafanyakazi 15, ombi halikutekelezwa na 2012/2013, shirika liliomba tena wafanyakazi 62 walipata kibali cha kuajiri 32 tu. Hivyo basi, *TBS* na *TFDA* wakifanya kazi pamoja watashirikiana wafanyakazi walionao ili mradi tu wafanyiwe mafunzo ili waweze kutekeleza wajibu wao ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu ya ujasiriamali katika kuendeleza biashara; nashauri elimu hii itolewe hasa kwa wale akinamama waliojiunga pamoja kufanya shughuli zao za biashara na waliopo katika viwanda vidogo vidogo *(SIDO)* ili kuwasaidia wawe na ufanisi katika shughuli zao. Hali hii itapunguza umaskini kwani watapata faida ya kazi yao wakiwa na ujuzi wa elimu ya ujasiriamali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *EPZ* na *SEZ*; Serikali ituambie eneo la *EPZ/SEZ* lililotengwa wananchi watalipwa lini fidia na maeneo hayo kuanza kutumika kama ilivyokusudiwa? Kwani wananchi wanashindwa kuendeleza shughuli zao katika maeneo yale kwani inajulikana Serikali imeshayachukua kwa ajili hiyo. Lini miundombinu ya kiuwekezaji itajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri maeneo hayo yatumike kama ilivyopangwa ili kuongeza uchumi na kuongeza ajira kwa wakazi wa maeneo husika. Vile vile maeneo yakikaa muda mrefu bila kutumika yanaweza kuvamiwa tena na wananchi kwani wataona hakuna kinachoendelea.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naipongeza Wizara kwa Hotuba nzuri inayoonesha nia ya kuinua sekta muhimu ya Viwanda na Biashara. Hakuna Taifa lolote duniani linaloweza kupiga hatua ya maendeleo bila kuimarisha sekta ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya kilimo ambayo inaajiri asilimia themanini (80%) ya Watanzania, haiwezi kupiga hatua kama hakuna viwanda, kwa sababu viwanda

ndiyo vinavyoweza kuongeza thamani ya mazao ya kilimo ili tuweze kupata bei nzuri ya mazao yaliyoongezewa thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa viwanda uko katika kutatua tatizo la ajira linalokabili vijana wetu wengi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa hatuna viwanda, maana yake ni kwamba, tunapeleka ajira huku ambako tutauza mazao yetu yakiwa ghafi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri ni kwa zao la pamba, asilimia kubwa ya zao la pamba tunalolima hapa nchini, tunauza nchi za nje zikiwa katika hali ghafi na kwa kufanya hivyo, maana yake kwanza tunapata bei ndogo ya pamba na pili tunapeleka ajira nje ya nchi kwa maana pamba ikifika huko nje ya nchi ndiyo kuna viwanda vya nyuzi na nguo na bidhaa nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunataka kusonga mbele kimaendeleo na kiuchumi hatuna namna, ni lazima tuwe na mkakati wa makusudi wa kuwa na viwanda vya kati na viwanda vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. VINCENT J. NYERERE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mungu sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia, kutoa kero na kuwasilisha mapendekezo na maoni yangu kuhusiana na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bidhaa bandia; mbali na juhudi zinazooneshwa na Serikali kwa kupambana na bidhaa bandia bado hali siyo nzuri na hali inatokana na ukubwa wa kazi ikilinganishwa na uchache wa watumishi, vifaa na fedha za kuifanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kweli tunayo nia thabiti ya kuzuia bidhaa bandia hapa nchini, basi ipo haja

ya kuongeza nguvu na pia sheria zetu kuhusu bidhaa bandia na adhabu ziangaliwe upya, huku kikosi kamili cha ufuatiliaji wa kazi za udhibiti kuundwa upya na kipewe uwezo kamili wa kuzuia, kukamata na kushtaki huku maabara zikijengwa katika kila *Entry Point* na bandari, mipaka na viwanja vya ndege ili kazi hiyo iweze kuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda; nipende tu kuleta masikitiko yangu kuhusu viwanda vya umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda vilijengwa siyo tu kupunguza umaskini kwa kutengeneza faida, bali kutoa ajira ambalo ndio lilikuwa lengo kuu la Serikali ya awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima kama Taifa tuangalie upya jinsi gani ya kuanzisha tena viwanda vingine vya umma kwa ajili tu ya kutoa ajira kwa wananchi ambapo faida yake haipo *Direct* kwa Serikali ila kwa wananchi na hii itapunguza sana, uhalifu na itapunguza lawama kwa wananchi wanaolaumu Serikali kwa ukosefu wa ajira. Pia bado inawezekana kujenga na kuvikopesha Vyama vya Ushirika na kuweka taratibu maalum ambazo kimsingi zitazuia na kuepuka ubadhirifu. Bado tunayo nafasi ya kujenga viwanda vichache kwa majaribio kabla ya kulifanya zoezi hilo nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninalosikitika nalo ni kuhusu biashara za maua ya *plastic* na pikipiki na baadhi ya bidhaa zinauzwa na wachuuzi wa Kichina hapa nchini. Lazima kuwe na tofauti ya wanaozalisha na wafanyabiashara. Serikali ihamasishe wawekezaji wa Kichina waje hapa nchini kujenga kiwanda kuliko kuleta bidhaa na wao kuja kuziuza hapa nchini. Ikiwezekana basi itungwe Sheria itakayoweza kabla ya bidhaa kuingizwa na mwekezaji, basi kwanza uwezekano wa kuweka viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukaguzi wa magari *(TBS)*; bado napenda kushauri sana ukaguzi wa magari ufanyike nje na ndani ya nchi ili kuwe na ushirikiano na

tuangalie jinsi ya kuokoa fedha za Watanzania zinazokwenda nje ya nchi kwani taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* ulionesha katika *USD* 8m ni 2.2m peke yake ndio fedha iliyokuja hapa Tanzania, hiyo inaonesha bado fedha nyingi sana za kigeni huenda au hubaki nje ya nchi na hii siyo nzuri kwa uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu waliokuwa wafanyakazi wa *MUTEX*; waliokuwa wafanyakazi wa *MUTEX* waliahidiwa humu Bungeni kuwa wangepewa nyongeza kwa fedha ambayo walishindwa kuipokea kwa kuwa ilikuwa ni kidogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu 834 ukiwagawanya shilingi milioni 70, kila mtu atapata shilingi 83,933/= ambapo haitoshi hata nauli ya mtu mmoja nauli ya kurudi walipotoka huko makwao kuja Musoma *(MUTEX)* kwa kulitumikia Taifa kama watumishi wa kiwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua juhudi ya Wizara ya kufuatilia fedha za malipo ya waliokuwa watumishi wa kiwanda hiki. Napenda sana kuiomba Serikali ikae na kuuthamini mchango wa waliokuwa wafanyakazi wa *MUTEX* ili walipwe na waondokane na adha hiyo ya kuilaumu Serikali, kwani sasa wamejenga chuki kubwa sana dhidi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mategemeo yangu katika majibu ya Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri ataeleza ni lini fedha ile itaongezwa ili kupunguza hasira ya waliokuwa watumishi wa *MUTEX*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea Chuo cha Elimu ya Biashara *(CBE)* Tanzania. Vipo vyuo vingi vya binafsi katika nchi, lakini Serikali inacho chuo kimoja ambacho kipo Dar es Salaam na kina Matawi Mwanza na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo hiki kipo katika hali

mbaya ukilinganisha na chuo hiki na Chuo cha Hombolo ambacho kinamilikiwa na TAMISEMI. Ukifika katika Chuo cha Biashara, Dar es Salaam huwezi kuamini kama kinamilikiwa na Serikali. Chuo hiki kipo katikati ya Jiji, lakini kinatia aibu, madarasa ni ya hovyo. Cha kushangaza sehemu ya eneo lake limeporwa na Wahindi na wamefanya kiwanda karibu na madarasa na Walimu na wanafunzi hupata kadhia kubwa wanapofundisha. Ni kwa nini Serikali imeruhusu ardhi ya chuo hiki kuchukuliwa na kuminya nafasi ya kujipanua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ikitazama chuo hiki kiwe na hadhi kulingana na elimu inayotolewa pale, kama TAMISEMI wameweza Serikali Kuu inashindwa nini? *CBE* ukusanyaji ada zaidi ya bilioni 12, lakini wanashindwa kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niongelee viwanda feki vilivyozagaa nchini. Vipo viwanda vya kutengeneza bidhaa mbalimbali kama mabati, *gypsum board*, na kadhalika. Viwanda hivi viko chini ya viwango na katika mazingira mabovu vingine viko katika nyumba za watu (makazi) viwanda hivi ni vya Wachina. Cha kushangaza zaidi viwanda hivi wamiliki wamepewa vibali vyote kama *TBS*, Leseni, *TIC* na kadhalika, Serikali inasema nini juu ya viwanda hivi. Pamoja na kuwa chini ya viwango, lakini pia wafanyakazi katika viwanda hivi ambao ni Watanzania wanafanya kazi kwa malipo duni na katika mazingira yasiyofaa.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kushauri au kuchangia kwa maandishi katika Wizara hii ya Viwanda na Biashara, ushauri wangu kimsingi umelenga katika maeneo muhimu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa la viwanda na biashara Tanzania linasababishwa na mambo mengi kutokuendelea, lakini suala la gharama za umeme na ukosefu wa umeme bora na wa kutosha ni sababu tosha za kuzorota kwa ukuaji wa uchumi katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwepo na umeme wa

uhakika na bora na gharama kubwa za nishati hiyo zimefanya viwanda vyetu vichache vilivyopo vishindwe kujiendesha vizuri na hivyo vingine kufa na vingine kuzalisha bidhaa ambazo baada ya uzalishwaji bidhaa hizo zinauzwa kwa bei kubwa na kupunguza uzalishwaji kwani watu wengi wenye kipato cha chini na cha kawaida wanashindwa kununua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, ili kuwepo na ufanisi katika viwanda na biashara zetu, ni lazima sana ufanisi wa kutosha katika sekta ya nishati uzingatiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine katika viwanda na biashara ni Serikali kutambua kuwa, riba za mabenki yetu ya kibiashara ni kubwa sana, hivyo kukatisha tamaa wafanyabiashara wa ndani ambao wana malengo ya kuanzisha biashara zenye sura ya kimiradi; kama viwanda na biashara kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana Serikali kuangalia uwezekano wa kusaidia suala la riba hasa kwa Watanzania wanaotaka kuanzisha viwanda na biashara kubwa kubwa katika Taifa letu, riba katika mikopo imekuwa ni kikwazo kikubwa sana kwa uanzishwaji wa viwanda. Kwani ilivyo sasa kiwango cha riba kinachotozwa ni kikubwa sana na hivyo kuvunja moyo watu wenye nia na malengo ya kuanzisha viwanda vidogo vya kati na vikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashaka yangu makubwa sana yako pia kwenye mradi wa Kurasini *Logistic Hub* ambapo mtazamo wangu unaona mradi huu hautaweza sana kusaidia kuendeleza nchi yetu hasa katika sekta ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kurasini *Logistic Hub* ukitazama malengo yake kwa ndani utaona ni kwa namna gani mradi huu utakavyosaidia kuua hata viwanda vichache ambavyo vitakuwepo, kwani kuwa na kituo kikubwa cha usambazaji wa bidhaa kutoka China tena bidhaa ambazo zimekwishatengenezwa ni hatari kubwa kwa uchumi wa viwanda vyetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha *General Tyre* utaratibu wa kukifufua umeanza na kimsingi napongeza juhudi hizi lakini cha kusikitisha ni kwamba, wakati kiwanda hiki kinafungwa kuna wafanyakazi wengi walisitishwa kazi, lakini mpaka leo wengi wao hawajalipwa mafao yao. Hivyo, naitaka Serikali iwe na utu kidogo na kufanya juhudi za kulipa watu hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie kwa kuomba Serikali kuwatazama wafanyabiashara wadogo (Machinga) kwa umakini na kuwatambua pia kama wazalishaji katika Taifa lao.

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwasilisha kwako mchango wangu katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kuhusu makadirio ya matumizi ya fedha ya ofisi yake kwa mwaka 2013/2014 kama ilivyowasilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri na wenye weledi uliotukuka. Pia nampongeza Naibu Waziri kwa uwezo mkubwa alioonesha katika utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya viwanda nchini imekuwa ngumu sana hasa vile ambavyo vilibinafsishwa kwa taasisi na wafanyabiashara. Vingi kati ya viwanda hivi vimebadilishwa matumizi havijaendelezwa kama ilivyokusudiwa na Serikali. Naishauri Serikali iangalie upya sera ya kutowekeza kwenye viwanda. Ni wakati mzuri sasa kuwekeza katika Viwanda vya Ubanguaji wa Korosho, Nyama na Nyuzi. Ikiwezekana wale ambao wameshindwa kuendeleza wanyang'anywe ili Serikali iwekeze mtaji wa kuviendesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na viwanda vikubwa kuhitaji mtaji mkubwa katika uwekezaji, naishauri Serikali iweke mkazo katika viwanda vidogo vidogo. Hivyo, *SIDO* wapewe mtaji wa kutosha ili kuwekeza na kuinua sekta ya viwanda nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za makusudi zifanyike kuhakikisha kuwepo na udhibiti wa bei za bidhaa ili kuondoa hali ya mfumuko wa bei usio na maelezo. Sheria ya mapato *Income Tax Act, Cap* 332 kifungu 33 kinazuia wafanyabiashara kupata *Super Profit*. Hivyo ili kumlinda mtumiaji ni lazima Serikali iweke udhibiti wa bei za bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali isimamie ipasavyo wafanyabiashara kutoka nje ya nchi kuvamia na kushiriki katika biashara ndogo ndogo, kama maduka ya bidhaa ambapo Watanzania wana uwezo mkubwa wa kuzifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Mizani apewe mtaji wa kutosha ili aweze kushiriki ipasavyo katika uwekezaji mpya katika sekta ya gesi. Hii itasaidia sana Serikali katika udhibiti wa mapato na bidhaa zitokanazo na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono jitihada za kuanzisha kiwanda cha kuua mazalio ya mbu kwa ushirikiano wa *NDC* na Serikali ya Cuba, jitihada ziongezwe ili ujenzi wake ukamilike kwa haraka ili vita dhidi ya *malaria* iwe rahisi na kuwapunguzia wananchi mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya viwanda inategemewa sana kukabiliana na tatizo kubwa la ajira nchini. Hata Mheshimiwa Rais wakati alipokuwa anafungua Bunge hili 2010 alionesha nia ya kukuza sekta hii ili kuweza kukabiliana na tatizo hilo na kupata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo viwanda vilivyochukuliwa na wafanyabiashara/wazalishaji kwa makusudi ya kuendeleza uzalishaji. Cha kusikitisha bado vipo viwanda ambavyo havifanyi uzalishaji kufuatana na mapatano na Serikali. Namwomba Mheshimiwa Waziri

anisaidie wakati anahitimisha ni viwanda vingapi havijaanza uzalishaji kufuatana na makubaliano na ni kwa nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sera ya Serikali ni kuinua viwanda vya nchini kwa kununua vitu vinavyozalishwa hapa nchini ili kuvijengea uwezo wa kifedha. Kinyume na hili, nataka Mheshimiwa Waziri atoe kauli leo, ni kwa nini Serikali na taasisi zake hupendelea kununua vifaa vinavyotoka nje ya nchi mfano, samaki, magunia, na kadhalika angali vitu vyote hivi vinapatikana hapa nchini. Ni kwa nini hifadhi ya chakula inanunua magunia toka nje ya nchi wakati wapo wazalishaji wa magunia nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya bidhaa za viwanda kama vile mabati, misumari, nondo, samaki vinapanda bei mara kwa mara, jambo linalowatesa sana wananchi katika ujenzi wa nyumba. Hata hivyo, hali hii hufanya kodi za nyumba kuwa juu na kuwaumiza sana wapangaji walio wengi. Namshauri Mheshimiwa Waziri na Serikali kuunda Tume ya Bei itakayomlinda mlaji ili kuondokana na tatizo la kupanda bei za vifaa vinavyozalishwa viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu pongezi kwa Mheshimiwa Waziri/Serikali; napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na watendaji wake wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya katika Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu soko la Kimataifa Makambako; soko la Kimataifa la Makambako liliahidiwa kuanza mapema sana, lakini hadi leo hakuna kinachoendelea. Aidha, wananchi ambao wapo kwenye eneo hili wanadai fidia, cha kushangaza hadi leo hakuna fidia yoyote iliyotolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri

atoe maelezo ni lini soko hili litaanza kujengwa na kufanya na lini wananchi hawa watalipwa fidia zao. Soko hili ni muhimu sana katika uchumi wa nchi na nyanda za juu Kusini. Makambako ni mpitio wa mikoa yote ya Kusini.

**MHE. MAGALLE JOHN SHIBUDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Wizara hii ni maelezo mema ya kutambulisha azma njema kwa ustawi wa maendeleo ya uongozi wa utawala bora wa maslahi jamii ya mchakato wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itambulishe na iwaarifu Watanzania inatekeleza juhudi zipi za kuipatia soko pamba mbegu ambayo inagusa maslahi ya wananchi wasiopungua milioni kumi (10) vivyo hivyo naomba ushuhuda wa dhati ambao ni ufafanuzi makini wa vitendo vinavyotekelezwa kuhusu pamba kuwa MKUKUTA kwa wakulima wa pamba kupitia Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *NDC* linasimamia maslahi mapana ya viwanda vya kugusa ustawi wa jamii na Taifa. Naomba maelezo ya kwa nini Serikali ina ukimya kuhusu *NDC* kuibua kiwanda cha uwezo mzito wa Kiwanda cha Kusindika Nyama kilicho sambamba na utajiri wa mifugo ambayo ipo katika jamii ya wananchi milioni 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maswa tuna eneo la kuwezesha Viwanda vya Ngozi na Nyama. Je, Serikali inatoa fursa zipi zitekelezwe na Halmashauri ya Maswa tupate viwanda hivi vya kuhudumia wigo mpana wa maeneo ya wafugaji wa Kanda ya Ziwa. Naomba maelekezo ya kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na kazi njema.

**MHE. SUSAN A.J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda ni eneo/muhimu la kuweza kukuza uchumi wa nchi yoyote ile na ndio maana nchi za Ulaya kupitia *Industrialization* au *Industrial Revolution* zilianza kuendelea kwa kasi kubwa. Ni jambo la kusikitisha kuwa, Tanzania iliyokuwa na Viwanda

vingi, sasa Viwanda hivyo vimebinafsishwa na kibaya zaidi havifanyi kazi zetu za asili. Matokeo vingine vimekuwa ma-*godown* na vingine kubakia magofu. Mfano, mzuri ni kiwanda cha *UFI* (*Ubungo Farm Implements)* ambacho kiliweza kutengeneza nyenzo za kilimo kama majembe, rato, sururu, mapanga na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa kuwa asilimia 80 ya Watanzania wakulima tena maskini, hivyo ilikuwa busara sana kuwa na kiwanda cha aina hii ili kuwafanya wakulima kupata bidhaa hizi kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kilimanjaro *Machine Tools* nayo hivyo hivyo, lakini kubwa zaidi ni kile cha Arusha *General Tyre* ambacho kilitengeneza magurudumu mazuri na yenye kudumu sana. Sasa hivi tunashuhudia *tyres* nyingi kutoka nje hususan Mashariki ya Mbali *good year, Dunlop, Michelin* na kadhalika. *Tyres* ambazo hazina ubora kama zilivyokuwa kwa *General Tyre.* Swali la kujiuliza ni je, Serikali haioni Sera ya ubinafsishaji ni janga kwa nchi yetu? Pia je, ni kwa nini Serikali inabinafsisha hata vile viwanda muhimu kwa nchi yetu? Ni vyema Serikali ikapitia Sera hii ya ubinafsishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwanda Vidogo *SIDO,* Shirika hili limefanya kazi kubwa ya kutoa elimu kwa wananchi na imesaidia sana vijana kujiajiri wenyewe. Ni vyema basi, Wizara isaidie Shirika hili ili liweze kusaidia vijana wetu hasa ikizingatiwa kwamba, ni vigumu sana vijana kuajiriwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS* ni chombo cha viwango Tanzania, lakini cha ajabu chombo hiki kimekuwa hakifanyi kazi yake vizuri na ndio sababu kila siku malalamiko hayaishi, bidhaa bandia zimejaa madukani. Je, tatizo ni upungufu wa rasilimali watu au vifaa kwa ajili ya ukaguzi au ni rushwa? Unakwenda dukani unauliza bidhaa unaulizwa unataka *genuine* au *fake* kwa maana ya *low quality,* je, ni kweli *TBS* hawayaoni haya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kuona

raia wa nje wakifanya biashara ambazo kimsingi zingefanywa na Watanzania. Nimeishi nje ya nchi na sikuwahi kuona wageni wakifanya biashara ndogondogo kama ilivyo Tanzania. Unapoona wenzetu Wachina wanauza vitu vodogovidogo vya kutembeza ni hatari na inaweza ikavunja amani kama ilivyofanyika Afrika Kusini miaka mitatu iliyopita.

**MHE. KOMBO KHAMISI KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukuza uchumi wa nchi kinahitajika kuwepo kwa kiasi kikubwa cha afya ya wananchi waliomo katika Taifa. Taifa ambalo lina watu wenye afya bora linasaidia kuongezeka kwa uzalishaji na nguvu kazi katika Taifa na vile vile husaidia kuongezeka kwa uchumi na pato la Taifa. Ni lazima na wajibu wa Serikali kukubali kuwekeza kisasa katika suala zima la matibabu, dawa na vitendea kazi pamoja na watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukuza uchumi wa nchi ni lazima Serikali ikubali kuvifufua Viwanda ambavyo kwa njia moja au nyingine vimechangia kuanguka kwa pato la Taifa:-

(1) Kuwepo kwa uhai wa Viwanda kutasaidia kuwepo kwa ongezeko la ajira, lakini kutakuwepo pia uchangiaji wa kukuza pato la Taifa.

(2) Kuanguka kwa Viwanda vya Kubangulia Korosho, Nguo na kuviweka nyuma Viwanda vya Tanga na kufikia hatua ya kufa kumehujumu uchumi wa nchi.

(3) Uingizaji wa bidhaa feki ndani ya nchi hususan madawa ya wanadamu.

*TBS* kuangalia Sheria zinazowaongoza zaidi kuongeza adhabu ili kudhibiti uingizaji wa bidhaa mbovu. Mawakala ni wachache sana hasa kwa China na India ambao wanakagua bidhaa kabla hazijapakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema Serikali ikalieleza Bunge hili, ni kwa nini Tanzania *packers* imekufa? Viwanda vya minofu ya samaki je, ni lini Serikali itavirejesha na

kuviimarisha Viwanda hivi. Serikali ina mkakati gani katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufa kwa Viwanda Vidogovidogo (*SIDO)* ambavyo vilikuwa vikitengeneza vipuri kumeua uchumi wa Taifa na pia kuangusha biashara kunahitaji kufufuliwa kwa *SIDO* ili tukuze uchumi wa Taifa. Tufufuwe Viwanda vya mbolea. Ni wakati muafaka wa Serikali kuweka mkazo katika uwekezaji wa Viwanda vya kimkakati na virutubisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chuma cha Ligunga, *Gas* na *Uranium Indicator* ya kukuza uchumi ni kukuza Viwanda vidogovidogo, mfano, *SIDO*. *UFI* ambacho Kiwanda hiki uzalishaji wake mkubwa ni zana za kilimo, lakini kwa sasa viko chini kabisa kiuzalishaji.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ufufuaji wa Viwanda Vidogovidogo hapa nchini ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa nchi na kuongeza ajira kwa vijana hapa nchini. Nashauri Wizara na Serikali kwa ujumla kutazama upya suala la ufufuaji wa Viwanda hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BRELA,* taasisi hii imekuwa ikisajili nembo na majina ya biashara mbalimbali hapa nchini, lakini taasisi hii imekuwa ikihusishwa kwa kiwango kikubwa na vitendo vya rushwa katika kuhudumia wateja wanaofika pale. Je, ni kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kutumia taasisi hii na kuunda kwa upya, lakini pia kufungua ofisi Mikoani ili kupunguza vishawishi vya rushwa. Ni watumishi wangapi wameshakamatwa na tuhuma hizi za rushwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Viwanda Vidogo Vidogo (*SIDO);* Viwanda hivi vimekuwa ndio tegemeo la wananchi hapa nchini. Hata hivyo, Viwanda hivi haviendelezwi na havina vifaa vya kisasa ili kutoa huduma kwa wingi na kwa ubora unaotakiwa. Je, Wizara ina mkakati gani wa kuendeleza Viwanda hivi Vidogo hapa nchini? Je, kwa kiwango gani *SIDO* katika Mikoa yetu inatengewa mafungu ya kutosha ili kutoa huduma kwa ufanisi kwa wajasiriamali?

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo *(SIDO);* Shirika hili ndilo pekee litakaloweza kuwafikia wakulima vijijini na kuweza kusambaza *machine* ndogo ndogo za kusindika mazao mfano, kutengeneza *jam, tomatopaste, juice, peanut butter* na kadhalika. *SIDO* ina mkakati mzuri kupitia vijijini, kila Wilaya kuzalisha bidhaa moja. Je, *program* hii imefikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo ya *SIDO* hayawezi kukamilika bila Serikali kuwapa *SIDO* fedha za kutosha. Fedha wanazopewa kila mwaka ni pungufu ya walizoomba. Tukumbuke siyo tu kusambaza Viwanda, inabidi watoe mafunzo ya kutumia mashine hizo, masomo ya ujasiriamali, wawezeshe wakulima jinsi ya kuweza kupata vifungashio ili waweze kuuza nje na kushindana na soko la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Viwango *(TBS);* Shirika hili ni kuhakikisha bidhaa zote zinatoza nje au kuzalishwa nchini zinakuwa na ubora na zisizokuwa na madhara kwa mtumiaji. Cha kusikitisha mpaka sasa hivi, bado kuna bidhaa nyingi madukani, mfano, vifaa vya umeme, magari, bado mteja anaweza kwenda dukani anaulizwa anataka *Original au fake,* hii ni hatari. Je, vifaa hivi vinaingiaje ndani ya nchi? Ndio maana kumetokea matukio ya nyumba kuwaka moto utokanao na *short* za umeme. Siyo hilo tu Serikali kupitia Bunge lako Tukufu iliwahi kutoa tamko ni marufuku kuuzwa kwa mitumba (nguo zilizovaliwa) nguo za ndani (brazia, chupi), lakini bila kuogopa vijana wanapita mitaani na nguo hizo wakiziuza mchana kweupe na taasisi hii ya *TBS* ikiwafumbia macho. Je, *TBS* imepuuza maagizo ya Bunge na Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Viwanda nchi zote zilizoendelea mfano China, Korea, Malasyia zote hizi zilihakikisha zinawekeza katika viwanda, lakini hapa kwetu viwanda vilibinafsishiwa kwa watu binafsi. Matokeo yake viwanda vingi havikuendelezwa na vingi kugeuzwa matumizi ya awali. Je, nini hatua ya Kiwanda cha Tanganyika *Parkers* cha Kusindika Nyama pale Kawe, Dar es Salaam.

Kiwanda hiki kilikuwa na mitambo yote tena inafanya kazi. Je, mitambo ile kwa sasa hivi ipo wapi? Hii ni sawa na kiwanda mama cha *Machine Tools* kilichopo Kilimanjaro. Hiki kilikuwa Kiwanda cha Kuzalisha Viwanda Vidogovidogo ni zaidi ya miaka sita, nimekuwa nikiulizia Kiwanda hiki, lakini Serikali imekuwa ikitafuta mwekezaji, je, mpaka leo bado inatafuta Mwekezaji? Je, mwekezaji asipopatikana Serikali ina mkakati gani na Kiwanda hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha *General Tyre* hiki ni Kiwanda kilichokuwa kinazalisha matairi yenye ubora katika Afrika ya Mashariki na ya kati. Ni jambo la aibu, Serikali kutoliweka maanani suala hili na kuruhusu Kampuni ya Kenya ya *Dunlop* ndio wana-*supply* matairi hapa nchini na kutupumbaza na kusahau kabisa kuhusu kufufua Kiwanda chetu. Serikali itupe majibu ya uhakika na *time frame* ni lini Kiwanda cha *General Tyre* kitaanza kazi?

**MHE. RAJAB MBAROUK MOHAMMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Viwanda katika nchi yetu bado halijaweza kusaidia katika pato la Taifa na ukuaji wa nchi sambamba na upatikanaji wa ajira hususan kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanguka na kufa kwa Viwanda vingi hapa nchini kumechangia kwa kiasi kikubwa kuzorota kukua kwa uchumi wetu. Moja ya vielelezo vya ukuaji wa uchumi wa nchi ni kuwepo kwa Viwanda Vidogovidogo. Malengo ya MKUKUTA ni kukuza Sekta ya Viwanda kwa asilimia 15 ili kuongeza thamani ya mazao yetu ya kilimo. Je, Serikali imewezaje kuwashawishi wenye Viwanda kuhamia vijijini badala ya kubaki na kuwekeza Dar es Salaam, je, ni namna gani Wizara itarejesha Viwanda ambavyo kwa sasa vimegeuzwa magodauni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ninukuu kauli ya Mheshimiwa Asha Rose Migiro alipokuwa anazungumza na viongozi katika Mkutano wa 15 wa *All Summit* ambapo alisema:- Afya ya mama na mtoto ndiyo chachu ama kielelezo cha Afya ya Taifa na Serikali inapowekeza katika Afya ya Mama na Mtoto ndiyo moja ya ishara za uchumi

kinara wa nchi. Aliendelea kusema afya na maendeleo ni mambo pacha. Tunahitaji kuwa na nguvu ya fedha, utashi wa Kisiasa na *Service delivery commitment* ili kukuza afya ya mama na mtoto.

**MHE. NAMELOK E.M. SOKOINE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto nyingi zilizopo katika Wizara hii bado kuna mafanikio mengi na ifikapo 2025 Viwanda vingi vitakuwa vimefufuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Wizara ifanyie haraka ufufuaji wa Viwanda vya *General Tyre,* Arusha Kiwanda hiki kilikuwa moja ya Kiwanda chenye kuzalisha matairi bora Afrika Mashariki. Kiwanda cha *Philips Arusha*, *Tanganyika Parkers* mjini Arusha na ukichukulia Mkoa wa Arusha kuna wafugaji wengi, hivyo wananchi wangepata ajira na kuweza kusindika nyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliuza Viwanda vya *NMC,* lakini cha Mjini Arusha kilikodishwa kwa Kampuni ya Monabai na Mzawa (Mtanzania). Jambo la kushangaza, Wizara haijampa Mkataba wa muda mrefu wala hawajamuuzia, wakati Mtanzania huyo amekopa pesa nyingi benki. Je, Serikali ina mpango gani wa kumuuzia au kumkodisha kwa mkataba wa muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaguzi wa magari nje ya nchi, kufanya ukaguzi wa magari nje ya nchi tunatozwa 450$, lakini fedha halali ni 150$, je, Serikali inasemaje juu ya hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* inafanya kazi nzuri sana kuwafundisha wajasiriamali wadogowadogo. Wizara iwezeshe *SIDO* fedha za kutosha wafungue matawi zaidi na kupanua wigo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Hotuba ya Waziri inatia moyo sana, nawaombea mafanikio katika utekelezaji wa mipango yao hii, lakini ninayo yafuatayo:-

Je, Serikali inayo dhamira ya kweli ya kuinua viwanda na biashara? Kama ndiyo, kwa nini fedha kidogo zilizoidhinishwa hazijatoka ni 30% tu? Naomba fedha za *Logistic Centre* zitolewe ili tupate manufaa yaliyotarajiwa. Fedha za *SIDO* na hasa *NEDF* ziongezwe ili wajasiriamali waweze kupata mikopo, lakini pia ni wakati sasa *SIDO* iwe Wilayani waliko watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Ngaka; kwa nini mradi huu ulianza bila kutatua kero za fidia kwa wananchi? Sasa hivi Serikali imeahidi ilipe fidia hii sasa mpaka ifikapo 15/6/2013. Naomba ahadi itekelezwe kuepuka vurugu kwa mradi na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika taarifa yake (*press release ya Tancoal* ya kwanza kabisa waliahidi kujenga Chuo cha Ufundi cha Ngaka. Mpango huu baada ya kubadilisha uongozi *Intraenergy* hauonekani ni lini kitajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi kwa Waziri kwa kuunda Tume ya pamoja ya kushughulikia *power station,* je, mazungumzo haya yatamalizika lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwa umahiri huo huo unaweza kuwakutanisha *REA, Tancoal, NDC* na *TANESCO,* kuona uwezekano wa kujenga mtambo mdogo wa MW 5-10 ili kufufua umeme kwa ajili ya wananchi wa Ntunduraro, Ruanda, Vijiji vya kati ya Litumba Ndyosi, Kinduila Juu na Chini mpaka Matiri. Mpango huu ni wa haraka zaidi na una matokeo ya haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwa umahiri huo huo hatuwezi kutafuta fedha za ndani kujenga huo mtambo wa umeme (*220MW*) ili kupunguza gharama na kuihusisha *TANESCO* zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mazingira; magari ya *Tancoal* yamesababisha vumbi kwa wananchi. Hivyo, barabara ya Kitai-Ruanda-Lituhi iwekwe lami kwa kushirikiana na wawekezaji, inawezekana la sivyo, mradi huu unaweza kufungwa kwa sababu ya mazingira.

**MHE. ALI KHAMISI SEIF:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi zinazohesabiwa kupata maendeleo ya viwanda zimeanza kwa kuwa na Viwanda vidogovidogo. Nchi ya India pamoja na kuwa na Viwanda vikubwa pia maendeleo yao yanategemea Viwanda vidogovidogo. Hapa nchini kazi hiyo ya kuvisaidia huvilea Viwanda vidogovidogo inafanywa na *SIDO*.

Leo uwezo wa *SIDO,* kifedha ni mdogo mno ukilinganisha na majukumu yake. Katika hali hiyo ni dhahiri Serikali bado haijakuwa makini kuwawezesha *SIDO* ili na wao *SIDO* waweze kuwasaidia wajasiriamali kuwa na Viwanda vidogo ili waweze kuongeza thamani bidhaa zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaotegemea zao la korosho kama zao la uchumi, mapato yao hayalingani sana na kazi inayotokana na kilimo hicho. Hii inasababishwa na bei isiyoaminika ya korosho na kukosa Viwanda vilivyokuwa vikitumika Kubangua Korosho hasa huko Kusini mwa nchi yetu, Viwanda hivyo vilibinafsishwa na mpaka leo havifanyi kazi. Serikali ina mpango gani wa kuwataka hao wenye Viwanda hivyo wanavifanyia matengenezo ili vifanye kazi iliyokusudiwa, kama si hivyo Serikali inahamasisha vipi ili Viwanda vipya vijengwe vya kuongeza thamani zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya ongezeko la Viwanda na uzalishaji wa bidhaa katika Viwanda hivyo, bado bidhaa zetu ni ghali ukilinganisha na bidhaa kama hizo zinazotoka nje, mfano, saruji ya hapa nchini ni ghali zaidi ukilinganisha na saruji kutoka nje. Hii hali itaendelea mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili pamba yetu ipate bei nzuri inabidi pamba hiyo iongezee thamani hapa nchini, lakini pia pamba hii ilitumika hapa nchini kwa kiwango kikubwa kwa kutengenezea nguo, lile suala la kutegemea pamba yetu kuuzwa nchi za nje utapungua. Sasa Serikali imejipanga vipi kuwashawishi wawekezaji wa Viwanda vya nguo hapa

nchini ili baada ya kuagiza nguo iwe sisi tunasafirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nampongeza sana Dkt. Kigoda na Naibu Waziri wake pia watendaji wote wa Wizara kwa kukabiliana na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda kupata maelezo ya Wizara kupitia bodi ya leseni ya maghala kwenye mpango wa stakabadhi ghalani kuwa inawasaidiaje Vyama vya Msingi vya Tandahimba na Newala ambavyo vimeibiwa korosho zao karibu au zaidi ya bilioni mbili na wenye Viwanda vya Newala I – *Agrofocus,* lakini Bodi ya Leseni za maghala iko kimya licha ya kufikishiwa kadhia hii.

**MHE. ABASI ZUBERI MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuwapongeza, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Wafanyakazi wote wa Wizara, kwa kazi nzuri. Nina swali moja tu; ni lini Wananchi wa Shimo la Udongo katika Kata ya Kurasini, Mradi wa *EPZ Tanzania China Logistic Centre* wataanza kulipwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha

**MHE. ENG ATHUMAN R. MFUTAKAMBA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini mkakati wa Wizara kufufua Kiwanda cha Nyuzi Tabora – *TABORATEX* kwani hakifanyi kazi tangu kubinafsishwa takribani miaka kumi sasa? Vijana Igalula wako tayari kuajiriwa katika Kiwanda hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazungumzo na mwekezaji mwingine kutoka Dubai na Pakistani yuko tayari kujiunga na mwekezaji huyu kama Wizara itahamasisha wote wawili kuendeleza mazungumzo. Mbunge atatoa ushirikiano kwani tayari huyu mwekezaji mwenza amekwisha kukikagua hicho Kiwanda japokuwa baadhi ya mashine zimeng’olewa na kuhamishwa!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tabora na hasa Igalula, tunafuga nyuki na asali ya ubora wa juu. Wizara inawasaidiaje wafugaji hawa wa nyuki kupata vifaa na kiwanda cha kuchuja asali na nta na kuuza soko la nje na ndani kwa bei ya ushindani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Benki Kuu ina jukumu la kuimarisha thamani ya fedha yetu, kudhibiti mfumko wa bei na pia kukuza uchumi mpana *(Macro-economics).* Amerika, Japani, Korea ya Kusini na Benki Kuu zao zimesaidia sana viwanda kukua. Je, *BoT* imesaidiaje Wizara hii kukuza viwanda Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, dola 480 milion kila mwaka zinatokana na Tumbaku Mkoa wa Tabora. Je, Wizara imehamasisha wawekezaji wangapi mpaka sasa kujenga Kiwanda cha Tumbaku Tabora ili ajira na thamani ya zao kuongezeka Tabora?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maembe ya kisasa yanastawi Tabora, Wizara ihamasishe tupate Kiwanda cha Matunda Tabora na hususan Igalula.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za wenzetu zilizoendelea; kwa mfano, Korea, Japani na kadhalika, zinategemea viwanda. Cha kushangaza, Tanzania viwanda vingi vimekufa na viwanda vilivyobinafsishwa havifanyi kazi wala havitoi ajira. Vilevile viwanda hivi vilivyobinafsishwa vingekuwa vinafanya kazi, tungepunguza tatizo la ajira ambalo ni tatizo sugu kwa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mpango gani wa kuvikagua Viwanda vyote vilivyobinafsishwa kwa wawekezaji? Kama wawekezaji hawa wameshindwa kuviendeleza viwanda hivi wanyang'anywe na Serikali iwakabidhi wawekezaji wengine ambao wana uhakika wa kuviendeleza.

Je, hawa wawekezaji waliopewa viwanda hivi

wakashindwa kuviendeleza na wakafanya uharibifu katika viwanda hivi (kuvitelekeza); na Wananchi ambao siyo waadilifu wakang'oa vyuma hivyo na kuamua kwenda kuuza vyuma chakavu; Serikali inawachukulia hatua gani za kisheria wawekezaji hawa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya wakulima wa matunda wamekuwa hawana soko la uhakika, vilevile msimu wa matunda, matunda haya yamekuwa yakiharibika mashambani. Je, ni lini Serikali itashirikiana na Shirika laViwanda Vidogo Vidogo *(SIDO)* na kuwezesha *SIDO* kujenga viwanda vidogo vidogo vya usindikaji wa matunda katika Mikoa ambayo inazalisha matunda kwa wingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajasiriamali wadogo wadogo (viwanda vidogo vidogo), wamekuwa wakihangaika sana kutafuta soko la bidhaa ambazo wanazalisha (soko la nje na soko la ndani).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na Wachina wengi ambao wanauza bidhaa ndogo ndogo Kariakoo; kwa mfano, maua na kadhalika na kusababisha hawa wajasiriamali wetu wadogo wadogo kukosa soko na hata ukiangalia hizo bidhaa zao wanazouza siyo madhubuti (feki). Je, Mheshimiwa Waziri haoni sasa kuna umuhimu wa kudhibiti hizi bidhaa ndogo ndogo ambazo zinaingizwa na Wachina ambazo siyo madhubuti ili wajasiriamali wa viwanda vidogo vidogo wapate soko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Wamachinga wamekuwa wakipata tabu, kwani hawapo Dar es Salaam peke yake hata nchi za wenzetu pia wapo. Askari wa Jiji wanawapiga Wamachinga hawa, kuwanyang'anya vitu vyao, kuwazidishia umaskini na wanakosa raha na amani. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwatafutia soko la uhakika Wamachinga hawa ili waepuke adha hii wanayoipata?

**MHE. BETTY E. MACHANGU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara, ilipaswa iwe na mjadala wa siku mbili na siyo siku moja. Hii ni Wizara muhimu, yenye kubeba uchumi wa nchi hii kupitia viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yaliyotamkwa na Mheshimiwa Waziri yatatekelezeka, hakika tutapanua na kuongeza Pato la Taifa na la Mtanzania. Nashauri Serikali ianzishe viwanda vya *lime* ili iuzwe katika migodi yote nchini badala ya kuacha migodi iagize *limestone* nje ya nchi. Ipo *limestone* nyingi Makanya, Same, Singida na maeneo mengi ya Tabora. Serikali iungane na Sekta Binafsi *(PPP)* ili maeneo hayo yaanzishe viwanda vya *limestone*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wawekezaji walionunua viwanda vya zamani na hawajaviendeleza, wanyang'anywe wapewe wanaoweza kuviendesha. Tanzania tunahitaji ajira. Uchumi wa nchi utaendelezwa na Sekta Binafsi. Waliouza mashine wadaiwe walipe. Mfano, Kiwanda cha Magunia Mkoani Kilimanjaro, leo hii ni *go-down*. Wizara ya Viwanda ifanye makubaliano na *Consolidated Holdings* iliyo-*coordinate* uuzwaji wa viwanda. Serikali ifute hati za viwanda vilivyouzwa ambavyo haviendelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja kubwa sana wapelekwe Waambata na Wakurugenzi wa Vituo vya Biashara katika Nchi kama China, Japani na kadhalika. Kamati ya Mambo ya Nje imelisema hili kwa miaka zaidi ya miwili. Diplomasia ya uchumi itafanikiwa waambata hao wakiwepo katika Balozi zetu muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SIDO* ni ya msaada sana kwa viwanda vyetu vidogo vidogo, hakuna haja kuagiza mashine nje ya nchi. *SIDO* wana utaalamu wa kutosha, wawezeshe viwanda vya kuongeza thamani katika mazao katika Kanda zetu Nchini; mfano, Rukwa - mahindi, Rukwa - mahindi, Ruvuma - mahindi, Kigoma - mahindi, Tanga - matunda, Kilimanjaro - tangawizi na ndizi, watengeneze wao mashine. Ajira zitapatikana, Pato la Taifa litapatikana na pato la Mwananchi litapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Afrika Mashariki linahitaji bidhaa hizi zilizosindikwa mfano unga, mafuta ya kula, *wine, tomato source, juice* na kadhalika. Serikali isaidie viwanda hivi vianzishwe na Sekta Binafsi katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ipange na Wizara ya Fedha, Serikali ilinde bidhaa za ndani na hivyo kuleta maendeleo kwa viwanda vilivyoko na vitakavyoanzishwa. Mali na bidhaa zinazotengenezwa na viwanda vyetu, bidhaa kama hizo zisiagizwe kutoka nje *unless* kama uzalishaji hautoshi. Mfano, Kiwanda cha Kibo Match Moshi, Serikali inakiacha kife kwa sababu ya madeni. Kiwanda cha kutengeneza na kusindika Kahawa Moshi, nacho kinaelekea kufilisika kwa sababu ya deni la *TRA/NSSF*, wakati Serikali inashuhudia mitambo chakavu ya miaka kabla ya Uhuru ikiwa ndiyo inatumika. Serikali inafanya nini kukinusuru kiwanda hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha Ngozi Mkoani Kilimanjaro (Himo), kinafanya *semi-processing* Tanzania na *final processing* Nairobi. Ajira zinakosekana kwa upungufu kama huu. Serikali isaidie kiwanda hiki ili kilete ajira kwa Watanzania na Pato la Taifa kutohaha na ngozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TBS* inaweza kufanya vizuri inatakiwa iungwe mkono. Kubadilisha Wakurugenzi kila leo, tena bila uwazi wa kutosha, unaleta hisia ya rushwa au *undugunization*. Wakurugenzi waajiriwe kutokana na *qualification, experience* na uwezo wao wa kufanya kazi. Aajiriwe Mkurugenzi aliye *qualified* katika fani ya *TBS (quality et cetera).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakaguzi wa bidhaa nje ya nchi, Kampuni zipewe *tender* kwa uwazi. Maslahi binafsi kipindi hiki yataua Taifa hili, *we have had enough*; ni wakati Utaifa ututawale zaidi. Yameandikwa mengi katika magazeti kuhusu Uongozi wa Wizara kutokutaka uwazi kuhusu *tender* za nje na ajira za ngazi ya juu katika *TBS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja.

**MHE. REBECCA M. MNGODO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Awamu ya Kwanza ya Uongozi wa Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu J. K. Nyerere hapa Tanzania, kulikuwepo na

kiwanda cha magari maarufu kama "Nyumbu". Uzalishaji wa magari hayo aina ya Nyumbu ungekuwa bado unaendelea, Wananchi wengi waishio vijijini na hasa wakulima wakubwa wa pamba, tumbaku, mahindi, ngano na kadhalika, wangepata unafuu kwa kuuziwa magari hayo kwa bei nafuu na hivyo kupata urahisi wa kusafirisha mazao yao hadi kwenye soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tupo katika *era* ya sayansi na teknolojia, nashauri Kiwanda kile kifufuliwe ili kuharakisha Maendeleo ya Nchi yetu kwa kuwa na magari yanayotengenezwa hapa hapa nchini. Yanayoweza kuwarahisisishia wakulima wetu katika maeneo mengi yenye kilimo kikubwa hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. JOHN PAUL LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na kuipongeza Serikali kwa kuhamasisha ujenzi wa viwanda vingi vya saruji hivi karibuni.

Viwanda hivi vinaonekana kujengwa zaidi Ukanda wa Pwani kuanzia Mtwara, Lindi, Pwani na Tanga na hivyo kuyaachia maeneo mengine husussan Kanda ya Kati na Magharibi bila Kiwanda cha kutegemea na hivyo bei ya saruji kuendelea kuwa juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa miaka mingi sasa nimekuwa nikiisihi Serikali ione uwezekano wa kuwashawishi wawekezaji wajenge Kiwanda cha Saruji eneo la Itigi, Manyoni, Mkoa wa Singida, kutokana na malighafi nyingi ya *gypsum* au *jas,* lakini ahadi zimechukua muda mrefu bila mafanikio. Naiomba Serikali irejee ombi hili kwa kuwashawishi wawekezaji kuwekeza eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kama haiwezekani kujenga Kiwanda cha Saruji, basi walau Kiwanda cha kuzalisha *Plastor of Pain (PoP)* kutokana na malighafi hiyo ya *gypsum*.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE**: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja hii na kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote, kwa Hotuba nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ilitenga eneo pale Makambako la kujenga Soko la Kimaitafa *to 1997,* hadi leo imefika miaka 16 hawajalipwa fidia pamoja na ahadi ya kufanya hivyo. Je, hilo eneo la ekari 300 utafanyika uthamini upya? Ni lini basi Wananchi wale watalipwa; na ni lini soko hilo litajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Njombe wanalima viazi mviringo, lakini soko lake ni tete na hasa wanunuzi kulazimisha Wananchi wajaze lumbesa. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuzuia tabia hii ya kutofuata sheria ya ujazo wa kilogramu 100 kwa gunia?

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali kupitia Wizara hii ya Uchumi Viwanda na Biashara katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko makubwa na ya muda mrefu ya wananchi katika Mikoa mingi ya nchi yetu kuhusu maeneo yaliyochukuliwa na Serikali kupisha mpango wa *EPZA.* Madai ya wananchi ni kushindwa kulipwa fedha za maeneo yao huku wakiendelea kuzuiliwa kuyatumia maeneo yao katika shughuli zao za kimaisha ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kuona hali ya fedha ya kuwalipa wananchi hawa. Naishauri Serikali iwaruhusu wananchi hawa kuyatumia maeneo haya mpaka hapo Serikali iwaruhusu wananchi hawa kuyatumia maeneo hayo mpaka hapo Serikali itakapokuwa tayari kuwalipa kwa tathmini mpya itakayofanyika muda huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua hatua zinazochukuliwa juu ya ufufuaji wa Kiwanda cha Urafiki kwani kwa muda mrefu imekuwa uzalishaji wa Kiwanda hiki

haueleweki. Je, ni hatua zipi zinachukuliwa kukiendeleza Kiwanda hiki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka pia kujua ni hatua gani zinaendelea kuchukuliwa katika kukifufua Kiwanda cha *General Tyre* Arusha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali itupatie majibu kuhusiana na mradi mkubwa wa Kurasini *Logistic Centre*. Ni kwanini umekwama kuanza hadi sasa wakati bajeti iliopita ziliidhinishwa 60 bilioni kwa ajili ya mradi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na faida nyingi zinazotarajiwa kupitia mradi huo utakapokamilika, lakini faida ya ajira za kuanzia 25,000, ambazo zinategemewa kuongezeka kadri muda utakavyokwenda: Je, Serikali haioni kuchelewa kuanza kwa mradi huu, kuna hatari ya kupoteza fursa hii adimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna taarifa kwamba mradi huu unamezewa mate na nchi nyingi za kiafrika. Hivyo, naiomba Serikali kwa umakini kabisa itueleze hatua za haraka iliyopanga kuzichukua kukamilisha uanzishaji wa mradi huu muhimu kwa manufaa ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali itueleze, ni mafanikio gani makubwa yaliyopatikana toka kuanza kwa utaratibu mpya wa ukaguzi wa mizigo nje ya nchi *(PVOC):* Je, malengo tuliyokusudia ya kupunguza uingizaji bidhaa hafifu umefanikiwa?

**MHE. NIMROD E. MKONO**: Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kupoteza muda, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia na kutoa maoni yangu kufuatia hotuba ya Bajeti ya Wizara hii kama ilivyowasilishwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, nianze kwa kusema kuwa sote tunajua kuwa hivi sasa Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi iko katika harakati kubwa za kukuza

uchumi wa Taifa letu ili kuupiga vita umaskini. Hili ndiyo lengo kuu lililoko kwenye Ilani ya Chama chetu. Kati ya juhudi zinazofanyika katika kutekeleza ilani hiyo ya kukuza uchumi ni pamoja na kuvutia wawekezaji wa nje na wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa minajili hiyo ya kuvutia wawekezaji, Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko inayo kazi kubwa sana ya kufanikisha lengo hili kuu. Kama Wizara hii ikilala, basi maana yake ni kuwa uwekezaji utadorora. Viwanda vitadorora na kufa. Matokeo yake kudorora huko ni Watanzania kupoteza ajira kwa kukosa kazi. Wakulima na wafanyabiashara kukosa masoko ya kuuzia bidhaa zao, wawekezaji kukimbia na mbaya zaidi Serikali kukosa mapato kupitia kodi na matokeo yake uchumi kuanguka na kufa kabisa. Haya yakitokea, wananchi watashindwa kupiga vita umasikini na kazi yote tunayofanya itakuwa kazi bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema, Wizara hii ya viwanda biashara na masoko ina kazi kubwa na nafasi ya kipekee ya kuvutia wawekezaji na kukuza uchumi wetu kutokana na majukumu ya Wizara. Hakuna mwekezaji ambaye atakuja kuwekeza sehemu ambayo mathalan anajua kuwa uwekezaji wake hautalindwa au hakuna ushindani halali wa kibiashara. Mwekezaji hawezi kuja kuwekeza kwenye soko ambalo limejaa bidhaa feki, soko lililojaa bidhaa bandia na hafifu kama soko letu lilivyo kwa sasa. Kwa mantiki hiyo basi, mchango wangu wa leo utajikita zaidi katika changamoto na matatizo sugu yanayoiandama Ofisi ya Wakala wa Usajili na Leseni za Biashara *(BRELA)* na hasa Kitengo cha Msajili wa Hataza *'patents'* na alama za biashara *(trade and service marks)* Ofisi ya *BRELA* iko chini ya Wizara hii na kitengo ninachozungumzia leo kinajulikana zaidi kwa Kiingereza kama *the Office of the Registrar of Patents, Trade and Services Marks.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *BRELA* ilianzishwa tarehe 28 Oktoba, 1999 chini ya Sheria ya *Executive agencies Act, no* 30 ya mwaka 1997. Ofisi ilianzishwa kufuatia Tangazo la Serikali *GN 8 October, 1999*, lengo la kuanzisha ofisi hii ilikuwa ni kupunguza urasimu usiokuwa na maana wa kiserikali. Kitengo

hiki cha masijili wa alama za Biashara na Hataza *(Patents)* kiko chini ya *BRELA*, lakini naamini ndiyo chenye matatizo makubwa sana kuliko kitengo kingine chochote. Matatizo yanayosababishwa na kitengo hiki, yanachangia kwa kiasi kikubwa sana kukatisha tamaa wawekezaji kuja kuwekeza na kufanya biashara hapa nchini. Yamkini ili mtu afanye biashara, anatakiwa awe au abuni alama ya biashara itakayomsaidia kutofautisha bidhaa zake na bidhaa za wafanyabiashara wengine. Alama za biashara ni kama chombo cha habari ambacho muuzaji au mzalishaji anakitumia kuwasiliana na wateja sokoni. Kutangaza na kuuzia bidhaa au huduma yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, basi alama za biashara ni kitu muhimu na chenye thamani kubwa sana sokoni. Kwa mfano, *AZAM PEPSI* au *COCA-COLA* ni alama za biashara zenye thamani kubwa ya mabilioni ya Shilingi na vinatumika kwa ajili ya vinywaji baridi na bidhaa nyingine. Alama hizi za biashara zinasajiliwa na kulindwa na sheria ya *(Trade and Service Marks Act 1986 CAP 326 REF 2002).* Sababu kubwa ya kusajili na kulinda alama hizi ni kuwa kama kila mtu angeruhusiwa kwa mfano kutengeneza pombe yake ya kienyeji mfano ulanzi halafu akaiita *PEPSI* au *COCA-COLA* maana yake ni kuwa biashara ya Makampuni haya makubwa ingekuwa imeshaharibika kabisa siku nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya kazi zinazofanywa na Ofisi ya *BRELA* ni kusajili hati za hataza na alama za biashara. Tatizo sugu linayoikabili ofisi hii ni kuwa shughuli hii ya usajili wa alama za biashara inachukua muda mrefu mno! Kazi ambayo nchi za wenzetu inachukua chini ya miezi mitatu hapa kwetu inachukua mwaka zaidi ya mmoja na wakati mwingine hata miaka zaidi ya mitano! Ni kitu cha kawaida kabisa kukuta ombi la kusajili alama za biashara lililopelekwa mwaka mmoja hadi mitatu iliyopita halijafanyiwa kazi yoyote na ofisi hii kabisa! Yaani lipo lipo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine hata ukifuatilia unaambiwa faili halionekani, yaani mtu amepeleka ombi la kusajili alama yake ya biashara amelipa ada

ambayo ni Sh. 50,000/= lakini kwa zaidi ya mwaka mmoja hadi mitatu hajajibiwa kama ombi lake limekubaliwa au la! Haiwezekani mtu akae ofisini akalie ombi la mtu kwa zaidi ya mwaka mmoja bila majibu na hapo hapo tuseme tunavutia wawekezaji? Tunavutia wawekezaji gani? Kwa kupiga ramli! Ushahidi wa ucheleweshaji huu uliopita kipimo upo na kama Waziri akitaka nitampatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo tisa, kumi ni pale ambapo unakuta ombi hilo limeshakubaliwa na limeshatangazwa katika gazeti kwa mujibu wa sheria, ada ya usajili ambayo ni Sh. 60,000/= imeshalipwa, lakini ofisi hii inashindwa kutoa cheti cha usajili kwa zaidi ya miaka hata miwili hadi zaidi. Kama taratibu za usajili zimekamilika, kikawaida kutoa cheti, haiwezi kuchukua zaidi ya siku mbili au tatu, lakini katika ofisi hii inachukua miaka miwili hadi mitatu na wakati mwingine zaidi ya miaka mitano. Narudia tena, ushahidi wa ucheleweshwaji huu wa kipuuzi upo mwingi na kama Waziri anataka nitampatia!

Mheshimiwa Mwenyekiti, ucheleweshwaji wa namna hii ni uzembe na matumizi mabaya ya Ofisi, haukubaliki hata kidogo, hata mtu atoe visingizio gani! Huu ni uzembe wa hali ya juu na hili halikubaliki hata kidogo! Nachelea kusema kuwa ucheleweshaji wa namna hii siyo kuvutia wawekezaji ila ni kufukuza wawekezaji! Mwekezaji hawezi kuja kufanya biashara na ofisi kama hizi. Bila alama yake ya biashara kusajiliwa kwa wakati, hawezi kuwa na uhakika kama sheria itamlinda huko sokoni!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbaya zaidi, ofisi hii haina kawaida ya kujibu hata barua za wateja wanaofuatilia maombi yao ambayo yamekwama katika ofisi hii miaka nenda miaka rudi. Ukiwa na bahati, sana sana utapewa jibu la mdomo kuwa faili halionekani. Faili litaachaje kuonekana! Kama ofisi hii inapoteza mafaili kiasi hiki, inasajili nini? Hii haikubaliki hata kidogo! Wengine hawawezi wakawa wanajenga uchumi kwa kuvutia wawekezaji huku wengine wanaubomoa uchumi huo kwa kukatisha tamaa wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utafiti wangu usio rasmi, nimegundua sababu kubwa zinazosababisha ucheleweshaji huu katika ofisi hii kuwa ni hizi zifuatazo:-

Uongozi mbovu na usiokuwa na maono. Kwa kiongozi yoyote mchapa kazi, *BRELA* ni kisima cha kutengeneza hela na kuingizia Serikali mapato. Kama maombi yote yanayopelekwa *BRELA* kusajiliwa yangekuwa yanafanyiwa kazi, kwa kila hatua na kwa wakati, mapato yake yangeongezeka sana. Vile vile kama Makampuni yote mfu yangefutwa au yanayoshindwa ku-*file returns* yangefuatiliwa na kupigwa faini kama sheria inavyoelekeza, *BRELA* ingetengeneza mabilioni!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalan niongelee kero ya ucheleweshaji wa utoaji matangazo wa maombi ya usajili wa alama za biashara. Hili nalo ni tatizo lingine sugu tena la kujitakia kwa mujibu wa sheria. Msajili wa Hataza na alama za biashara anatakiwa achapishe jarida ambamo atakuwa akitangaza maombi ya usajili yaliyoletwa kwake kwa usajili. Lengo la kutangaza ni kutoa fursa kwa watu wengine kupinga au kutoa maoni yao kuhusu ombi lililotangazwa. Jarida linalochapishwa na ofisi hii linajulikana kama *"The Patents Trade and Service Marks Journal"* na linatakiwa liwe linachapishwa mara moja kwa mwezi. Kila tangazo moja linalotolewa humu, mwombaji lazima alipie Sh. 15,000/= lakini cha ajabu ni kuwa kuna ucheleweshaji mkubwa wa kutoa hata kijarija hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya mwaka 2,000 maombi yote yalikuwa yanatolewa kwenye gazeti la Serikali. Ili kuharakisha utoaji wa matangazo, Msajili alianza kuchapisha jarida hili baada ya kutungwa kwa sheria ndogo za alama za biashara za mwaka 2000 *(The Trade And Service Marks Regulations 2008 GN 40 of 2008)* kijarida chenyewe ni rahisi mno kukiandaa, unahitaji tu komputa moja na *printer* moja basi. Pamoja na urahisi wa kutengeneza kijarida hiki, cha ajabu ni kuwa hata utoaji wa kijarida hiki nako kuna ucheleweshaji uliopindukia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utashikwa na mshangao ukiambiwa kuwa kuna maombi mengi ya usajili hayajatangazwa kwa miaka zaidi ya miwili hadi mitatu wakati kazi kama hii ingefanyika kirahisi kama kungekuwa na uongozi makini na uwajibikaji. Japo huu ni mwezi wa tano naambiwa kijarida hiki mwaka huu kimetoka mara mbili tu badala ya kutolewa japo mara moja kila mwezi. Kuna nini hasa kinachozuia uchapishaji wa maombi yote yaliyo tayari kwenye hili jarida? Kwa nini wasichapishe *volume* hata tano kwa kila mwezi ili kumaliza msongamano wa haya maombi? Kwa nini wasiajiri mtu mmoja au wawili ambao kazi yao itakuwa ni hii ya kuanda a hiki kijarida tu? Kuna tatizo gani? Naomba Mheshimiwa Waziri afuatilie uzembe huu na atupe majibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani hata kazi rahisi ya kuchapisha jarida lao la matangazo ambalo kila anayetangaza kule analipia Sh. 15,000/= na linauzwa shilingi 5,000/= lishindwe kutoka kila mwezi kama inavyotakiwa. Yamkini wakati *BRELA* kuna *application* zaidi ya 3000 zinasubiri matangazo tangu mwaka 2012. Jarida hili lilitoka mwaka 2012 mwezi Novemba. Mwezi Desemba wa mwaka 2012 halikutoka! Januari mwaka huu halikutoka! Februari likatoka na maombi yaliyotangazwa ni machache ukilinganisha na yanayosubiri kutangazwa! Mwezi wa Machi halikutoka! Nasikia la mwezi Aprili ndiyo limetoka wiki iliyopita na kwa minajili hiyo la mwezi Mei halijatoka na halitatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama siyo uzembe ni nini? Kwani kuna ugumu gani na gharama gani kutoa hicho kijarida kila mwezi? Kwanza kiko *in black* and *white* na hakifanyiwi *binding* yoyote. Ni ku-*print* tu. Lakini utashangaa inamchukua mtu zaidi ya miezi minne kukitoa, wakati kinatakiwa kutoka kila mwezi. Mimi nafikiri dawa ni kubinafsisha tu *BRELA* ili apatikane mtu anayejua maana ya kufanya na kusajili biashara na alama za biashara. Mbona wenzetu Kenya wameweza? Ukiingia kwenye mtandao wao unakuta majarida yao ya kila mwezi na kila mwaka kuanzia Januari mpaka Desemba, yapo mtandaoni katika tovuti yao ya *http://wwe.kipi.go.ke/index.php/past-ip-journals.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wenzetu Wakenya, jarida lao linatolewa kila mwezi na linaingizwa mtandaoni kila mwanzo wa mwezi ukitembelea matandao wa *BRELA* kwenye tovuti yao ya *http://www.brelaz.org/?section =publication &page=journals*, unachokutana nacho ni aibu na kituko! Wame-*post* vijarida 10 tena vya zamani vya mwaka 2010 basi! Hii ni aibu na ni uzembe uliopindukia! Mheshimiwa Waziri tupia macho *BRELA* na peleka vijana wenye bongo zinazochemka na wachapa kazi na sio wazembe na wapiga kelele kwenye vyombo vya habari wakati ni madudu tu yanafanyika pale!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchache wa watumishi ofisi hii ya Msajili wa Hataza na Alama za Biashara ina upungufu mkubwa sana wa wasaidizi wa msajili *(assistant registrars)* Ofisa Masijala, Wachunguzi *(examination officers)* makarani, Makatibu Mahsusi na Watumishi wengine mbalimbali ukilinganisha na maombi yanayopelekwa katika ofisi hii kila mwaka. Mimi nafikiri watumishi wote pale na hasa wanaotakiwa washughulikie maombi ya usajili hawazidi kumi. Ni vigumu kwa idadi hii ndogo ya watumishi kushughulikia maombi yote yanayotolewa kwenye ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wakala wa Usajili na utoaji leseni za biashara ni ofisi inayojitegemea, nashauri waajiri wafanyakazi wa kutosha mara moja. Kwani fedha zote wanazokusanya kama ada na tozo mbalimbali wanapeleka wapi? Gharama ya kupeleka ombi la kusajili alama moja ya biashara ni Sh. 50,000/=, na tangazo lake ni elfu Sh.15,000/= na ya cheti ni Sh. 60,000/=, jumla ni Sh. 125,000/= achilia mbali tozo nyingine ndogo ndogo za ziada! Kwa fedha zote hizi, kwanini hawaajiri watumishi wa kutosha na kumaliza kero hii ya ucheleweshaji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namshauri Waziri afuatilie hili na ahakikishe kuna wafanyakazi wa kutosha pale wenye elimu na ari ya kuchapa kazi na wenye kusimamiwa barabara kufanya kazi siyo kugeuza ofisi ya Serikali kijiwe ili Taifa letu lisonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mishahara midogo na ukosefu wa motisha kwa wafanyakazi ukifika katika ofisi hii utaona mara moja kuwa wafanyakazi walioko pale wamekata tama. Hawana motisha wala ari ya kufanya kazi. Sababu kubwa ni kuwa mishahara na marupurupu yao ni midogo mno! Kwa kuwa Wakala wa Usajili na utoaji leseni za biashara ni ofisi inayojitegemea. Nawashauri waangalie jinsi ya kuwahamasisha wafanyakazi wao. Kwanini wasiwaige wenzao wa *TRA* wakalipa mishahara inayovutia? Kwani mishahara ya hawa watumishi inalipwa na nani? Fedha zote wanazokusanya wanapeleka wapi kama hawawezi kuzitumia ili kuleta tija?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukosefu wa vitendea kazi na uwekaji wa kumbukumbu mbovu, hili nalo ni tatizo lingine sugu. Ofisi hii ina upungufu mkubwa sana wa vitendea kazi na hasa komputa, uwekaji wa kumbukumbu katika ofisi hii bado unategemea makaratasi na mafaili yake yanahifadhiwa vibaya. Mbaya zaidi sehemu mafaili haya yanakohifadhiwa siyo salama na mara nyingi nyaraka muhimu zinapotea. Ni kitu cha kawaida kabisa katika ofisi hii kukuta nyaraka mbalimbali ulizopeleka kusajili maombi yako hazipo na ukiuliza unaambiwa hazionekani, leta nyingine!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nchi za wenzetu zinahifadhi kumbukumbu zao vizuri na hasa kwenye mtandao wa komputa ofisi hii kwao kutumia komputa kuhifadhi kumbukumbu bado ni ndoto. Katika ofisi hii ukitaka kupata taarifa za alama fulani ya biashara iliyosajiliwa pale ni lazima usubiri utafutiwe faili uletewe. Bado haijawezekana kufanya *search* au kutafuta habari za faili fulani kwa kutumia *computer*. Mara nyingi ukitaka taarifa za alama fulani ya biashara unaambiwa faili halionekani! Hii inatokea mara nyingi tu na siyo mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeambiwa na mmoja wa wapiga kura wangu kuwa mwaka 2008 ofisi hii ilijaribu kuanza

utaratibu wa kutumia *computer* kuhifadhi kumbukumbu na kushughulikia maombi ya usajili wa alama za biashara. Naambiwa pia kuwa walijitahidi sana kwani ukipeleka ombi lako, linaingizwa kwenye *computer* na unapatiwa namba ya ombi lako.

Naambiwa pia kuwa hii ilifanikiwa kwa msaada wa *World Intellectual Property Organisation (WIPO)* lakini sasa naambiwa kuwa shughuli hii yote imetumbukia nyongo. Maombi mengi ya usajili yaliyopokelewa tangu mwaka 2008 hayajafanyiwa kazi yoyote kwa sababu eti ule mfumo wao wa *computer* waliouanzisha uime-*crash*, zimegoma, zimesinzia, zimeharibika, sijui zimetafunwa na kirusi gani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yaani sisi badala ya kutumia *computer* kuturahisishia kazi, sasa zinafanya kazi zisiende kabisa. Namwomba Mheshimiwa Waziri afuatilie hili na alishughulikie mara moja. Hatuwezi kuvutia wawekezaji kwa kuwaambia kuwa oh, samahani mzee, maombi yenu ya kusajili alama za biashara mliyoleta tangu mwaka 2012 hayawezi shughulikiwa kwa sababu *computer* zetu zimeugua kifafa! Huku ni kufanya mchezo na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukosefu wa mafunzo ya mara kwa mara kwa wafanyakazi na usimamizi wa kutosha wa kazi, pia nadhani kazi haziendi kwenye ofisi ile kwa sababu hakuna utaratibu wa kuhakikisha watumishi pale wanapewa mafunzo ya mara kwa mara ili kwenda na wakati. Pili, nadhani usimamizi wa kazi pale uko legelege. Kwa nini tusiwe tunapeleka watumishi hawa waende kwa wenzetu wakajifunze wao wanafanyaje kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naambiwa kuwa wenzetu pale Kenya wamepiga hatua nzuri sana katika ofisi yao ya usajili wa Hataza na Alama za Biashara. Kila mtumishi pale anajua anachotakiwa kufanya na siyo kuhudhuria ofisini ili

mradi siku iende. Wenzetu mtumishi akifika ofisini anakabidhiwa idadi ya mafaili ya kushughulikia kwa siku hiyo na kama hatayamaliza, basi itamlazimu afanye kazi kwa muda wa ziada na hata siku za wikiendi ili amalize *assignment* yake. Namshauri Mheshimiwa Waziri aliangalie pia hili alifuatilie kwa umakini ili ofisi hii ibadilike. Lazima nasi tubadilikie jamani! Muda wa kufanya kazi kwa mazoea ulishapitwa na wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, mimi naamini kabisa tutaweza kuvutia wawekezaji kama tukimaliza matatizo haya madogo madogo ambayo ni kero kubwa sana. Mara nyingi hivi vitu vidogo vidogo ndivyo vinayokatisha tamaa. Haya mambo ya njoo kesho au keshokutwa hayatatufikisha popote. Huu ni muda wa kubadilika na ningeshauri Waziri afuatilie kitengo hiki. Mwekezaji anachotaka ni vitendo na siyo ahadi au maneno. Anataka kujua muda na ratiba ambao ombi lake litashughulikiwa na kukamilika na kifanyike kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashindwa kuelewa, kwa nini *BRELA* wanasuasua katika huduma zao? Cha kushangaza, badala ya kuboresha kwanza huduma zao ili watu wapate *value for money*, wanakuja na hekaya za abunuasi za kuongeza ada za usajili, tena wanataka baadhi zilipwe kwa dola za Marekani badala ya fedha za kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kifupi ni kuwa, uzembe wa *BRELA* umepitiliza na unakifu. Mfano tarehe 4 Novemba, mwaka 2009 walizindua kitu wanaita Mkataba wa Huduma kwa Wateja, yaani *Client Service Charter* na ukiangalia ukurasa wa tisa wanaonyesha muda utakaotumika, mathalan kushughulikia ombi la kusajili alama za biashara. Walidai kuwa watakuwa wanajibu ndani ya wiki mbili na itatangazwa na kusajiliwa ndani ya siku 90. Huu wote ulikuwa ni uongo na sanaa ya hali ya juu, maana hawafuati walichoahidi na hata ukiandika barua ya malalamiko kwa Mtendaji Mkuu wa *BRELA* kuhusu ucheleweshaji unaofanywa hupati jibu!

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi utadaije kuwa utasajili wa alama ya biashara ndani ya siku 90 wakati hata kijarida chako unachotakiwa utoe kila mwezi kinakushinda na inachukua zaidi ya miezi minne kutoa nakala moja? Mimi nashauri Mheshimiwa Waziri aifuatilie na aifumue *BRELA,* atoe mwongozo na kama nilivyosema, kama anahitaji ushahidi wa haya niliyosea nitampatia mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu kule Uingereza maombi kama haya ya kusajili alama ya biashara lazima yashughulikiwe ndani ya kipindi cha wiki mbili. Ndani ya wiki mbili lazima ujue kama ombi lako limekubaliwa au hapana. Ndani ya mwezi mmoja lazima liwe limetangazwa kama mleta maombi amemaliza taratibu zote za ndani ya siku tisini *(90 days)* lazima liwe limesajiliwa na cheti kutolewa. Kwa wenzetu kama ombi lako halijashughulikiwa katika kipindi kilichoonyeshwa kwenye mwongozo, basi ni lazima utapewa maelekezo tena kwa maandishi, ni sababu ipi inachelewesha ombi lako na unatakiwa ufanye nini ili ombi lako lisonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kwani ni nini kinamshinda huyu msajili wetu? Au hata kazi kama hii tunasubiri *management* kutoka nje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo naunga mkono hoja.

**MHE.SALUM KHALFAN BARWANY**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na kugundulika kwa gesi asilia nchini kuwa na changamoto kadha zimekuwa zikijitokeza kuhusiana na manufaa yatokanayo na rasilimali hii. Kuna migogoro kadhaa imejitokeza kwa wananchi kwamba kwa sasa hawaoni faida yoyote kuhusiana na rasilimali hii. Serikali kupitia Mawaziri wake akiwemo Waziri Mkuu wameshawahi kuonyesha dhamira ya kutaka wananchi ambao maeneo yao rasilimali hii inatoka wananufaika kupitia viwanda vitakavyojengwa huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata katika hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa kupitia vyombo vya habari alizungumzia umuhimu wa kuwepo viwanda vitakavyozalisha malighafi zitokanazo na gesi kama mbolea *plastic* na nilu. Naomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake alieleze Bunge na wananchi wa Lindi na Mtwara ni lini ujenzi wa viwanda hivi utaanza na ni maeneo gani yametengwa kwa shughuli za ujenzi wa viwanda hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri imegusa maeneo kadhaa kuhusiana na ukanda wa uwekezaji *(EPZ)* kama Bagamoyo Mkuranga na kadhalika, lakini sijasikia kabisa Mkoa wa Lindi ukiingizwa katika *zone* hiyo. Sababu ni nini? Hakuna maeneo au kuna ukiritimba gani unaosababisha kutotengwa kwa maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la korosho, limekuwa likileta kero na manung'uniko kila mara huku wananchi wakilalamikia bei ndogo ya zao hilo. Aidha, kwa upande wa viwanda vyake, vimebinafsishwa na kwa sasa vimegeuzwa maghala ya kuhifadhia mazao na vitu vingine.

Naomba Mheshimiwa Waziri katika majumuisho yake aeleze kuna mpango mkakati gani wa kuhakikisha zao la korosho lina pata soko la moja kwa moja kutokana na kuuza korosho ghafi na/au zile zilizokuwa *Processed* badala ya kusubiri wanunuzi wa sasa ambao tayari wanaonekana ni tatizo kwa maendeleo ya wakulima wetu?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, orodha yetu imekwisha na jioni hii ya leo Mheshimiwa Mtoa Hoja atakamilisha hoja yake. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni ya leo.

*(Saa 6.57 mchana Bunge liliahirishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, naomba kumshukuru Mungu, kwa kunipa afya hii leo na naomba niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, ambao wameonesha kwamba, wanampenda sana Waziri wangu, lakini hawakipendi Chama cha Mapinduzi. Napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia na kujibu baadhi ya hoja zilizojitokeza katika Hotuba ya Waziri wa Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naunga mkono hoja iliyo mbele yetu kama ilivyowasilishwa na Mheshimiwa Dokta Abdallah A. Kigoda, Waziri wa Viwanda na Biashara, kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali ya CCM kupitia Wizara ya Fedha, kwa kuwa sikivu na kufanya marekebisho ya Bajeti ya Maendeleo, Fungu 44 - Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014. Kwa kuzingatia ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bajeti, pamoja na Kamati ya Kudumu ya Sekta ya Uchumi, Viwanda na Biashara kuhusu mahitaji mapya ya Fungu 44 la Wizara ya Viwanda na Biashara na Masoko, Serikali imeongeza shilingi bilioni 30 kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa *EPZ Development Project, Code Number 4933, Kurasini Logistics Hub,* ambao upo chini ya Kifungu cha Namba 1003 - *Policy and Planning,* kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014. Hivyo, Mradi huu utakuwa na jumla ya shilingi bilioni 31 ikijumuisha shilingi bilioni moja ambazo tayari zimetengwa kwenye Mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa mwaka 2012/2013, Serikali imekuwa sikivu vilevile, imetoa jana shilingi bilioni 25 kwa ajili ya kukamilisha fidia ya Mradi huu wa *EPZ* huko Kurasini. Hii inajumuisha na fedha ambazo zimetengwa kwa mwaka unaokuja, yaani shilingi bilioni 30 pamoja na ile moja, bilioni 31, ukiunganisha na bilioni 25 za mwaka huu ambao unaishia Juni, jumla inakuwa shilingi bilioni 55, ambazo zinatosha kwa awamu hii ya kwanza ya Mradi huu katika

eneo hilo la Shimo la Udongo, lenye hekari 38.12. Kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali na hasa kama nilivyosema kwamba, tunaipongeza sana Kamati ya Bajeti pamoja na Kamati ya Kisekta ya Uchumi, Viwanda na Biashara, kwa kazi nzuri hii ambayo wanafanya kusaidia pale ambapo inabidi isaidiwe. Kipaumbele ambacho kilikuwa mbele yetu hiki cha *EPZ* kusema kweli kama tusingefanya bidii hii kupitia Kamati hizi, ingekuwa ni pengo kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndiyo maana natanguliza kabisa shukurani zangu kwa Kamati hizi mbili ambazo zimefanya kazi nzuri sana kwa Wizara hii ya Viwanda na Biashara kwa wakati kama huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii, kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote, mtuunge mkono kwa kupitisha bajeti hii ili itupe nafasi ya kutekeleza wajibu na majukumu yetu kwa Mwaka wa Fedha wa 2013/2014 kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi, Waziri wangu, Menejimenti ya Wizara, pamoja na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hii na Watumishi wote, tumedhamiria na tunakusudia kufanya kazi hii muhimu ambayo ipo mbele yetu. Wajibu wetu mkubwa tulionao kwa hivi sasa ni kuibadilisha nchi hii kiuchumi ili tufikie nchi yenye kipato cha kati *(Middle Income Country),* ifikapo mwaka 2025 na hii ndiyo dhamira na hii ndiyo kauli ambayo sisi tunafanya nayo kazi kama Wizara, kama Watumishi wote wa Wizara pamoja na Taasisi zake zote kwamba, angalau nchi hii ifikie kwenye hatua ya kuwa nchi ya kipato cha kati ifikapo 2025. Ni kazi kubwa ambayo ipo mbele yetu, nawasihi sana Wabunge wote ambao mko hapa, tushirikiane sisi wote kwa pamoja kutekeleza azma hii ambayo ipo mbele yetu chini ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeamua sasa kuongeza na kuendeleza viwanda vidogo, tunaendeleza viwanda vya kati na vile vikubwa. Hii ni pamoja na kukuza na kuendeleza biashara kubwa na ndogo kwa kupanua wigo wa masoko ya ndani pamoja na yale ya nje kwa bidhaa zilizoongezwa

thamani. Sisi sote tunaelewa kuwa, hakuna nchi iliyoendelea bila viwanda. Sekta ya Viwanda ndiyo Sekta pekee ambayo inaweza kupunguza kama si kuondoa kabisa umaskini uliopo nchini kwa kuongeza ajira kwa vijana wetu na kuongeza kipato chetu. Tutekeleze sasa kwa mafanikio makubwa, yaani *big results, now* kwa kushirikiana pamoja na wawekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuanza kujibu hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge, nakushukuru wewe binafsi tena kwa kunipa nafasi hii. Kutokana na muda, naomba kusema kwamba, hoja zote za Waheshimiwa Wabunge zitajibiwa kwa maandishi na kusambazwa kwa Waheshimiwa Wabunge wote muda siyo mrefu wakati tupo hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huu wa jumla, sasa napenda kufanya majumuisho kwa kutoa maelezo mafupi, yenye ufafanuzi kwa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge, zilizotolewa wakati wakichangia Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, alipokuwa akiwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato ya Wizara yake, pamoja na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, alipokuwa akiwasilisha Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara yake, pamoja na Hotuba ambazo zilishatangulia za baadhi ya Mawaziri ambao Wabunge wamechangia na hoja hizo zinahusiana moja kwa moja na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kwa ruhusa yako nijikite kwenye hoja ambazo zipo *very specific,* ambazo zimechangiwa na Waheshimiwa Wabunge katika kuunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki, alitaka kujua kwa vile *CAMARTEC* imeonesha uwezo wa kutengeneza trekta, sasa ni wakati mwafaka kwa Serikali kuiwezesha iweze kuzalisha matrekta mengi zaidi. Nasi tunasema kwamba, hii ni mojawapo ya Taasisi za Utafiti chini ya Wizara hii ya Viwanda na Biashara. *CAMARTEC* inatoa changamoto nyingi

kubwa katika kuendeleza viwanda kupitia utafiti pamoja na kutoa huduma kwa wadau wa Sekta hii. *CAMARTEC* wanabuni trekta dogo la matumizi mengi ambalo linasaidia sana kwa wakulima wadogo na wale wakulima wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara, imekuwa ikisaidia *CAMARTEC* kupitia fedha za maendeleo ambazo ndizo zilizotumika kutengeneza trekta hilo linalojulikana kama *fast tractor. CAMARTEC* inahitaji jumla ya shilingi bilioni nne kwa kufungua kiwanda cha kutengeneza matrekta. Vilevile Wizara kupitia Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC),* tayari imefanya mpango wa kuipatia *CAMARTEC* eneo kwa ajili ya kujenga kiwanda husika pale *Kilimanjaro Machine Tools.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa bajeti, *CAMARTEC* imeanza mazungumzo na Benki ya Rasilimali Tanzania, yaani *Tanzania Investment Bank (TIB),* ili kuweza kupata mkopo wa shilingi bilioni nne kuiwezesha kushiriki kuanza kuzalisha matrekta. Makubaliano haya ya awali kati ya *CAMARTEC* na *TIB* tayari yamekwishakamilika na upembuzi yakinifu, yaani *feasibility study* imeanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mbunge wa Mufindi Kaskazini, anapenda kujua Kiwanda cha *MPM* Mgololo pamoja na kwamba kinazalisha karatasi, lakini hakina kiwanda cha kutengeneza mifuko. Mifuko mingi inatengenezwa Kenya. Sasa alitaka kujua kwa nini kiwanda hiki cha *MPM* Mgololo hakina uwezo wa kutengeneza mifuko. Kiwanda cha *MPM* Mgololo kisheria hakiruhusiwi kutengeneza mifuko, kwa kuwa watakuwa wanakiuka Shera za nchi. *MPM* Mgololo ndiyo wazalishaji pekee Tanzania wa bidhaa ya karatasi toka malighafi ya miti na hivyo kama wataanza kujikita kwenye biashara ya kutengeneza vifungisho ni dhahiri kwamba, watamiliki soko na kukosekana ushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nchi nzima ina viwanda sasa hivi vipatavyo vinane vikubwa vya kufungashia au vya kifunganishi vya karatasi, ambazo wangeweza

kutengeneza *MPM* Mgololo ambao hawaruhusiwi kisheria. Kwa hiyo, viwanda hivi vinane naona vitakidhi hii shughuli au hii kazi ya kutengeneza mifuko badala yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Ezekiel Maige, Mbunge wa Msalala, pamoja na Wabunge wengine; Mheshimiwa Munde Tambwe - Mbunge wa Viti Maalum Tabora, Mheshimiwa Said Juma Nkumba - Mbunge wa Sikonge na Mheshimiwa Murtaza Mangungu - Mbunge wa Kilwa Kaskazini, wao wanapenda Serikali ije na mkakati wa uhakika wa kufufua viwanda vya kuchakata pamba na mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi nasema, takwimu zilizopo zinaonesha kuwa, vipo viwanda 60 vya kuchakata pamba hapa nchini. Viwanda hivi vipo katika Mikoa inayolima pamba kwa wingi, ambapo Mkoa wa Mwanza kuna viwanda 21, Mkoa wa Shinyanga una viwanda hivi vya pamba 29, Mkoa wa Mara una viwanda vinne, vilevile Kagera kuna viwanda vya pamba, Morogoro, Kilimanjaro, Pwani na Manyara. Mikoa hii ya Kagera, Morogoro, Kilimanjaro, Pwani na Manyara, wana kiwanda kimoja kimoja cha pamba. Viwanda hivi vina uwezo wa kuchakata marobota yapatayo 327,074 ya pamba kwa mwaka wakati uzalishaji ni takribani marobota 228,051 kwa mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi vinamilikiwa na Vyama vya Ushirika chini ya usimamizi wa Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika na kampuni binafsi. Wizara ya Kilimo kupitia Bodi ya Pamba, yaani *TCB,* imeandaa mkakati wa kuendeleza Zao la Pamba, ambapo kilimo cha mkataba kati ya wakulima na wanunuzi wa pamba kinatekelezwa. Kwa upande mwingine, mkakati wa kuendeleza sekta ya nguo na mavazi umeandaliwa na unaendelea kutekelezwa na Wizara ya Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kiwanda cha Mbolea, kama nilivyosema, Wabunge hawa wanataka kujua kuhusu Kiwanda cha Mbolea; mkakati uliopo ni kujenga. Wizara kupitia *NDC,* imeendelea na juhudi za kuanzisha

viwanda vya kemikali na mbolea kwa kutumia gesi asilia huko Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Mjini, anapenda kujua kiwanda cha kusindika tumbaku kitajengwa lini Tabora? Wizara inatekeleza mkakati unganishi wa kuendeleza Sekta ya Viwanda, ambao moja ya vipaumbele ni katika kuongeza thamani mazao ya kilimo, ikiwemo zao hili la tumbaku. Kwa hiyo, azma ya kujenga kiwanda Tabora ipo pale pale na sehemu kubwa ya viwanda hivi ambavyo naviongelea tayari imeshaongelewa na Mheshimiwa Waziri wakati anahitimisha Bajeti yake hii ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Omari Nundu, Mbunge wa Tanga Mjini, anataka kujua kwa nini wakulima wameacha kulima katika maeneo yao ambayo yametengwa kwa ajili ya *EPZ.* Suala hili liangaliwe tena upya ili liweze kutoa nafasi kwa maeneo ambayo yametengwa lakini hakuna kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wananchi waliopo katika maeneo haya yaliyotengwa kwa ajili ya *EPZ,* ambayo taratibu za utoaji ardhi hazijakamilika, Serikali imewaruhusu kuendelea na shughuli za kimaendeleo ambazo siyo za kudumu ili kutowakwamisha katika shughuli zao za kila siku za uzalishaji mali. Kwa hiyo, hivi ninaposema, mamlaka hii ya *EPZ* inatenga maeneo mbalimbali katika nchi nzima, Mikoa yote Tanzania nzima, kule ambako utaratibu huu haujakamilika, haina maana kwamba wale ambao maeneo yao yametwaliwa yakae bure tu. Kwa hiyo, ruhusa inatolewa kwamba, wanaweza kuendelea na shughuli za kilimo mpaka hapo ambapo taratibu zitakamilika za kutwaa maeneo hayo chini ya *EPZ* pamoja *SEZ.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Hezekiah Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa, anataka kujua kiwanda cha kusindika zabibu katika eneo lake kitapatikana lini, kwa sababu Chilonwa kuna zabibu za kutosha. Nimjulishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, utaratibu wa kujenga

kiwanda cha kusindika zabibu katika eneo hilo upo. Nampongeza Mheshimiwa kwa juhudi anazozifanya katika Jimbo lake na maeneo mengine ya Mkoa wa Dodoma kutokana na kujishughulisha na kilimo hiki cha zabibu. Mkoa wa Dodoma na Wilaya zake pamoja na maeneo ya Mvumi na Kongwa ni maarufu sana katika kilimo hiki cha zabibu na kweli haja ipo ya kujenga kiwanda cha kusindika zabibu ili Mkoa wa Dodoma uendelee kuzalisha mvinyo. Kiwanda hiki ambacho kitajengwa eneo la Chilonwa kitasaidia wakulima wa eneo la Kongwa, Mvumi na Chilonwa yenyewe, kwani watapata kiwanda cha kusindika zabibu na hivyo kupata mvinyo kwa wingi. Zabibu zinazalishwa nchini zinaongezwa thamani kwa kubadilisha bidhaa kama mvinyo na hivyo kukuza ajira na kuongeza kipato kwa Wananchi.

Mheshimiwa Albert Ntabaliba, Mbunge wa Manyovu, yeye anataka kujua Soko la Mnanila Kasulu litajengwa lini? Maandalizi ya ujenzi wa soko katika eneo la Mnanila kupitia Mradi wa *District Agriculture Sector Investment Project* (*DASIP),* yamefikia hatua za mwisho. Soko hili ni moja ya masoko saba ya mipakani ambayo yatajengwa kupitia Mradi huu. Maeneo mengine ambayo yanahusika ni Mtukula kule Misenyi, Kabanga kule Ngara, Kwenda kule Karagwe, Mrongo, Remagwe kule Tarime na Busoke kule Kahama. Zabuni za ujenzi wa masoko haya zimetangazwa mwezi Aprili mwaka huu na ujenzi wa masoko hayo unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2013 na kukamilika katika kipindi kisichozidi miezi sita.

Mheshimiwa Dkt. Agustino Mrema, Mbunge wa Vunjo, ameomba kuharakisha ujenzi wa soko la matunda na mbogamboga la Himo na Soko la Nafaka Lokolova. Nataka nilieleze Bunge hili Tukufu kwamba, Tarehe 17 Mei, 2013, keshokutwa, kuna swali hili litajibiwa ndani ya Bunge hili Tukufu, nafikiri sitakuwa natenda haki kujibu sasa hivi. Kwa ufupi ni kwamba, Mkoa wa Kilimanjaro umeingia makubaliano na Benki ya *TIB* kujenga soko la mbogamboga la Himo na soko la nafaka kule Lokolova. Majibu mengine kamili atayapata tarehe 17 Mei, 2013 kipindi ambacho nitakuwa najibu swali la msingi kwa swali lake hili.

Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Magharibi, alisema Wilaya ya Ikungi inazalisha sana miwa na inafaa kwa uzalishaji wa sukari. Wizara iangalie uwezekano wa kupata mashine kwa ajili ya kuanzisha viwanda vidogo vya kuzalisha sukari. Kwa muda mrefu, Shirika la *SIDO* limekuwa na suala la kubuni na kutengeneza mitambo midogo ya kusindika miwa, lakini mpaka sasa halijafanikiwa kutengeneza mashine hizo. *SIDO* itajitahidi kutafuta teknolojia hiyo nje ya nchi ili kuwaunganisha Wananchi wote wakiwemo wale wa Ikungi wanaozalisha miwa waweze kuzalisha kwa teknolojia hiyo na kuweza kuanzisha viwanda vidogo vya kusindika miwa. Hivyo, ni suala la subira, Mheshimiwa Missanga kipindi ambapo teknolijia hii mpya itakuwa imekamilika, jambo hili litawezekana. Tuvute subira ili jambo hili nalo liweze kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja ya Mradi wa *Tanzania – China Logistic Centre* uliidhinishiwa shilingi bilioni 60 kwa mwaka 2012/13, ambazo zilikuwa ni fungu maalum. Wakati napongeza Kamati zile mbili; Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara na Kamati ya Bajeti, kwa kutenga kiasi cha shilingi bilioni 30 mwaka huu ambao tunaombea bajeti. Niseme tu kwamba, mwaka 2012/2013, Serikali imekuwa sikivu imetoa shilingi 25 bilioni katakana na kiasi cha shilingi bilioni 60 kilichokuwa kimeombwa. Fedha hizi zitalipa fidia kwa Wananchi wa Kurasini ambao wataathirika na Mradi wa *Tanzania – China Logistic Centre*. Kwa suala hili, naomba nitoe majibu kwamba, Wizara inaendelea kufuatilia uwekezaji wa ujenzi wa miundombinu katika maeneo ya *EPZ* na ulipwaji wa fidia kama nilivyosema awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwamba, Serikali ihimize uzalishaji wa mbegu za mafuta ya kula nchini na pia iongeze udhibiti wa viwanda vinavyoagiza mafuta nje ya nchi, kusudi badala yake yatumike yanayosafishwa hapa nchini. Wizara ya Viwanda na Biashara, inatambua umuhimu wa kuzalisha mbegu bora ili kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula ndani ya nchi na kupunguza uingizaji wa mafuta kutoka nje. Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, inaendelea na utafiti wa mbegu bora za kukamua

mafuta. Mafuta yanayoagizwa kutoka nje yanatozwa kodi kulingana na *degree of processing*, ambapo mafuta yanayosafishwa hutozwa asilimia 25 na *semi-refined* asilimia kumi, kwa ajili ya kudhibiti uagizaji wa mafuta kutoka nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nihitimishe kwa kuwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge na kuwaomba kuunga mkono hoja hii iliyo mbele yetu na kuipitisha. Lengo likiwa ni kuhakikisha kuwa, matarajio ya Watanzania kwa Sekta hii yanapatikana kwa kupata baraka za Bunge ili kuwezesha utekelezaji wa malengo yanayotekelezeka, ambayo yamesheheni katika bajeti hii. Kuunga kwenu mkono hoja hii ni muhimu sana ili kutoa fursa ya kuelekeza uchumi wetu unaozingatia mahitaji ya nyakati tulizonazo sasa na nyakati zijazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Nakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara. Sasa namwita mtoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kukushukuru wewe. Pili, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote, kwa michango yao, ambayo wameitoa hapa Bungeni leo katika kujadili hoja yetu ya Wizara ya Viwanda na Biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge waliochangia ni 61, kumi wamechangia hapa Bungeni kwa kuzungumza na Wabunge 51 wamechangia kwa maandishi. Napenda kuwahakikishia kwamba, kwa sababu ya muda, tutaandaa majibu haya vizuri na tutayawasilisha kwa Waheshimiwa Wabunge.

Namshukuru sana Naibu Waziri, kwa utangulizi alioutoa na kwa kweli amegusia mambo mengi ya kimsingi, ambayo ni maeneo yaliyoguswa sana na michango ya Waheshimiwa Wabunge katika kujadili bajeti yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi, Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa na Kamati yake yote, kwa msaada mkubwa waliotupa katika kuifanya bajeti yetu kufikia kiwango hiki hapa leo. Tunakiri kwamba, Kamati hii kwetu sisi kama Wizara ndiyo *think tank* yetu. Kwa hiyo, ushauri wanaoutoa na kwa sababu tunafanya kazi kwa karibu, ni ushauri ambao tunaupokea moja kwa moja. Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Highness Kiwia, Waziri Kivuli wa Wizara hii, kwa hoja mbalimbali ambazo amezitoa. Nina hakika kwamba, utoaji wa hoja hizo ni katika kuboresha shughuli nzima zitakazofanywa na Wizara yetu na wala si kutokutilia maanani lugha inayotumika katika kutoa hoja hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wizara ya Viwanda na Biashara, tunachokiangalia hivi sasa ni kuona ni jinsi gani nchi yetu itafufua utaratibu mzima na mchakato mzima wa kujenga viwanda ili kuhudumia Sekta mbalimbali za Uchumi katika Taifa letu. Ndiyo maana tunasema sasa hivi haileti mantiki kuzungumzia kiwanda kimoja kimoja, lazima wote tuangalie *process of industrialization*. Tukifika hapo, tutajikuta lile lengo letu la kuelekea 2025 na kuwa *semi-industrialized country* tunaweza tukalifikia kwa jitihada zetu wote. Sasa hivi tunafuatilia mkakati unganishi wa ujenzi wa viwanda ambao tunauita *Integrated Industrial Development Strategy,* ambao wengi wa Wabunge hapa mnaufahamu. Mkakati ule ukiusoma kwa makini, umegawa Sekta ya Viwanda katika maeneo matatu.

Kwanza, lazima nchi yetu ihangaikie na ishughulikie ujenzi wa viwanda mama na ndiyo maana tunaweka msisitizo mkubwa sasa kwenye miradi ya chuma, makaa ya mawe na hivi sasa tumepata *gas*. Tunaelewa kwamba, hivi ndiyo vitakuwa viwanda vyetu *basic* na viwanda hivi vitatupa hatua ya kuelekea kwenye ujenzi wa viwanda nchini. Vilevile katika mkakati huu, tunaangalia viwanda vya kati, sekta ya nguo, viwanda vya kemikali, lakini pamoja na hayo, tunaangalia viwanda vya usindikaji wa mazao yetu ya kilimo ili kuongeza thamani ya mazao yetu na bidhaa zetu tunazouza katika masoko. Hatimaye kama maelezo mengi

yalivyotoka kwa Waheshimiwa Wabunge, tunaangalia suala zima la uendelezaji wa viwanda vidogo vidogo kupitia Taasisi mbalimbali hususan *SIDO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote tunafahamu, sasa hivi tukiangalia mfumo wa ujenzi wa viwanda katika uchumi wowote na katika nchi yoyote, hata nchi za mashariki ya mbali na nchi zinazoendelea; tunaona moja kwa moja kwamba, uzalishaji mkubwa unafanywa na *small and medium scale enterprises*, ndiyo wanaozalisha kwa wingi ukilinganisha na vile viwanda vikubwa. Sasa ndiyo maana tunasema, katika mkakati huu wa *Integrated Industrial Development Strategy*, hapo ndiyo tunapopaangalia. Tukishafika hapo, masuala ya biashara na masoko yanafuatilia na hatimaye sekta hii sasa kufanya kazi bega kwa bega na Sekta ya Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Hotuba ya Waziri Kivuli na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, wamezungumzia suala zima la ubinafsishaji. Suala la ubinafsishaji kama nilivyosema mwanzo, ni vyema sote tukalielewa vizuri, kwa sababu tunapozungumzia ubinafsishaji ni lazima tuelewe maana yake ni nini. Maana yake kubwa ni kuondoa umiliki wa umma katika viwanda vyetu na kupeleka kwenye sekta binafsi. Njia zinazofanyika ni pamoja na kuuza kiwanda moja kwa moja au kiwanda kile kupewa wafanyakazi na *management* au kununua *share* (Hisa) au kuingia ubia au kukodisha baadhi ya viwanda hivyo.

Kimsingi, baada ya kuleta taratibu za *Tanzania Investment Centre* na taratibu nyingine, maana yake moja kwa moja ni utaratibu wa kukubali kwamba, sasa katika uendeshaji wa viwanda, moja kwa moja tutategemea sekta binafsi na katika ile miradi ambayo ni mikubwa, ndipo tutaingia katika utaratibu wa *Public Private Partnership*. Sisi hili tukilielewa, linatueleza moja kwa moja kwamba, sasa hivi tukizungumzia Sera ya Ubinafsishaji *is outdated,* tunachoangalia ni yale matokeo yake yaliyojitokeza. Inaweza ikatokea hoja kwamba, ubinafsishaji viwanda vingi vimekufa, lakini ni vizuri tukapima kwamba kuanzia miaka hiyo

ya 90 mpaka sasa, tuna viwanda vingapi vipya na vya aina gani? Viwanda vingapi vimeanzishwa kupitia Sekta Binafsi au ushiriki kati ya Serikali na Sekta Binafsi na kadhalika.

Leo nilipozungumzia hotuba yangu, nilielezea kwamba, kwa muda wa miaka sita, *EPZ* na *SEZ* tayari mpaka sasa ina viwanda zaidi ya sabini vipya vinavyofanya kazi. Vilevile kuna viwanda vingine sasa hivi tayari tunataka ku-*employ* katika maeneo haya. Vyote hivi ni viwanda katika nchi hii.

Mheshimiwa Naibu Waziri, amezungumza hapa kwamba, viwanda vinavyochakata pamba hapa Tanzania ni vingi sana. Tunachotaka kusema ni kwamba, tuna haja ya kuangalia ni maeneo gani tuyape umuhimu mkubwa ili kuinua sekta yetu ya viwanda.

Suala la *shareholding* ya Mradi wa Umeme wa Upepo kule Singida, kuna masuala yamejitokeza hapa, lakini nafurahi kwamba, Mheshimiwa Waziri Kivuli amesoma na wale *shareholders.* Nimefuatilia na *BRELA,* sikuona katika Wajumbe wale kwamba, kuna Mbunge au ndugu yake Mbunge au yeyote yule. Sasa kama kuna taarifa nyingine zinaweza kupatikana kutoka *BRELA*, nadhani zitaweza kuthibitisha hilo, lakini mimi kama Waziri, sikuliona katika maelezo haya.

Kiwanda cha *General Tire* tunakipa umuhimu mkubwa, ambacho amekizungumzia Mheshimiwa Kiwia. Hiyo tumekwishasema, kimezungumzwa pia na Mheshimiwa Ntukamazina. Vilevile, hata katika Bajeti ya mwaka ujao, tumekitengea kiwanda hiki karibu shilingi bilioni sita, tunataka kifufuke kwa sababu kinazalisha zao muhimu sana hasa katika sekta ya usafiri.

Mheshimiwa Ntukamazina, ametoa hoja mbalimbali; Wizara ianzishe Viwanda vya Zana za Kilimo na taratibu za kufufua viwanda vingine kama *Mang'ula Complex*; hili tunaendelea nalo sasa hivi na ndiyo maana katika hotuba yangu nimesema, tayari *CHC* imeshaanza kuitisha wamiliki wote wale wenye viwanda ambavyo havifanyi kazi na kati

ya hao, wako *Mang'ula Complex* wameshafika kule, wamepeleka *Business Plan* zao na nina hakika kwa kuendelea hivi, tunaweza tukafikia mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Mheshimiwa Dkt. Augustine Mrema, aliuliza katika mchango wake kwamba, hatukutaja masoko yake mawili yale ya Himo. Sisi tulifikiria yale ni ya Kimataifa siyo ya mipakani. Pale tulikuwa tunazungumzia masoko ya mipakani, lile tumeshali-*categorise* ni soko la kimataifa, kwa hiyo, ndiyo maana hatukulitaja. Kile kiwanda kinachojengwa Himo mjini, tunajua kwamba kuna utaratibu ambao kiwanda kikijengwa, Wizara kwa kushirikiana na *NEMC* lazima itoe kibali; tutafuatilia hili na kuona uhalisi wa kiwanda hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Gaudence Kayombo, amezungumzia suala la Ngaka, ambalo ni muhimu kwa sababu ule ni moja ya Mradi himili katika ujenzi wa uchumi wetu hasa tukizingatia kwamba, kile ni mojawapo ya kiwanda mama. Kama nilivyosema kwenye maelezo yangu asubuhi, tutalifuatilia suala hilo vizuri na tayari kwa bahati nzuri, *NDC* imeshashirikisha Uongozi wa Wilaya, wa Mkoa na hata Mheshimiwa Mbunge, ameonesha moyo mkubwa sana kushiriki katika suala hili.

Tunachotaka ni kwamba, Mradi ule uendelee usiathirike na Wananchi waelewe kwamba ule Mradi ni wao na wao wau-*support* badala ya kuleta matatizo ambayo hayatasumbua eneo la Ngaka peke yake, bali yatasumbua uchumi wetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha, amezungumzia sana masuala ya *SIDO.* Umuhimu wa kutenga fedha za kutosha katika Taasisi hii ili kusaidia wajasiriamali wadogo na wafanyabiashara ndogo ndogo na wale wenye viwanda vidogo. Hili vilevile limezungumziwa tena na Mheshimiwa Deogratias Ntukamazima, Mheshimiwa Namelok E. M. Sokoine, Mheshimiwa Susan Lyimo, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, Mheshimiwa Stephen Wassira, Mheshimiwa Kombo Hamis Kombo, Mheshimiwa Lucy

Owenya na Mheshimiwa Murtaza Mangungu. Hili tunalielewa vizuri na ndiyo maana tumekuwa tunajitahidi sana, pamoja na fedha za ndani tunazozipeleka *SIDO*, tuna utaratibu maalum wa Programu ya *Movie,* ambayo inapata fedha kutoka nje ambazo zinasaidia ku-*supplement* fedha ambazo wanapewa *SIDO* katika kuendeleza sekta hiyo ya viwanda vidogo vidogo na biashara ndogo ndogo.

Mheshimiwa Peter Msigwa, ameniuliza Serikali inaweka mikakati gani kuondoa matatizo ya Machinga. Hoja niliyoitoa asubuhi, ni hoja ambayo mimi kama Waziri niliyepewa dhamana ya kuendesha biashara, biashara ndogo, wajasiriamali, ninaitoa kwa uzoefu kwamba, hawa tunaowaita Wamachinga, wengine wanaitwa wale wanao-*offer door to door services*, hawapo Tanzania peke yake. Wapo katika nchi nyingi tu Duniani, wote Waheshimiwa Wabunge hapa ni mashahidi, ukienda Morocco utawakuta, South Africa utawakuta, London unawakuta, lakini ni watu ambao tuko nao katika maeneo yetu. Sasa bugudha hizi wanazozileta Wamachinga kwa Serikali au kwa Halmashauri na bugudha wanazopata Wamachinga kutoka Halmashauri ni lazima sasa tukae tuziweke sawasawa. *(Makofi)*

Zipo *By Laws* ambazo zinaweza zikafanyiwa kazi, hawa wana Taasisi zao, kama nilivyozitaja mchana, kuna VIBINDO, ASBO, TAMDA, zipo kama sita hivi. Tunaweza tukazungumza tu, tukakuta Wamachinga wanafanya kazi zao, wanaingiza riziki zao na tatizo kubwa katika nchi hii ni ajira na wanaohusika ni vijana. Kwa hiyo, ndiyo maana nasema kwamba, hili ni suala ambalo tunatakiwa tushirikiane kati ya Serikali, Halmashauri za Mji na wao wenyewe Wamachinga ili kuliweka sawa; hiyo ndiyo ilikuwa maana yangu kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Mheshimiwa Shibuda Magalle, aliulizia kwa nini tusiweke kiwanda kikubwa cha nyama kule Shinyanga. *(Makofi)*

Napenda kukuhakikishia Mheshimiwa Shibuda kwamba, tayari *NDC* imeshafanya tafiti na sasa hivi

inaendelea kutafuta wabia na tutaangalia utafiti walioufanya, kama umepitwa na wakati tutawaagiza warudie tena *feasibility study* hiyo, ili tuweze kuanzisha viwanda hivyo muhimu katika maeneo yale. Tuna mifugo mingi nchini, viwanda kama hivi vitasaidia sana katika suala zima la kuongeza mlolongo wa thamani ya fedha.

Mheshimiwa Asaa Othman Hamad, amezungumzia umuhimu wa *Kurasini Logistic Centre,* kwa kweli ile ni muhimu sana. Nami nasema kwamba, kama alivyoeleza Mheshimwa Waziri, sasa hivi tumekwisha kupata bilioni 25 na tunachotaka kufanya mara moja ni kuzitoa fedha hizi pale Kidongo Chekundu, ili tuchukue zile eka 38, kazi ya kuanzisha hii *Logistic Center* ianze. *(Makofi)*

Tunajua kwamba, pale tutaweza kupata ajira, biashara itakua, lakini pana *multiplier effect* kubwa sana katika miradi kama hii na ndiyo maana tunasema, tukishamaliza kukamilisha kulipa fedha zile, tayari mara moja Wachina wanaingia na bilioni 600, tunapata ajira ya watu elfu 25, tutakuwa tumejenga utaratibu mzuri katika uchumi wetu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, hilo tunalifuatilia kwa karibu sana, hili pia limezungumziwa na Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete, Mheshimiwa Khatib Said Haji, Mbunge wa Konde, Mheshimiwa Gaudence Kayombo, Mbunge wa Mbinga Mashariki na Mheshimiwa Haji Khatib Kai, Mbunge wa Micheweni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limezungumzwa kwa kina sana ni lile ambalo amelizungumzia Mheshimiwa Nimrod Mkono, Mbunge wa Musoma Vijijini. Mimi nataka nikuhakikishie Mzee Mkono kwamba, hoja zote ulizozitoa tumezikubali na mimi kama Waziri, nitazifanyia kazi. Kitu kikubwa nilichoanza kukifanyia kazi pale *FCC*, palikuwa na uongozi wa kukaimu na sasa tumeshafanya mpango wa kupata *CO* ambaye siyo tena wa kukaimu. Najua kuna programu mbalimbali zinazokwenda pale kushirikiana na

*World Intellectual Property Organisation* ku-*automate* sehemu ya pale.

Naelewa kwamba, *BRELA* tuna utaratibu wa kujenga ofisi na kiwanja tumekwisha kupata. Sasa napenda kukuhakikishia kwamba, ushauri ulioutoa na hasa tukizingatia kwamba tija imepungua pale, tutahakikisha kwamba, eneo lile linafanya kazi kwa ufanisi. Nimeshtuka uliposema tunachukua siku 120 kutoa *documentation*, lakini wenzetu Kenya wanachukua siku chache. Ushauri wako tumeuchukua na ninakuhakikishia kwamba, tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo limechangiwa ni suala zima la mpango mkakati wa kuhakikisha Zao la Korosho ghafi na zilizobanguliwa zinapata soko la moja kwa moja, badala ya mfumo wa sasa wa kusubiri wanunuzi na kuonekana kuwa ni tatizo kubwa kwa wakulima. Hili amelizungumzia Mheshimiwa Salum Barwany, lakini vilevile amelizungumzia Mheshimiwa Asaa Hamad, aliposema viwanda vya Korosho tunafanyaje; hicho ndiyo kilio.

Kwanza, tukiangalia suala la viwanda vya korosho, sasa hivi kumeshatokea utaratibu mzuri sana; *NSSF*, wamesema wao wapo tayari kutoa asilimia 60 za uwekezaji na wawekezaji wale kutoa asilimia 40 ili kukarabati viwanda hivi. Mimi nafikiri hiyo ni fursa ambayo tunatakiwa tuichukue haraka sana na kwa taarifa yako, sasa hivi tayari kuna viwanda vitatu; Kiwanda cha Mtama, Newala na kingine kimojawapo tayari vimeshaingia katika utaratibu huu. Vingi vya viwanda hivi matatizo yake makubwa ni ukosefu wa mitaji. Kwa hiyo, hilo ni eneo ambalo tutaweza kuhamasishana na Wizara ya Kilimo, wanaosimamia sekta inayosimamia viwanda hivi ili kuvifanyia kazi. *(Makofi)*

Vilevile, Mheshimiwa Barwany ni nia ya Serikali sasa hivi na tuko katika maandalizi ya kuanzisha soko la bidhaa za mazao *(Tanzania Commodity Exchange)*. Tunadhani mfumo wa soko huu kwa zao kubwa kama korosho, utaleta ushindani wa bei na kwa kuwa utawashirikisha wanunuzi

wengi wa ndani na nje ya nchi, tunaweza kupata soko la uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limejitokeza tena suala la haki miliki, nimeshalizungumza katika hotuba yangu na tayari nimeshatoa agizo kwa *COSOTA* waanze mchakato wa kuona kwamba wanaweka Kanuni. Ingewezekana kabisa tukasema tungoje marekebisho ya sheria, yakachukua muda mrefu, lakini nadhani mabadiliko ya Kanuni yanaweza kuweka sawasawa hali hii na kuhakikisha kwamba, wasanii ambao nao ni vijana wengi tu wanaotafuta kazi katika nchi yetu, wakaanza kupata mapato yao na kupunguza tatizo hili la ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda unavyoonekana, unatutupa mkono, lakini kama nilivyosema mwanzoni, hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge ni nyingi sana, tutajaribu kuzijibu zote, tutawakabidhi watazisoma na ushauri waliotupa katika ufuatiliaji tutafuatilia.

Kabla sijamaliza, kulikuwa na tatizo linalohusu, nadhani ni Tandahimba kama sitakosea kwa Mheshimwa Njwayo; kulikuwa na wakulima wa Korosho ambao waliweka korosho zao katika kiwanda fulani na baadaye wakaambiwa korosho zile zimepotea. Taarifa tulizozipata ni kwamba, huyo aliyesema kwamba korosho zile zimepotea, ameona ni afadhali suala lile liende mahakamani. Kwa hiyo, suala hilo litakwenda mahakamani, nadhani litafuatiliwa kwa utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, narudia tena kukushukuru sana na kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote. Naishukuru Kamati ya Fedha na Uchumi, Viwanda na Biashara na Kamati ya Bajeti. *(Makofi)*

Waheshimwa Wabunge, tunataka kwenda kwenye Mkakati wa *Integrated Industrial Development Strategy*. Tunaomba mtupe fedha hizi tuanze, kumi inaanza na moja

na sasa hivi tuko kwenye tatu, hakika Mungu akijaalia, tutakuwa na viwanda katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA UJENZI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 44 – Wizara ya Viwanda na Biashara**

Kif. 1001- *Administration and HR Management* ... .... .... .... ..... ...... Tshs. 7,101,168,000

**MWENYEKITI:** Utaratibu wetu mnaufahamu, watakaobahatika ndiyo hao hao.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza, kwa furaha kabisa, nashukuru kupata hii nafasi kwa sababu niliomba kuchangia na bahati mbaya sikufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo ningelisisitiza kwenye suala zima la *EPZ*, nchi nyingi hasa za Mashariki ya Mbali kama vile Malaysia, Thailand, Indonesia, hata China yenyewe, walipata mafanikio makubwa kutokana na maamuzi yaliyokuwa na vitendo ndani yake. Maamuzi ya kwenye vitabu hayamfikishi mtu katika maendeleo halisi. *(Makofi)*

Leo, kwa mara ya kwanza kabisa nasimama katika Bunge hili na kusema kwamba, Kamati ya Biashara na Viwanda, ninaipongeza na ninaipongeza kwa umahiri wake wa kuleta haya marekebisho. Kama ingelikuwa haya hayakuletwa ya kuongeza bilioni 30 katika *Kurasini Hub,* basi leo pengelitoka maji hapa. Kwa nini nikasema hivyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu *Kurasini Project* au *Hub* au *Logistics Hub* ni pahala ambapo patatoa ajira isiyopungua 25,000. Siku zote tunalia vijana hawana kazi; ni hapa pa kuanzia, ingawa hizi fedha zilizotengwa bado hazijafikia kiwango kinachotakiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sanya, omba ufafanuzi.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Naam!

**MWENYEKITI:** Omba ufafanuzi wa kifungu hicho, kwa sasa unachangia. Unatakiwa uombe ufafanuzi. Unazo dakika tano za kuomba ufafanuzi.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Sasa ninachoomba hapa ni kutaka kujua; tumepewa bilioni 30 na huu mpango ni bilioni 60. Bilioni 30 zitatolewa tena mwaka 2014 au tutasuasua kwa milioni moja au milioni moja na laki tano kama tulivyokuwa tumeanzia mwaka jana ili tumalize hili suala kwa vile suala hili linagombaniwa sana na baadhi ya nchi za Kiafrika kutaka kuchukua hii nafasi ambayo sisi leo tumeikwamua kwa asilimia 50? *(Makofi)*

Je, mwaka 2014 tutamaliziwa hizi bilioni 30 ili hii *Project* imalizike tutoe ajira na nchi ipate faida na viwanda viwepo? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godfrey Zambi.

Waheshimiwa Wabunge, tuliposema dakika tano, ilikuwa kwa watu watano tu. Upo upungufu wa muda, tunatoa fursa kwa wengine na wao waweze kutoa mchango wao. Kwa hiyo, tukiweza kuchangia kwa muda mfupi, mkitaka dakika tano tano, ninayo orodha ya watu watano hapa. *(Makofi)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Ninataka nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri au maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, faida ya kujenga viwanda nchini ni pamoja na kuhakikisha kwamba, Wananchi wetu wanafaidika na bei ya mazao au bidhaa zinazotengenezwa katika viwanda hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotokea kule Mbeya, nitoe mfano tu; kuna Kiwanda cha Saruji. Bei ya Saruji inayozalishwa Mbeya, inauzwa kati ya Sh.16,000, Sh.17,000 mpaka Sh.18,000. Saruji hiyo hiyo inayozalishwa katika Kiwanda cha Saruji pale Mbeya, ukienda Mikoa ya Morogoro na Dar es Salaam, inauzwa hadi Sh.14,000 mpaka Sh.15,000. Sasa Wananchi wa Mkoa wa Mbeya kile kiwanda kilipo wamekuwa wanajiuliza; kwa nini bei ya saruji Mbeya ambako inazalishwa ni kubwa zaidi kuliko maeneo mengine ambako wanaipeleka na kwa gharama za usafiri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko makubwa sana kutoka kwa Wananchi wa Mkoa wa Mbeya; inawezekana kuna bidhaa nyingine na maeneo mengine ya namna hiyo. Tunamwomba Mheshimiwa Waziri atueleze. Tunajua Serikali haihusiki na uzalishaji, lakini masuala ya bei na udhibiti wake, haya hayawezi kuachiwa watu wauze wanavyotaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunamwomba Mheshimiwa Waziri, awaeleze Wanambeya na Watanzania wengine ambako inawezekana kuna viwanda, lakini wanashindwa kufaidika na viwanda hivyo kwa sababu tu ya bei kuwa kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Kwanza kabisa na mimi napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa kupeleka fedha kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, kwa ajili ya malipo ya *EPZ.* Niliongelea suala hili mwaka 2012 na akaahidi na fedha zimepelekwa, lakini sasa kuna utata; nilipomwuliza Mheshimiwa Waziri

aliniambia zimeenda bilioni 2.5, lakini Wananchi kule wanasema wametangaziwa bilioni 1.2. Kinachowashangaza zaidi, tayari *EPZ* walishaenda kufanya tathmini. Sasa hivi Halmashauri imeenda inafanya tathmini upya na mbaya zaidi tathmini hiyo inapunguza ekari, inapunguza ukubwa wa eneo ambao tayari *EPZ* walishaifanya. Tunajua Serikali ina dhamira njema ya kuhakikisha wale Wananchi wanalipwa na wengi ni wazee.

Sasa wanataka kujua; Mheshimiwa Waziri atamke zimeenda kiasi gani, kwa sababu sasa hivi kuna wengine wanasusia, haiwezekani mtu ana ekari tano alipwe fidia shilingi 1,000,000, mwingine shilingi 500,000 na wale ni wazee wa muda mrefu kule, siyo vijana kama mimi labda wangelisema wanachakachua au wanafanya ujanja ujanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Mheshimiwa Waziri awaeleze Wananchi wa Tairo, ni kiasi gani ambacho kimepelekwa; hizo bilioni 2.5 ambazo uliniambia au bilioni 1.2 ambazo Wataalam wa Halmashauri wanaenda kuwaambia kule? Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. INNOCENT E. KALOGERIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua suala la Kisera; ni vyema kuwa na viwanda vidogo vidogo na kueneza teknolojia rahisi ili kuleta maendeleo kwa watu wetu.

Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa Kitaifa katika kuimarisha *SIDO* na hasa ukitilia maanani hata Ofisi za *SIDO* Mikoani na Wilayani hazifanyi kazi vizuri?

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru Mheshimiwa Innocent, *specific* ameuliza suala la sera na ndiyo hasa kifungu hiki. Sasa kila mtu akianza kuuliza suala la kiwanda chake kwenye Jimbo lake itakuwa tatizo. Mheshimiwa Zitto!

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mfupi uliopita nimepokea *message* inasema hivi; sikiliza nyimbo hifadhi katika simu yako au tuma *dedication* ya nyimbo kali na mpya kwa kupiga 15600, shilingi 19 kwa dakika

moja na usajili wa shilingi 30 kwa siku tu. Hii ni baadhi ya mifano ya *promotion* ambazo Makampuni ya Simu yanafanya kwa kutumia kazi za sanaa.

Agizo ambalo Mheshimiwa Waziri amelitoa leo, kwa vyovyote vile Wasanii wetu na hasa Vijana wa Bongo Fleva watakuwa wamelipokea kwa furaha kubwa sana. Kwa sababu sasa wataondoka kwenye unyonge wa kunyonywa kutokana na kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yni kwamba, tulivyoanza hizi kelele za kutaka Makampuni ya Simu na wachuuzi *(Content Providers)*, waanze kuwalipa Wasanii haki zao stahili. Baadhi ya Makampuni, yameanza kuwajaza mamilioni Wasanii wetu mbalimbali. Leo hii msanii Mwana FA, ametoa taarifa yake kwenye vyombo vya habari, inaonesha kwamba, amelipwa Sh.18,000,000 katika kipindi cha miezi mitatu, wakati siku chache zilizopita alikuwa analipwa Sh. 1,000,000, Sh. 2,000,000, Sh.600,000.

Kwa hiyo, hizi juhudi zinaonesha kabisa kwamba, zinaweza zikazaa matunda na agizo lako kwa *COSOTA*, kuweka hizi kanuni kuhakikisha biashara hii sasa inakuwa *regulated* vizuri, itaweza kuwasaidia sana vijana wetu na kuweza kutengeneza ajira. Kilio ambacho wasanii wa muda mrefu kama akina Sugu, akina Kitime na kadhalika, sasa kitakuwa kimepata jibu lake mwafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo moja ambalo nilikuwa ninaomba litolewe ufafanuzi na Mheshimiwa Waziri. Kwa mujibu wa Kanuni Na. 3 ya Sheria ya *COSOTA* ya mwaka 1999 inasema kwamba; Vituo vya Televisheni na Redio vinapaswa kwanza kupata leseni kutoka *COSOTA,* kwa ajili ya kuendesha kazi ya kupiga miziki na kadhalika.

Pili, kulipa mirabaha kwa Wasanii ambao nyimbo zao zinatumika. Kanuni hii ipo kwa mujibu wa Sheria ya Hatimiliki, lakini haitekelezwi. Hata Televisheni ya Taifa au Redio ya Taifa kama *TBC* na *TBC1* hawalipi mirabaha hiyo lakini ipo kwenye Sheria.

Tatizo lililopo ni kwamba, tunaambiwa *TCRA,* hawatoi taarifa hizo kwa *COSOTA* ili kuweza kupata lile pato ghafi na waweze kuwagawia wasanii. Ninaomba sasa utoe agizo la kuhakikisha kwamba, Sheria hii inatekelezwa ili wasanii wetu waweze kupata haki zao jinsi inavyostahili na tuweze kumalizana na jambo hili kuanzia tarehe 1 Julai, 2013. Ninaomba maelezo yako Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imebahatika kuwa na rasilimali nyingi sana na tumebahatika pia kupata wawekezaji katika sekta mbalimbali. Je, ni lini Serikali itakuja na sheria mahususi ya kuweza kuwabana hawa wawekezaji ili waweze kuchangia asilimia fulani ya pato lao kwa jamii; yaani *Corporate Social Responsibility* badala ya sasa hivi tumeona wawekezaji wengi wanachangia tu kile wanachoguswa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru. Mheshimiwa Suzan Lyimo.

**MHE SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wote tunatambua kwamba, wanawake hapa Tanzania ni zaidi ya asilimia 51. Wanawake hawa kutokana na mfumo dume, walishindwa kuingia kwenye vyombo vya maamuzi, lakini *majority* wamejiingiza zaidi kwenye masuala ya kiuchumi na wengi wao ni wajasiriamali.

Ninaomba kauli kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, wana mkakati gani kuhakikisha wanawasaidia akina mama hawa katika kupata masoko? Ninaelewa kwamba, kuna *NGO* mbalimbali kama *EOTF,* ambayo imekua ikiwasaidia akina mama; lakini Serikali ina mikakati gani kuwasaidia akina mama hawa ambao wanajitahidi sana katika suala zima la kiuchumi hapa nchini?

Ninakushukuru. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. ABBAS Z. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Kisera la *EPZ.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya ziara Viongozi wa Wizara ya Viwanda, Viongozi wa Ardhi na wenyewe wa *EPZ,* tukaongea na Wananchi wa Kurasini, nikiwa mimi Mbunge, Mkuu wa Wilaya na Diwani, wakatuelewa, hakukuwa na mgogoro. Tuliwaahidi Wananchi wale mwezi huu wa Mei, ndiyo tutaanza kuwalipa na hao wakubwa walisema tayari wanazo shilingi bilioni 60 mkononi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo ninamwomba Mheshimiwa Waziri, aniambie ili nikawaambie Wananchi wangu ni lini tutaanza kuwalipa kwa sababu tayari tuliwaahidi tutaanza kuwalipa mwezi Mei, 2013? Pale Shimo la Udongo pembeni ndiyo kuna Mtaa wa Kurasini, ambao leo una miaka karibu saba, Wananchi wale hawajalipwa fidia. Sasa Mheshimiwa Waziri ungeliniambia ni lini tunakwenda kuwalipa ili nikawaambie na zile bilioni 60 sasa hazipo zipo shilingi bilioni 30? *(Makofi)*

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninataka kupata ufafanuzi kuhusu suala la *EPZ Neema Tanga*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la *EPZ* ni kuhusu fidia na niliuliza mwishoni mwa mwezi huu kwenye kipindi cha maswali. Mheshimiwa Naibu Waziri alinijibu kuwa, watalipwa kabla ya mwaka wa fedha kwisha na zikipatikana fedha kutoka Hazina. Leo alipokuwa anatoa ufafanuzi kwenye hoja za Wabunge, alimjibu Mheshimiwa Omar Nundu, kwenye maeneo ambayo utaratibu haujakamilika, taratibu hizo nadhani ni za kulipa fidia, wanaweza wakaruhusiwa wakaendelea na shughuli zao za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti hapo nimepata mashaka sana, ninamwomba Mheshimiwa Waziri atoe ufafanuzi, kwa sababu atakuwa anawachanganya Wananchi. Kwanza, mashaka yangu makubwa ni kuwa pesa hizi sasa hazipo na hawajui watalipwa lini. Kwa hiyo, inawachanganya sana kisaikolojia. Vilevile kuna wengine ambao walikuwa wamejenga nyumba za kudumu tu, siyo wale ambao walikuwa wakilima.

Sasa wakiambiwa wafanye shughuli za kiuchumi ambazo siyo za kudumu, labda ni kilimo ambacho kutokupanda miti ya kudumu na nyinginezo. Sasa na wale ambao wamepata matatizo kama hayo watawafidia vipi? Ninaomba Serikali isifanye siasa, inyooshe maneno ili Wananchi wasichanganyikiwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru. Mheshimiwa Lwanji.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri asubuhi ya leo hii, ameainisha mafanikio mengi tu upande wa uwekezaji hasa kwenye viwanda vya saruji. Nimeangalia ninavyoona Sera hii kidogo naona kama kuna tatizo, kwa sababu viwanda vingi hivi vimewekwa upande mmoja wa nchi na kuacha maeneo mengine bila viwanda hivi vya saruji, ambavyo tunavihitaji sana na hasa Kanda hii ya Magharibi. Ukiangalia upande wa Mkoa wa Singida, kuna malighafi nyingi tu ya *gypsum* pale, ambayo magari huja kuchukua kila siku kupeleka katika viwanda vingine mbali na mahali hapo.

Ningelipenda nipate ufafanuzi juu ya sera hii kwamba ni lini maeneo haya ambayo hayana viwanda muhimu vya Saruji yatakumbukwa?

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, mkitaka ufafanuzi kwa maswali machache wengi tutapata nafasi. Mheshimiwa Maryam.

**MHE. MARYAM S. MSABAHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa na swali la kisera. Viwanda vingi viko mikononi mwa wawekezaji na havifanyi kazi na havitoi ajira. Viwanda hivi vimekuwa sasa vinachukuliwa vyuma chakavu, vinauzwa na kubomolewa. Je, Serikali ina tamko gani kuhusu viwanda hivi na hao

wawekezaji kama havifanyi kazi virejeshwe mikononi mwa Serikali au viwanda hivi vibinafsishwe tena?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba majibu.

**MHE. JOHN S. MAGALLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami ninashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninachangia kwa maandishi, niliomba kauli ya Serikali kuhusu masuala ya Programu ya Viwanda na Masoko kwa Mazao ya Mifugo pamoja na Pamba. Ikitambulika kwamba, Zao la Pamba, linategemewa na Watanzania wasiopungua milioni 14 na Mazao ya Mifugo Wananchi wasiopungua bilioni 25.

Je, Mheshimiwa Waziri sasa atatoa kauli gani elekezi, ambayo itatekelezwa kuhakikisha ya kwamba, wanaongeza thamani ya mazao ya pamba kwa kuwa na *Commercial Attachees,* kwa sababu Balozi zetu hazina madalali wa kuuza pamba; hivyo, hivi sasa hatuna mashindano ya bei ya pamba, bei ya pamba ni dhulumati. Ninaomba ukombozi wa Serikali na vivyo hivyo ninakukaribisha Maswa tuje tujadiliane. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru. Mheshimiwa Mkono.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii.

Mimi langu ni la kisera tu. Nimeshukuru sana Waziri ameeleza vizuri kwamba, hiyo hoja ni nzuri na ataifanyia kazi. Suala kubwa ni *time;* tunaposema kazi ya *BRELA* mojawapo kubwa ni kusajili Hati Hataza na Alama za Biashara na *time is of the essence.* Hiki Kitengo kimeshindwa kufanya kazi. Tulijaribu mwaka 1999 kuki-*reform* na kufanya kwamba *something unique* itokee.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mkono, tunakuomba uongeze sauti kidogo.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Naam!

**MWENYEKITI:** Sogelea *mic,* ongeza sauti kidogo au hamia *mic* nyingine.

Waheshimiwa Wabunge, tunaomba utulivu kidogo.

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Ilikuwa ni kwamba, lazima wabadilishe, mwaka 1999 walisema urasimu ukome tunaunda *BRELA.* Mpaka sasa, *BRELA* badala ya kuundwa upya imekuwa inasuasua, haifanyi kazi na watu *incompetent* wamo mle ndani. Katika mambo ya alama za biashara, *time is of the essence;* swali langu ni hili; je, mta-*reorganize* upya ama ni kubadilisha watu tu lakini *system* inabaki vilevile? Hili ndilo lilikuwa swali langu la msingi. Ahsante sana.

**MWENYEKTI:** Haya ninakushukuru. Mheshimiwa Mwaiposa!

**MHE. EUGEN E. MWAIPOSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi swali langu pia ni la kisera. Nilipokuwa ninachangia kwa maandishi nilimwomba Mheshimiwa Waziri wakati wa hitimisho anieleze ni kwa nini Serikali pamoja na Tasisi zake, zinanunua bidhaa zinazozalishwa viwanda vya nchi za nje, zikiwepo samani za kutumia maofisini, pamoja na magunia yanayotumika kuhifadhi nafaka?

Nikamwomba pia kwamba, kwa sababu Sera ya Serikali ilikuwa ni kuchochea viwanda vyetu kwa kuwahamasisha Wananchi wanunue bidhaa zinazozalishwa katika viwanda vyetu vya ndani; sasa anieleze kwa nini Serikali yenyewe haiwi mfano mzuri wa Sera hiyo?

**MHE. MTUTURA A. MTUTURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana.

Sera Kuu ya Serikali yetu Tukufu ya Chama cha Mapinduzi ni kuondoa kero za Wananchi; hiyo ndiyo Sera Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kutokana na maelezo yake juu ya namna ya kulinusuru zao la korosho, ameeleza kwamba, kutakuwa na mpango wa kuanzisha viwanda. Mpango huu kwa namna yoyote ile ni mpango wa muda mrefu na msimu huu unaokuja wananchi wa Tunduru na maeneo mengine wanategemea kuuza korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, misimu miwili mfululizo kutokana na sheria hii ya Stakabadhi Ghalani, Serikali pamoja na Vyama vya Ushirika vimeshindwa kusimamia sheria hii mpaka wananchi wakaweza kupata tija.

Je, Serikali kupitia Wizara hii ambayo ndiyo iliyotunga sheria ile ya Stakabadhi Ghalani, haioni kwamba, sasa hivi ni wakati muafaka sheria hii wakaisimamisha mpaka pale aidha, viwanda hivyo vitakapokuwa tayari au watakapoleta marekebisho sahihi kwa ajili ya Sheria hii?

**MHE. ENG. ATHUMANI R. MFUTAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Swali langu la kisera linahusu zao la misitu, zao la asali. Wizara ina mpango gani katika kuwasaidia wafugaji wa nyuki ili asali wanayovuna iongezewe thamani na pia sera ya kutafuta masoko ya nje ili wapate bei nzuri ya asali pamoja na nta?

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa dakika moja ama mbili.

Mwaka jana wakati tukijadili Wizara hii, nilizungumza na Mheshimiwa Waziri Kigoda kuhusu madai ya waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Matairi cha *General Tyre* ambacho leo tumekiona kwenye bajeti na tuna-*appreciate* kazi nzuri ambayo inafanywa na *NDC* ili kukifufua. Lakini sasa Waziri anasema pesa ndiyo zimetumwa kuwalipa waliokuwa wafanyakazi na wapo wanaokiri kwamba kweli wamelipwa, lakini wapo ambao wanalalamika kwamba, hawajalipwa kabisa na ndiyo swali ambalo nililiuliza mwaka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wasiwasi wangu isije ikawa kwamba pesa zimetoka Wizarani, lakini kule chini kuna watu wamezipiga dafrau. Naomba Mheshimiwa Waziri atuambie tu kwamba, ana uhakika kama watu wote kweli wamelipwa? Kama pengine taarifa si sahihi, basi nimpe baadhi ya watu na namba zao za simu ili awasiliane nao na walikuwa wafanyakazi ili wampe madai yao na wamwambie ni kwa jinsi gani ambavyo hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kupata ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusu wafanyakazi wa *General Tyre*. Nashukuru.

**MHE. EZEKIA D. WENJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna viwanda vingi nchi hii ambavyo vilifungwa ghafla, vingine vilifungwa taratibu vikiwa kwenye mikono ya Serikali. Matokeo yake ni kwamba, kuna wananchi ama wafanyakazi wengi sana waliokuwa wanafanya kazi kwenye viwanda hivyo ambao hawakulipwa *terminal benefits* zao, kwa mfano, Kiwanda cha *Mwatex* kilichopo Jijini Mwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninachohitaji kutoka kwa Waziri ni kwamba, je, Waziri yuko tayari kufanya *stock taking* kujua kwamba viwanda vilivyofungwa vikiwa chini ya Serikali, ni wafanyakazi wangapi ambao hawakulipwa *their terminal benefits* na wengine walikwenda wakafungua kesi kwenye Mahakama mbalimbali katika maeneo mengi nchi hii ili wafanye *stock taking* kutumia *reference* kesi ya *MWATEX* Mwanza ili wafanyakazi waweze kulipwa haki zao. Napenda kupata ufafanuzi.

**MHE. SUZAN L. A. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kitabu cha Waziri, ukurasa wa nane amezungumzia suala la MKUKUTA na Kilimo Kwanza ili kuondoa umaskini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanaolima mpunga, maana miaka yote wanasema wananchi wa korosho na pamba, lakini sasa hivi kilio kikubwa ndani ya nchi yetu hususani Wilaya ya Kilombero *KPL* wakulima wapatao 3,000 walihamasishwa na wakalima mpunga wakapata sana mwaka jana na mwaka huu wamepata sana, lakini cha kushangaza Serikali ikaingiza sokoni mchele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba majibu ya Serikali, wananchi hawa wakulima wa mpunga hususan kuanzia Kilombero na Tanzania nzima, je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea thamani mchele wao ili wapate kuuza?

**MHE. VICENT J. NYERERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ubinafsishaji wa viwanda, Kiwanda cha *MUTEX* pia kilibinafsishwa kwa bei ya kutupwa na waliokuwa wafanyakazi wa *MUTEX* 834 waligoma kuchukua shilingi milioni 70 walizokuwa wametengewa kwa sababu zilikuwa hazitoshi, wakigawana kila mtu anapata sh. 83,000/=. Mheshimiwa Waziri akijibu swali langu alisema, Serikali itawaongeza fedha hizo, lakini mpaka sasa hawajapewa fedha. Wamenituma niulize na wameomba nisimung'unye maneno, je, Serikali ya CCM imewadhulumu? Wanaomba ufafanuzi.

**MHE. JOSEPH O. MBILINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Waziri amezungumzia suala la Serikali kuwatambua Wamachinga kwa namna ambayo sijawahi kumsikia kiongozi wa juu wa Serikali akizungumzia kwa maana *honestly* na dhamira.

Sasa basi, wakati Serikali imeshaonesha dhamira na iko tayari kukaa chini kupitia Vyama vyao ambavyo Mheshimiwa Waziri amevitaja, amesema vipo kama sita, wakati tunaelekea kwenye hilo, kwa nini Serikali sasa isitoe

tamko kwamba, Wamachinga popote wanapofanya shughuli zao katika mipaka ya Tanzania wasibughudhiwe mpaka pale Serikali itakapokaa na kujadiliana nao *way forward* kwamba, tunakwenda kufanya nini huko mbele katika mazingira ya amani na utulivu kwa sababu Serikali imeshawatambua na kuwakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitajidhulumu nafsi kama nisipokushukuru na kukusifu Mheshimiwa Dkt. Kigoda kwa namna ulivyo-*present* leo na kujibu hoja za Wabunge kama Dokta na kama Waziri wa Serikali bila kuonesha kama Mwenezi wa Chama kama alivyofanya Mheshimiwa Magufuli jana. (*Makofi*)

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi kwenye hili suala la Kurasini *Logistic Hub*. Nina mashaka kidogo na kwamba jambo hili linaweza likaenda likaua kabisa viwanda vya Tanzania, kwa sababu kinachoonekana hapa ni kwamba, ni Wachina wanakwenda kuwa na *mega wholesale* katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna yoyote ile ikitokea hivyo, maana yake ni kwamba, hata vile viwanda vidogo ambavyo Serikali imeanza kuvisaidia vitakwenda kufa, kwa sababu Wachina watakuja na *products* zao zikiwa zimeshatengenezwa kabisa. Maana yake ni kwamba, watu watakuwa wananunua bidhaa hapo Kurasini na viwanda vidogovidogo ambavyo vimeanza kuchipukia na ambavyo Serikali imeanza kutilia mkazo vinaweza vikafa kabisa kwa sababu Tanzania itakuwa ni kama *mega wholesale* ya bidhaa za China ambazo tayari zipo *ready made.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi juu ya jambo hili.

**MHE. HIGHNESS S. KIWIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza nianze na kumpongeza Mheshimiwa

Waziri Kigoda kwa namna ambavyo leo hii ameweza kuyapokea maoni ya Kambi ya Upinzani tofauti na ambavyo Mawaziri wengine wamekuwa wakifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye suala la kisera linalohusiana na kero kubwa inayotokana na mfumo wa ushuru ambao *TRA* sasa wanautumia kwa upande wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi, hususani magari. Kwa sasa *TRA* hawa hawazingatii tena taarifa ya ununuzi wa magari haya, wao sasa wamekuwa kama ni wauzaji wa magari maana wana bei zao, unanunua gari lako nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokwenda kwenye hatua ya *import duty,* wao wanakwambia wewe umenunua kwa shilingi milioni tano, wanakwambia gari hili thamani yake ni shilingi milioni kumi. Sasa huu ni ukandamizaji, lakini pia ni kuingilia mfumo wa *negotiation* baina ya muuzaji na mnunuzi.

Sasa napenda nipate kauli ya Waziri juu ya mfumo huu ambao ni kandamizi na unanyanyasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. MARIA I. HEWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kuna kaulimbiu inasema, maisha bora kwa kila Mtanzania, mgawo wa Viwanda vya Saruji uko Tanga, Dar es Salaam, Mbeya na sasa hivi mnapeleka Mtwara. Maisha bora kwa Kanda ya Ziwa angalau Kikanda tukaweka Singida au Kigoma au Tabora angalau Mwanza. Je, Mheshimiwa Waziri anasema nini baada ya Mtwara, anaifikiriaje Kanda ya Ziwa?

**MHE. GAUDENCE C. KAYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kisera mradi wowote unapoanza uwe wa Serikali au wa wawekezaji wa nje, lazima wananchi wanaohusika katika eneo kama watalazimika kuondoka walipwe fidia. Jambo hili limekuwa tofauti pale Mtunduwalo katika mradi wa Ngaka. Naomba ufafanuzi.

**MHE. DEOGRATIUS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Katika mchango wangu wa maandishi nilieleza jinsi Ngara inavyopakana na Rwanda na Burundi na hatuko mbali na Congo na nikaishukuru Serikali kwa soko la Kimataifa la Kabanga, lakini nikaiomba Wizara iangalie soko la mpakani la Mrusagamba ambako kuna biashara nyingi sana kati ya Burundi na Tanzania. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Wachangiaji wote walioomba wamepata nafasi na tumetimiza wachangiaji 27. Samahani, Mheshimiwa Sakaya!

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Napenda tu kupata ufafanuzi kutoka kwa Serikali kuhusiana na hoja yangu ambayo nimeitoa wakati nachangia kwa maandishi. Niliomba suala kuhusiana na mwekezaji Mhindi wa Kiwanda cha Karatasi, Mgogolo, huko Mufindi ambaye amekiuka mkataba wake. Wakati anachukua ule mkataba mwaka 2005 alikubaliana kwamba, awalipe watumishi wote haki zao kabla hajaingia mkataba mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake hakuwalipa mpaka leo, watumishi 750 hawajapata kulipwa maslahi yao mpaka leo. Lakini pia mwekezaji huyu amekuwa anawalipa mshahara baada ya siku 60, lakini sheria inasema ni mwezi mmoja, mtu alipwe, lakini yeye analipa mishahara miezi miwili. Naomba kujua Serikali inasema nini kuhusiana na mwekezaji huyu wa Kiwanda cha Karatasi Mufindi.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana, wachangiaji 28 na wote mmepata nafasi *within 30 minutes, which is very good.*

Mheshimiwa Waziri majibu, mtajigawa kutokana na maswali mbalimbali.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali ni mengi, lakini tumegawana kidogo hapa na naomba nianze kujibu swali la Mheshimiwa Sanya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Sanya anataka kujua kama ile albaki baada ya kupokea shilingi bilioni 30 kutoka Serikalini...

**MWENYEKITI:** Weka *Microphone* vizuri!

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Sanya ametaka kujua kwamba kutokana na deni lile la shilingi bilioni 60 ambalo lilikuwa ni la mradi wa *EPZ,* sasa Serikali imetoa shilingi bilioni 30, je, hii albaki italipwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema wazi kwamba, Serikali sikivu ya CCM sasa hivi imetenga fedha katika bajeti hii ya mwaka 2013/2014 kiasi cha shilingi bilioni 30 ambazo zitalipwa mwaka huu wa bajeti ambayo tunaiomba 2013/2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema vile vile kwamba ipo shilingi bilioni 25 ambayo tumepokea jana kuhusu mradi huu. Kwa hiyo, jumla hapa itapatikana shilingi bilioni 55 na kwenye bajeti ya mwaka 2013/20134 kulikuwa na shilingi bilioni moja ambayo ilitengwa kabla ya nyongeza ya shilingi bilioni 30, kwa hiyo, kuna jumla ni shilingi bilioni 56 ambazo Serikali sikivu italipa kuhusu mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunasema kwamba tukipokea hizi fedha za jana shilingi bilioni 25 za bajeti hii ambayo inaishia Juni pamoja na zile bilioni 31 ambazo zinakuja kwenye bajeti inayofuata ya mwaka 2013/2014 na tumesema kwamba, fedha hizi kwa awamu ya kwanza kwa eneo ambalo lipo Shimo la Udongo ambalo lina ekari 38.12, hili tutaanza nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu Serikali sikivu imesema kwamba, hili deni lingine ambalo linabaki ili kutimiza azma ya deni lote ambalo ni bilioni 60 maana yake sasa limepanda mpaka 94, litalipwa mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Mheshimiwa Mtemvu ambalo nalo kidogo linahusiana na hili linatokana na kwamba ahadi ambayo Serikali iliitoa kuhusu malipo ya...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri usirudie swali, jibu tu!

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sawa!

Suala la Mheshimiwa Mtemvu tunatoa ahadi kwamba ahadi ilikuwa ni Mei, lakini pesa tumepokea jana. Kwa hiyo, utaratibu utafanywa wa malipo ya fidia, kwa hiyo, wananchi wa Shimo la Udongo wataanza kulipwa.

Mheshimiwa Mwidau alizungumzia kuhusu Tanga, bahati mbaya kwenye swali lake hatuwezi kujibu hili, lakini kwa sasa hivi nasema kwamba Tanga kuna mradi ambao ulikuwa unahusu maeneo makuu matatu ambayo ni Tanga, Bagamoyo na Songea, Ruvuma. Sasa huu ni mradi wa *Mini Tiger* Tanga – Bagamoyo ambayo jumla ilikuwa ni shilingi bilioni 50.2...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaomba utulivu!

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Bilioni 50.2 na tayari tulishapokea bilioni 10.9 kuhusu miradi hiyo Tanga ikiwemo. Sasa baada ya kupokea bilioni 10.9, albaki ambayo imebaki Serikali imeahidi kwamba inaliangalia na tutaweza tukawasiliana nao kabla ya mwaka huu kwisha tuangalie mradi huu wa *min tiger* ambao unahusu maeneo haya ya Tanga, Bagamoyo na Ruvuma ili iweze kulipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Mwaiposa anasema kwamba, samani na magunia yananunuliwa nje, badala ya hapa ndani. Naungana naye mkono kwamba, tulinde bidhaa za ndani, kauli yetu sisi kama Wizara tunasema kwamba, nunua bidhaa Tanzania, jenga Tanzania. Bunge

limeonesha mfano, kwani Ofisi za Waheshimiwa Wabunge samani zote zitatengenezwa na Magereza. Kwa hiyo, tuunge mkono hilo kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la Mheshimiwa Lema ambalo ni kuhusu *Kurasini Logistic Centre* ambapo anasema kwamba, baada ya kuingiza Wachina, kwa hiyo Wachina wata-*dominate* kiasi kwamba viwanda vidogo vidogo vitakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema si kweli hata kidogo, kwa sababu nia yetu kubwa ya kuleta wawekezaji wenye uwezo mkubwa sana, wanakuja na shilingi bilioni 600 na *impact* yake ni kwamba, wataajiri wafanyakazi 25,000 na sisi tumesema wazi kwamba, sasa hivi ni *Big Results Now* na huko ndiko tunakokwenda, kwa hiyo, hiyo ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba nimwachie Mheshimiwa Waziri ili aweze kuendelea na maswali mengine. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri!

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara katika hoja hii ya mshahara wa Waziri kuna masuala matatu ambayo yamejitokeza, nayo ni masuala yanayoingiliana moja kwa moja na masuala ya Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni suala la Mheshimiwa Shibuda ambalo ni suala la pamba na mkakati uliokuwepo; ni kweli kwamba, kwenye zao la pamba kuna zaidi ya Watanzania 40% wanashiriki kwenye zao la pamba, lakini kwa sasa hivi tatizo tulilokuwa nalo ni tatizo la ubora wa pamba na uzalishaji mdogo tuliokuwa nao, tija yetu bado ni ndogo sana.

Kwa hiyo, sisi kwenye upande wetu wa kilimo, jambo ambalo tumejikita kufanya sasa hivi ni kutengeneza mkakati ambao tutazunguka kwenye pande zote za uzalishaji wa pamba ili tutengeneze mazingira ya kuondoka kwenye uzalishaji ambao unazingatia kilo 400 kwa ekari twende tufike kwenye kilo 1,000 au 1,200 kama wanavyofanya wakulima wengine kwa daraja la wastani, lakini na pamba yenyewe lazima iongeze ubora ili iweze kuongeza ushindani kwenye masoko ya dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni la Mheshimiwa Mtutura ambaye ameuliza kama tatizo la korosho kwa misimu miwili, tatizo lililotokea ni tatizo la mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Nadhani Mheshimiwa Mtutura anafahamu na kwenye hoja ya Wizara ya Kilimo tulisema, tatizo siyo mfumo wa Stakabadhi Ghalani kusema ukweli, bali ni usimamizi uliotokea kwenye mfumo huo na uharibifu mwingine wa makusudi uliotokea kwenye mfumo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wake wa tatizo la Tunduru, nimelisema wakati tunamaliza hoja ya Kilimo, tatizo la Tunduru linafanana na tatizo la Mkuranga na baadhi ya Wilaya za Mkoa wa Lindi na Mtwara. Viongozi wetu wa Ushirika wengine kusema kweli wametuhujumu katika suala hili na bado tupo kwenye kuwafanyia uchunguzi na uchunguzi umekamilika kwenye baadhi ya maeneo na matatizo ya viongozi wa ushirika hata kwake Tunduru yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusiuangalie tu mfumo tukasema mfumo wa Stakabadhi Ghalani una matatizo, ulipofanya vizuri wakulima wamenufaika, lakini baada ya watu kuingia, ni matumizi mabaya ya *Government guarantee* na *monopoly* pia ya soko na ndiyo maana tunasema kwamba, tukiuondoa mfumo wa Stakabadhi Ghalani sasa hivi mbadala wake ni nini? Tukiondoa mfumo wa Stakabadhali Ghalani maana yake turudi kule tulikokuwa na kule tulikokuwa hakukuwa kuzuri sana kwa mkulima vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi kama Serikali tumejipanga, mfumo wa stakabadhi ghalani utaendelea, lakini tutabaki na usimamizi mkali zaidi. Kusema kweli kama tulivyosema, katika hali hii, ni vizuri tufahamishane kwamba, hatutaoneana haya katika hili, anayedhulumu wakulima ataumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni la Mheshimiwa Susan Kiwanga ambaye amezungumzia suala la mchele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima tuwe wakweli. Mpunga unavunwa mwezi wa Tano, Sita na Saba na mwezi wa Nane unakamilika kuvunwa. Hatua iliyochukuliwa na Serikali ya kuingiza mchele, imeamuliwa kwenye Baraza la Mawaziri mwezi wa Kumi na Mbili mwishoni ambapo bei ya mchele sokoni ilikuwa ni shilingi 2,700/= kwa kilo. Mpunga uliokuwa unavunwa mwezi wa Tano, Sita na Saba ni katika maeneo ya huko Bahi, Kyela, Idodi, Mpanda na kwingineko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa yako na Bunge hili mpunga uliovunwa bei ya juu kwa wakulima ilikuwa ni shilingi 35,000/=. Sasa wachuuzi walikuwa wanakwenda, mtu ananunua magunia 500 au 1000, anahifadhi ndani ili baadaye mwezi wa kumi na moja mpunga ule alionunua kwa shilingi 25,000 au 30,000 auuze kwa shilingi 100,000/= hicho ndicho kilichokuwa kinatokea. Huwezi kuniambia kwamba, mkulima alikuwa amebaki na gunia zake 100, amekaa nazo miezi sita, siyo kweli! Nimetoka Bahi nimekwenda Mpanda, Idodi, maeneo yote niliyojaribu kuuliza nimekuta waliokuwa na mpunga kweli wapo lakini ni wachuuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulichosema na mwaka huu tumekisema tena kwamba, jamani sasa hivi tumekwenda Bahi tumekuta mpunga unavunwa, watu wananunua kwa sh. 30,000/= lakini watauhifadhi ili baadaye wauuze kwa sh. 100,000/=. Sisi kama Serikali jukumu letu ni kumlinda mkulima kwa maana ya kwamba, hiyo bei ya sh. 30,000/= anayopewa leo ni ndogo sana. Jukumu letu pia ni kumlinda mlaji. Tukiruhusu mchele uuzwe shilingi 2,800/= kwa kilo mfumuko wa bei utapanda na utafikia hatua ya juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niseme wazi kwamba, hatua hii imechukuliwa na sasa hivi tunaona mchele kwa wastani umesimama kwenye bei ya kati ya sh. 1,700/= na 1,800/= kwa kilo ambalo ndilo lilikuwa lengo la Serikali. Lengo la Serikali siyo kumuumiza mkulima. Hata hii hatua iliyochukuliwa na Serikali, haikumuumiza mkulima, imewaumiza walanguzi waliokwenda wakanunua magunia, wengine wana magunia mpaka 10,000/= ndani mwao wameyafungia, wanasubiri nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika. Haya Mheshimiwa Dkt. Kigoda!

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Zambi kwenye misingi ya biashara kuna tofauti za bei, price *differential,* lakini vilevile tofauti hizi zinaweza kuleta hoja ya kuhodhi bei. Namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kunipa taarifa hii. Namhakikishia nitaifuatilia nipate majibu yake ni kwa nini sementi inauzwa bei ghali pale inapozalishwa kuliko kule inakopelekwa?

Mheshimiwa Ester Bulaya, bila wasiwasi wowote *EPZ* imepeleka shilingi bilioni 2.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Innocent Kalogeris, tutaimarishaje *SIDO*? Kwanza tunajitahidi sana kuhakikisha tunatenga bajeti kubwa katika Wizara yetu. Pamoja na kuzipangia bajeti kubwa, tunaziingiza katika utaratibu wa kupata mpaka fedha za kigeni na ndiyo maana mnaona *programs* mbalimbali kama *movies*, ambazo zinaangaliwa na *SIDO*. Kwa hiyo, tunaamini tukiziimarisha kifedha zitaweza kusaidia wajasiriliamali wengi.

Mheshimiwa Zitto Kabwe wazo lake tumelichukua. Vile vile nasema hapa itabidi tushirikiane na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Kwa sasa hivi nina taarifa

kwamba *COSOTA* wameingia ubia kwa utaratibu wa *PPP* kuangalia ni jinsi gani sasa wasanii wanaweza kupata malipo yao kutoka *TV* na redio. Tuliangalia hilo, tunalifuatilia na tutawapeni *feedback*.

Mheshimiwa Ritta Kabati, ameongelea juu ya wawekezaji kutoa, wanaita *social corporate responsibility*?

**MWENYEKITI:** Hivyo hivyo.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli si lazima, lakini mwekezaji yeyote ambaye ni makini na mahiri ni lazima alifikirie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuwawezesha wanawake, tunafanya maonesho ya Saba Saba ambapo tunawakaribisha wanawake wengi. Vile vile ukiangalia kupitia *SIDO*, orodha ya wajasiriamali kwa tafiti tulizofanya wanawake ni karibu asilimia 54.7 ukilinganisha na wanaume ambao ni asilimia inayobakia, lakini wanawake ni wengi zaidi. Kuna taasisi inayoendeshwa na Mama Anna Mkapa, *Equal Opportunity Trust Fund* ambayo inaendelea na akinamama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi na Balozi wa Marekani tulianzisha *AWEP - Africans Women Entrepreneurship Program*, ambayo inaendeshwa na Wamarekani na Serikali yetu ya Tanzania ambapo wanawake sasa watapata fursa ya kupeleka bidhaa zao katika soko la *AGOA*, Marekani. Kwa hiyo, kuna taratibu nyingi zinafanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwidau, suala la, ahaa, tayari ameshajibiwa.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Lwanji, amesema Viwanda vya Saruji vimewekwa upande mmoja wa nchi. Inawezekana ni kweli kutokana na malighafi inayopatikana huko, lakini sasa hivi kama mnavyofahamu tutakuwa na Kiwanda cha Kusindika Mafuta kikubwa sana katika Afrika Mashariki cha *Mount* Meru *Millers*, Singida

ambacho kitahusisha karibu wakulima 100,000. Tayari tumeshakipa kibali na taratibu za kuanzisha uzalishaji zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilizungumzwa suala la kwamba viwanda vingi havifanyi kazi, mashine zinauzwa kama chuma chakavu, Serikali inafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu...

**MWENYEKITI:** Samahani Mheshimiwa Waziri, ungemtaja na Mheshimiwa aliyezungumzia suala hilo.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani sana, ni Mheshimiwa Mariam Msabaha. Kama nilivyosema katika hotuba yangu, *CHC* imeanza kuwaita wale wote ambao viwanda vyao havifanyi kazi na vinasuasua. Ndiyo maana tuliishaanza na viwanda vinne au vitano. Tutahakikisha kwamba wale ambao tutaona hawataweza tena itabidi tuvichukue viwanda vile ili viuzwe au vichukuliwe na Serikali ili kufanyiwa shughuli nyingine.

Mheshimiwa Nimrod Mkono, aliongelea suala la urasimu na *incompetency*. Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, lakini hapa Bungeni siwezi kumwambia kwamba, sasa hivi nita-*reorganize*, ni lazima nikaangalie. Lakini ni suala ambalo kama nilivyosema kwenye maelezo yangu ya awali, tutalifanyia kazi kuona *FCC* inafanya kazi na inakuwa ni *efficient entity* ya kutoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mfutakamba amezungumzia zao la asali. Kama Mheshimiwa Mbunge atakavyoona, Wizara ya Viwanda na Biashara kwa makusudi kabisa, sasa inafanya Maonesho ya Kitaifa ya Zao la Asali. Lengo lake ni kuhamasisha uongezaji wa thamani ya zao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwa sababu maonesho haya ni ya Kitaifa, yanasaidia kuleta watu wengine ambao wanahitaji asali yetu na hivyo kuwa ni soko.

Hivi karibuni tunaanza mradi mzuri tu wa asali, sehemu za Singida ambapo Mheshimiwa Waziri Mkuu, alikwenda kufungua maonesho yale kuhusiana na zao hili hili la asali. Kwa hiyo, jitihada zinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie Mheshimiwa Nassari bila kusita kwamba, tumepeleka shilingi milioni 83. Kwa hiyo, akaulizie huko, labda matatizo wakati mwingine yanatokea huko, lakini nimethibitisha kabisa kwamba tumepeleka shilingi milioni 83.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Wenje kwamba, tuko tayari kufanya *stock taking,* wala hatuna matatizo. Lakini nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba, tukishapata hiyo *stock taking* na *figures* hizo kama tulivyopata za *MUTEX* na *MWATEX* tutazipeleka *CHC,* wakaziangalie ili waweze kuona Hazina inaweza kutoa kiasi gani cha hizo fedha kama kweli zipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Vincent Nyerere, ameongelea suala la wafanyakazi 584. Nimweleze Mheshimiwa Mbunge kwamba, nalifahamu sana na leo tena nimeongea na *CHC*, kwa sababu sasa liko mikononi mwa *CHC*. Nadhani hili linahitaji tulizungumzie kwa ukaribu zaidi kuliko kutoa majibu ya haraka haraka ili hasa kupata uhakika ni kwa nini Halmashauri kule haitaki kuchukua hizi fedha? Wale wanasema fedha zipo. Sasa hilo tatizo liko katikati, lakini ni suala ambalo tunaweza tukalifuatilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Sugu kwamba, kutoa tamko sasa hivi kwanza ni lazima tuangalie ule utaratibu wa vile VIBINDO wanafanya nini, wanasema nini, na hizo Halmashauri. Tukifikia hatua tukakaa katika mkao mzuri, tutatoa tamko mara moja, lakini *we are serious* kwamba, hawa ni wajasiriamali, wanatafuta riziki zao, hivyo ni lazima watafute na ajira ni tatizo katika nchi yetu. Kwa hiyo, hilo hatuwezi kuliacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwambie Mheshimiwa Highness Kiwia kwamba, kero ya ushuru wa *TRA* tumeipokea,

tutalipeleka kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha au *TRA* ili kuona wanaweza kulitolea kauli gani maana ni suala la *TRA* kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Maria Hewa, amesema Singida tunapeleka viwanda na hata hicho cha *Mount* Meru, sasa sijui ulisema cha saruji au cha nini! Mwanza tutaangalia uwezekano huo, lakini moja ya eneo tunalolisemea sasa hivi ni maeneo yote haya. Kigoma inaondoka kwa sababu imeshatenga eneo la *EPZ*, nadhani na Tabora na Mwanza pia, haya ni maeneo ambayo tukipata wawekezaji tutawaita waje huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Kayombo ni kwamba, Serikali haiwezi kuingia mahali mpaka iongee na wadau. Nadhani suala hili tumeshalifikisha mahali ambapo sasa Serikali na wadau tunazungumza. Ni kwamba, hatujafikia mahali ambapo tunakubaliana kuhusu huu ulipaji wa fidia. Hata hivyo, nina hakika, tumalizeni hili ili kiwanda chetu kule kifanye kazi kwa faida ya watu wa Ngaka, Mtunduwalo na uchumi wa nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja ya Mheshimiwa Ntukamazina. Nakubaliana na hoja yake, tutaangalia utaratibu wa kujenga soko la mpakani Mrusagamba, lakini naomba pia Mheshimiwa Mbunge ahamasishe Halmashauri yake ili na sisi kama Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Mfuko wa *ASDP* tuone tunasaidiana vipi kuanza masoko haya kwa sababu ni muhimu kwa uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Magdalena Sakaya, amezungumzia kuhusu Kiwanda cha Mgololo. Kwa kweli nimekifuatilia sana, hawalipwi baada ya siku 60. Walikuwa wanachelewa kulipwa, lakini sasa *almost* wanalipa *on time*, lakini siku 60 hapana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watumishi wengine 750 kama Mheshimiwa Sakaya atakumbuka vizuri, hili suala walilipeleka Mahakamani. Kwa hiyo, sasa hivi mimi na wenzangu na Ofisi ya Waziri, Uwezeshaji, tunataka kujaribu

kulidadavua litoke nje ya Mahakama ili tuone tunafanyaje katika kulitatua nje ya Mahakama na kuwapa haki zao wale wafanyakazi. Maana yake likiwa Mahakamani litachukua muda mrefu na inawezekana hata mwekezaji akashinda, *you never know*. Sasa ni afadhali tulitoe nje tuone namna ya kulishughulikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kujibu hayo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri bado una la Mheshimiwa Susan Lyimo na Mheshimiwa Amina.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lile la Mheshimiwa Lyimo kuhusiana na uwezeshaji, nilimjibu lile la *African Women Entrepreneur program AWEP*.

**MWENYEKITI:** Okay, uliunganisha na la Mheshimiwa Kabati, sawasawa. Haya la Mheshimiwa Amina.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la Mheshimiwa Amina pia nimeshalijibu.

**MWENYEKITI:** Okay.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002 - *Finance and Accounts*... ... ... ... Sh. 422,884,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*... ... ... ... ...Sh. 2,780,334,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1004 - *Government Communication Unit*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh.161,520,000/=

**MWENYEKITI:** Endelea Mheshimiwa.

**MHE. REBECCA M. MNGODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naitwa Rebecca Michael Mngodo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hii *subvote* 1004, kasma ya 220600, *Clothing, Bedding, Footwear, and Services*. Popote ninapoiona hii kasma inanitia maswali mengi sana kwa sababu labda siku za nyuma ilikuwa inahitajika, lakini sidhani kwa wakati kama huu ambapo tuna watoto wengi ambao wamefiwa na wazazi kwa UKIMWI, tunahitaji kununulia watu *bedding, footwear, and services* ambazo hatuzielewi ni zipi. Hii kasma inaonekana hata katika *Administration and Human Resources Management*. Ningeshauri kwamba kasma hii iondolewe na fedha yoyote ambayo iko katika kasma hii ielekezwe katika ku-*strengthen* mambo yanayohusu watoto na wanawake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, *item* 220600 *subvote* 1004 kuna shilingi 6,000,000/=, ukurasa wa 243.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hii *item* 220600 ya *clothing, bedding, footwear and services* ni kwa ajili ya kugharamia sare za watumishi katika maonesho ya sekta za viwanda na biashara.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1005 - *Internal Audit Unit*... ... ... ... ... ...Sh. 174, 200, 000/=
Kif. 1006 - *Legal Services Unit*... ... ... ... ... Sh. 86,114,000/=
Kif. 1007 - *Management Information System*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 207,197,000/=
Kif. 1008 - *Procurement Management Unit*... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ....Sh.196,537,000/=
Kif. 2001 - *Industry*... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 4,170,485,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Small and Medium Enterprises Division*... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 5,441,588,000/=

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *subvote* 2002 kifungu kidogo 270800, *Current Grant to Non – Financial Public Units – (General)*

**MWENYEKITI:** *Okay*!

**MHE. HASNAIN M. MURJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *Current Grant to Non – Financial Public Units – (General).* Sisi Mtwara pale tuna vikundi vya akinamama, huwa wanabangua korosho na vile vikundi korosho zao ni nzuri kwa sababu wanabangua kwa mikono. Hata hivyo, wanapata tatizo kubwa sana katika *packing*.

Sasa je, hizi shilingi bilioni 4.7, zitawasaidiaje ili kuweza kupata *packing machine* pamoja na vifungashio ili na wao pia waweze kuuza mazao yao katika soko la *AGOA* kama alivyosema Mheshimiwa Waziri? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni kwa ajili ya taasisi za viwanda na biashara na siyo taasisi za akinamama.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3001 - *Commerce*... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 1,932,608,000/=
Kif. 4002 - *Commodity Market Development*... ... ... ... ... ... ..Sh. 6,981,354,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO WA MAENDELEO**

**Fungu 44 – Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko**

Kif. 1003 - *Policy and Planning*... ... ... ... Sh. 56,080,179,000/=

Kif. 2001 - *Industry*... ... ... ... ... ... ... ... ...Sh. 15,616,100,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 2002 - *Small and Medium Enterprises Division*... ... ... ... ... ... ... ... ... Sh. 6,224,594,000/=

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kupata ufafanuzi katika kasma ya 4486, *Agriculture Sector Development Programme*. Kwenye fedha za ndani hakujatengwa chochote. Kama unavyojua tumetoka kupitisha mpango maalum wa kukuza ajira kwa vijana wanaojihusisha kwenye sekta ya kilimo na hapa inahusu viwanda vidogo vidogo. Kuna vijana wengi ambao ni *graduates*, wamemaliza vyuo na baada ya kukosa ajira wameamua kuanzisha viwanda vidogo vidogo kupitia kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepitisha bajeti ya Wizara ya Kilimo, hakuna fedha yoyote ambayo imetengwa kwa ajili ya kuhakikisha inasaidia vijana. *Trend* hii pia inaendelea katika Wizara hii, hakuna fedha zozote ambazo zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa kuhakikisha vijana ambao wana-*invest* kwenye kilimo wanaweza kujikomboa na tatizo kubwa la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kupata ufafanuzi kutoka kwa Waziri, ni kwa nini hawajatenga fedha zozote za ndani katika kifungu hiki na badala yake wanategemea fedha za nje ambazo ni ndogo na hatuna *guarantee* nazo?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, fungu hili ni *ASDP* na ni mapendekezo ya wafadhili. Wafadhili huwa wanapendekeza kwamba, watafadhili katika eneo hili. Fedha hizi ni za kuimarisha mfumo wa taarifa za masoko na kuendeleza ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa hizo ambazo zinatumika katika mradi huo.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 4002 - *Commodity Market Development*... ... ... ... ... ... ...Sh. 965,770,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**TAARIFA**

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa taarifa kuwa, Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2013/2014, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote. Naomba sasa Bunge lako Tukufu liyakubali makadirio haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka 2013/2014 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nakushukuru sana.

Mheshimiwa Waziri hili suala la Wamachinga na bodaboda, ambalo juzi Mheshimiwa Waziri Mkuu alilitolea maelezo vizuri sana. Suala la Mama Lishe, hawa wana mahitaji kama sisi. Naomba Wizara yako pamoja na

Halmashauri ziweke utaratibu wa kuhakikisha na hawa wanajiona ni sehemu ya Taifa hili na wao wapatiwe heshima. (*Makofi*)

Tumeweka suala la MKURABITA, lakini watu wengi hawaelewi MKURABITA. MKURABITA ni Mkakati wa Kurasimisha Biashara za Wanyonge, na hii ni sera ya Chama cha Mapinduzi. Sasa sisi chama ndiyo tuwe wa mbele kusimamia suala hili. (*Makofi/Kicheko*)

Baada ya maneno haya, nakushukuru wewe Mheshimiwa Waziri na Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri mliyoifanya leo.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Sasa naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Kicheko)*

*(Saa 1.04 jioni Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Alhamisi, Tarehe 16 Mei, 2013 Saa Tatu Asubuhi)*